

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 21 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):-**

Taarifa za Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara, Idara na Serikali na Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka 2009/2010 (*The Annual Report and Audited Accounts of Tanzania Revenue Authority for The Year 2009/2010*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 86

**Posho za Madiwani**

**MHE. ZARINA SHAMTE MADABIDA** aliuliza:-

Diwani ni Kiongozi muhimu sana wa kusimamia utekelezaji wa mipango yote ya Kata, na kumsaidia Mbunge kumudu majukumu yake. Lakini pamoja na majukumu

mengine ya kusimamia maendeleo ya wananchi katika maeneo yao, wanapata posho ya shilingi 120,000/= ambayo ni kidogo sana ikilinganishwa na majukumu makubwa waliyonayo:-

Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuongeza viwango vya posho za Madiwani kulingana na kupanda kwa gharama za maisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Waheshimiwa Madiwani ndio wasimamizi wakubwa wa utekelezaji wa Mpango ya maendeleo ngazi ya Kata.

Aidha, ni kweli kuwa majukumu ya Madiwani yameongezeka hasa baada ya kuanzishwa dhana ya upelekaji madaraka kwa wananchi yaani (*D by D*). Kwa kuzingatia hilo Serikali imekuwa ikiboresha maslahi ya Madiwani ikiwemo posho na stahili mbalimbali kwa lengo la kuwarahisishia utekelezaji wa majukumu yao. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitekeleza ahadi yake ya kuongeza posho za Madiwani kama ifuatavyo:-

(i) Posho ya mwezi shilingi 120,000/= ambapo shilingi 60,000/= ni ruzuku ya Serikali Kuu;

(ii) Posho ya kikao shilingi 40,000; na

(iii) Posho ya madaraka kwa wenyeviti/meya viwango ni kati ya shilingi 100,000 na 350,000/=.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa utekelezaji wa Mpango wa kupeleka Madaraka kwa Wananchi yaani (*D by D*) umesababisha rasilimali nyingi kupelekwa katika ngazi ya mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kuhitaji usimamizi wa karibu chini ya Waheshimiwa Madiwani. Aidha, wakati najibu sehemu (a) ya swali la Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, kuhusu maslahi ya Madiwani katika Kikao cha Nane (8) cha Bunge hili nilieleza kwamba azma ya Serikali ni kuendelea kuboresha posho za Waheshimiwa Madiwani kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu. Hivyo, naomba Waheshimiwa Madiwani watambue kuwa Serikali hii ni sikivu na itaendelea kutekeleza azma hiyo kama ilivyokusudiwa.

**MHE. ZARINA SHAMTE MADABIDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini atakubaliana na mimi kwamba ni miaka sasa mitatu tokea kima hicho kipandishwe. Lakini vile vile

tumeshuhudia katika kipindi hiki ndiyo kumekuwa na mfumko mkubwa sana wa kupanda kwa vitu vingi sana.

Je, Serikali haioni kwamba sasa hivi imefika kweli kipindi wakati ambapo hizi posho ziongezwe hasa ukilia maanani kwamba hawapati mshahara?

Je, Serikali haiwezi sasa basi kama haiwezi kupandisha posho hizi sasa hivi kuwaruhusu Madiwani wapate asilimia japo ndogo katika makusanyo yao kutoka kwenye Manispaa zao ili posho zipande?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, haya yanayosemwa hapa, tiliyazungumza Dar es Salaam na katika Kamati yetu ile ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, alisema kwamba ni nini ambacho tunakusudia kufanya kwa maana ya kuboresha hizi posho za Madiwani zinazozungumzwa hapa. Wakati huo huo tulipokuja hapa Wabunge mbalimbali wamezungumza hapa ndani kwa uchungu mkubwa sana kuhusu posho hizi za Madiwani na wakati huo huo hata jana nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge wakizungumza hapa.

Wamezungumza kwa uzito mkubwa kuhusu posho za Madiwani. Sisi wenyewe kama Wizara tumekwenda katika Mikoa yote tiliyokwenda na Halmashauri zote kila mmoja amekuwa namna ya kuboresha posho za Madiwani.

Hakuna mtu yoyote Mheshimiwa Spika ambaye ana ubishi na hilo. Hata wewe mwenyewe huwezi kubisha katika jambo hili linalozungumzwa hapa. Tulipokwenda tukasema sasa tunataka kufanya kazi hii na naomba Waheshimiwa Wabunge watuamini tunaposema kwamba Serikali hii ni sikivu, ni Serikali ambayo inasikiliza kuhusu matatizo ya Madiwani. Nataka watuamini kwamba ni kweli kabisa tunavyosema hivyo, ndivyo anavyoamini Mheshimiwa Rais wetu, ndivyo anavyoamini Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi na sisi wote kama Wizara.

Nataka nikuambie leo hapa Mheshimiwa Spika, jambo hili tunalijadili, idadi yetu ya Madiwani imeongezeka. Sitaki nitumie takwimu hapa, kwa sababu nitaonekana kwamba natetea. Lakini niseme tu kwamba wakati tulipoanza kufanya kazi hii yako mambo mengi ambayo katika Sheria zetu yanaonekana kwamba yanakinzana na jambo linalozungumzwa.

Kwa mfano, suala la posho, iko Sheria inayozungumza kuhusu hilo. Kwa mfano, suala la kuwapa mishahara, iko Sheria inasema hivyo. Kwa mfano suala la kuwapa *exemption* Madiwani, iko Sheria. Mheshimiwa Waziri Mkuu, niseme hapa, ametuagiza kama Wizara kwamba tusimame tuangalie namna ambavyo tutamshauri ili hayo yote ambayo yanaonekana kwamba yanazuia posho hizi ziweze kutoka kama zinavyosemwa hapa yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kanuni ya kusonga ugali ni kuacha maji yachemke. Mimi naomba tu mtuamini kwamba maji yakishachemka kazi hiyo itafanyika na watuamini kwamba tutafanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Asante Mheshimiwa Spika kunipa fursa hii niulize swalii la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anakubali kabisa kwamba Madiwani ni watu muhimu sana kwenye kufuatilia maendeleo majimboni kwetu na kwa kuwa wakati tunapofanya kampeni tunasema mafiga matatu, figa la kwanza linahudumiwa vizuri, figa la pili linahudumiwa vizuri, figa la tatu tunalitekeleza amba ni Madiwani, sasa Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani au kauli gani kwamba tubadili Sheria zetu za fedha na Sheria za Halmashauri ili kwamba ikishindikana kuwaboreshea maslahi yao basi Madiwani nao waweze kukopa vyombo vya usafiri kama vile wanavyokopa Mawaziri, kama vile wanavyokopa Wabunge? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hii *theory* ya mafiga matatu ni sahihi kabisa. Hapa sisi tunaamini katika utawala na uongozi wa pamoja. Nataka niseme tu hapa, anazungumza juu ya Sheria mambo ya *exemption*.

Mambo ya *exemption* yana Sheria yake, watumishi wa Serikali, Wabunge kama inavyoelezwa, wenye mishahara, na vitu vingine. Madiwani wanapata posho, ukisema kwamba unawa-*exempt* unasema kwamba unawapa mimi, waende na wao wakanunue nao magari, unajiliza unawakata nini, unawakata posho na nini.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema kwamba mtupe nafasi sasa tuhuise haya mambo yatakapokuja hapa tukiyaleta hapa tukija wote sisi hapa tukazungumza mambo haya, hakuna hela ya Serikali inayotumika bila kupata kibali cha Serikali kwa maana ya Bunge hapa na sisi tuombe itakapokuwa imetokea hivyo baada ya kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi tutatekeleza yote yale ambayo nyinyi mtakuwa mmeelekeza hapa. Kwa hiyo naomba mtuamini kwamba tutafanya kazi hiyo na mtaona ambacho kitafanyika.

Na. 87

**Ujenzi wa Barabaraza Zinazounganisha  
Kanda mbili za Nkasi Kusini**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-**

Jimbo la Nkasi Kusini lililogawanyika katika kanda mbili ambazo zinajitegemea katika masuala yote ya kijamii na kiuchumi lina tatizo kubwa la mawasiliano ya barabara zinazounganisha kanda hizo. Wakati wa uchaguzi mkuu 2010 Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kuboresha barabara hizo za Kitosi-Wempembe, Nkana-Kala na Namanyere-Ninde.

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza mchakato wa kutengeneza barabara hizo tatu kama utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais?
- (b) Kwa kuwa barabara hizi ni mzigo usiobebeka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Je, Serikali iko tayari kuzichukua na kuzihudumia barabara hizo kupitia wakala wake (*TANROADS*)?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kuboresha barabara zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge, kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Rais, Halmashauri katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara ilifanya ukarabati wa barabara kama ifuatavyo:-

1. Barabara ya Kitosi – Wampembe yenyе urefu wa kilometa 68 imefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi yaani (*spot improvement*) kwa shilingi milioni 8 urefu wa kilometa 6;
2. Barabara ya Nkana – Kala yenyе urefu wa kilometa 67 imefanyiwa matengenezo ya muda maalum yaani (*periodic maintenance*) urefu wa kilometa 1 kwa shilingi milioni 15; na
3. Barabara ya Namanyere – Ninde yenyе urefu wa kilometa 60 imefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi yaani (*spot improvement*) kwa gharama ya shilingi milioni 7 umbali wa kilometa 5 na kujenga makalvati mistari 9 kwa gharama ya shilingi milioni 14.5.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa usafiri wa Serikali za Mitaa (LGTP), barabara ya Nkana – Nkala itafanyiwa ukarabati wa daraja lenye urefu wa mita 3 kwa kujenga sehemu ya juu yaani (*deck slab*) ya zege kwa gharama ya shilingi milioni 8.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza kwa vitendo ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara katika mwaka wa 2011/2012, imetenga shilingi milioni 9 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi, shilingi milioni 42 kwa ajili ya

matengenezo ya muda maalum na shilingi milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa makalvati katika barabara ya Namanyere – Ninde.

(b)Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa barabara hizi kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa kilijadili na kuridhia barabara hizi zipandishwe hadhi kuwa barabara za Mkoa. Maombi haya yamewasilishwa Wizara ya Ujenzi na yatafanyiwa kazi ikiwa ni pamoa na kuzitembelea ili kuhakiki kama zinakidhi vigezo vilivyopo kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa barabara ya Nkana na Nakala kwa barabara ya kutoka Kitosi, Wampembe na Nkana-Nkala yanatokana na kutokuifahamu vizuri barabara hiyo ilivyo korofi. Namwomba Mheshimiwa Waziri awe tayari kufuatana na mimi kwenda kuziona hizi barabara mbili?

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, waanchi walipaza sauti zao kwa Mheshimiwa Rais baada ya kuona kwamba Halmashauri yao haina ubavu wa kuzihudumia barabara hizi. Ndiyo maana Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa pia ikaridhia na kukubali kwa sababu hizo. Kiwango kinachotajwa kwamba kimeshughulikiwa sioni kama kinafanana na heshima ya kupaza sauti kwa Mheshimiwa Rais kwamba zimeshughulikiwa kwa kiwango hicho.

Je, katika bajeti hii Waziri yuko tayari kuniongezea pesa ili barabara hizi ziweze kuokoa akina mama ambao wamekuwa wakifia njiani kwa sababu ya kukimbizwa kwenda kwenye huduma za kliniki? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Ndugu yangu mwuliza swalii anafahamu kwamba pale TAMISEMI Wilaya yake ina mwakilishi mzuri sana ambaye ni Waziri wa Nchi, TAMISEMI ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa anaifahamu vizuri sana barabara hiyo.

Kwa hiyo wala hatuhitaji kufunga safari kwenda na mimi nataka niungane naye kwamba barabara hii kwa kweli ukitoka pale mjini kwenda kule bondeni imechafuka sana. Ombi lake kwamba Serikali tuangalie namna gani ya kuweza kuongeza fedha zinazotengwa. Tunaahidi kufanya hivyo kwa kadri fedha zitakavyoruhusu. (*Makofi*)

Pili, nadhani maelezo yamekwishatolewa kuhusu barabara kuchukuliwa na *TANROADS* kwamba kinachotakiwa Halmashauri yenyewe kupendekeza, kupeleka kwenye vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Ikishapitisha huko inaletwa Serikalini, wenye dhamana ya *TANROADS* watatafakari na watafanya maamuzi kwa kadri itakavyoona inafaa.

Kwa hiyo nataka nimhakikishie Ndugu yangu Mipata kwamba kilio hiki cha barabara TAMISEMI tuko pamoja na Wilaya ya Nkasi. (*Makofi*)

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, swal namba 87 lina tatizo lilopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Barabara ya Kalambanzite-Ilemba ni barabara muhimu sana kiuchumi, kihuduma na kisiasa.

Lakini ni barabara ambayo inahitaji zaidi ya bilioni moja katika matengenezo na ndiyo maana Halmashauri ya Wilaya na Mkoa ulitoa maombi kwamba barabara hiyo ipandishwe ichukuliwe na *TANROAD* maana Halmashauri haina uwezo wa kuitengeneza hiyo barabara. Sasa katika maombi hayo Mheshimiwa Waziri anatamka nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, maelezo yake jiografia ya jimbo lake, jiografia ya Wilaya ya Nkasi zinafanana. Jambo lake litatazamwa kwa uzito ule ule kama tutakavyotazama tatizo la Nkasi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba niongezee tu kwamba Wizara ya Ujenzi tayari ina taarifa ya barabara hizo mbili ambazo ameziongelea mwuliza swal la msingi ambazo zinaombewa na Bodi ya Mkoa kupandishwa hadhi kuwa barabara za Mkoa.

Barabara hizo ni Kitosi-Wampembe yenyе urefu wa kilomita 68 na barabara ya Nkana kwenda Nkala yenyе urefu wa kilomita 72 lakini hatuna taarifa kuhusu barabara ya Namanyere kwenda Ninde ningemshauri tu Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI afuate utaratibu tu wa kuiombea kupandisha hadhi.

Mheshimiwa Spika, maombi haya yameelekezwa kwenye Kamati maalum ya kutathmini mambo ya aina hiyo ili hiyo Kamati iweze kumshauri Waziri wa Ujenzi ipasavyo. (*Makofi*)

Na. 88

### **Wakimbizi Waliopewa Uraia**

**MHE. ANNA M. MALLAC** aliuliza:-

Wilaya ya Mpanda ilipokea wakimbizi waliokuwa wanaishi katika makazi ya Mishamo na Katumba lakini wengi wao walirejea makwao:-

- (a) Je, ni wakimbizi wangapi walipewa uraia na kuendelea kuishi katika makazi ya Katumba na Mishamo?
- (b) Kwa sababu Katumba na Mishamo yamebinafishwa na hawa waliokuwa wakimbizi sasa ni raia. Je, hawa wa uraia wa kupewa watapelekwa wapi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa AnnaMarystella J. Mallac, Mbunge, wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, zoezi la kutoa uraia kwa wakimbizi wa Burundi walioingia Tanzania 1972 lilifanyika kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995. Kwa kutumia sheria hiyo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aliridhia kuwapa uraia wakimbizi 162,156.

(b)Mheshimiwa Spika, wakimbizi wa Burundi waliopewa uraia wa Tanzania walioko katika makambi ya Katumba na Mishamo Wilaya ya Mpanda na wale walioko Ulyankulu Wilaya ya Urambo Mkao Tabora, bado hawajasambazwa katika Mikoa kama ilivyokusudiwa hapo awali. Hivi sasa Serikali inalitafakari suala hili upya kufuatia maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ANNA M. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri, nina swal la nyongeza. Kwa kuwa, wakimbizi waliorejeshwa makwao baadhi yao wamekuwa wakirudi Tanzania, kupitia njia za panya. Na katika kurudi kwao vitendo vya uhalifu wamekuwa wakiviedeleza kama vile uporaji katika Ziwa Tanganyika kwa wavuvi, utekwaji wa magari na uwindaji haramu.

Mheshimiwa Spika, Je, Serikali inafanya mipango gani katika kuhakikisha wanawakamata na Watanzania wa mkoa wa Rukwa kwa ujumla na Wilaya ya Mpanda, wanabakia katika hali ya usalama?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa AnnaMarystella J. Mallac, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama taarifa za Mheshimiwa Mbunge ni sahihi, za kwamba wakimbizi ambao walirudishwa makawao tayari wanarudi nchini Tanzania. Wizara ya mambo ya ndani ya nchi kwa kushirikiana na Kamati za ulinzi na usalama katika Wilaya na Mikoa, hasa katika Mkao aliouzungumza hapa Mkao wa Rukwa, tutashirikiananao ili kufanya doria na ukaguzi ili kuwabaini hao raia ambao wamerudi ili tupate nafasi ya kuwarudisha makwao.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na suala la ujambazi, kama ilivyo hata kwa raia wa Tanzania, ni jukumu la Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kupitia Jeshi la polisi ni

jukumu letu kuhakikisha kwamba raia ambao wanafanya vitendo vya uhalifu na wageni ambao wanaingia kwa kupitia njia za panya wanafanya vitendo hivyo hivyo vya uhalifu. Ni jukumu letu kuhakikisha kwamba tunawasaka na tukiwapata basi tutachukua hatua zinazostahiki.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tuendelee kushirikiana; yeze kama Mheshimiwa Mbunge anayetoka katika Mkoa huo na Viongozi wenzake wa mkoa. Waendelee kutupa taarifa, tutachukua hatua zinazostahiki ili kuhakikisha ulinzi na usalama kwa wananchi wanaoishi katika mkoa wa Rukwa na wananchi wengine wanaoishi katika maeneo mbalimbali ya mikoa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, Makambi ya Wakimbizi ya Katumba, Mishamo na Rubufu, ni moja ya maeneo ambayo yametambuliwa kwa ajili ya ukulima mkubwa wa Kampuni ya Kimarekani ya *Agro Soil*. Na inasemekana kwamba wakimbizi hao wanasantazwa ili kuweza kupisha wakulima hawa na kampuni hii ya Kimarekani kwa ajili ya kulima.

Naomba Mheshimiwa Waziri, alithibitishie Taifa, kwamba mpango wa kuwasambaza wakimbizi ni kwa sababu, ya kupisha wakulima wakubwa waweze kulima kwenye Makambi hayo ya wakimbizi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa, Kabwe Zitto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sijapata taarifa juu ya kusambazwa kwa wakimbizi hawa katika maeneo mengine, kwa sababu tu tunataka hilo eneo ambalo walikuwa wanaishi wakimbizi, linataka kupewa kwa raia mmoja wa Marekani, taarifa hizi kwangu ni ngeni. Kama nilivyosema awali, Serikali ilipofanya maamuzi ya kuwapa uraia wakimbizi wenye asili ya Burundi 162,156 ilikuwa na dhamira ya kuwagawa hawa katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu dhamira ya Serikali; kwa kuwa, tunaamini kwamba hawa raia wenye asili ya Burundi, walitaka uraia wa Tanzania kwa sababu wanaipenda sana Tanzania na watanzania. Kwa kuwa, wanawapenda watanzania kwa namna zote, tulihisi kwamba njia bora ni kuwagawa katika mikoa mbalimbali ili wapate nafasi ya kujifunza mila na desturi za watanzania. Ili na wao wajifunze ukarimu na tabia na silka njema za watanzania, ndio ilikuwa madhumuni hayo. Na wala hakukuwa na madhumuni ya kutenga hilo eneo kwa ajili ya mkulima huyo aliyesema kutoka Marekani. (*Makofii*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa njia panda kwenye maudhui mazima ya kukubali kuwapa uraia watu 162,156 wa nchi moja kwa wakati mmoja. Lakini kwa kuzingatia na hasa kwa kuzingatia kwamba

Watanzania wengi wanauwana leo katika mabonde ya Kiru na maeneo mengine kutokana na uhaba wa ardhi. Lakini bado swali langu linabaki kwamba.

Je, kwa wakimbizi mnaowatawanya katika maeneo kame kama ya Simanjiro, ambayo tatizo la maji ni kubwa na kilimo hakiwezekani katika maeneo hayo, ina maana mtawapa na ng'ombe wa kuja kufuga huko?

Maana hatuko radhi kutenga maeneo yetu ya ufugaji ili yaanze kulimwa na wageni wanaokuja wakati sisi wenyewe tulyahifadhi kwa ajili ya ufugaji?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Kaka yangu Ole-Sendeka, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie maelezo yangu ya awali.

Mheshimiwa Spika, nilisema hapo awali ni kweli kulikuwa na dhamira hiyo ya kuwagawa hawa wakimbizi katika mikoa 16. Lakini Serikali ya watu, inayosimamia maslahi ya watu, wananchi wake na viongozi wanapotoa hoja juu ya jambo fulani, Serikali iliyo makini kama Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni lazima iwe sikivu. Tumesema tunesikia, tunalitafakari jambo hili ili kutafuta njia iliyo muafaka itakayowardhisha Watanzania juu ya jambo hili.

Tutakapopata njia mufaka, basi tutakuja kwenu kuwashirikisha na kuwaelimisha juu ya umuhimu wa kufanya jambo hili. Kama tubadilishe uamuzi au tuendelee na uamuzi wa awali baada ya Watanzania kushiriki kikamilifu na kukubali juu ya uamuzi ambaa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeufanya, baada ya kufanya mashauriano zaidi na viongozi pamoja na wananchi wa maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Na. 89

#### **Vigezo Vya Utoaji Misaada Kwa Kampuni ya African Barrick**

**MHE. STEPHEN J. MASELLE (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI)** aliuliza:-

Migodi ya dhahabu ya Bulyanhulu na Buzwagi katika Wilaya ya Kahama, iko katika Majimbo mawili tofauti na migodi yote hiyo iko chini ya mmiliki mmoja, *African Barrick*, ambaye amekuwa akisaidia miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Wilaya kama vile ujenzi wa Sekondari na Zahanati pamoja na misaada mingine ya kijamii lakini kwa taratibu zisizo za wazi:-

(a) Je, ni vigezo gani kampuni ya Barrick inavitumia kutoa misaada hiyo ya kijamii kwa mfano vifaa vya michezo kwa vijana wa Kahama?

(b) Je, Kwa nini mgodi wa Buzwagi umeshindwa kuwasaidia wananchi wa kijiji cha Chapalwa kama inavyofanya kwa vijiji jirani vya Mwendakulima na Mwima

kuwajengea angalau Zahanati au kukarabati shule ya msingi Chapalwa ambayo imechoka sana na iko umbali wa mita 500 kutoka uzio wa mgodi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuleta maendeleo kwenye maeneo yanayozunguka Mgodi, Mgodi wa Buzwagi hufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Wilaya ya Kahama, Tarafa na wadau wengine wa maendeleo katika Wilaya. Mpango wa Maendeleo wa Wilaya hupitiwa kwa pamoja kwa kushirikisha wadau wote na tathmini ya mahitaji ya kijamii, hufanywa kwa pamoja ili kuwa na uelewa wa vipaumbele vya maendeleo. Vipaumbele hivyo huingizwa kwenye mpango wa utekelezaji wa Wilaya. Baada ya hatua hii, Mgodi unaandaa mpango wake wa kusaidia jamii zinazozunguka migodi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la awali, suala hili la kusaidia ama ujenzi wa shule ya msingi ama zahanati ya chapulwa, ni suala ambalo linatakiwa lijadiliwe na liangaliwe namna ya kulipatia ufumbuzi wakati wa kutathmini mipango ya utekelezaji ndani ya Halmashauri ya Kahama, ambapo Mheshimiwa Mbunge ni mdau.

Taarifa niliyokuwanayo inaonesha kuwa mgodi wa Buzwagi, umechangia katika maeneo na shughuli mbalimbali katika vijiji vya Chapulwa, Mwime na Mwendakulima.

(c) Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, afikishe ombi la kusaidiwa matengenezo ya kuboresha hali ya shule ya Chapulwa na Zahanati yake, kupitia utaratibu uliopo.

**MHE. STEPHEN J. MASELLE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri, atawaeleza wananchi wa Shinyanga na maeneo mengine yenye mgodi kwamba suala la kusaidia huduma za jamii kama shule, maji na afya, sio suala la hiyari bali ni suala la kisheria, migodi hiyo inapaswa kuchangia maendeleo ya maeneo husika?

(b) Je, mgodi wa Buzwagi, utakuwa tayari sasa, kama swali la msingi lilivyoulima katika kipengele cha (a), kusaidia timu ya mpira ya *Shinyanga United*, ambayo imefanikiwa kuingia katika hatua ya ligi daraja la kwanza, ili iweze kwenda kushiriki ligi kuu ya *VODACOM*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maselle, kwa niaba ya Mheshimiwa Lembeli.

Mheshimiwa Spika, suala la kusaidia huduma za jamii zinazozunguka mgodi, masuala haya yako kwenye utaratibu wa *Corporate Social Responsibility*, ambayo Serikali inakubaliana na waendelezaji wa mgodi, si kwa masuala ya mgodi wa madini tu lakini kwa miradi mingine iliyopo.

Sasa linapokuwa kwenye mkataba ambao Serikali inaingia pamoja na muendelezaji wa mradi huo, linakuwa ni suala ambalo tumekubaliana, linatekelezwa kwa mujibu wa tulivyokubaliana linapokuwa nje ya mkataba ule, linakuwa suala la hiyari.

Mheshimiwa Spika, lakini katika masuala yale ya Buzwagi, mimi binafsi nilikwenda Buzwagi na Mheshimiwa Mbunge, tumekaa pale na watu wa Mgodi 2008, 2009, na hata mahusiano yaliyopo sasa hivi baina ya Buzwagi na maeneo ya Mwendakulima, Chapulwa pale, na Mwime, yanatokana na makubaliano tuliyosema na tuliafikiana kwamba, kuna mambo ya kimkataba lakini pia na busara ipo.

Kwa hiyo, katika masuala yale baada ya pale ukiangalia mgodi ule kusema kweli umesaidia baadhi ya mambo mbalimbali na ndio maana nimeshangaa kidogo kwamba hiki kishule kiko kama mita 500 tu kutoka pale kwenye uzio, lakini haijasaidia. Tumeongea na watu wa *Barrick* wamesema kwamba watawasaidia lakini maombi yapitie kwenye utaratibu ule wa kupitia kwenye Halmashauri, ambapo Mbunge na Diwani wote wanahusika.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la *Shinyanga United*. Kwanza napenda kuwapongeza ndugu zangu wa *Shinyanga United*, kwa kufanikiwa kuingia kwenye Ligi Kuu ya *VODACOM*. Lakini ninaamini kwamba pale Shinyanga, wadau wa Shinyanga na hii ni kama timu ya Mkoa, wako wengi.

Kwa hiyo, ninawashauri wadau wote wa Shinyanga wapitishe kikapu kwa wadau wote wa Maendeleo ya Mkoa wa Shinyanga. Wako pale watu wa Mwadui, wako akina AlHilal, wako watu wengine wengi tu, ili lisiwe jambo la *Barrick* na mkiwafikishia *Barrick* nao kwa sababu ni wadau wa Shinyanga, nao ninaamini kwamba kwa pamoja wahusika wote watahusika katika kuifanikisha *Shinyanga United*, kushiriki vizuri zaidi katika ligi ya *Vodacom*.

Na. 90

#### **Hitaji la Umeme Katika Jimbo la Busanda**

**MHE. LOLESLIA J. M. BUKWIMBA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kupeleka umeme wa *MCC* katika vijiji vya Bukoli, Nyarugusu, Rwamgasa na Katoro, katika mwaka wa fedha uliopita (2010/2011) lakini hadi sasa ahadi hiyo hajatekelezwa.

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huu ili wananchi wapate huduma hii kwa Maendeleo yao?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kukamilisha utekelezaji wa mradi wa umeme katika vijiji alivyovitaja vya Bukoli, Nyarugusu, Rwamgasa na Katoro, kuititia ufadhili wa *MCC*. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, vijiji hivi vimo katika mpango wa utekelezaji kwa mwaka huu wa fedha unaokamilika 2010/2011 na vitakuwemo katika mpango kazi wa utekelezaji wa mradi katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umeshaanza ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 shughuli zifuatazo zilifanyika:-

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa taratibu za manunuzi ikiwemo kutangaza zabuni za kumpata Mkandarasi na kupatikana Mkandarasi wa kutekeleza kazi hiyo katika maeneo hayo ya Busanda, ambayo ni kampuni ya *Symbion Power LLC* kutoka Marekani.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ni kukamilisha hatua ya upimaji wa kina wa njia za umeme na kuweka alama za zege (*beacons*), kuainisha wigo wa njia ya kusambazia umeme na kazi ya uthamini wa mali na mazao ya wananchi ambao wataruhusu kuitisha miundombinu ya umeme kupita maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, vile vile mradi ulikamilisha tathmini za awali na kukamilisha taratibu za malipo na malipo kwa waathirika sahihi wa mradi, kazi ambayo inaendelea na itakamilika mwishoni mwa mwezi Septemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, shughuli za ujenzi kwa Mkoa wa Mwanza, zikiwemo kusafisha njia, kuchimba mashimo na kusimika nguzo zimeanza tangu mwezi Mei, 2011. Aidha, katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, shughuli za ujenzi zitaanza mwezi Agosti, 2011.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika maeneo ya Busanda kuna maeneo ambapo huduma za kijamii ambazo ni muhimu sana kwa wananchi ambazo hazikupitiwa na mradi huu wa *MCC* lakini zinahitaji umeme huu, hasa katika Kituo cha Afya cha Kashishi ambapo akina mama wengi huenda wakati wa kujifungua usiku, huwa wanatakiwa kulipa 1,000/= kwa ajili ya mafuta ya taa. Wakati sehemu hizo umeme huu wa *MCC* haukupitia.

Je, ninaiuliza Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba sehemu kama hizi kituo cha Afya cha Kashishi pamoja na shule za Sekondari kama Kamena, Nyamalimbe, Busanda na Nyakamwaga, kwamba zipatiwe umeme kama sehemu nyingine?

Mheshimiwa Spika, lakini pia swal la pili, ningependa kufahamu kwamba huu umeme wa *MCC*, utahusika pia katika kusambaza umeme katika kaya kwa sababu wananchi wengi wa vijiji kipato chao ni cha hali ya chini.

Kwa hiyo, je, umeme huu wa *MCC* utaweza kusambaza umeme huu katika Kaya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taswira ya miradi ya *MCC* iko miradi ina sura kama 5, lakini hii ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Bukwimba, ipo katika *package* ile ya 5 ambayo ni *transmission and distribution*, inakwenda kwenye Wilaya kama 24 katika Mikoa 6. Fikra yake ni kwamba pale ambapo umeme umeishia miradi hii itasogeza umeme mpaka kwenye vijiji hivyo 86. Sasa ikishafika pale, tutatafuta kama Serikali, ama kupitia Serikali ama kupitia *TANESCO* ama kupitia *REA*, kukamilisha zile kazi za usambazaji ambazo hazitafikiwa na *MCC*.

Mheshimiwa Spika, kuna pesa kwenye *MCC* zilitengwa, dola milioni 47 zimekwenda *Symbion* kwa ajili ya miradi yake na dola milioni 27 au 24 nadhani zimekwenda *Pike*, kwa ajili ya miradi ambayo inafanywa na *Pike*. Sasa baada ya pale wakishakamilisha, watakapofikia wao fikra ilikuwa kwamba, *TANESCO* au Serikali au *REA*, kwa utaratibu ambao tunafanya maeneo mengine, uendelee pale ili kufikisha umeme kwenye maeneo kama yale ya Kashishi, Nyamahimbe na Nyakamwaga.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, mimi mwenyewe nimefika kwenye maeneo hayo na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ni mdau wa maeneo hayo. Kwa hiyo, tunayafahamu vizuri na tunaomba tumhakikishie Mheshimiwa Bukwimba, kwamba umuhimu wa kufikisha umeme hasa kwenye hii zahanati ya Kishishi, tunaifahamu vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili suala la *MCC* katika Kaya, nadhani nimelijibu katika swalii hili la kwanza, kwamba wao watafikisha umeme kama ilivyokuwa katika makubaliano ya kimkataba kulingana na ufadhili ule wa *MCC*.

Katika kuendeleza kwenye maeneo ambayo wananchi wanahitaji umeme, hilo ni suala ambalo litakuwa katika Mamlaka ya Serikali, *REA* na taasisi nyingine kama inavyofanywa kwa maeneo mengine ambayo hayana mradi wa *MCC*.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza masuala ya miradi ya *MCC* ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumza yanafanana sana na mradi wa *MCC* ambao upatikana kule Kigoma na kwa kuwa nimezungumza na Waziri muda mrefu uliopita kwamba mkoa wa Kigoma pamoja na kuwa na uhaba mkubwa wa umeme kwa maana ya kwamba unazilisha *Megawatt* 11 lakini ni mkoa ambao una ziada ya umeme kwa maana kwamba hata hizo 11 hazitumiki zote na sababu kubwa ya *distribution*. Sasa nikamtaka Waziri wakati ule, kwamba kwanini wasiangalie mradi ule wa *MCC* badala ya kuanza na *generation* waanze na usambazaji ili kusudi *megawatt* za ziada takriban 6 zitumike wakati tunasubiria *generation* badala ya sasa mkoa ambao unauhaba mkubwa wa umeme na bado ibaki na ziada ya umeme, naomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa David Kafulila, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa David Kafulila kwamba jitihada iliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) katika miaka miwili iliyopita ya kuipatia Kigoma umeme ni jitihada kubwa sana. Miaka mitatu iliyopita Kigoma ilikuwa ina *megawatt* 2, leo Kigoma ina *megawatt* 11 alahamkulilahi. Naomba sasa nimsaidie Mheshimiwa Kafulila kwamba pale kwenye mradi wa Kigoma, Kigoma kulikuwa na miradi miwili, mmoja ni Malagarasi umesimama kidogo.

Taarifa hii ni taarifa ya *MCC* ya jana mchana saa nane. Kwa ruhusa yako nusu dakika tu, inasema hivi kuhusu Kigoma. Kigoma “*distribution network rehabilitation and network extension another activity for Kigoma is the preparation of technical document and bills of quantities for distribution, network rehabilitation and network extension study covering Kigoma Town. When completed an agreement will be made how to take the package on board as part of big transmission and distribution already contracted out on to one contract. The consultant has completed the study and building package is ready for negotiations*”. Kwa hiyo, kwa kutambua kwamba hii Malagarasi imesimama tumeshakubaliana na *MCC* kwamba kile kipande cha kuongeza *network distribution* Kigoma iendelee. Wamekubali na mazungumzo yanaendelea Mheshimiwa mambo yatakuwa mazuri *ishallah*. (*Makofii*)

**SPIKA:** Muda hautoshi, tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, utauliza swalii.

**Athari za Mfumuko wa Bei kwa Wananchi wa Kipato cha Chini**

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Mfumuko wa bei unaathirika kwa kiwango kikubwa bidhaa muhimu katika soko, na hali hiyo inagusa wananchi wengi hasa wale wenye kipato cha chini.

Je, Serikali ina mikakati yoyote ya kuwasaidia walaji hao wa kipato cha chini dhidi ya athari hii ya bidhaa za sokoni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mionganii mwa vyanzo vya mfumuko wa bei nchini ni pamoja na kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia, kutokupatikana kwa umeme wa uhakika na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaathiri uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua athari zitokanazo na mfumuko wa bei kwa wananchi wa kipato cha chini imeanza kuchukua hatua ya kuuza sehemu ya chakula kutoka katika hazina ya nafaka ya Taifa kwa bei ya chini. Aidha, kupitia upya mchanganuo wa tozo zilizopo katika bei za mafuta kwa lengo la kuzipunguza na kupunguza makali ya bei za nishati kwenye mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo Serikali inachukua hatua ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kusimamia kwa karibu zaidi ujazi wa fedha kwenye uchumi;
- (b) Kuongeza uzalishaji wa nishati kwa kutumia vyanzo mbalimbali;
- (c) Kukamilisha taratibu za ununuzi wa mafuta kwa wingi (*bulk purchase*);
- (d) Kuongeza upatikanaji wa chakula kwa kuhimiza kilimo cha umwagiliaji maji; na
- (e) Kuimarisha miundombinu ya barabara ili kupunguza gharama za usafirishaji wa mazao na bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi kuendelea kulima mazao yanayostahimili ukame, kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji maji na kijiwekeea akiba za chakula cha kutosha kila kaya. Aidha, sekte binafsi inahimizwa kushiriki kikamilifu katika uwekezaji kwenye kilimo na nishati ili kusaidia kupunguza za gharama za maisha kwa wananchi hasa wenyewe kipato cha chini na kukuza uchumi wa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Kigoda, swali la nyongeza, umeridhika, okay, Mheshimiwa Mnyika swali la nyongeza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hatua kuu ni kutoa mahindi kwenye ghala la chakula pamoja na kupunguza tozo.

Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali kwamba kwa kuwa Serikali inafahamu kabisa kwamba kupunguza tozo kwenye mafuta hakutapunguza bei ya mafuta kwa zaidi ya asilimia tano. Je, ni kwanini Serikali haioni umuhimu wa kupitia upya kodi za mafuta ambazo zinachangia takribani asilimia kati ya asilimia kati 26 mpaka 30 kwenye bei ya mafuta ili kutekeleza kweli azma ya kupunguza bei ya mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyika kama ifuatavyo:-

Kitu ambacho Serikali imekusudia kufanya ni kupunguza makali ya maisha siyo kupunguza tozo. Kwa hiyo, ikiwa tozo zitaonekana katika *analysis* hazitatosha Serikali itaangalia hatua nyingine ambazo inahisi zitafaa. (*Makofii*)

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa siyo waadilifu na kwa mara nyingi huwa wanauzu bidhaa mara tatu au mara nne ya bei au ya gharama hizo. Je, Serikali inasemaje, kuhusu Tume ya bei ambayo itasaidia sana kumlinda mlaji? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Katika mwisho wa mwa miaka ya tisini, Serikali ya Tanzania iliamua kwenda kwenye soko huria, soko huria Waheshimiwa Wabunge linachangamoto zake na hili ni moja ya kitu tunachotakiwa hapa tufanye ni kuhakikisha kwamba tunajipanga na hawa wafanyabiashara ambao si waaminifu tunawachukulia hatua za kufaa ikiwa pengine kuwanyima leseni au hatua nyingine ambazo zipo. Kwa hiyo, Serikali kwa sasa haina mawazo ya kurudisha Tume ya bei mpaka ione kwamba imeshindwa kupitia hizi hatua nyingine ambazo zinakubalika kwenye soko huria.

## **Serikali Kufadhili Mafunzo ya Law School**

### **MHE. SADIFA JUMA KHAMIS aliuliza:-**

Wanafunzi waliomaliza shahada ya sheria hutakiwa kujiunga na *Law School* ili hatimaye watambulike kama wanasheria na kwamba Serikali haitoi ufadhili wowote katika masomo hayo:-

- (a) Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwasaidia fedha ya ada (*Tuition fee*) na malazi (*Accommodation*) wanafunzi hao?
- (b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wanafunzi wasiokuwa na uwezo ili waweze kujiunga na masomo hayo muhimu?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Bodi ya mikopo ya Wanafunzi wa mikopo ya elimu ya juu iliyoundwa chini ya sheria Na. 9 ya mwaka 2004, hutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za elimu ya juu, waliodahiliwa kusomea Stashada ya juu yaani *Advanced Diploma* na Shahada *Degree* katika vymo vya elimu ya juu.

Mkopo huu hutolewa kwa wanafunzi anapokuwa masomoni katika maeneo yaliyoainishwa katika kifungu Na. 16 cha sheria tajwa ambayo ni chakula na malazi; vitabu na viandikwa; mafunzo kwa vitendo; utafiti; mahitaji ya vitivo na ada ya mafunzo.

Mheshimiwa Spika, wanaojiunga na *Law School* huwa tayari wameshahitimu masomo yao ya Shahada ya Sheria. Hivyo, mafunzo ya *Law School* ni mafunzo ya *internship/apprenticeship* kama ilivyo kwa fani za afya na uhandisi. Kwa kuzingatia matakwa ya sheria iliyoanzisha Bodi ya mikopo, Serikali haiwajibiki kuwapa mkopo wa ada, chakula na malazi wahitimu walio chini ya mpango wa *internship*.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali langu la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa wahandisi na madaktari wanapata hizi fedha, Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia ni lini na hawa wanafunzi wa Sheria na wao watapatiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mbunge wa Donge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba hawa wanafunzi wa Law School wanakuwa wameshamaliza tayari shahada ya kwanza. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu haiwajibiki moja kwa moja kuwapa fedha ya Bodi ya Mikopo kutokana na sheria yenewe ya Bunge hili Tukufu lilitunga mwaka 2004.

Lakini sasa kuhusu fani zingine za uhandisi pamoja na fani za Udaktari, Afya, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba wao wanalipwa na mimi niseme kwamba sijafanya utafiti kwamba hizo sehemu zingine wanalipwa posho hizo. Lakini kwa sababu Serikali ni moja na Waziri wa Afya yupo hapa na Waziri wa Miundombinu na Ujenzi wapo hapa, tunachoweza ni kushirikiana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kuonana na watu wa Wizara ya Sheria na Katiba, tuone kama uwezekano upo kwenye Wizara zao kwamba tunaweza tukaanza sasa kuwalipa hawa vijana wanaokuwa kwenye *internship*. (*Makofi*)

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa suala la *Law School* limekuwa likisumbua wanafunzi wengi. Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuingiza *Law School* kama mtaala ili wanafunzi wasome moja kwa moja wakimaliza wanaenda kuajiriwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana shule ya sheria (*Law School*) imeanza mwaka juzi wakati sheria hii ya mikopo ilikuwa imeshaanza siku nyingi. Kwa hiyo, labda utaratibu ufanyike ili kuweza kuwa *included* kwenye huu utaratibu. Lakini kimsingi wao hawako kwenye huu utaratibu, hao unaosema ni ufundu na wengine tayari wako katika ile sheria ahsante.

Na. 93

### **Ujenzi wa vyuo vya ufundu na Ualimu Mbogwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Kutokana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanikiwa katika mpango wa upanuzi wa elimu ya msingi na sekondari kwa kila Kata hapa nchini, upo pia umuhimu wa kuanzisha ujenzi wa vyuo mbalimbali vya ufundu, Ualimu na Afya ili wananchi wafaidike kupata elimu ya juu zaidi:-

Je, Serikali itakubali ombi la wananchi wa Mbogwe la kuwajengea chuo cha Ufundu (*VETA*) na chuo cha Ualimu ili wananchi wapate elimu na wawze kujiajiri wenewe?

## **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua umuhimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa maendeleo ya nchi yetu, Serikali kupitia Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na mwaka 2010 pamoja na ahadi nyingine, ilitoa ahadi ya ujenzi wa chuo cha ufundi stadi katika kila wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kutekeleza ahadi ya kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila wilaya ili kuwapatia wananchi wake wakiwamo vijana wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari stadi za kuwawezesha kujajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa ujenzi wa chuo cha mafunzo ya ufundi stadi hutanguliwa kwanza na zoezi la kutambua stadi zinazohitajika kufundishwa katika eneo husika kwa kushirikisha uongozi wa wilaya na jamii husika. Utambuzi stadi ulifanyika katika wilaya ya Bukombe kabla haijagawanywa kuundwa wilaya mpya ya Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wilaya mpya ya Mbogwe ilikuwa sehemu ya wilaya ya Bukombe ambako utambuzi wa stadi ulishafanyika, Wizara yangu itapitia upya stadi hizo ili kubaini stadi zinazohitajika katika wilaya ya Mbogwe na wilaya ya Bukombe. Aidha, kwa kuwa wilaya ya Mbogwe mpya ipo jirani na wilaya ya Bukombe mama ambayo ni mionganoni mwa wilaya 28 zitakazoanza kujengewa vyuo hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali ikiendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

Kwa sasa nawashauri wananchi wa wilaya ya mpya ya Mbogwe watumie chuo cha ufundi stadi Shinyanga kupata mafunzo ya ufundi stadi.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Masele ameridhika au kama hamjaridhika unasimama haraka au namwita mtu mwingine.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa nchi yetu ina utaratibu wa kisheria wa kuwa na chuo cha ualimu wa *Grade A*, katika kila mkoa.

Kwa bahati mbaya Mkoa wa Shinyanga mpaka sasa hakuna chuo cha *Grade A* hata kimoja wakati mikoa mingine kuna vyuo zaidi ya kimoja.

Je, mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kutujengea chuo cha ualimu *Grade A*, katika mkoa wetu wa Shinyanga?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo. Kuhusu ujenzi wa vyuo vya walimu, ujenzi wa vyuo wa walimu unategemea maoteo, yaani *projection* ya mahitaji ya walimu nchini ikilinganishwa na idadi ya walimu wahitimu katika vyuo vya ualimu na vyuo vikuu vilivyopo.

Vilevile vyuo hivi vya ualimu ni sawa kama na vyuo vikuu ni vya kitaifa na kwa hiyo, havifuati ueneo. Kwa hiyo wanafunzi wa maeneo ya Mbogwe, Bukombe, Shinyanga wanapata nafasi katika vyuo vingine kadri ya vilivyojengwa kwenye mikoa mingine hapa Tanzania.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa kuwa kama alivyoongea yeye mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri umuhimu wa vyuo hivi vya ufundi katika Wilaya na kwa kuwa wilaya nyingi hapa Tanzania hazijapata hizi shule za ufundi na kwa kuwa katika mpango wa maendeleo wa mwaka huu zimetengwa milioni 100 tu ambazo hazitoshi kujenga hata chuo kimoja. Sasa ni lini Serikali itatenga fedha nyingi za kutosha ili iweze kujenga vyuo vingi kiwemo Meatu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Vyuo vya VETA ni gharama sana, takriban shilingi bilioni nne mpaka sita pamoja na kuweka vitendea kazi na vyombo vingine. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inashirikiana na Benki ya *ADB*, yaani *African Development Bank* na tumeandika maandiko mengi sana kwa ajili ya kuomba fedha ili vyuo hivi viweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa katika mchakato wa kukamilisha Vyuo vya VETA kila Wilaya, bado tulikuwa tunakamilisha Vyuo vya Mikoa. Kwa mfano, Mkoa wa Dar es Salam chuo kimeshakamilika, Mkoa wa Lindi na Pwani, tunaendelea kukamilisha ujenzi huo wa Vyuo vya Mikoa halafu tunakuja kwenye Vyuo vya Wilaya, ambavyo tayari wataalamu wetu wameshafanya stadi za kukamilisha ujenzi wake katika Wilaya 28. Tumeanza na Wilaya ya Makete na ninadhani kwa mwaka huu chuo hicho kitakamilika.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali inafanya maandiko mbalimbali, kwa kutumia fedha za ndani tutaanza polepole kukamilisha ujenzi wa vyuo hivyo.

## **Matumizi ya Bandari Tulizonazo**

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa Bandari ya Dar es Salaam inakuwa na kiwango cha juu cha ufanisi ili wafanyabisahra toka nchi jirani wasikimbie na kulikosesha Taifa mapato?

(b) Je, kwa nini Serikali inapanga kujenga bandari mpya ya Bagamoyo wakati bandari zilizopo zikiwepo za Tanga na Mtwara hazijatumiwa ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina mikakati ifuatayo ya kuboresha Bandari ya Dar es Salaam:-

- (i) Kuongeza kina cha langoo la bandari, yaani *entrance channel* ili kuwa na kina cha mita 14 kutoka mita 12 na upana wa mita 240 kutoka mita 140 kwa sasa ili kuruhusu meli kubwa kuingia bandarini.
- (ii) Bandari kuwa na maeneo ya kufanya kazi ya kuhudumia mizigo nje ya bandari pamoja na kushirikisha sekta binafsi kwenye vituo vya kuhifadhia mizigo, yaani *Inland Container Depots – ICDs* na *Container Freight Stations* sehemu ya kuhifadhia mizigo hiyo na Container.
- (iii) Ujenzi wa Gati mbili za kuhudumia *Container Gati Namba 13 na 14* utaongeza uwezo wa Bandari kutoka *Container* futi 20 zipatazo 410,000 za sasa hadi *Container* za ukubwa wa futi 20 zipatazo milioni 1.2.
- (iv) Ujenzi wa Boya kubwa la kupakulia mafuta mchanganyiko, yaani *Single Point Mooring – SPM* lenye uwezo mkubwa wa kuhudumia meli za mafuta hadi ukubwa wa tani 120,000 na hivyo kupunguza msongamano wa meli ndogondogo zinazoleta mafuta kwa sasa.
- (v) Ununuzi wa vifaa vya kuhudumia shehena kama *Crane* na kadhalika.
- (vi) Kuimarisha mtandao wa *computer* ili kuboresha na kurahisisha shughuli za utendaji kazi wa bandari na kuimarisha ulinzi.
- (vii) Kuweka utaratibu ili mamlaka ya Bandari (*TPA*), Mamlaka ya Mapato (*TRA*) na Kampuni ya Kuhudumia Makontena Bandarini (*TICS*), ziweze kutoa huduma saa 24 kila siku. Mikakati hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, Mpango Kabambe wa Kuendeleza Bandari Tanzania, yaani *Port Master Plan* wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari, umebainisha umuhimu wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo kutokana na ongezeko kubwa la shehena katika Bandari ya Dar es Salaam. Madhumuni ya kujenga Bandari ya Bagamoyo ni kusaidia

uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam, ambayo imeshindwa kumudu ongezeko la shehena inayopita katika Bandari hiyo kutokana na eneo finyu la upanuzi. Aidha, ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo utasaidia shughuli za eneo maalum la kiuchumi, yaani *Economic Processing Zone – EPZ*, ambazo zitaendelezwa Bagamoyo. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo umefanyiwa upembuzi yakinifu, yaani *feasibility study* na umeonesha unafaa, yaani *feasible*. Ripoti imebainisha kuwa, Bagamoyo itakuwa bandari ya kisasa yenye kina cha mita 14 na hivyo kuruhusu meli kubwa zenye uwezo wa kubeba *foot container 20* ambazo 7,000 hadi 8,000 kwa wakati mmoja kuja Tanzania. Aidha, Serikali ina mpango wa kuziendeleza Bandari za Mtwara na Tanga, Bandari ya Mtwara inaandaliwa kuwa lango la biashara katika Ukanda wa Mmaendeleo wa Mtwara, yaani *Mtwara Development Corridor* hususan katika uchukuzi wa Mafuta, Gesi, Mbolea, Karatasi, Korosho, Chuma na Makaa ya Mawe.

Bandari itatumwa pia na nchi za Malawi na Msumbiji Kaskazini na itakuwa kichocheo cha maendeleo katika ukanda huo. Kazi zilizofanyika kwa sasa katika Bandari ya Mtwara ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu ili kubainisha mahitaji ya bandari, sambamba na mahitaji ya Ukanda wa Mtwara. Kununua vifaa vya kuhudumia mizigo bandarini na kufanya maandalizi ya ujenzi wa Gati Namba Tatu utakaoanza mwaka 2011/2012.

Mpango wa Bandari ya Tanga kuboresha huduma za Bandari iliyopo sasa na kujenga Bandari mpya eneo la Mwambani. Kwa sasa katika Bandari ya Tanga, vifaa mbalimbali vimenunuliwa ikiwemo Matishari, yaani *Barge* na pia kuimarisha sakafu, yaani *pavement* katika eneo la kuhifadhi makontena.

Kuhusu Bandari ya Mwambani, lengo la Serikali ni kuifanya kuwa lango la kupitisha mizigo, yaani *gateway* kwa ajili ya shehena inayokwenda Kaskazini mwa Tanzania, yaani Uganda, Rwanda, Burundi na Sudani Kusini, baada ya ujenzi wa Reli ya Arusha - Musoma na Bandari ya Musoma kukamilika.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Bandari ya Dar es Salaam ina vifaa vya kushushia au kupakulia makontena vyenye uwezo wa kushusha makontena 30 kwa saa lakini vinafanya kazi chini ya kiwango, yaani vinapakua makontena 15 tu kwa saa. Je ni kwa nini?

(ii) Je, uzembe huu ni lini utaisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu kwa kifupi kwani jibu lako lilikuwa ni refu mno.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tuna aina mbili ya *crane*; kuna *crane* ambayo ni SSGC ambayo inapakua mizigo kutoka kwenye meli kwenda kwenye nchi kavu, *shift to crane show gantry*, ambayo inatembea kwenye reli na inatoa mizigo mizunguko 24, yaani 24 *swings*; lakini TPA inayo *mobile cranes* ambazo matumizi yake ni mchanganyiko, yaani *multipurpose*. Kwa hiyo, ufanisi unaotolewa kwa hizi *crane* zetu za TPA unatosha, lakini tutaendelea kuuboresha.

Mheshimiwa Spika, hakuna uzembe kwani jitihada zinafanyika. (*Makofit/Kicheko*)

Na. 95

### **Kukamilika kwa Uwanja wa Ndege wa Songwe**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Serikali iliahidi kuwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Songwe ungekamilika ifikapo mwezi Mei, 2011:-

Je, mpaka sasa mpango wa kukamilika kwa Uwanja huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kweli Serikali iliahidi kwamba, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe ungekamilika ifikapo Mei, 2011. Hata hivyo, ujenzi ulikuwa bado kukamilika ilipofika tarehe hiyo kwa kuwa ujenzi wa kiwanja ulisimama kwa muda. Kusimama huko kulitokana na hali ya malighafi ya ujenzi iliyotumika kutokidhi viwango japokuwa wakati wa kuchukua *sample*, yaani sampuli na kujaribiwa kwenye maabara na Mshauri Mwelekezaji ilionesha inafaa kulingana na vigezo vya Mradi. Kwa bahati mbaya, mara baada ya Mkandarasi kutumia malighafi hiyo katika kiwanja ilionesha kuwa ni chini ya kiwango. Hali hii ilisababisha kutofautiana kati ya Mhandisi Mshauri na Mkandarasi, jambo ambalo lilipelekea kuchelewa kwa Mradi.

Mheshimiwa Spika, hali ya *sample* kuwa tofauti kutoka sehemu moja hadi nyingine ni ya kawaida katika ujenzi, kwani tabaka la udongo huweza kutofautiana katika eneo linalokaribiana.

Mheshimiwa Spika, tofauti hiyo kati ya Mhandisi Mshauri na Mkandari imetatuliwa baada ya Serikali kuingilia kati na suluhisho kupatikana. Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa miundimbonu ya kiwanja zikiwemo barabara ya kurukia na kutua ndege, yaani run way, barabara ya kiungio, yaani *taxiways*, maegesho ya ndege, yaani *apron*, barabara ya kuingilia kiwanjani, yaani *access road* na barabara za ndani, yaani *connecting roads*. Aidha, ujenzi wa jengo la abiria na majengo muhimu ya kiwanja unaendelea pamoja na mfumo wa maji safi na taka.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kiwanja cha Ncha Songwe utakamilika mwezi Desemba, 2011.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa, ninaomba kumwuliza maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) kuwa Mradi huu umechukua takriban miaka kumi sasa; ni muda mrefu sana. Pamoja na sababu ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja za kuchelewa lakini vilevile Serikali imekuwa ikichelewa sana kutoa fedha kwa wakati, jambo ambalo limesababisha Jengo la Utawala, Jengo la Wageni na *Control Tower* kutokamilika. Je, Waziri yuko tayari kutoa fedha yote iliyotengwa kwa Mradi katika Bajeti hii ya Mwaka 2011/2012 ili iweze kukamilisha Mradi huu katika muda aliopanga?

(ii) Muda wa miezi sita uliobaki kukamilisha Mradi huu ni mfupi sana, ninaomba Waziri aniambie ni lini mara ya mwisho ametembelea Mradi huu? Na kama ametembelea au hajatembelea; je, yupo tayari sasa kufuatana na mimi mwenyewe pamoja na Wabunge wengine wa Mkoa wa Mbeya twende kwenye eneo hili la Mradi tukahakikishe kama kweli Mradi huu utakamilika katika kipindi cha miezi sita?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatenga shilingi bilioni 11, fedha za ndani na shilingi bilioni tisa, fedha za nje, ambazo zitakamilisha Mradi huu na fedha hizo zimeshapangwa kwenye bajeti, tungeomba Waheshimiwa Wabunge wapitishe maombi ya makadirio ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimeshakwenda katika Uwanja wa Ndege wa Songwe na kutembelea. Ninataka kumhakikishia kwamba, tuko tayari tutakwenda tena kuutembelea na Wataalamu wetu pamoja na TAA, tumewaweka kule kuhakikisha muda wa Desemba 2011, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe unafunguliwa kuchochaea uchumi wa maendeleo wa Mkoa wa Mbeya na taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda umepita sana, ninaomba mnaposimama kuuliza maswali ya yongeza mwangalie na muda, huo ndiyo unatuongoza wote.

Mmejitahidi kidogo kuuliza maswali mafupi ya nyongeza, lakini mnawenza kufanya vizuri zaidi. Mawaziri majibu yenu yakiwa marefu usidhani wanakushangilia, wanakuzomea. Wanapogonga meza hawashangilii bali wanakuzomea, ndiyo maana ninawaambia mjibu maswali kwa kifupi halafu tuendelee na mambo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, leo kuna wageni hapa, ambao ni wanafunzi kutoka *Central High School Dodoma*, wapo wanafunzi 51 na Walimu wao, ninaomba wasimame. Ahsante sana. Someni kwa bidii, huo ndiyo urithi wenu uliobakia.

Tuna wanafunzi wengine 67 na Walimu kumi kutoka Shule ya Msingi Muningani, Wilaya ya Kondoa, ninaomba wasimame pamoja na walimu wao. Ahsanteni sana Walimu kwa kuwaleta watoto ili waweze kuona shughuli za Wabunge wao. Ahsanteni sana wanafunzi msome kwa bidii.

Matangazo ya kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi H. Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, mara baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati, ambacho kinapasa kukutana katika Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana watakuwa na Kikao Ukumbi Namba 219 Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa *CCM Caucus*, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM, leo saa saba mchana, baada ya kusitisha Bunge wakutane Ukumbi wa Pius Msekwa.

Nina tangazo la Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, anasemekana ye ye ndiye Katibu wa Wabunge wa CCM, Mkoa wa Mwanza, anawatangazia Wajumbe wake wakutane Msekwa B, saa saba mchana. Saa saba ninaona wote mnagongana huko huko mtajua wenyewe mtafanyaje.

Ofisi inatangaza kwamba, Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Maskauti, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, anapenda niwatangazie Wajumbe wa Chama hicho kuwa, leo tarehe 21 Juni, kutakuwa na kikao saa saba katika Ukumbi wa Msekwa. Sasa pale mtakwenda kugongana, lakini mtajua wenyewe namna mtakavyogongana.

Ninafikiri jana Waheshimiwa Wabunge zaidi ya kumi wamepata barua kwa *dispatch book* kuhusiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha Chang'ombe kwamba, kuwe na kikao baada ya maswali hapa, kuna kikao kidogo sana, sasa mtakutana wapi; ninafikiri mratibu atakuwa pale nje atawapeleka, mimi sijui lakini kama mmekosa pa kwa kukutana, basi mkakutane *Speaker's Board Room*. Wabunge zaidi ya kumi ambao wamepitia Chuo Kishiriki cha Chang'ombe, mtakutana baada ya maswali kwani mtakuwa na mukutano mfupi halafu mtarudi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo tunaendelea. Leo hii tutakuwa na wachangiaji wachache tu kwa kipindi cha asubuhi, kipindi cha mchana tutamwomba Waziri na Manaibu Waziri wake, waanze kujibu hoja, kwa sababu tutakuwa na kazi pia ya kuitisha bajeti hii kwa jina la Mbunge mmoja mmoja. Kwa hiyo, tutakuwa na kazi

nyingi, itabidi mchana tusiendelee na majadiliano tuingie kwenye shughuli ya kujibu hoja hizi.

Kwa hiyo, ninaomba Wabunge wote, popote mtakapokuwa saa 12 muwe mmesharudi hapa; ni vizuri pia mkasikiliza Waziri anajibu nini, maana mtakaa huko, mmechangia kwa siku tano msiposikiliza Mawaziri wanajibu nini basi tena mtakuja kuanza kuuliza maswali yale yale mliyojibiwa. Kwa hiyo, ninaomba kipindi cha mchana wote mrudi hapa muweze kumsikiliza halafu tutapiga kura. Kwa hiyo, wote mnaombwa muwepo hapa, kura yako moja ina maana kubwa sana katika upitishaji wa bajeti hii.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERÄ, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, baada ya tangazo lako hilo la shughuli ya jioni leo ninaomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni ya 150 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Nne wa Bunge unaoendelea pamoja na shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, unatakiwa kuitisha Bajeti ya Serikali kufuatana na masharti ya Kanuni ya 98, pamoja na kujadili na kuitisha Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mujibu wa Kanuni ya 106; na kwa kuwa ili kuwezesha Bunge kutekeleza shughuli hizi kikamilifu na kwa wakati huo huo kuiwezesha Serikali kuanza utekelezaji wa hatua mbalimbali zinazoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali na Muswada wa Sheria ya Fedha inabidi Bunge litengue Kanuni kadhaa za Bunge zinazotumika kwa sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1); na kwa kuwa katika Mkutano wa Wabunge wote uliofanyika tarehe 15 Juni, mwaka huu katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Wabunge wote kimsingi tulikubaliana umuhimu wa kutengua kanuni husika; hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Nne, Kanuni ya 79(2) na 106 zitenguliwe kama ifuatavyo:-

(1) Kanuni ya 79 (2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, uamuzi wa Bunge juu ya mambo yote utapatikana kwa kura za Ndiyo au Siyo, itenguliwe na badala yake utumike utaratibu wa kura ya Ndiyo au Hapana. Hata hivyo, taratibu nyingine maalum zinazohusu Bunge kuitisha au kutopitisha Bajeti ya Serikali zitabaki kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 98. (*Makofî*)

(2) Kanuni ya 106 inayoelekeza kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha utajadiliwa na kuitishwa baada ya Muswada wa Fedha za Matumizi itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao utumike: Baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kuitisha Muswada wa Fedha za Matumizi, Muswada wa Sheria ya Fedha utajadiliwa na kuitishwa kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sehemu ya Nane ya Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, ninaomba nitoe maelezo kwa sababu ninapenda watu wafuate tunachoamua na siyo waweke wanavyotaka kuelewa. Kile kifungu cha 79 tunachosema maana yake wakati mwagine kunakuwa na tatizo, mtu akisema ndiyo na mwagine akasema siyo, kama hujasikia “si” ya mwanzo unafikiri wote wamesema ndiyo, na ndiyo maana tunataka iwe hapana, hapana inajitegemea sana kuliko siyo na ndiyo. Ninadhani kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, tulikubaliana kwenye mkutano wetu tuliokuwa tunaangalia namna ya kuzielewa vizuri kanuni.

Kanuni ya 106 kama ilivyo katika Kanuni zetu hizi, ingebidi baada ya kufanya maamuzi ya Bajeti hii tungeendelea na Hotuba ya Waziri Mkuu, tungeendelea na Hotuba za Wizara moja moja mpaka hiyo tarehe 30, mwezi Agosti. Wakati huo Serikali haiwezi kukusanya kodi kwa sababu hatujapitisha Sheria ya Kodi. Kwa hiyo, miaka miwili iliyopita na mwaka huu pia tunataka tupitishe Kanuni ya 106 kabla ya Kanuni ya 107, ambayo ni *Appropriation Bill*. Hiyo *Appropriation Bill* ni kwamba, baada ya kujadili sekta moja moja, mwishoni tunasema tulichokuwa tunazungumza hapa wakati wote ni trilioni 13 kuunganisha Wizara zote, ni hilo tu wala hatujadili tunapitisha. Kwa hiyo, tunasema hilo litafanyika lakini turuhusu Serikali iendelee kufanya kazi zake na mara nyingi inaonekana kwamba, baada ya sisi kuitisha Bajeti, tunamaliza mwezi Septemba, waanze kutumia Sheria yetu ya *Finance* inakuwa tayari ni Desemba na mvua zimeanza kunyesha, miradi mingi inakosa fedha kwa sababu kipindi kile cha mvua hakuna namna. Kwa hiyo, utakuta fedha zile zinabaki mpaka tunakutana tena na mwaka huu wakati hazikutumika. Kwa kufanya hivi, tunairuhusu Serikali kuendelea na makusanyo ya kodi na Miradi yake kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ninadhani nimetoa maelezo kwa faida ya Wananchi, Waandishi wa Habari na ninyi wenyewe Wabunge tuliishazungumza huko nyuma. Sasa nitawahoji kuhusu haya maamuzi mawili.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni zilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Hapana; ni kwa bajeti tu siyo kwa maamuzi mengine. (*Kicheko*)

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante. Nitawaita Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Sylvester Mabumba, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Freeman Mboge na Mheshimiwa Habib Mnyaa. Ninafikiri nianze na hao.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwashukuru Wananchi wote wa Jimbo la Babati Vijijini, kwa kunichagua kuja kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. Ninaomba nilishukuru Bunge lako kwa kuendesha vikao kama inavyotakiwa na pia ninaishukuru Wizara ya Fedha na Waziri wa Fedha, kwa kuleta Bajeti ambayo imeleta matumaini kwa Wananchi waliokuwa wengi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii pia kutoa mtazamo wangu, wengi wetu hapa kila mmoja amechangia kwa mtazamo wake. Waliokuwa wengi baadhi yao walichangia kuwa Bajeti hii inatakiwa tuipange na Serikali ipange kutokana na vyanzo vyetu nya mapato ya ndani, lakini nitakuwa na mtazamo tofauti kidogo. Mara nyingi katika mipango tunapanga kutokana na kile ambacho tunatarajia. Ingekuwa wakulima wanapanga kama sasa hivi baadhi ya Wabunge walivyokuwa wanataka tupange kutokana na vyanzo vyetu, tusingekuwa na sisi tunapata mazao. Wakati Mkulima anapopanga kulima, ye ye hapangi kwa kutarajia kwamba, mvua haitanyesha, kwa hiyo, ninaomba hata hao wenzetu ambao wanasema tupange kutokana na vyanzo vyetu, tupange kwa matumaini, mkulima analima kwa kutarajia mvua itanyesha na hata Serikali yetu imepanga kwa kutarajia kwamba, mapato yatapatikana na hiyo misaada ambayo tunaihitaji itapatikana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishukuru Serikali kwa jitihada zake na bajeti hii nzuri ambayo ina matumaini kwa Wananchi wengi, kwa kuleta vipaumbele hasa katika Sekta ya Umeme, Maji, Barabara, Miundombinu na Kukuza Ajira na katika sekta muhimu ambayo inaa jiri 80% ya Watanzania na ambayo Watanzania wanaitegemea kwa 100%, hii ni Sekta ya Kilimo ambayo ni Sekta muhimu kuliko zote.

Ninaomba nishukuru jitihada ya Serikali katika Sekta ya Nishati, mambo ya umeme. Katika suala la umeme...

**SPIKA:** Hebu punguzeni minong'ono jamani, wanaotoka watoke lakini taratibu.

**MHE. JITU V. SONI:** Tunaishukuru Serikali kwa kuweka mikakati na mipango mizuri ili Wananchi wengi wapate umeme, lakini ningependa kutoa ushauri katika baadhi ya maeneo umeme upo, yaani nyaya zinapita, miundombinu ipo lakini *TANESCO* imeshindwa kusambaza umeme kutokana na bajeti finyu ambayo wanayo. Tungependekeza kwamba, katika maeneo hayo basi, Serikali pamoja na *TANESCO* ikubali kama kuna Wananchi au baadhi ya wawekezaji ambao wako tayari kuuvuta ule umeme kwa gharama yao na baadaye *TANESCO* iweze kuwalipa kutokana na bili. Ingefanyika katika maeneo hayo, mahali ambapo *TANESCO* haina bajeti kwa hivi sasa waweze kukopeshwa na hao Wananchi au wawekezaji ili umeme ule uwafikie watu wengi.

Kwa mfano, katika jimbo langu kuna maeneo ya Madunga, Haisamu, umeme upo transfoma zimefungwa lakini *TANESCO* imeshindwa kusambaza na Wananchi wako tayari kwa kuchangia kiasi fulani ili umeme ule uendelee kusambazwa na katika kiwanda

cha pamba ambacho kimejengwa hivi karibuni, ambapo kuna tatizo la umeme kwa muda mrefu.

Wao wapo tayari kutafuta mkopo kutoka sehemu nyingine ili TANESCO iweze kuwawekea hivyo vifaa na baadaye wakatwe katika bili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine, ninaomba *TANESCO* iangalie kwa kupitia Mfuko wa REA. Ule Mfuko ungeendelea kutengewa mafungu ya kutosha ili umeme uende vijijini. Umeme ni kichocheo cha maendeleo, mahali ambapo hakuna umeme na maendeleo basi yanakuwa yanarudi nyuma, maeneo ambapo umeme unatakiwa hasa uende ni vijijini na siyo katika maeneo ya mijini tu. Sehemu kubwa ya pesa ambayo inatengwa sasa hivi hata ukipelekwa kwa mfano katika Jimbo la Babati au majimbo mengine, unakuta ile pesa inatumika kwa kusambaza umeme pale pale mjini au katika miji midogo lakini vijijini haipelekwi.

Asilimia kubwa sasa hivi ingetakiwa ipelekwe vijijini ili ichochee maendeleo. Maeneo ambapo tunahitaji umeme katika Jimbo langu ni Mamire, Riroda, Madunga na kata nyinginezeli ili uweze kusaidia Wananchi kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali kuwa, pamoja na kuwa bajeti ni nzuri na wametenga fedha nyingi, kutoptana na vyanzo vyetu vya mapato na ile misaada tunayotegemea, lakini bado asilimia kubwa ya hizo fedha itaendelea kubaki katika miji au miji midogo, haiendi vijijini na ndiyo maana Wananchi waliokuwa wengi huko vijijini wanakimbilia katika hiyo miji midogo au miji ambapo wanakuja kupata shida kwa sababu hawana kazi na ile miji inashindwa kumudu idadi ya watu ambao wanahamia pale. (*Makofii*)

Fedha nyingi zingelenga vijijini, basi ungekuta watu wangebaki vijijini, wangeendeleza biashara zao na maendeleo yangekuwepo, wangebaki na familia zao, ndugu zao na kilimo kingeendelea kukua kwa sababu ndiyo mahali ambapo kuna watu wengi. Wengi wa wafanyakazi wanakataa kwenda kukaa huko vijijini kutoptana na hali duni ya maisha ambayo iko kule, unakuta hakuna barabara, hakuna maji, hakuna umeme na hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, sehemu kubwa ya hizi fedha ninaomba ielekezwe vijijini ili maendeleo yawe kwa usawa kwa watu wote na isibaki kuwa katika miji midogo na katika miji mikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Barabara ninaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambayo imefanya kwa kuongeza barabara za viwango vya lami na changarawe katika maeneo mengi hapa nchini. Kwa mfano, katika Majimbo ya Babati Mjini na Vijijini, barabara kutoka Minjingu – Babati – Dareda – Kateshi – Singida ni kichocheo kikubwa cha maendeleo.

Tunaipongeza Serikali kwa kazi hiyo kubwa, lakini pia tunaiomba iendelee kuangalia namna ya kusaidia barabara kupitia pale Dareda kwenda Dareda Mission katika Hospitali ya Wilaya, ambayo sasa hivi ndiyo inayotegemewa na barabara hiyo

hiyo inakutoka Dareda kwenda Mission hadi Dongobesh Haydom katika Hospitali ya Rufaa, ambayo inahudumia karibu mikoa mitatu.

Barabara ya kutoka Babati -Kiru - Kuta - Mbulu ambayo itachochea kwa sehemu kubwa maendeleo na itafanya masuala ya uchukuzi na maendeleo katika maeneo hayo kuwa na nafuu. Barabara nyingine ambazo ni muhimu kwa Wilaya ya Babati ni ambazo zinaunganisha Wilaya na Wilaya, barabara inayotoka Babati – Galapo – Mamire kuelekea kule Simanjiro na Kiteto ni barabara muhimu sana ambayo huwa inatengewa fedha ndogo sana. Tunaomba Serikali iangalie itengewe fedha kwa asilimia kubwa ili ichochee maendeleo.

Mbali na hiyo, barabara za vijijini tunaomba Serikali iangalie namna ya kuzitengea fedha za kutosha, lakini pia ikubali ushauri, kuna maeneo huko vijijini ambako tunapata shida sana kwa sababu vifaa vipo, kuna watu ambaao wana vifaa vyta kutengeneza barabara, kuna taasisi ambazo ziko tayari kujitolea, lakini *procurement system* inakataa kwamba, hivyo vifaa visitumike na *tender* inatolewa kwa watu binafsi au kwa wakandarasi ambapo kwa ile fedha kidogo ingeweza kufanya kazi kubwa zaidi. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali iangalie namna ambapo kuna vifaa watu wanajitolea mfumo uweze kubadilishwa na vile vifaa viweze kutumika ili hizo barabara za vijijini pia ziendelee kuwa katika kiwango bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sekta nyingine ambayo ni muhimu ni ya Maji. Tunaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti katika Sekta hiyo, maji ni uhai, maji ndiyo maisha. Tunaishauri Serikali mbali na hiyo iendelee kuangalia namna ya kuhakikisha kwamba, Wananchi wengi hasa wale wa vijijini, wanaendelea kupata maji bora na salama.

Kwa sasa hivi sehemu kubwa ya hii bajeti imelenga katika miji hasa wa Dar es Salaam, lakini pia ikumbukwe kwamba, katika nchi hii kuna miji mingine mingi tu pamoa na vijiji wanahitaji maji hayo hayo ambapo 80% ya Watanzania huwa wanaishi vijijini na ambaao pia wanahitaji maji yaliyo safi na salama, kwa sababu pia hudhoofisha afya zao na wao ndiyo nguvu kazi ambayo inategemewa na nchi hii.

Katika eneo la maji pia tungeishauri Serikali katika baadhi ya wilaya au mikoa, inunue zana za kuchimbia maji, kwa mfano, makatapila au *bull dozers* ili maeneo ambapo hakuna maji ya chini au mifereji au maji ya asili ya chemchemi, basi waweze kuchimbwa mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua na ili Wananchi wengi wa huko vijijini waweze kupata maji safi na salama. Kuna maeneo mengi hata maji ya chini yakichimbwa, unakuta yana madini ya *floride* ambayo hudhoofisha afya za Wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yana shida ya maji katika wilaya yetu na ambayo tunaomba Serikalia iyaangalie ni ya Tarafa ya Mbugwe, Kata ya Dabili na Kata ya Ufana, ambapo Wananchi wengi wanapoteza muda mrefu badala ya kufanya kazi ya maendeleo ya kilimo na ufugaji, wanabaki kwenda kuchota maji na wanaopata shida

kwa sehemu kubwa ni akina mama na watoto ambao ndiyo wanaofanya kazi hiyo ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sekta nyingine ambayo tunaishukuru Serikali imeiangalia ni Kilimo. Hii ndiyo Sekta ambayo inaa jiri 80% ya Watanzania, lakini 100% ndiyo wanategemea Sekta hii. Tunaishukuru Serikali kwa bajeti iliyotenga katika Sekta ya Kilimo, lakini bado tunasema ni bajeti ndogo sana. Ukilinganisha bajeti ya mwaka jana na bajeti ya mwaka huu, hiyo bajeti haijaongezeka chochote. Ukilinganisha thamani ya pesa ya mwaka jana na mwaka huu bado ni ndogo na bado ukizingatia kwamba, kitengo kile cha umwagiliaji ambacho kilikuwa kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji kimekwishaletwa katika Wizara hii ya Kilimo, lakini bajeti ambayo ilikuwepo ya umwagiliaji kule haijahama na hicho kitengo kuhamia Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, bajeti ya kilimo imeendelea kupungua badala ya kuongezeka.

Katika Sekta ya Kilimo, tunaomba kuishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia wakulima wadogo ambao ndiyo wengi, mara nyingi pesa zinazotolewa wao wakiwa kama walengwa haziwafikii. Leo hii tunaishukuru Serikali kwa mfumo mzuri wa vocha za pembejeo, lakini tunashauri kwamba, waendelee kukubali maoni yetu; kuna maeneo kwa mfano katika wilaya yangu, ambayo yana misimu tofauti, lakini yako ndani ya wilaya moja. Vocha hizo za pembejeo zingepelekwa mapema kipindi ambacho vocha zinapelekwa, sasa hivi unakuta tayari Wananchi wameshapanda mazao yao. Nyanda za Juu, kwa mfano kule Bashneti, Madunga wanapanda kuanzia mwezi wa nane na vocha kwetu zinakuja kuanzia mwezi wa tisa na pili uangaliwe utaratibu wa kuboresha hiyo *system* ya vocha na mbolea ambazo zinatolewa. Ushauri uchukuliwe kutoka kwa Wananchi wenyewe ili wajue ni aina gani ya mbolea ambayo wanataka kutumia na pia Serikali ianzishe vituo vya kupimia udongo katika kila wilaya ili Mwananchi anapotumia mbolea awe na uhakika na aina ya mbolea anayotumia na imnufaishe yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hiyo Sekta ya Kilimo kuna kodi ambazo ni kero. Kodi ambazo zipo katika zana za kilimo ambazo zingeondolewa ingemsaidia huyu mkulima mdogo mdogo wa kawaida ili na yeye aweze kuona unafuu katika maisha. Kodi ambazo zinazotozwa katika kilimo leo ni za *spear* za trekta, matairi ya trekta, trela za trekta, hata *motor vehicle licence* ambayo leo hii inalipiwa na trekta na hoja kubwa kwa upande wa Serikali inakuwa kwamba, hizo trela zinafanya kazi ya usafirishaji kwa kubeba takataka au makontena kule bandarini. Kwanza; ni aibu kabisa kwa nchi kama yetu, kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam, trekta kukutwa inabeba takataka, badala ya kufanya usafi, ninaona kwa maoni yangu, inaendelea kuchafua ule mji. Kwa nini trekta hizo ambazo hazifiki hata 50 ndani ya nchi nzima zinazofanya kazi mijini wakulima wote wahukumiwe kwa ajili ya hayo matrekta machache?

Mheshimiwa Spika, pia katika suala la majembe ya matrekta, sahani za majembe, *bearings* na vifaa mbalimbali vya umwagiliaji vyote vinatozwa kodi na ukiwaliza wataalamu wanakwambia ni *multipurposes*, wao wangetueleza kwamba, vifaa kwa mfano sahani ya jembe la trekta inakuwaje *multipurpose*.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja wa wachangiaji wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012, asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda nikupongeze wewe mwenyewe Spika na timu yako ya Wenyeviti, kwa jambo moja muhimu na kubwa kabisa ambalo limefanyika au limetokea la kubadilisha hali ya hewa hapa Bungeni kwenye mijadala. Katika siku mbili zilizopita, nimeshuhudia utulivu na watu wakizingatia zaidi hoja kuliko malumbano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa ujumla kwa bajeti yake hii ambayo nimeipitia binafsi kwa kina na vina na nimeridhika kabisa kwamba, Bajeti hii ni ya Ukombozi, kwa sababu misingi yake imetokana kwanza na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambao tumeupitisha juzi. Kama hiyo haitoshi, wakati wa kuchagua vipaumbele, Bajeti imezingatia maeneo au sekta ambazo nikizitaja kwa haraka haraka mchango wake kwenye Pato la Taifa kwa mwaka 2010 ilikuwa asilimia 70.6, haya yalikuwa ni maeneo ya uchukuzi, ujenzi, umeme na gesi, kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bajeti kuzingatia Pato la Taifa na kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano; ni dhahiri kabisa kwamba, Bajeti hii pamoja na michango ambayo inatolewa na Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kuiboresha hatimaye bajeti hii ikitekelezwa vizuri basi tutaweza kufika kule tunakotarajia. Wakati tunazungumzia juu ya suala la Serikali kutekeleza Bajeti ni vyema tukakumbushana kwamba, sisi Wananchi wenyewe nao pia tuna sehemu kubwa kabisa ya kushiriki kikamilifu ili kuweza kuhakikisha kwamba, Serikali inafanikiwa katika utekelezaji wa bajeti hii. Ule msemo wa “*Yes we can*” siyo maneno tu peke yake, ingawa baadhi ya wachangiaji waliona kama huu ni msemo ambao umenukuliwa kutoka mahali pengine kule Marekani, lakini ningependa kuwakumbusha tu kama wanaona tabu kutumia “*Yes we can*” watumie usemi wa Mwalimu Nyerere; “*It can be done play your part*” au “Inawezekana timiza wajibu wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Sekta zote ambazo zimehusishwa kwenye Mpango wa Maendeleo na zikaingia kwenye Bajeti ni dhahiri kabisa suala la wataalamu katika Sekta zote hizo na hasa upande wa sayansi na teknolojia linajitokeza wazi. Bila wataalamu, hakuna uwezekano wa kuweza kupata mafanikio kwenye utekelezaji wa Bajeti hii. Tunahitaji idadi ya wataalamu wa kutosha kwa maana ya kutosha kwa idadi, lakini kutosha kwa umahiri, yaani waweze kuwa mahiri kwenye fani zao katika ngazi zote. Muhimu pia ni suala la maadili kwamba, maadili ya taaluma kwa wataalamu ni suala ambalo lina umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la uwiano, ninazungumzia juu ya suala la uwepo wa wataalamu katika ngazi zote. Tukitoa mfano rahisi niseme kwamba, Daktari wa ngazi ya juu ambaye ana shahada katika utendaji wa kazi zake, hawezi kufanya kazi bila ya kuhitaji, kwa mfano, *Laboratory Technician* au Mtaalamu wa Maabara. Upande wa Uhandisi vilevile Mhandishi mwenye shahada ya elimu ya juu, hawezi kufanya kazi peke yake bila kuwepo *technician* na wataalamu wa ngazi ya chini, yaani *artisans*. Kwa

hiyo, idadi, uwiano na umahiri ni masuala muhimu sana kuhakikisha kwamba, tunaweza kuwa na wataalamu wa kutosha. Dhana hii inatokana pia na ukweli kwamba, wakati wa utekelezaji wa Miradi, maana yale maeneo tuliyo chagua yote yana Miradi mikubwa ambayo yatatumia fedha nyingi sana katika utekelezaji wake, bila kuhakikisha kwamba, tuna *base* ya kutosha ya wataalamu wa ndani hata utekelezaji wenyewe wa Miradi utafanya fedha zitakazotumika nyingi ziweze kwenda nje kama wataalamu watakaotumika ni wataalamu wa kutoka nje. Kwa hiyo tujiimarishe zaidi katika kuhakikisha kwamba, tunajenga *base* ya wataalamu watakaotosha kwa idadi na umahiri kama nilivyosema, lakini pia kwa uwiano unaostahili.

Eneo moja kubwa ambalo limeachwa na ninafikiri nitoe ushauri na kusisitiza ni kwamba, lazima tuimarishe wataalamu wa ngazi ya kati, kada ambazo ni za taaluma ya *Diploma* na *Certificates*. Moja kwa moja hapa nitatoa maoni kwamba, hata kwenye kutenga bajeti ya mafunzo; tulivytenga bajeti ya mafunzo au ya uwezeshaji ile asilimia sita iliyotokana na *development skills levy* tulisema asilimia mbili iendelee kubaki kwenye ngazi ya chini kabisa, ngazi ya kati ikawa imeachwa na asilimia nne inapendekezwa kwenda elimu ya juu kwenye ngazi za shahada.

Mheshimiwa Spika, nitoe ushauri kwa Serikali tuweze kufanya marekebisho kidogo ili asilimia tatu ibaki elimu ya juu kwa ajili ya ku-*address* tatio la upatikanaji wa fedha kwa Bodi ya Mikopo, asilimia moja iende kwenye mafunzo ya elimu ya kati iweze kwenda ku-*support* kada ya kati kwa ajili ya umuhimu nilioutaja kwamba, hapo ndiyo wataalamu wataweza kufanya kazi zao sawa sawa, wakati asilimia mbili ikibaki kule chini kwa wale *artisans*. Tuwe na wataalamu wetu wa kutosha na mahiri ili ushiriki na utekelezaji uweze kusababisha fedha ziweze kubaki hapa ndani, lakini pia kuweza kufanya hilo soko lisitekwe na wageni. Tumeingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wakenya wanakuja kwa *speed* kubwa na wao kwenye kada hii ya kati ya *technicians* wako mbali na wanao wengi wa kutosha tusipoangalia watakuja hapa na watachukua kila kitu wataacha sisi tukibaki watupu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia *technology transfer*; teknolojia itaweza kubaki hapa kwa kuwa ule ushiriki mdogo wa wale wataalamu wa nje utaweza kuwafanya wataalamu wa ndani waweze kubaki na ujuzi fulani. Pia ni kwa sababu ya uendelevu kwamba, baadaye Miradi hii utekelezaji wake unakuwa na kipindi cha matengenezo au *maintenance period*, tusipobaki na wataalamu wetu wenyewe miundombinu itakayokuwa imetengenezwa pale itakosa watu wa kuweza kuisimamia. Kuhusiana na suala la wataalamu vilevile, ninapenda nitoe tafsiri hapa ya kada ya kati jinsi ilivyo, siyo tu kwenye Sekta ya Uhandisi peke yake wataalamu katika fani za afya, kilimo na mifugo, kote huku kuna vipaumbele katika Bajeti hii. Pia kwenye Mpango wa Maendeleo hali huko ni mbaya sana na inahitaji *intervention* ya kuweza kupanga bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo, vyuo vyua kati kwa ujumla kwa taarifa kutoka Baraza la Taifa la Ufundu, tunavyo vyuo 245 ambavyo kwa ujumla wake vinafanya vyuo 30 peke yake ndiyo vinavyojihusisha na sayansi na teknolojia. Kwa usahihi zaidi vyuo sita peke yake ndiyo vinafundisha *engineering technicians* ambao ni muhimu sana katika utekelezaji Miradi hii ambayo tumeitaja hapa. Umuhimu hapa

unajitokeza wazi kabisa kwamba, tunatakiwa ku-boost medium au middle level cadre ili iweze kutusaidia katika maendeleo ya Taifa letu ambayo yatakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo kuhusu Miradi inayotekelzwa upande wa Ukanda wa Kusini au *Mtwara Corridor*:

Sina matatizo juu ya barabara kwa sababu hili tumeshasema kwamba, tunaendelea nalo vizuri, isipokuwa kipande kimoja tu cha Mangaka kwenda Tunduru, ambacho tume sema kwamba, ile *preliminary design* pamoja na *feasibility study*, ziongezewe kasi ili tuweze kuona pia kipande kile kinakamilika kwa ujenzi wa barabara kiwango cha lami. Juu ya suala la reli ya kutoka Mtwara kwenda Mchuchuma hadi Liganga ni muhimu sana Mradi huu nao ukatengewa fedha kwa wakati mwafaka ili utekelezaji uweze kuwa wa manufaa hasa katika kuakikisha kwamba ile barabara inaweza ikalindwa ili iweze kudumu. Kwa *experience* tulioiona mahali pengine, barabara peke yake ikiwa *over-loaded* na shehena za mizigo na uzito ukawa mkubwa kiasi kile, barabara zile zinakuwa hazidumu. Sisi tungependa barabara hii ya Mtwara – Masasi – Mangaka – Tunduru – Songea mpaka Mbambabay, idumu na msaada mkubwa utakuwa ni wa hii reli ambayo itatakiwa iwe imekamilika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa *ku-design* ile reli ni maombi yangu kwamba, waangalie *route design*, hiyo reli itakapopita isipite mbali sana na Mji wa Tunduru, kwa sababu kwa kupita jirani kwanza tutafupisha umbali kutoka Tunduru Mjini kwenda kwenye kituo cha karibu cha reli na kwa hiyo hatatalazimika tena kutenga bajeti kubwa ya barabara ya lami, ambayo itawenza kutuwezesha kutumia barabara hiyo kwa ukamilifu. Upande wa umeme nilikwishasema na ninataka nirudie tena kwamba, wakati Kigoma walikuwa wanasema Wilaya imeanzishwa mwaka 1920, Wilaya ya Tunduru ilianzishwa mwaka 1905. Sisi pia bado hatuna umeme wa uhakika, bado tunatumia jenereta ni maombi yangu kwamba, Serikali ichukulie kwa uzito wake kwamba, Gridi ya Taifa inapita mpaka inafika karibu na sisi lakini baadaye inaturuka inakwenda upande mwingine; sasa ni wakati mwafaka kufikiria juu ya Tunduru vilevile.

Mheshimiwa Spika, upande wa madini, ninapenda kuungana na wachangiaji wengine waliosisitiza juu ya suala la kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo na ningependa wachimbaji wa Ng'apa, Muhuvesi na maeneo kama hayo, waweze kunufaika kwa ukamilifu, waweze kufanyiwa uboreshaji wa shughuli zao za utafutaji, uchimbaji na uchanjuaji wa madini pamoja na biashara yenyewe ya madini. Suala la utaalamu kwa Kusini, tatizo kubwa zaidi ni *geographical location*. Niungane na wale waliosema kwamba, sasa tunahitaji upendeleo maalum kwa maeneo ambayo yanafikika kwa ugumu. Ninao mfano mmoja rahisi wa kwamba, ukitangaza kazi wengine wanakwepa kwenda kwenye maeneo Fulani, Tunduru ikiwa ni mojawapo. Sasa suluhisho mojawapo ni lile la kuwapa mamlaka au kuzipa mamlaka Halmashauri zinazohusika kutangaza kazi hizo, kwa sababu kuna uwezekano Wananchi wenyewe taaluma na sifa hizo wakawa wapo kwenye maeneo hayo hayo. Ninao mfano kabisa hapa wa Mhandisi ambaye ni mhitimu wa shahada, ambaye analazimika kurudi kwenye kazi yake ya awali ya ualimu kwa sababu nafasi ya kuajiriwa kama Mhandisi haijapatikana, lakini wakati Wilaya ina *serious shortage* ya Wahandisi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nishiriki kutoa mawazo yangu katika hoja hii inayoendelea ya Bajeti ya Mwaka 2011/2012. Awali ya yote, ninapenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ninaunga mkono kutokana na sababu zifuatazo; kwanza, vipaumbele ambavyo bajeti yetu imeainisha imelenga katika kutatua shida na kero zinazowakabili Wananchi wetu hapa Tanzania. Nitaanza na kipaumbele cha umeme.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la nishati, ninaipongeza Serikali kuona umuhimu wa kuwa na nishati ya uhakika kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi hapa Tanzania. Nishati ya uhakika itasaidia maendeleo ya kijamii, mfano, tunaamini kila nyanja ya maisha yetu tunahitaji nishati majumbani, viwandani, hotelini na sehemu zinginezo. Wakati wa shida ya umeme, Wananchi wetu hupata usumbufu mkubwa; kwa mfano, kukatika kwa umeme kwa muda mrefu kuliwasumbua sana wafanyakazi viwandani. Ninaamini matajiri walipunguza wafanyakazi kwa sababu ilikuwa ni mzigo kuendelea na watu ambaa hawazalishi. Hata hoteli zilipunguza wafanyakazi, kwa sababu ilikuwa vigumu kuendelea nao kwa kuwa walikuwa hawaleti tija. Kwa hiyo, ninaipongeza Serikali kuainisha nishati kama moja ya vipaumbele vyake katika bajeti yetu hii. Ninaomba Serikali ihakikishe baada ya Bunge lako Tukufu kuidhinisha Bajeti hii leo, itekeleze kwa vitendo nia yake hii ili watu wetu wapunguziwe usumbufu wa maisha unaotokana na shida ya nishati.

Mheshimiwa Spika, pili, ninapenda kuongelea kipaumbele cha kilimo na umwagiliaji. Sekta ya Kilimo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Asilimia kubwa ya Wananchi wetu wanategemea kilimo kuendesha maisha yao. Kilimo ndiyo hutoa ajira na sasa tunapotilia mkazo Kilimo Kwanza, ninaomba Serikali ihakikishe kwamba, tamko hili la Kilimo Kwanza linatekelezwa kwa vitendo. Kilimo Kwanza kitapanua wigo wa ajira kwa Wananchi wetu, tutaongeza uzalishaji kwa vile sisi tunategemea kilimo kusafirisha mazao yetu sehemu mbalimbali kupata fedha za kigeni, basi ni muhimu sana kuhakikisha Sera ya Kilimo Kwanza tunaitekeleza kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Mwaka 2010 iliyotolewa na Wizara ya Fedha, nchi yetu urari wa kibiashara na washirika mbalimbali una nakisi kubwa. Ukiangalia biashara kati ya Tanzania na Ulaya, unakuta kuna nakisi ya Dola milioni 318.7. Pia biashara baina ya Tanzania na SADC ina nakisi ya Dola milioni 202.6, hali hii siyo nzuri sana maana tunaagiza zaidi kutoka maeneo hayo kuliko tunavyoweza sisi kuuza katika kanda hizo na tunakuwa waagizaji wakubwa siyo wauzaji. Kwa vile tunakuwa siku zote hatunufaiki na tunapotaka nchi yetu iwe nchi ya kipato cha kati, haiwezekani kwa nchi ambayo haiwezi kuuza nje na kuweza kuongeza mapato yake. Mapato machache tunayoyapata tunayatumia kuagiza bidhaa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana tukazie katika tamko hili la Kilimo Kwanza. Tunahitaji huduma ya utafiti katika Sekta ya Kilimo itiliwe mkazo kuweza kutafiti na kubaini aina gani ya mbegu mazao yaweze kuzalishwa katika kila Kanda ya nchi yetu.

Pia utafiti utiliwe mkazo kutafiti maradhi yanayosumbua mazao ambayo Wananchi wetu wanalima, niiombe Serikali kwamba, kutokana na hali ya ukame ambao mara nyingi Wananchi wetu wanapata, lakini pia maradhi ambayo wanapata mazao yetu Serikali iweke fungu maalum kwa ajili ya kufidia wakulima ili kuwatia moyo na kuwaongezea ari ya kushiriki zaidi katika uzalishaji. Ninapenda niishauri Serikali kwamba, katika kilimo ni pamoja na uvuvi, maeneo yote ambayo yanahuksika na uvuvi basi Serikali ihakikishe inawapatia wavuvi zana za kisasa ili kuhakikisha kwamba Sekta ya Uvvi inakuwa moja ya mhimili unaochangia kupanua wigo wa ajira, lakini pia kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la miundombinu. Ninaipoongeza Serikali kuainisha miundombinu kuwa ni moja ya vipaumbele vyake. Kwa vile miundombinu ni eneo pana sana, tuna masuala ya reli, barabara, bandari na mengineyo; sasa tuangalie yale ambayo tunaweza kuyatekeleza katika bajeti yetu hii ndogo, tusichukue mambo yote wakati bajeti yetu haitoshelezi, tufanye jambo moja tulifakishe mwisho tuone litachangia vipi maendeleo ya nchi yetu. Tunaamini tukifufua reli yetu tutanufaika sana, kwa sababu tutaweza kusafirisha mizigo ya nchi jirani, ambazo hazina bahati ya kuwa na bandari.

Kwa kufanya hivyo, nchi yetu itaweza pia kuongeza mapato yake ya ndani na hivyo kuweza kupata nguvu zaidi ya kutoa huduma bora kwa Wananchi wetu. Serikali inategemea kodi ili kuweza kutoa huduma kwa Wananchi wake. Pasipo kodi za uhakika, haiwezi kutoa huduma kwa Wananchi. Ninaomba miundombinu ambayo Serikali itakuwa imedhamiria kuifufua basi iifufue ili iweze kuhudumia maendeleo ya nchi yetu. Tunaamini barabara ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Vita Kawawa, alielezea hapa kwamba, ukanda wa maeneo yao kuna chakula cha kutosha. Tukumbuke Mheshimiwa Stephen Masselle, Mbunge wa Shinyanga Mjini, alisema Wananchi wa Shinyanga, sasa hivi wanateseka sana, chakula ni haba, wanapewa kilo kumi kwa kaya; huku ni kutaka kuua Wananchi wetu. Kama kuna chakula cha kutosha kule Kusini, ninaishauri Serikali ikisafirishe kuwafikia Wananchi wa Kanda ya Shinyanga na kwingineko, ambako Wananchi wana uhaba wa chakula. Katika eneo la miundombinu, baadhi ya wachangiaji hapa walisema kwamba, kama tutashindwa kutumia fursa hii ya kijiografia, Mataifa ambayo hayana bandari sasa hivi, yanaanza kuelekea sehemu nyinginezeli yaachane na Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na pia kule Mtwara.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali tusipoteze fursa hii kuacha kufufua reli yetu na pia kuacha ku-*improve* huduma ya bandari ya Dar es Salaam, maana yake tunataka kujiua wenyewe. Zambia, Rwanda Burundi, Uganda na DRC wakiacha kufanya biashara na sisi maana yake uchumi wetu utadorora kwa vyovoyote vile.

Kwa hiyo, naishauri Serikali, mandhari yote haya tunayajua, basi tufanye kazi kuhakikisha kwamba fursa hii tunaitumia ipasavyo. Naomba nizingumzie pia eneo la ajira kama kipaumbele kilichoainishwa na Serikali. Naipongeza Serikali kuona hili kama ni kero inayosumbua watu wetu hasa vijana. Naomba Serikali ijipange vizuri kuhakikisha kwamba tunapanua ajira kwa manufaa ya vijana wetu. Ili tuweze kupanua ajira, nashauri Serikali pengine tuangalie na kufanya mapitio kwenye mitaala ya elimu, iweze kutayarisha vijana, sio kwa ajili ya kuajiriwa maofisini, iandae vijana kwa ajili ya kuajiri wenyewe wamalizapo masomo yao. Lakini ili hili lifanikiwe, haiwezekani anayetoka shuleni leo aweze kuajiri. Tunaomba pawepo na mifuko ya kuwapatia mikopo nafuu isiyokuwa na masharti ili ile azma ya kuwawezesha kuajiri iweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la rushwa. Rushwa ni adui wa haki. Katika Chama cha Mapinduzi tunasema, sitatoa wala kupokea rushwa. Naomba nia hii ya Chama cha Mapinduzi tuizingatie kwa vitendo, tupinge rushwa kwa nguvu zote. Nashawishika kusema kwamba pengine TAKUKURU imeshindwa kufanya kazi. Kama imeshindwa, nashauri na Idara ya Usalama wa Taifa idhibiti suala la rushwa. Idara ya Usalama wa Taifa imefanya kazi nzuri, ndiyo maana leo nchi yetu ina amani, imeweza kugundua njama zile ambazo haziitakii mazuri nchi yetu. Kwa hiyo, nashauri TAKUKURU na Usalama wa Taifa washirikiane. Kwanza, wanaojiriwa katika TAKUKURU wafanyiwe *vetting* na Idara ya Usalama wa Taifa kuangalia uadilifu wao. Usalama wa Taifa watatusaidia kuajiri watu ambao wana uzalendo katika Idara hii ya TAKUKURU, vinginevyo tutapiga kelele kila siku hapa kwamba rushwa inaendelea, mafisadi wanaendelea; kwanini waendelee wakati Serikali imeunda Idara hii na kuifanyia maboresho? Nina wasiwasi sana na TAKUKURU. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie suala la mfumko wa bei. Naipongeza Serikali kwa uamuvi wa kudhibiti masuala ya bei. Tukiachia, tunaona majirani zetu wamepata misukosuko mingi kwa sababu wananchi wamepiga kelele kuhusu shida za maisha kutokana na mfumko wa bei ambao wameshindwa kuimudu. Afrika Kaskazini imeingiwa na machafuko kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kuamua kwa dhati kabisa kwamba itadhibiti Mfumko wa bei ili kupunguza kero za maisha kwa watu wetu. Naomba itekeleze masuala haya kwa vitendo na sio kwa maneno. Leo hii tutapitisha bajeti hii, ichochee na kuitia moyo Serikali yetu na kuhakikisha kwamba haya ambayo imetuletea mbele yetu inayatekeleza kwa vitendo, kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia pia kuhusu uamuvi wa Serikali kudhibiti matumizi. Tunaomba Serikali ihakikishe kwamba fedha ambazo zinaidhinishwa hapa zinatumika kwa malengo ambayo yanakusudiwa. Tukiwa na matumizi ambayo hayaeleweki, hatuwezi kufikia lengo ambalo tunalikusudia. Tunaomba matumizi ya Serikali yaeleweke. Pale ambapo Maofisa wanaohusika, Makatibu Wakuu na zile Idara ambazo zinajitegemea wameshindwa kutekeleza maagizo ya Serikali, basi wawajibike. Naomba tuanze na utamaduni pale ambapo mtu anahisi hawezu ku-deliver asisubiri kuambiwa ondoka, aondoke kwa hiari yake, atalinda heshima yake. Lakini kama atawajibishwa na mamlaka iliyomteua itakuwa ni aibu kwake na aibu kwa Taifa pia.

Kama sisi tuna imani naye, Mheshimiwa Rais amemteua kwa mapenzi, basi atimize matarajio ya Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mawazo yangu katika Bajeti ya Serikali. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Kambi ya Upinzani na wachangiaji wake wote kwa kuja na hotuba mbadala ambayo ina mambo ya msingi ambayo kama yakizingatiwa, basi yataleta mchango mkubwa katika kuboresha hali ngumu ya maisha yanayowakabili Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na suala la umaskini uliokithiri mionganoni mwa jamii zetu. Mimi natoka Mkoa wa Singida, ni kati ya Mikoa ambayo kama takwimu ziko sahihi, bila shaka ni wa kwanza kwa umaskini katika Mikoa yote. Naomba pia niungane na mchangiaji wa jana Mheshimiwa Mbunge wa Kisarawe aliyekuwa akiongelea suala la Mikoa maskini ambayo iko nyuma kimaendeleo, kwamba sasa imefika wakati kwa Serikali kutoa kipaumbele kwa Mikoa hii, iwekwe mikakati ya makusudi ili kuweza kupunguza pengo kubwa la umaskini kati ya Mikoa na Mikoa. Kwa hiyo, naomba Mkoa wa Singida, Serikali iuangalie kwa namna ya pekee tunapozungumzia suala la umaskini Mkoa wa Singida nao uangaliwe kwa namna ambavyo utaweza kukwamuliwa kuondokana na hiyo orodha ya Mikoa maskini kabisa. Lakini sio tu kwamba tunaomba huruma, lakini kuna fursa ambazo zinapatikana katika Mkoa wa Singida. Mimi naomba niongelee machache.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida unazalisha alizeti. Sasa hivi tunajua kwamba watu wanaojali afya zao, wanapenda kula mafuta ya alizeti na ukiongelea mafuta ya alizeti, basi yale yaliyo bora kabisa yanatoka Mkoa wa Singida. Pamoja na fursa hiyo ambayo tunaweza tukaitumia ili kuinua hali ya maisha ya wananchi wa Singida, alizeti hii bado inalimwa katika kiwango duni kwa kutumia zana duni na kwa hiyo kama hali hii ikiachwa iendelee jinsi ilivyo, bado haitaweza kuwanufaisha wananchi wa Mkoa huo. Naiomba Serikali kutumia kauli mbiu yake ya Kilimo Kwanza ambacho kwa kweli katika Mkoa wetu wala hakionekani, ifanye jitihada ya kuongeza au kuboresha uzalishaji wa zao la alizeti katika Mkoa wa Singida. Naiomba Wizara ya Viwanda na Biashara isaidie wananchi kusindika ili kupata mafuta ambayo kwa kweli yana bei nzuri katika soko la ndani na kwa hiyo, wananchi wanaweza kufaidika kwa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Singida kuna asali, hivi leo ukipita baada ya Manyoni, katika vijiji vya Isuna, Nkuhi, Mkiwa, mnaona wananchi wanauza asali kwenye chupa, ili kuongeza zao la asali, sidhani kama inahitaji gharama kubwa sana na hasa fedha za kigeni. Naiomba Serikali ifanye jitihada za makusudi kuwasaidia wananchi wa vijiji hivyo juu ya ufugaji bora wa nyuki ili waweze kuzalisha asali vya kutosha ili waweze kuuza katika soko la ndani hata soko la nje kwa sababu asali ina bei kubwa katika soko la ndani na la nje. Hizo ni fursa chache ambazo zinapatikana katika Mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna madini. Mimi napata shaka, ninapoongea Singida kuna hivi vitu na madini pia yapo, lakini bado ni Mkao wa kwanza kwa umaskini. Kuna mgodi wa madini wa dhahabu kule Sambaru, Londoni, lakini sielewi vijiji vinavyozunguka Londoni vinafaidikaje na dhahabu iliyopatikana hapo.

Kuna misururu na misafara mingi ya wachimbaji kutoka sehemu mbalimbali za nchi na nje ya nchi wamevamia eneo hilo kwa ajili ya uchimbaji wa dhahabu, lakini sijui kama wananchi wa Mkao wa Singida hususan wa maeneo ya Mang'onyi, Sambaru, Londoni kwenyewe wananaufaikaje na dhahabu inayochimbwa katika eneo lao?

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa la maji, Wilaya ya Singida Vijijini. Naiomba Serikali katika miradi yake ya maendeleo ya kupeleka maji safi vijijini, basi wahakikishe kwamba wanatatua tatizo la maji kwa kuchimba visima virefu. Mkao wetu ni mkame kama mnavyojua lakini tukichimbiwa visima virefu, basi tunaweza tukapunguza tatizo la maji ambalo linatukabili.

Mheshimiwa Spika, nikitoka katika Mkao wangu wa Singida, nitupie macho kidogo Bajeti ya Serikali kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mfumko wa bei unachangia kwa kiasi kikubwa na bei kubwa ya mafuta. Wachangiaji wengi wameshaongea kuhusu bei ya mafuta. Labda nitarudia, lakini nami sina budi kusema naona nini katika bei ya mafuta. Kuna tozo nyingi katika bei ya mafuta na bahati mbaya matozo haya yanafanywa na Taasisi za Serikali ambazo wala hazijiendeshi kibashara kwa sababu mwisho wa siku zinapata bajeti yake ya mwaka kutoka Wizara zao mama.

Mheshimiwa Spika, kuna tozo zaidi ya kumi ndani ya lita hiyo hiyo moja ya mafuta ambayo Mtanzania wa mwisho au mnunuzi wa mwisho ndiyo anailipia. Kuna kitu kinaitwa *destination inspection fee* ya *1.2% of FOB*, hii inatozwa na *TRA*. Lakini japokuwa *TRA* inatoza *destination inspection fee*, *TRA* wenyeve hawafanyi hiyo *inspection*, lakini wamekuwa wakitoza hiyo tozo. Sasa mimi sisemi tu ipunguzwe, nasema iondolewe kwa sababu inatozwa isivyo. *TRA* wanatoza tozo ambayo hawaifanyii kazi. Kuna tozo nyingine ambazo zinatozwa na Mashirika mengine kama *EWURA* na tunaambiya katika *total collection of EWURA*, *TRA* wanachukua *10%*. Sasa hizi ni tozo ambazo *TRA* hazijaoneshwa katika mapato ya Serikali katika bei ya mafuta. Kwa hiyo, kama *TRA* na wao wanachukua *10% of the total EWURA collection* na yenyewe naona siyo sawa kama ni halali, basi iwe *declared* ionekane kwamba katika kodi za Serikali zile mbili zilizooneshwa, basi kuna *10% ambayo inatoka EWURA na kwenda TRA*.

Mheshimiwa Spika, kuna *ocean loss*. *Ocean loss* ya *0.5% of CIF*. Sasa hapa ndiyo nashangaa, kwanini *ocean loss* iingizwe katika bei ya mafuta? Kwanini mnunuaji wa mwisho alipie *ocean loss* kwa sababu ile imetokea wakati mafuta yako safarini wakati yanaletwa nchini. Hivi ni kwanini iwekwe katika bei ya mnunuzi wa mwisho? Hii ni tozo ambayo naona inapaswa nayo kufutwa. Lakini kana kwamba haitoshi, hizi tozo zinatozwa kwa dola ya Marekani na kuna *costs* nyingine za kuweka vinasaba katika mafuta. Haya mafuta yameshafika nchini, lakini tozo hii inatozwa kwa dola ya Marekani kwa sababu ya kuporomoka kwa thamani ya shilingi yetu, tozo hizi zinapokuwa kwa

fedha ya kigeni zinafanya bei inakuwa ya juu sana. Sasa sioni uhalali ni kwanini tozo hizi zitozwe kwa dola ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, lakini tozo hizi kwa ujumla wake tunajua kwamba zinachangia kwa asilimia 2.6 katika bei ya mafuta. Sasa Serikali imesema itazipitia, sasa wakizipitia naamini kabisa hazitaweza kuleta punguzo la bei ambalo litampa nafuu Mtanzania. Imefika wakati sasa ile *excise duty* yenyewe iangaliwe nayo. Serikali inapata mapato yake kupitia *excise duty* kwenye mafuta ya Sh. 339/= kwa lita.

Sasa wananchi kama hali imekuwa ngumu kiasi hiki, imefika wakati muafaka Serikali ipunguze hiyo *excise duty* kwenye mafuta na kama *ita-affect* mapato ya Serikali, basi ni bora vyanzo vingine vya mapato viangaliwe kuliko kuendelea kuchukua kwa walaji wa mafuta au watumiaji wa mafuta ambao kwa kweli kwa sasa hivi wanashindwa kumudu gharama kubwa ya maisha kutokana na bei ya mafuta ilivyo juu. *Excise duty* na yenyewe iangaliwe, ipunguzwe kwa sababu hiyo ni kubwa na italeta *impact* ya kutosha katika bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka kwenye suala la mafuta na mfumko wa bei naomba niongelee pia *fine* ya makosa ya barabarani kama ilivyoletwa katika Bajeti ya Serikali. Kipindi kilichopita, *fine* za makosa ya barabani ilikuwa Sh. 20,000/= kwa kosa. Lakini safari hii akisoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alisema kwamba itaongezeka kutoka Sh. 20,000/= kwenda 50,000/=, lakini katika kitabu chake cha hotuba ilikuwa imeandikwa laki tatu. Sasa hapo kuna utata, sielewi kama itapanda kutoka Sh. 20,000/= kwenda Sh. 50,000/= au kutoka Sh. 20,000/= kwenda laki tatu. Lakini hata nikichukulia hiyo ya kupanda kutoka Sh. 20,000/= kwenda Sh. 50,000/=, bado nina shaka. Bado *fine* hii ni kubwa ukizingatia kwamba wanaofanya makosa barabarani ni Watanzania ambao pia ni wa vipato vidogo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na dhana nzima ya usalama barabarani. (*Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mawazo yangu ama mchango wangu kuhusiana na bajeti ambayo tunaelekeea kwenda kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, nitaomba nijielekeze kwenye eneo moja tu la msingi na nitaomba Waheshimiwa Wabunge wanielewe kwa sababu nazungumza kwa nia njema kabisa. Kuna jambo ambalo limezia mvutano ambao naweza kusema ni mvutano ambao ni wa msingi kwa sababu ya makusudio ya hoja yenyewe, kuhusiana na suala la posho. Mimi kama Mwenyekiti na Mbunge, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, napenda kuweka msimamo vizuri ili tueleweke tunazungumzia nini na Wabunge wapime kwa uzito wake na sio kwa uzito wa rangi ya bendera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima kama viongozi tujifunze kuwa viongozi na kufanya maamuzi magumu. Tunapokuwa tunafanya maamuzi magumu kuhusu Taifa, tuwe tayari kuwa *victim number one*, na kama tutashindwa kufanya maamuzi magumu kwa sababu tumeshindwa kutafuta utashi wa kisiasa wa kutafuta suluhisho, tutakuwa hatulitendei haki Taifa la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua uzito wa gharama katika Taifa na uzito wa gharama hizi za maisha haziko kwa Wabunge peke yake, hazipo kwa Watumishi wa Umma peke yake, zipo kwa Watanzania wote. Tutafute suluhisho gani hapa?

Mheshimiwa Spika, tumejadili suala la posho za Watumishi wa Umma, kwa bahati mbaya sana tafsiri ambayo imekuwa inapewa uzito kwenye vyombo vyahabari, inazungumzia posho za Wabunge, Wabunge ni sehemu ndogo sana katika kada nzima ya Utumishi wa Umma katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, *let us face it*, tunachoongea ni nini? Wengine wamepotosha wakasema CHADEMA wanakusudia pengine kufuta posho zote za Wabunge, hapana! Haujawa msimamo wetu na hautakuwa msimamo wetu. Wengine wakaenda hatua nyininge wakisema mbona wao wenyewe wanachukua posho hizo, hoja ya msingi siyo uchukuaji wa posho, hoja ya msingi ni ubadilishaji wa sera inayoruhusu posho hizi. Sisi tunesema kitu kimoja, Wabunge ni sehemu ndogo sana ya Watumishi wa Umma, na tunapofanya maamuzi kwa kuangalia maslahi ya kundi ndogo la Wabunge 350 tulipo ndani humu, tunahalalisha mambo hayo hayo kufanya na maelfu ya Watumishi wengine wa Umma katika kada ya Menejimenti kuweka viwango vikubwa vya posho ya vikao ambayo tungeweza kuiepuka.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hoja kwamba, mishahara ni midogo, hiyo ni jambo lingine, mishahara siyo midogo kwa Wabunge, mishahara ni midogo kwa kada nzima ya Utumishi wa Umma katika Taifa hili, na kama ni *ku-review* mishahara hilo ni jambo la msingi ninalolizungumza, tufanye mambo yetu kwa uwazi na uadilifu bila kufanya kwa vificho.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya nchi nzima ziko 133. Unakwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya, unakuta Wakuu wa Idara, wako kwenye Kikao cha UKIMWI, kwamba mpaka leo Wakuu wa Idara wako kwenye Semina ya UKIMWI ya kuwaeleza namna ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI. Sasa lile fungu linalopelekwa la UKIMWI Wilayani linatumika kwenye Vikao vya Wakuu wa Idara, wanafundisha athari na namna ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI. Kama leo kuna Kiongozi ambaye amefika ngazi ya kuwa kiongozi na hajui madhara ya UKIMWI, hastahili kuwa kiongozi. Matokeo yake Jumatatu tuna Semina ya UKIMWI, Jumanne tuna Semina ya Mazingira, Jumatano tuna Semina ya Ajira, Watumishi wa Umma wanapoteza muda mrefu wa kufanya kazi, ile *man power* haiheshimiwi tena, kwa sababu watu wanazunguka kwenye vikao kusaka posho. Hatuwezi kujenga Taifa la Posho, tutaweza kujenga Taifa lenye uwajibikaji na *productivity*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote tunasimama ndani humu tunakiri nchi hii maskini, wote tunalalamika umaskini humu ndani, tunalalamika umaskini lakini tunaishi kitajiri, halafu tunawaambia Watanzania tunataka kuwaondolea umaskini. Tunashindwa kuchukua maamuzi magumu pale yanapogusa maslahi yetu. Mimi binafsi nitasema hatuwatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tunapoweka viwango vya posho za vikao, Wabunge wanapata posho za vikao hizi *sitting allowance* siyo hela nyangi kimsingi. Mimi binafsi naweza nikasema siyo hela nyangi za kiwango cha kutisha, lakini ile *principle* ndiyo naizungumzia.

Mheshimiwa Spika, katika mashirika mengine ya Umma, watu wanalipana posho shilingi milioni moja kwenye *sitting allowance* kwa sababu Wabunge mmehalalisha ninyi kujilipa *sitting allowance*. Kuna taasisi za Kiserikali zinalipana shilingi milioni mbili, milioni 1.5 kwenye kulipana posho mbalimbali za vikao. *Why?* Kwa sababu uhalali umehalalishwa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tufike mahali tufanye maamuzi kwa faida ya wananchi na siyo kwa faida ya sisi binafsi wala kwa faida ya kushindanisha Vyama vyetu. Tuangalie ni nini tunaweza kukifanya kwa maslahi ya umma. Kama tuna hoja ya kwamba mapato ya Wabunge ama Watumishi wa Umma ni midogo, ni midogo zaidi kwa Watumishi wa kada ya chini. Watu ambao wanafaidi *sitting allowance* ni *segment* ndogo sana ya Watumishi wa Umma ambao wapo kwenye mamlaka ya maamuzi. Askari wetu wa kawaida watapata wapi posho hizi? Walimu wetu wa kawaida, Manesi wetu wa kawaida watapata wapi posho hii? Hawa wenzetu wanahemea mishahara ya mwezi, mwezi ukianza mpaka mwisho wa mwezi ndiyo anakwenda kupokea mshahara na bado unacheleweshwa, hawa watakuwa wageni wa nani?

Mheshimiwa Spika, tunasema, kama tunaweza kuangalia mfumo mpya wa ulipaji wa umma, mfumo mzima uangaliwe.

Mheshimiwa Spika, mbali na athari za pesa zinazotumika, kuna athari kubwa nimezungumza ya muda unaopotea kwenye vikao ambavyo siyo vya tija. Wabunge ninyi ni mashahidi, leo ni Wabunge wangapi ama Watumishi wangapi wa Umma ukiwaambia kuna kikao kisichokuwa na posho wanakwenda? hawaendi, kwa sababu kikao hakina posho. Tutajengaje nchi ambayo hatuwezi kwenda kwenye vikao kwa ajili ya majukumu yanayotukabili kwa sababu tunaogopa posho? Mimi nina imani Wabunge wa Vyama vyote tunaweza kuwa na ujasiri wa kutafuta njia halali za kuishi bila kuwakwaza wananchi wetu. Tukwazane kwenye mambo ya msingi, siyo ubishi. Tunapoteza muda wa Serikali, tunazungumza habari ya posho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zimekuja hata hoja kwamba kuna sheria. Ni kweli kuna sheria. Lakini ni Bunge hili hili linalotunga sheria na ni Bunge hili hili linarekebisha sheria. Kama tuna dhamira na utashi wa kweli, tuna uwezo wa kulitumia Bunge hili kubadilisha sheria. Hata kesho tutapitisha hapa *Finance Bill* ambayo tunabadilisha sheria

kumi na tatu mbalimbali ili kuwezesha bajeti ya Serikali kufanya kazi. Kama tungekuwa tuna nia, tungefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, umekuja Mpango wa Miaka Mitano unazungumzia jambo hili. Ni mpango wa Serikali hii, siyo mpango wa Serikali ya Uganda. Lakini tunashangaa tunapitisha Mpango kwa mbwembwe, tunajipongeza kwa mbwembwe, tunafika mahali tunaona kwamba maudhui ya Mpango ni taabu kwa sababu unagusa maslahi yetu. Hatuwezi tukawa *statesman* kama tunaangalia *interest* zetu binafsi, na siyo *interest* za Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo, ninakwenda kwenye suala la magari ya Umma. Naomba ku-declare *interest* kwamba, kwa mujibu wa wadhifa wangu, mimi nimepewa gari, *Land Cruiser* mpya kabisa, na sizungumzii suala la gari moja la kwangu au la Waziri Mkuu au Waziri yeoyote au Mkuu wa Mkoa. Tunazungumzia dhana nzima ya gharama ya kuendesha magari ya umma. Hii ni nchi moja ya ajabu sana. Mimi nina bahati ya kuwa kwenye *Private Sector* na nina bahati ya kuwa katika *Public Service*, wanaoendesha magari mapya ni Watumishi wa Umma tu. Kama kuna Wafanyabiashara nchi hii kwenye *Private Sector* wana uwezo wa kwenda dukani kununua gari mpya, hawafiki asilimia moja ya wafanyabishara katika nchi hii. Lakini Watumishi wa Umma tunajichana kwenye magari ya bei mbaya, hata wale *donors* wanaotusaidia, washirika wetu wa kimaendeleo hawatumii magari tunayoyatumia Watanzania. Ni lazima tukubali ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumesikia kauli ya Waziri anasema kwamba magari haya tutaacha kuyanunua. Kauli hizi zimetolewa siku nyingi tangu Mheshimiwa Mramba akiwa Waziri wa Fedha kwenye Bunge la Nane, lakini dhamira ya kweli haipo. CHADEMA tunasema nini na Upinzani tunasema nini? Jamani, *let us agree*, haya magari yote tuyapige mnada baada ya miezi sita, Watumishi wa Serikali wakopeshwe magari, tukitoka kwenye Utumishi wa Umma, hakuna mmoja wetu anakwenda kununua gari jipya, tunatumia magari mapya kwa sababu tupo kwenye Utumishi wa Umma. Tukitoka kwenye utumishi wa Umma, tunakwenda kununua *RAV4*, tunakwenda kununua Suzuki, tunakwenda kununua *Mark II*, huku ni ku-mis-use office. Tuuze magari yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii nchi gani jamani? Rais anatembelea *Land Cruiser*, Makamu wa Rais anatembelea *Land Cruiser*, Waziri Mkuu anatembelea *Land Cruiser*, Waziri wa kawaida, *Land Cruiser*; Spika, *Land Cruiser*; Katibu wa Bunge, *Land Cruiser*; Kiongozi wa Upinzani Bungeni, *Land Cruiser*; Mkurugenzi wa Wilaya, *Land Cruiser*; Mkuu wa Wilaya, *Land Cruiser* na Wakuu wa Idara, *Land Cruiser*. Basi, tingesema magari angalau haya ya bei kubwa yabaki kwa Viongozi Wakuu, wengine tutumie magari ya kawaida. Kama mtu anataka kutumia *Range Rover*, *Rolls Royce*, *Porsche*, tumia mshahara wako ama vyanzo vyako vya mapato ununue gari unayoihitaji. Tuache kutumia pesa za umma kwa ajili ya magari haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunaotumia magari haya, tukiulizana, ni wangapi tukitoka hapa tunaweza kutumia magari haya? Tukitoka kwenye Utumishi wa Umma, watu wakopeshwe magari. Kama mtu anataka kununua gari yoyote ya gharama yoyote

achukue, kama nchi nyingine wanavyofanya. Tuokoe hizi pesa jamani tukawasaidie watoto wetu na wananchi wetu, tukanunue *ambulance*. Tunaacha kwenda kununua *ambulance*, tunakwenda kununua bajaji za *ambulance*, halafu sisi tunanunua *Land Cruiser*.

Mheshimiwa Spika, tunasafiri *First Class*; nimesema leo nijikite hapa kwa sababu inaniumiza sana. Unatoka hapa unakwenda *Washington DC* unatumia *British Airways*, ukisafiri kwa *Economy Class* unalipa dola 1,200. Kwa mfano, kutokana na *season*, ukisafiri na *Business Class* unalipa dola 6,000.

Sisi Watanzania tukiwemo Wabunge tuna-opt kuchukua *ticket* ya dola 6,000 kwenda *Washington DC* wakati tunaweza tukaokoa dola 5,000 zikasaidia wananchi wetu. Tuna hadhi gani? Tunajipa hiyo hadhi katika nchi maskini kama hii! Tunajipa hadhi kwamba ni lazima tusafiri *Business Class*, kwa utaratibu gani? Tunasafiri kwenda Ulaya na Mabalozi wanasafiri *Economy Class* sisi ambao tunapewa pesa za misaada tunasafiri *Business Class* ama *First Class*. Akisafiri Rais, Waziri Mkuu ndiyo anafunga kabisa *Business Class* yote wanakaa Wasaidizi na Walinzi na Wapambe. Jamani!

Mheshimiwa Spika, huu siyo uamuzi mgumu kuwekeana mazingira kwamba tunafanya mkakati wa makusudi bila kujali Chama cha Siasa. Tuokoe gharama tusafiri *Economy Class*. Mtu akitaka kwenda *First Class*, akitaka *Private Charter*, akitaka *helicopter* atafute kwa uwezo wake na siyo kwa uwezo wa Serikali. Jiulizeni ni wangapi tunatoka kwenye Ofisi za Umma tunarudi Mitaani tunathubutu kusafiri *First Class*, hata ndege yenye ni taabu. Lakini kwenye Ofisi za Umma tunajifanya eti tuna hadhi sana kwa sababu sisi tuna pesa za bure za kutumia.

Mheshimiwa Spika, tuna matumizi makubwa ya Serikali ambayo kila siku yanaongezeka, na kila siku yataongezeka kama hatukuonyesha mfano Wabunge katika Bunge la Kumi, kwamba tunajali hoja za Taifa na siyo hoja za Vyama. Tuibane Serikali na Serikali na ninyi muwe tayari kubanwa. Tuwe na utashi wa kuisaidia nchi hii. Tuoneshe kwa vitendo siyo kwa maneno.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze kwa kifupi sana kwa sababu muda haupo, ni *Institutional Corruption* katika nchi. Tunatumia *Public Procurement Act* kununua matumizi ya Umma, lakini hamna hata mtu mmoja asiyejua kwamba *glass* moja inayouziwa Serikali inaweza ikauzwa mara mbili ya bei pamoja na kwamba mfumo mzima wa ununuvi umefanyika.

Kuna ununuvi ambao ni *syndicated*, wauzaji katika Serikali wana-*syndicate*. Kuna *tender process*, lakini tunajua kabisa wanauziwa vitu bei ya  *fifty percent to hundred percent above the market price*. Sheria inafuatwa na CAG akienda kukagua, hakuti chochote kwa sababu lile jambo limepangwa, limekuwa *syndicated*, makampuni yana-*collude* na Watumishi wa Serikali wizi unafanyika.

Mheshimiwa Spika, tangu nimekuwa Mbunge, nimepewa Mabegi ya Vikao vya Semina na sijui nini, jumla ni mabegi 18 Dar es Salaam, na Mabegi sita, Dodoma mabegi kama 24.

Mheshimiwa Spika, hayo mabegi ya kazi gani? Tunaona ni jambo la kawaida, ukisikia Semina kidogo, watu wamevaa kofia, wamevaa *t-shirt*, wamevaa beji na mabegi mkononi. Wabunge mna mabegi hata hamyatumii, mnakwenda kugawia ndugu zenu, ule ni wizi wa pesa za umma. Ni kwa sababu tumehalalisha wa kukubali utaratibu kama huo. Kama ni lazima Mbunge, apewe begi la kwenda kwenye Semina, basi anaweza akapewa *good leather bag* ambayo itadumu miaka minne, tukaachana na kuruhusu kila Wizara, kila Shirika, kila Taasisi, kwenye Semina ni kofia, *T-shirt* na mabegi.

Mheshimiwa Spika, ule ni mkakati wa maksudi wa watu kutafuta pesa, tunagawiwa *diary* tunabeba nyingine mpaka kwa kutumia Wasaidizi. (*Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Said Ramadhani ajiandae.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni bajeti ya mwanzo katika Bunge hili la Kumi, na mimi niwapongeze Wananchi wa Jimbo la Mkanyageni kwa kunichagua na ninaahidi nitawatumikia kama Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nikipongeze Chama changu cha *CUF* kwa kupidisha jina langu. Tatu, nimpongeze Rais wa Awamu ya Sita - Dkt. Shein pamoja na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* - Mheshimiwa Seif Sharif Hamad kwa ujemedari wao na ujasiri wao waliobadilisha mfumo wa siasa Zanzibar, kwa kusaidiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Kikwete na wakaweza kuifanya Zanzibar tulivu yenyе mwelekeo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahenga wanatuambia, zumari likipulizwa Zanzibar wanacheza Maziwa Makuu. Kwa maana hiyo, tuna tamaa kubwa zumari hilo ambalo limeshapulizwa Zanzibar na mabadiliko haya ya Katiba yanayokuja, tutegemee pia kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa upande wa Tanzania Bara au upande wa Jamhuri ya Muungano mwkaa 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho katika pongezi lakini si kwa umuhimu, nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Shein pamoja na Makamu wake wawili kwa kukaa na kushauriana vizuri na kuliokoa hili jahazi hivi sasa.

Mhehimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa nijielekeze katika malalamiko ya wananchi. Serikali inakiri kwamba imeweza kujikusanya mapato kwa kulinganisha na bajeti yake ya mwaka uliopita kwa asilimia 93. Imekusanya shilingi trilioni 5.5 kati ya

walizozibajeti shilingi trilioni sita. Wizara zote nyingine zinakiri kukusanya makusanyo kwa asilimia 87 mpaka 91 ya makisio yao.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la muhimu hapa, naomba lizingatiwe. Katika bajeti zote, hii ya Serikali na zitakazofuata za Wizara, katika makadirio yaliyofanyika kwa mwaka uliopita, mara nyingi sana katika makusanyo tunapewa takwimu mpaka mwezi Machi. Kwa mfano, bajeti ya mwaka 2010/2011 takwimu tunazopewa mpaka Machi, 2011, ukibahatika sana katika Wizara utapewa mpaka Mei. Kwa hiyo, miezi mitatu ya Aprili, Mei na Juni makisio yale, kwamba kimekusanya kiasi gani hakijulikani. Wala hakuna sehemu yoyote inayo-reflect tena kwamba katika bajeti inayokuja ionekeane kwamba ile miezi mitatu mingine kilikusanya kiasi hiki. Naomba Waziri atuelekeze ni namna gani Serikali itakuwa na mpango wa makusanyo ya miezi mitatu ambayo hatuoni katika vitabu. Pesa hizi zinakwenda wapi na zinahakikiwa namna gani? Hatuwezi kuziona, isije kuwa ndiyo tatizo lingine la ufisadi!

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pamoja na Serikali kukiri na Wizara mbalimbali kukusanya na bajeti za kawaida kuwa na matumizi mpaka kwa asilimia 87-90, kuna Wizara mbili zinalalamikiwa sana na wananchi, ambayo ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Kila Mbunge akisimama hapa, kuna matatizo ya Wizara hizo. Wizara hizi mbili zinashindwa hata kulipa bili za umeme kiasi kwamba inaifanya TANESCO na ZECO kuwa matatizoni. Hapa pana tatizo la kiutendaji: Je, bajeti zao hawajui kuzipanga vizuri au kuna matatizo Hazina hawatoi fedha kwa Wizara hizi au kuna matatizo gani?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kila siku iwe matumizi ya kawaida yanapatikana kwa asilimia 90, lakini kuwe na malalamiko makubwa. Nitatoa mfano halisi mmoja na kuna mifano lukuki. Tarehe 18 Machi, 2008, Vijana, Askari Polisi wapatao 300 kutoka Unguja na Pemba walipewa uhamisho kwa barua PHQ/Z/AD21/VOL7/181, wakapelekwa Mikoa ya Mtwara, Singida, Lindi, Kigoma na Mikoa tofauti. Vijana hawa wakapewaa pesa ya uhamisho tu, walipewa pesa ya nauli, fedha yao na stahiki yao ya uhamisho mpaka leo hii hawajapewa toka mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni zilipatikana sijui shilingi bilioni tatu wakaambiwa anayetaka achukue asiyetaka aache kwa ujeuri, kiasi kwamba hawa vijana hata pesa ya likizo hawapewi. Ni matatizo. Suala hili haliwezi kuachiwa liendeleee. Wanafunzi na Wafanyakazi wakikosa stahiki zao, wanaandamana. Majeshi yetu yana staha na ni matiifu. Wao wafanye nini kama hatukuwasaidia sisi Wabunge, au tunataka mpaka majeshi yetu nayo yaandamane nchi hii itakalika tena?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangularie suala hili, vikosi vyetu vyote na majeshi yetu wapewe stahiki kwa muda, wasihangaishwe. Hali kadhalika, kuna wastaafu waliopo Zanzibar wa Jeshi la Polisi na wote wa Muungano, stahiki zao zote wanaambiwa ni lazima waje Dar es Salaam. Ile BOT iliyopo Zanzibar ni ya nini? Hakuna Hazina kule? Kwa nini wa Arusha hawaendi Dar es Salaam? Kwanini wa Dodoma hawaendi Dar es Salaam iwe wa Zanzibar tu kila siku aje Dar es Salaam? Tutafutiwe ufumbuzi wa haraka. Hii ni kero kubwa sana ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, tuje katika bajeti yenyewe ukurasa wa tano na wa sita wa bajeti hii ya Serikali unazungumzia makali ya maisha. Haya makali ya maisha yamezungumziwa, kuna sababu bei za mafuta, kuna sababu za maharamia, kwa hiyo, meli za mizigo zimeongezwa ziko sababu nyingi kibao. Halafu Serikali imejaribu kutafuta *solution*, namna gani wataondoa. Lakini hizi sababu wanazotaka kuondoa, naona bado zina matatizo. Kwa mfano, hizo kodi tu ikiwa katika kila lita moja ya mafuta iwe *EWURA*, kuna *percentage* yake, *TBS* kuna *percentage* yake, *TIPPER*, *TRA*, *SUMATRA* na kadhalika ya zile kodi muhimu za Serikali *exercise duty* na nyngine.

Mfumo huu wa kwamba lita moja ya mafuta kuna kodi 25, hata kama hiyo *bulk procurement* ikija, basi bado makali ya maisha hayawezi kuondoka kwa mtindo huu. Isitoshe, hiyo *bulk procurement* tumeizungumzia miaka miwili sasa iliyopita haijakuwepo, kwa nini? Sheria tumeshapitisha, kwa nini haijatekelezwa? Ni kwa sababu ya urasimu na Serikali kutoona tatizo liko wapi? Hivi sasa kuna mgongano baina ya bandari, baina ya *TPDC* baina ya *TIPPER* haijulikani kila mmoja anavuta kwake kana kwamba wako Serikali tofauti. Hili ni tatizo. Kwa hiyo, *bulk procurement* haiwezi kufanikiwa. Kwanza huu mgongano uondoke na *bulk* ikiondolewa *means* hata ikija kwa mtindo wa kodi zote hizi bado makali ya maisha yatakuwepo na mwananchi hatujampatia unafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine lililosababishwa na ukali wa maisha katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anatuambia ni ajira, nakubaliana naye. Ajira imekuwa ni tatizo. Lakini tatizo hili la ajira sababu inatoka wapi? Kwanza niishukuru mashirika ya simu kwa kuongeza ajira kubwa. Tuyapongeze sana mashirika ya *Zantel*, *Vodacom*, *Tigo*, *Airtel* na kadhalika, yamesaidia ajira. Lakini kwa bahati mbaya, Serikali hii na hasa Wizara ya Kazi, kuna tatizo kubwa la uhamiaji. Kuna tatizo kubwa *TIC*. Katika sekta ambayo inaa jiri wageni wengi na kuacha wazawa Watanzania wenye ujuzi kama huo ni sekta ya utalii hasa mahotelii. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitakupa hii *document* sasa hivi, hii ni mfano wa hoteli moja tu kuna majina ya wafanyakazi, katika Sekta ya Mameneja 29, Watanzania ni wawili tu. Hii ni mfano wa hoteli moja tu, kuna mahotelii ngapi katika sekta ya utalii? Kwa hiyo, wote hawa kuna sheria tumeipitisha wenyewe kwamba kama sekta hakuna watalaam mwisho watano, watafutwe wa kigeni. Leo inakuaje hoteli moja kuna Mameneja 29 na Serikali inatazama? Haya ni matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naona kengele imeshapigwa na yako mengi. Tatizo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni hii tathimini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni ambayo Mheshimiwa Waziri amezungumzia. Hapa pana tatizo moja. Katika kila jambo nchi hii kuna kitu kimoja, imekuwa wimbo ndani ya Bunge, mshauri mwelekezi, upembusi yakinifu. Leo tunatafuta mshauri mwelekezi wa kimataifa kwa kukopa kimataifa aje hapa atufundishe kukopa na kulipa. Imo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba utuombee kwa Serikali itupatie *list* yote ya washauri waelekezi miaka mitano iliyopita na hawa wapembusi yakinifu tuone thamani gani

wanalipa. Mna sababu! Hivi karibuni tu shirika moja tu lilifanyiwa *feasibility study* tena watu walikaa Ulaya dola milioni mbili. Sasa washauri waelekezi hawa wako wangapi? Hebu tuelezwe. Halafu Serikali ina mpango wa kukopa katika kipindi cha miaka mitatu dola 1,500,000. Lakini hivi sasa wameshakamilisha mpango wa dola milioni 408, lakini angalia katika Mkoa katika soko la mitaji, katika mkopo ambao Serikali imeshafanikisha wa milioni 408, tayari kuna milioni 40 zimeshatoka. Ni tozo na bima. Huo mkopo wa milioni 408 hatujaupata, tayari unatoka milioni dola 40, ni fedha nyingi sana. Leo tunatafuta mshauri mwelekezi wa kutufundisha kukopa na kulipa.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa sana, kama Serikali, tutaendelea na mtindo wa namna hii, maendeleo yako mbali mno. (*Makofi*)

Mwisho, nijielekeze katika suala linguine, naona muda unakwenda. Mwezi Augosti, 2007 lilitolewa tamko hapa la Serikali, tamko hili lilihusu kwa ufupi *dollarazation*, yaani matumizi ya fedha za kigeni kulipia bidhaa za huduma katika soko la ndani, *dollarazation*. Sababu zilizotolewa katika tamko hili la Serikali na hali halisi ilivyo ni tofauti kabisa Serikali, inatudanganya.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano. Tukitazama uhakika kwa takwimu za Serikali na takwimu ninazojua mimi mwenyewe fedha yetu namna inavyodondoka na Wabunge kila siku wanapiga kelele kwa suala hili kuanzia mwaka 1979, 1980 dola moja ya Marekani ni Sh. 7/= za Tanzania. Lakini ilipofika mwaka 1988 dola moja ya Marekani ni Sh. 125/= za Tanzania. Ilipofika mwaka 1990, dola moja ya Marekani ni Sh. 450=/. Hivi leo tunavyozungumza, dola moja ni Sh. 1,600=/. Nchi zilizoendelea wanathamini fedha yake.

Wizara ya Fedha na Benki Kuu wanafanya nini kunusuru fedha yetu isidondoke? Mikakati gani iliyopo, sera kamilifu za kutoa thamani kwa fedha yetu tukathamini fedha yetu tukaiheshimu fedha yetu? Leo hatuna tatizo na sheria ya *exchange rate* ya mwaka 1992 ilioanzisha *Bureau de Change*, tatizo siyo *Bureau de Change*, tatizo ni mfumo wa nchi kutoheshimu fedha yetu. Leo wewe ukitoa thamani ya kitu chochote kama ni hoteli kama ni nini kwa thamani ya dola unaidhalilisha sasa hivi. Tutaonana kwenye Bajeti ya Waziri Mkuu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SAIDI RADHAMANI BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, nianze nami kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu. Lakini pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chalinze ambao wamenipa kura nyingi sana na hatimaye kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema, kama hujui uendako, huwezi kupotea. Kama unajua uendako, kuna mawili, ama upotee ama ufile salama. Kwa bahati nzuri bajeti yetu ya mwaka huu imekuja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mpango ambao maana yake umetupa uelekeo wa kule ambako tunataka kwenda, kwa maana kwamba siku ya siku tutajiuliza tumefanikiwa kwa kiasi gani ama tumeanguka kwa kiasi gani kutokana na mpango huu uliopo? Lakini nashukuru kwa nafasi hii niliyopewa

angalau ni nafasi ya mwisho kuchangia na kwa hakika walio wengi wamechangia, lakini nami nitatoa mchango katika maeneo mawili, matatu kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri na inatekelezeka, wasiwasni kwamba: Je, itatekelezeka kwa kiasi gani? Je, malengo yetu ambayo tumeyapanga kwenye Mpango wetu wa Maendeleo ya Miaka Mitano yatafikiwa kwa kiasi gani? Mimi nashukuru kwamba katika maongezi ya ujumla ya Waheshimiwa Wabunge, nilichokigundua, wote wanaongelea tu kwamba naomba angalau kifanyike hiki, kifanyike kile. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba mwisho wa siku tuunge mkono bajeti hii ili yale mapungufu ambayo tunaona kwenye Majimbo yetu yaweze kukamilika. Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu na nina uhakika yale ambayo nitasema yatatiliwa maanani.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie eneo la pili la kilimo ambalo ni sekta mama kwa nchi yetu. Takribani wananchi zaidi ya asilimia 75 wanaajiriwa huko. Lakini nimefarijika sana kwamba kwa dhana nzima ya Kilimo Kwanza, imeleta maendeleo makubwa kwenye nchi yetu. Kilimo kimepanda kutoka asilimia 3.2 mwaka 2009 mpaka asilimia 4.2 mwaka 2010. Haya ni maendeleo makubwa kwa kilimo, ambapo tumejionea wazi kwamba katika Mpango huu wa Kilimo Kwanza, mazao mbalimbali yaliweza kupanda. Mazao ya Chakula yamepanda kwa kiasi kikubwa, mazao ya biashara yamepanda kwa kiasi kikubwa, lakini pia mazao ya mafuta nayo yamepanda kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto kubwa hapa, naomba nieleze. Tunashukuru sana kwamba sasa tuna Mpango mahususi wa kuboresha kilimo chetu. Nchi yetu takribani imeingiza matrekta 1,800 kwenye soko japokuwa lengo ni kuingiza matrekta 3,000 maana yake 1,200 yatakuja baadaye. Kuna habari kwamba, Serikali ya Marekani nayo itatupatia matrekta 4,000.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kitu kimoja hapa kidogo lazima tukiangalie vizuri kuhusu upatikanaji wa matrekta haya. Kuna matatizo makubwa! Tatizo la kwanza, bei zake ziko juu sana. Hili naiomba Serikali iliangularie kwa kina sana. Katika ule utaratibu wenyewe ili matrekta haya wakulima waweze kuyapata, yana wadhamini wawili. Hapa nitaeleza kwa kirefu kidogo. Wadhamini hawa ni yule wakala ambaye anaunganisha soko la matrekta na walipo wakulima.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mdhamini mwininge anaitwa *PASS - Private Agricultural Sector Support*. Utaratibu ukoje? Huyu mdhamini ambaye hafahamu matrekta yanapatikana wapi lakini pia anajua kwamba wenyewe kuhitaji wanapatikana wapi. Inachukua muda mrefu sana kwamba huyu mdhamini amtafute huyu mtu anayehitaji matrekta kupitia *SACCOS* zao na akishampata aende kwa *PASS (Private Agriculture Sector Support)*.

Hata kule naye akienda *PASS* atapitia yale maombi yote ya wakulima, mwisho wa siku naye lazima arudi tena kule waliko wakulima akajiridhishe mwenyewe kupitia

kwenye *SACCOS* zao. Kama hiyo haitoshi, ripoti ikikamilika, lazima sasa aipeleke *TIB* Benki ya Uwekezaji. Benki ya Wawekezaji nao bado hawataamini taarifa za *PASS*, nao watakwenda kuwa-*assess* hawa wakulima wenye uhitaji mmoja mmoja au kwenye vikundi vyao.

Mheshimiwa Spika, mlolongo wote huu ili trekta moja liweze kupatikana kwa utaratibu huu inachukua siyo chini ya miezi sita. Sasa haya matrekta 1,800 ambayo yameletwa na Serikali kwa utaratibu huu yatakwisha lini? Ndio maana sasa hivi kila kona ukienda katika nchi yetu mfano hapa Dodoma matrekta yamejaa kibao kwa sababu utaratibu wa kuweza kuyatoa unakuwa na urasimu huu ambaa nimesema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka jana mwaka 2010 *TIB* ni matrekta yasiyo zidi 150 yameweza kutolewa kuwapatia wakulima. Hii hatufiki hata kidogo. Mimi nina ushauri ufuataao, kwa sababu watalaaambao wako *TIB* wa kuandaa michanganuo ile, sambamba na watalaaambao wako kule *PASS*, pia wanapatikana kwenye Halmashauri zetu za Wilaya. Kwa nini Serikali isione njia mbadala sasa ama pamoja na kutumia *PASS* au *PASS* waachwe watumie Halmashauri zetu za Wilaya waweze kuandika hii michanganuo kwa umahiri zaidi?

Mimi naamini tukifanya hivi, basi zana za kilimo wananchi wetu watazipata kwa wingi zaidi na kwa wakati angalau nafuu. Watalaaambao wanasema kama utatumia njia hii wananchi kuanza kutafuta trekta mpaka kupata siyo zaidi ya miezi mitatu tofauti na miezi sita ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema kwamba ni vizuri sasa Halmashauri angalau nazo zihusike sana kwenye jambo hili? Kama nilivyosema, watalaaambao wanaopatikana na *PASS* na *TIB* pia wanapatikana kwenye Halmashauri zetu na wapo wengi sana. Wale watalaaambao kwenye Halmashauri za Wilaya wao hawa ndio wanajua wakulima gani wanapatikana wapi na hivyo kuweza kuweka mambo sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, sasa naomba niende kwenye barabara kwa haraka kidogo. Nashukuru sana, bajeti imelenga katika kuendeleza barabara. Hapa kuna jambo moja ambalo lazima tulisemee. Maeneo mbalimbali ya nchi yetu, wananchi wetu nyumba zao nyingi zimewekwa X, kwa maana kwamba wavunjiwe. Mimi naunga mkono jambo hili. Hata hivyo, kuna mambo mawili, matatu lazima yawekwe sawa. Maana ule muda wa kuanza kuweka X nyumba, na mpaka muda mwananchi aliyewekewa X alipwe, inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna matatizo makubwa; wewe fikiria, mtu amestaafu kazi leo, anaamua kujenga nyumba yake, inafikia nyumba bado kupaua tu anawekewa X anaambibiwa asiendelee tena kujenga nyumba. Lakini malipo yake mpaka pale alipoishia yanachukua zaidi ya miaka miwili au mitatu. Je, hata muda huu akilipwa ile thamani ambayo fedha ameitumia ni sawa sawa kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hili, lakini changamoto nyingine kubwa inayopatikana, baadhi ya watu wameamua kuchukua mikopo kutumia nyumba zao kama

dhamana. Wakati wataalam wa benki wanafanya mahesabu yao, inafika muda sasa watalaam wanakuja kwenye nyumba ili wajionee na hatimaye watoe fedha, wanakuta nyumba ile imewekwa X na hivyo hawatakuwa tayari kutoa fedha kwa ajili ya kumwendeleza huyu mwananchi. Hili nalo ni tatizo lingine.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo lingine ni pale mtu mwagine amejenga nyumba yake, anataka kuweka umeme kabla wataalam wa *TANESCO* hawajaja kuweka umeme wanakuta tayari nyumba yake nayo imewekwa. Lazima kwa kweli Serikali iweze kujipanga. Kwa ujumla wake ndio nilitaka kusema kwamba Serikali iangalie kwamba ule muda wa kuweka X nyumba kwa maana ya kwamba isiendelezwe ili tayari kubomolewa, muda ukifika, usichukue muda mrefu ili kuweza kuwanusuru watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga 4% ambayo ilikuwa inapatikana kwenye *skill development levy* kwa ajili ya kuweka kwenye Bodi ya Mikopo. Hii itatusaidia sana. Lakini wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba hata kama fedha hii ikipatikana, basi niwaombe sana watu wa Bodi ya Mikopo, kuna dhana sasa imejengeka kwamba ama kule watu wanafanya mchezo mchafu kwa maana kwamba watu wengine wasiostahili kupewa fedha wanapata fedha hizi za mkopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala*, aliyenijalia uzima na afya njema na kuchangia bajeti ya mwaka 2011/2012.

Nishukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa viongozi wangu wa Kitaifa wa Chama cha *The Civic United Front*, Chama cha Wananchi kinachoongozwa na Mwenyekiti mahiri Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, Makamu Mwenyekiti, Machano Khamis Ally na Katibu Mkuu, Maalimu Seif Sharif Hamad ambaye amekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Serikali ya Umoja wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende moja kwa moja kwenye mchango wangu na nianze kwenye ukurasa wa 40 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri inayosema kwamba misingi na shabaha ya bajeti ya mwaka 2011/2012 ni Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Watanzania hawahitaji maneno mazuri ya vitabuni, wanachohitaji ni mapinduzi ya kweli na umaskini ndani ya hali halisi ya wananchi vijijini uondokee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha, inasononesha, haipendezi hata kidogo tangu mwaka 2008, 2009 na 2010, wananchi wa Halmashauri ya Kilwa wamekuwa wakilalamika kwa Serikali juu ya utaratibu mbaya, mbovu na usiofaa juu ya uuzaaji wa zao la ufuta katika Vyama vya Ushirika vya Msingi katika mfumo unaojulikana kama Stakabadhi Ghalani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wamelalamika muda mrefu, wamekuwa wakilia muda mrefu na wameona utaratibu huu hauwezi ukawaondolea umaskini. Wao wamekuwa na mpango mwengine, wamegundua masoko mengine, lakini kilio chao muda mrefu wamekuwa hawasikilizwi. Katika hili tarehe 7 Julai, 2001, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa walikubaliana kabisa na wananchi hawa waandae mazingira, wauze ufuta wao popote wanapotaka ili mradi waweze kuboresha maisha yao. Cha kusikitisha, baada ya maamuzi hayo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, muda si mrefu baada ya siku ishirini na nne, tarehe 31 Mei ,2011 ngazi ya Mkoa ikabadilisha kabisa maamuzi hayo na ikapelekeea sasa ni lazima wauze ufuta wao katika mfumo uleule wa Stakabadhi Ghalani, hilo ni jambo baya, si zuri kwa wananchi na wananchi wananyonywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hili wananchi wa Wilaya ya Kilwa kwa mfumo wa Stakabadhi Ghalani ambapo wanawauzia Vyama vya Msingi vya Ushirika, wanawauzia shilingi elfu moja, wanapouza katika masoko mengine ambayo yana bei zaidi wanauza elfu moja na mia tano, mnapokuja hapa mkatumbia sasa kwamba Serikali ina mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini, ni kweli au ni vitabuni tu mmeandika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini wakulima hawa wananyonywa, wameandaa mazingira mengine ambapo soko lao linapatikana ni kwa nini wasiwaachie kuza kwa bei ya elfu moja na mia tano. Mnawalazimisha lazima wauze kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika kwa shilingi elfu moja? Nadhani kuna MKUKUBI yaani Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Binafsi katika ngazi ya Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani hata kidogo tunaimbaimba MKUKUTA, MKUKUTA, MKUKUTA, kumbe kuna MKUKUBI uliojifisha, ni tatizo. Naiomba Serikali iangalie kwa makini, izingatie mawazo ya wananchi wa Kilwa Kusini juu ya matatizo yao ya kuza ufuta katika masoko ambayo yataleta tija kwa kuboresha maisha yao na kuondolewa umaskini kwa dhati kabisa na sio kwenye vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii niwapongeze kwa dhati kabisa wakulima wa ufuta wa Kilwa Kusini, vijiji vya Ruhatwe na Kikole, Kata ya Kikole, Inokwe na Lilegawage, Kata ya Ligawage, Njilinji na Nakiu, Kata ya Njilinji, Mavunji na Mandawa, Makanga na Kata ya Kiranjeranje, nasema ahsanteni sana, kaeni kamba, tutaendelea kuwateteeni kwa nguvu zetu zote, tuhakikishe kwamba huo MKUKUBI katika ngazi ya Mkoa unakufa, mnauza katika soko lenu la shilingi elfu moja na mia tano mnakotaka kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, mara nyingi tumekuwa tukiangalia utaratibu gani ambao wenzetu wa Kusini hasa kuanzia Tunduru pamoja na Mikoa ya Lindi na Mtwara, Mikoa ambayo inazalisha korosho wataweza kuondokana na umaskini. Tunajua sote kwamba korosho ambazo zinazalishwa asilimia 70 zinazosafirishwa nje ni ghafi, asilimia 30 ya korosho zinazosafirishwa ndiyo safi. Tunaiomba Serikali iandae mazingira ya kukaa na wenye viwanda hivi vichache, kuandaa mazingira ya kupatikana kwa viwanda vingine vikubwa zaidi ili asilimia kubwa ya korosho ambazo zitasafirishwa ziwe safi na sio ghafi. Huo utakuwa ni mkakati wa kweli wa kuweza kukuza uchumi na

kupunguza umasikini. Kwa hiyo, ndugu zangu wale wa Newala, Tandahimba, Masasi, Nanyumbu, Mtwara Mjini, Mtwara Vijiji, Nachingwea, Liwale, Kilwa, Ruangwa wataondokana na umaskini wa kweli na sio ambao unaandikwa katika vitabu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, sasa nije katika rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu ametujalia. Lazima tukiri na tukubali, Mwalimu Nyerere alishatuambia kwamba kama rasilimali ile ya madini hatuwezi kuiendezea vizuri basi ni vyema ibakie kwenye, ibakie ardhini kulikoni kutopata faida inayostahili. Wachimbaji wadogowadogo wa madini wana malalamiko makubwa, wachimbaji wadogowadogo wa Mererani, *Tanzanite* wanachohitaji wao ni kuona jinsi gani bei nafuu ya vifaa vyao vya kuchimbia madini. Wachimbaji wadogowadogo wanachoangalia wao zaidi katika bajeti hii ni namna gani ambapo bei za baruti za kulipulia miamba itapungua. Hilo ndiyo wanalojua wao, wale wa Nyamongo, Geita na maeneo mengine yote wana imani kwamba Serikali ikiwa makini itaangalia wachimbaji wadogowadogo ni vipi ambavyo wataondokana na umaskini katika bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala zima la kusafirisha mchanga kupelekwa nje ya nchi kwenda kusafishwa limeongelewa kwa kasi sana na mimi nataka niseme tu kwamba Serikali ni vyema isikie kilio cha kweli na kama ni *tissue* ya kufuta machozi ya Wabunge tuangalie utaratibu mzuri na ulio imara zaidi. Kunduchi kuna maabara ya kusafishia mchanga, lakini kwa kiasi fulani inaelekeea Serikali bado haijatoa mkakati ulio mzuri zaidi wa kuweza kupanua maabara hii ili waweze kusafisha mchanga zaidi. Ni aibu siku zote kupeleka kusafisha mchanga nje, kinachopatikana hakijulikani mbali ya dhahabu lakini kuna shaba na madini mengine mbalimbali. Katika hili, naomba Serikali iliangalie kwa kasi na kwa kina kabisa.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye usimamizi na udhibiti wa fedha za umma, ukurasa wa 34. Tanzania ni mwanachama wa *APRM, African Peer Review Mechanism*, Mpango wa Nchi za Afrika Kujitathmini. Hivi Serikali, ninyi mkiwa ni wanachama wa *APRM* mnajitathmini kiasi gani ambapo siku zote sisi Wabunge tunadhihirisha hapa, lakini wanaachiwa wajanja wachache wanaziiba, kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001/2002, Serikali imekiri hapa Bungeni shilingi milioni 874.2 zimechukuliwa na wajanja wachache, mwaka 2002/2003 shilingi milioni 910.5 zimechukuliwa, mwaka 2003/2004 na wao wakachukua chao mapema, shilingi milioni 470.7, mwaka 2004/2005, shilingi bilioni 1.4 mwaka 2005/2006, shilingi milioni 691.1, mwaka 2006/2007 shilingi bilioni 2.3, mwaka 2007/2008 shilingi bilioni 3.5, mwaka 2008/2009 shilingi bilioni 3.1 na mwaka 2009/2010 shilingi bilioni 11. Tanzania ni mwanachama wa *APRM*, mpango wa nchi za Kiafrika za kutathmini, mlitathmini vipi juu ya fedha zetu ambazo zinachukuliwa? Tunapokuja na hoja hapa Bungeni ili Bunge liidhinishe shilingi trilioni 13.5, lakini je fedha hizi mtazizibiti zisiende kwa wajanja wachache? Tunaposema wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* warejeshwe, tuna hoja, kwa sababu wangapi wamechukua fedha hizi wameachiwa? Mwaka 2009/2010, Halmashauri 30, Watendaji 921 walichukua fedha, 14 wakashushwa madaraka, mmoja akapewa onyo, mmoja akashushwa mshahara. Ni kwa nini wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* pekee yake waondoshwe, mbona hawa mmewaachia, kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tusiwe na *double standards*, tuangalie utaratibu ulio mzuri, kama ni nidhamu, kama kwenye nyumba mtoto akikosa anapewa viboko, basi viboko vya kwanza wapewe wale wenye dhambi na dhambi kubwa ni kwa wale wanaochukua fedha za umma, hakuna dhambi kubwa kama kuchukua fedha za umma. Kama watoto wetu sisi tuwaangalie kwa kina kabisa, kama kuna matatizo tukae nao kitako na tuangalie na kama hoja yao ni kupatiwa fedha, fedha hizo tuwapeni kwa busara kabisa ili wareje katika masomo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niangalie jambo lingine kwa harakaharaka kwa sababu muda unakwenda suala zima la tatizo la maji katika Mkoa wa Tabora. Mara nyingi tumekuwa tukisema na Wabunge wa Tabora wamekuwa wakisema na sisi Wabunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tunaendelea kusema, Serikali ina mpango gani wa kurudisha ule utaratibu wake wa zamani kwamba mabomba ya maji yanayotoka Shinyanga kutoka Ziwa Victoria yatapelekwa Tabora, maji ya Tabora sio salama, sio mazuri, rangi yake ni maziwa, ukifika kule unawaonea huruma wananchi, hili ni suala kubwa na zito. Naomba Serikali ikae kitako iangalie kwa umakini mkubwa jinsi gani ambavyo wananchi wa Tabora, wananchi kwa ujumla wote katika maeneo mbalimbali wanaweza kupata maji safi na salama katika mradi ule ambaeo Serikali imeahidi mara nyingi.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala zima la uvuvi kwa harakaharaka. Rasilimali hii bado haijapatiwa nafasi yake ya kufanyiwa kazi kwa ukamilifu na Serikali. Tumeambiwa juzi hapa kuna meli 71 ambazo zinavua katika Bahari Kuu na tunapata dola milioni 2,740,400 na kwa miezi mitatu katika leseni zake ni dola elfu 12 za Kimarekani, lakini je ni kiasi gani wanavua haijulikani, kuna meli zaidi ya mia moja zinavua katika maeneo yetu lakini hazikamatwi lakini wale ambaeo wana nyavu ndogondogo mnazichoma moto. Naomba Serikali iangalie kwa umakini mkubwa juu ya utaratibu mzima wa kuzikamata meli hizi ambazo zinavua katika bahari zetu na moja kwa moja inaonekana wanavua uvuvi ambaeo sio mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika hili sasa kwa nini tusikae na vyuo vyetu mbalimbali, tukaanda mazingira mazuri ya kutafuta wasomi katika Vyuo Vikuu ili wajijunge na *fishing industry* ya kweli, ili tuweze kuboresha shughuli zetu hizi za uvuvi, hili ni jambo zuri. Viwanda vya kusindika samaki havijatosha, kama Serikali tuna mkakati gani wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini? Tusiwe na maneno mengi ya kwenye vitabu na utekelezaji mdogo na huo ndiyo wasiwaso wa Waheshimiwa Wabunge walio wengi. Tumekuwa tukisema mara nyingi hapa Bungeni utekelezaji wa shughuli hizi ukoje?

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ikubali kwamba inaendeshwa na binadamu na kuna makosa yanafanyika, ni vyema Serikali baada ya kilio kutokea kwa Waheshimiwa Wabunge, itafakari ione ni mbinu na mkakati gani unachukuliwa kujirekebisha ili machozi ya Waheshimiwa Wabunge yafutwe hata kama kwa *tissue* na *tissue* ya Serikali kwa Wabunge ni kusikiliza wanachosema na kuamua ni jinsi gani ambavyo mtawezza kutekeleza majukumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nafikiri kilio changu kimesikika, machozi mtayafuta japo kwa *tissue* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Nashukuru sana. (*Makofit*)

**SPIKA:** Mmh! Haya ahsante, kufuta kwa *tissue* itakuwa imechakaa kabisa baada ya muda mfupi. Sasa nimwite Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na Mheshimiwa Salvatory Machemli ajiandae.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze na mimi kutoa mchango wangu katika mkutano huu wa Bunge la bajeti unaoendelea hivi sasa.

Kwanza kabisa, napenda niipongeze Serikali kwa kuja na mpango kamambe wenye kulenga katika kumpunguzia matatizo mwananchi wa kawaida wa Tanzania hii. Bajeti imejielekeza vizuri katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu ya uhakika ya barabara, reli na mkongo wa Taifa. Mkongo wa Taifa tumeona jinsi ambavyo umekuwa ukisaidia katika kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na mawasiliano ya uhakika na katika kuhakikisha kwamba shughuli zao mbalimbali za kawaida na zile ambazo ni za msingi zinapatikana katika maisha yao ya kawadia.

Mheshimiwa Spika, nchi yejote ili iweze kuendelea inahitaji kuwa na mkakati mzuri wa mawasiliano na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imeliona hilo ndiyo maana katika bajeti yake imekuja na mkakati mzuri wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na barabara za lami. Niombe barabara yetu ya Masumbwe, Lugunga, Mbogwe, Lulembela mpaka Butengo na Lumasa ikiwezekana katika bajeti hii ifikiriwe kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme nalo ni la muhimu kwa sababu tunapokuwa na umeme wa uhakika, Serikali itakuja kufikia hatua ya kuweza kubadilisha uwezekano wa kuwa na treni zinazoendeshwa kwa mafuta, tuje na utaratibu wa kuwa na treni zinazoenda kwa kasi, zinazotumia nguvu ya umeme. Maana tutakapokuwa na treni inayoweza kwenda kasi na inayoweza kubeba mizigo kwa kiwango kikubwa zaidi itazisaidia zaidi barabara tunazozijenga kwa hela nyingi ziweze kuishi kwa muda mrefu zaidi na ziweze kusaidia katika kuchangia maendeleo ya Taifa hili kwa urahisi zaidi na kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kwa mwaka huu imetenga shilingi bilioni 2781.4 tofauti na mwaka jana ambapo tulikuwa na shilingi bilioni 1505.1. Hatua hii inaonesha wazi kabisa kwamba Serikali imeliona hili la kwamba mawasiliano yanapokuwa yako imara na ya uhakika, maendeleo yanakwenda kasi. Wote ni mashahidi kwamba barabara ya kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ndiyo iliyokuwa ya lami tu, kutoka hapa Dodoma kwenda Mwanza kulikuwa hakuna lami, hakika maendeleo na hata bidhaa zilikuwa zinafika Mwanza na maeneo mengine ya Kanda ya Ziwa zikiwa zimepanda bei zaidi kwa sababu mfanyabiashara alikuwa anatumia muda mrefu zaidi katika kusafirisha bidhaa zake. Naipongeza Serikali kwa sababu sasa inaona namna gani ambavyo tunaweza tukapiga hatua zaidi katika kuhakikisha kwamba mawasiliano yanakuwa ya uhakika zaidi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la nishati. Serikali kwa mwaka huu wa fedha napo imekiweka kipengele cha nishati na madini kuwa nacho ni kipaumbele muhimu na ni kweli nchi hii imejaliwa kuwa na madini ya aina mbalimbali ambayo kwa kiwango kikubwa yanawanufaisha wageni. Sasa naomba Serikali kuanzia sasa ifike mahali isimamishe kutoa leseni kwa wawekezaji wakubwa ili tuweze kutumia wataalamu wetu ambao wamekuwa wakitumika katika makampuni ya wageni kwa kuwa ukiangalia tangu mwaka 2000 kuna umri wa zaidi wa miaka kumi tangu kwa mfano Mgodi wa Geita umezinduliwa pale. Mgodi wa Geita baada ya kuwa umezinduliwa mwaka 2000 mpaka leo ni miaka kumi. Ukiangalia sasa ni akina nani wanafanya kazi katika mgodi ule, walio wengi ni Waswahili, haohao Watanzania ndiyo walioweza kushiriki katika hatua mbalimbali za kuanzisha mgodi huo. Wamefanya *exploration*, wamefikia hatua ya kuanza uzalishaji na hata sasa wengine kuwa na uzoefu walioupata katika mgodi ule wamekuwa wakajiriwa katika nchi za Congo, Zambia na hata huko Botswana. Watanzania hawa wamesomeshwa na fedha ya Serikali, niombe na kuishauri Serikali kwamba sasa ifike wakati ipange utaratibu wa namna nzuri ya kuweza kuwatumia Watanzania hawa badala ya kuwaacha wakaendelea kuwa wanatumiwa na wageni na matokeo yake jasho lao linatumiwa na wageni zaidi, nashauri Serikali kufungua migodi yake.

Mheshimiwa Spika, suala la maji. Suala la maji nalo ni suala muhimu, Watanzania hawa wanahitaji kuwa na huduma nzuri ya maji safi na salama, nashukuru kwamba Serikali katika mpango wake wa bajeti mwaka huu imeweka suala hili liwe katika kipaumbele pia. Sasa nniombe Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi ione uwezekano wa kutupatia maji safi na salama katika miji yetu ya Masumbwe na Bukombe hata Geita, kwa sababu maeneo haya yote yako karibu sana na eneo lililoko Ziwa Victoria lakini kwa bahati mbaya wananchi wengi wanapata shida kupata maji. Maji Geita Mjini ni tatizo na kutoka Ziwa Victoria kuja Mjini Geita ni kilomito 21 tu lakini Serikali imeweza kusafirisha maji kwa umbali mrefu kutoka Mwanza mpaka Shinyanga na Kahama lakini imeshindwa kusogeza maji kwa karibu kama kilometra 21 tu kuingia mjini Geita. Nniombe Serikali ilifikirie suala hili na kuweza kuwapatia wananchi wale maji salama ya kunywa na kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, labda nijielekeze katika suala la kilimo. Serikali imekiweka kilimo kuwa nacho kipaumbele katika bajeti hii, ni suala la msingi. Sasa katika kilimo niseme kitu kimoja, hata Chama chetu cha Mapinduzi tunasema kwamba ni Chama cha Wakulima na Wafanyakazi lakini kwa bahati mbaya sana nimegundua kwamba Serikali imekuwa haiwapi umuhimu wakulima, kwa nini? Kuna wakati inatokea kwamba wananchi wetu wanapokuwa wamelima pamba au mazao ya chakula, Serikali inazuia wasisafirishe nje au watu wa nje wanapokuja kuyanunua, Serikali inasema wasiuze, wakati shughuli za kilimo ni ngumu na ndio maana watu wengi hawajishughulishi na kilimo kwa sasa hivi kwa sababu wanajua kwamba kilimo hakina tija. Sasa inapotokea mtu amelima mazao yake vizuri anahitaji sasa ayasafirishe kuyapeleka hata nchi za nje Serikali inazuia, inasema kwamba inabidi wananchi hawa wauze mazao haya ndani ili kuweza kudhibiti mfumuko wa bei. Ni vyema bei ikapanda ili kusudi mwananchi huyu na yeze aweze kupata maslahi katika suala zima la kilimo. Mazao yake anapokuwa amelima

analima kwa ajili ya chakula chake lakini ile ziada inapokuwepo anatakiwa aiuze na anapoiuza anapata faida kwa sababu alitumia gharama katika kuandaa shamba, kupanda mpaka kuja kuyavuna.

Mheshimiwa Spika, tuangalie kwa mfano zao la pamba. Mwaka jana kutokana na m dororo wa uchumi bei ya pamba ilishuka. Serikali kwa makusudi mazima ili wafidia wafanyabiashara wale wa zao la pamba lakini kwa bahati mbaya sana wakulima wa Jimbo langu Bukombe na Mbogwe kule pamba ilikomea bei ya shilingi 500, kuna maeneo mengine wakapata bei ya shilingi 1,000/. Sasa sikujua kwamba kulikuwa na tatizo gani wengine wapate bei tofauti na ile bei ya wenzao. Kwa hiyo, hii tofauti ya shilingi 500 mkulima akawa amekula hasara lakini hapa sasa Serikali sijajua ilikuwa na utaratibu gani wa kuweza kuhakikisha kwamba inawapa fidia wafanyabiashara hawa amba walikuwa wanunuwa pamba kwa wakulima lakini haohao waliofidiwa hawakuweza kuifikisha hiyo fidia kwa mkulima ambaye ni mlengwa. Tuombe sasa kwa wakati huu ambapo Serikali inatoa kipaumbele katika suala zima la kilimo basi iwatazame pia hao wakulima na kuona kwamba wakati mwingine isihakikishe wafanyakazi peke yake ndiyo wanaolindwa, mkulima anakuwa ni mtu wa kuzalisha tu. Wakulima hawa ndiyo wanaotusa idia na hata sasa hivi wako kule wakishughulika ili kusudi Taifa hili liendelee kuwepo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naitwa Salvatory Machemli, nikiwa na maana chemli ndogondogo halafu zikiwa nyingi inakuwa machemli, ni mwanga wa Ukerewe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nianze tu kumshukuru Jemedari na Kamanda wetu Dkt. Willibrod Slaa, kwa kazi kubwa aliyoifanya mpaka leo CHADEMA tuna Wabunge wengi wa kutosha na mashine za kazi. Vilevile pia nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kuwakilisha bajeti nzuri ya Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa nimetoa shukrani, mimi kwa ujumla nasema siungi mkono hoja. Kwa nini siungi mkono hoja? Jana nimewasilisha swali langu linalohusiana na tatizo la maji. Wabunge wengi kilio chetu kimekuwa ni maji ikiwemo na Ukerewe inayozungukwa na maji kwa asilimia 90. Leo mnatuambia tuunge mkono hoja tena kwa vigelegele binafsi, siungi mkono hoja. Siungi mkono hoja kwa sababu Wilaya ya Ukerewe na Jimbo la Ukerewe kwa ujumla lilijaliwa kuwa na pampu za kusukuma maji zilizowekwa na Awamu ya Kwanza chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Tuna pampu zaidi ya tisa au kumi. Katika Mji wa Nansio, kuna pampu ya kusukuma maji. Kijiji cha tatu kutoka Nansio, kijiji cha Chabilungo kina pampu ya kusukuma maji. Kijiji cha tatu tena kutoka pale, kijiji cha Ihebo kina pampu ya kusukuma maji. Kijiji cha tatu tena kutoka pale, kijiji cha Bukonyo kina pampu ya kusukuma maji. Kijiji cha tano kutoka pale, kijiji cha Bugolola kina pampu ya kusukuma maji. Kijiji cha saba, kijiji cha Bukindo kina pampu ya kusukuma maji na Kisiwa cha Ukara maeneo ya Bwisha kuna pampu ya kusukuma maji na cha kushangaza zaidi

kwenye Kisiwa kidogo kuliko vyote Kisiwa cha Irugwa vilevile kina pampu ya kusukuma maji. Leo Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kuziimarisha zile pampu kuwaondolea Wakerewe tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, nimeuliza kuhusu suala hilo badala ya kujibiwa ni lini Serikali ya Awamu ya Nne ina mpango wa kuondoa tatizo la maji, naambiya tunachimbiwa visima vya maji Ukerewe, inatuingia akilini? Sikuisoma hiyo ndiyo maana naona sasa huu ni muujiiza ndani ya miaka 50 kwenye eneo lililojaliwa pampu za kusukuma maji kama Ukerewe leo maji yanakuwa ni hadithi. Ndiyo maana ya mimi kutounga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nikiachana na tatizo la maji ambalo limekuwa ni kilio cha watu wengi na Wabunge wengi akiwemo na Mbunge wa Ilemela jirani yangu ambaye naye anazungukwa na Ziwa Victoria naye anapiga kelele kuhusu maji, Wabunge nao wamelia kilio hicho kwamba maji wengine ni maziwa siyo maji lakini siyo maziwa yaliyoboreshw, ni maji ambayo yanafanana na maziwa, hatujui sasa ubora wake.

Mheshimiwa Spika, nikiachana na tatizo hilo, Serikali ya Awamu ya Nne imekuja na mikakati mingi, mara kilimo ni Utu wa Mgongo, mara Kilimo Kwanza lakini kwa ujumla mimi nasema kwamba hizi ni hadithi za kusadikika. Kwangu haiguswi kabisa na mkakati wa kilimo Kwanza kwa sababu kule hatuna zao la biashara. Kule mkakati mnaoleta sijui MKUKUTA II, MKUKUTA III, Ukerewe haiguswi. Ndiyo maana nasema kwamba mimi MKUKUTA kwangu ni hadithi. Serikali inanyamaza kabisa haiwafikirii wananchi wa Jimbo lile kwamba watapata zao gani mbadala ili waweze kuishi. Sasa hivi wananchi wale wanaishi kwa kutegemea Ziwa Victoria, wavuvi wadogowadogo lakini kwa sababu hatuwaonei huruma, wale wavuvi wadogowadogo wenyewe wanachomewa nyavu zao tena kwa mateke, magumi na risasi mgongoni, inasikitisha sana.

### **WABUNGE FULANI: Mmh!**

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Nimesema suala la risasi, nimesikia wenzangu wanaguna. Ukienda kule, siku moja tembelea Kisiwa cha Ukerewe, kuna majambazi yanatoka katika nchi jirani ya Kenya, Uganda na Somalia. Wao wakikutana na wavuvi katika Jimbo lile, wanawaambia mseme moja kwamba kamata lugala. Maana ya kukamata lugala ni kwamba sasa ushike kwenye kingo za mtumbwi halafu wanakata mikono. Hawa ndiyo Wakerewe ambao wamesaulika katika Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, Ukerewe ilikuwa imejaliwa wakati tunalima pamba enzi hizo, tukawa na mashine ya kusindika mafuta ya pamba yanayotokana na mbegu lakini sijui Awamu ya Nne inafikiria nini kuhusu mashine ile, imekaa *idle*. Kuna sehemu zingine wanapolima pamba wanashindwa kuja hata kuwasaidia au waibadilishe matumizi basi kama kuna uwezekano kwa kuwa tuna matunda ya kutosha Ukerewe basi ibadilishiwe matumizi yake iwe mashine ya kusindika matunda ili watu waweze kuza matunda yao.

Mheshimiwa Spika, njaa. Tumesikia takwimu za Waziri wa Chakula na Ushirika, akatuambia kwamba wana tani zaidi ya 10,000 na kitu kwenye maghala ya chakula. Hivi kuna *process* gani zinazotumika kutoa chakula kwenye maghala ya chakula kuwafikia wananchi wa kawaida wakiwemo wananchi wa Ukerewe? Kumekuwa ni *formality* tu za kuwa tunesema kwamba chakula kipo, Serikali ina chakula cha ziada, mbona hakitoki? Au mtupe *style* ya kujua kwamba sasa tutumie *style* gani ili muweze kusikia kwamba wananchi kule wanakuwa na njaa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania kwa asilimia 70 wanakula mlo mmoja wakiwemo wananchi wa Ukerewe lakini Serikali inapiga kelele inasema kwamba ina chakula cha ziada kwenye ghala la chakula. Ukiangalia wakifunua tu hivi, unakuta magunia yamepangana, unasubiri yaende wapi? Waziri wa Chakula, tunaomba sasa zisiwe hadithi za mapokeo, tunaomba chakula hicho kiwafikie wananchi kwa muda muafaka ili wasife na njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi wakati tunasomewa bajeti, tulisikia kwamba kuna tozo ya adhabu za barabarani *traffic notification*. Nasikitika sijui ni bajeti gani imepitisha hii, watu wameanza kukamatwa barabarani wanadaiwa laki tatu mpaka elfu hamsini. Hebu niambieni ni bajeti ipi imepita na Bunge lipi limepitisha mpaka leo Askari waanze kuifanyia kazi? Mimi napenda nisikubaliane na adhabu hii, ina *element* fulani za rushwa, tunawatengezea watu chakula, tunawatengezea ma-*traffic* chakula kwamba huna shilingi laki tatu, nasema laki tatu kwa sababu ndizo zilizoandikwa, ingawa nasikia kuna marekebisho ya elfu hamsini, lakini mimi naongelea lile lililoandikwa pale ni laki tatu. Ukitosa laki tatu, Mheshimiwa Spika ukitoa hata laki moja atapokea, hatakuandikia barua, siyo rushwa hiyo? Kwa hiyo, napenda nisikubaliane na hili. Ni adhabu kubwa mno, hailingani na makosa yenyewe yalivyo.

Mheshimiwa Spika, tuangalie na barabara zetu zenyewe ndizo zinazosababisha magari yawe hivyo. Hakuna gari ambalo *Traffic* akilisimamisha lisikutwe na makosa zikiwepo barabara za Jimbo langu la Ukerewe. Kwa muda wa miaka 20-25, kule greda wameiona awamu hii baada ya Machemli kuingia. Baada ya Machemli kuingia ndiyo wameiona greda inakwenda kwenye Jimbo lile. Sasa niambie gari zilizopo kule zina hali gani? Juji *SUMATRA* wamekwenda kule wanakamata magari, gari moja wanatoza shilingi laki mbili na nusu kwa barabara zenyе mabonde utafikiri bonde la ufa zilizopo Ukerewe, ni kuwaonea wananchi.

Mheshimiwa Spika, hizi barabara haziko Ukerewe peke yake. Hizi barabara ziko Ukerewe na maeneo mengi ya Tanzania ingawa Wabunge wenzangu hamtaki kukubali lakini mnayo mashimo. Wizara ya Ujenzi imeomba zaidi ya shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya Wizara yake wanaomba zipitishwe, nilipomuuliza Waziri wa Ujenzi kwamba katika hii shilingi trilioni 1.3 barabara ya kuanzia Bunda – Kisorya - Rugezi mpaka Masonga imo? Akaniambia haimo, kwa sababu hiyo siyo *trunk road*. Aaaah! Yaani bajeti yote hiyo barabara za Mkoani zinakosekana? Pesa zinakwenda wapi Mheshimiwa Spika zaidi ya shilingi trilioni 1.3 ziende kwenye Wizara moja halafu barabara za Mkoani zisiwemo! Hizi ni hadithi za mapokeo. Tuna *trunk road* ngapi ambazo kama zitaidhinishiwa shilingi trilioni 1.3 na barabara za Mikoa zisiguswe halafu tutazijadili lini barabara za Mkoani?

Mheshimiwa Spika...

## T A A R I F A

**ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Taarifa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68. Napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge aliyejikuwa anazungumza juu ya barabara aliyoitaja ya kutoka Bunda - Kisyla hadi Nansio ambayo ni kilomita 93. Kwanza iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba ni *trunk road*. Pili, iko katika hatua ambazo walishamaliza upembuzi yakinifu kwa kujengwa kwa kiwango cha lami na kwamba barabara hiyo japo mwenzangu hakuwepo Kisyla pale kwa sababu ndiyo Jimbo la Mwibara, Mheshimiwa Rais alisema kwamba barabara hii ni ya kiuchumi na itajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, asiseme kwamba hiyo barabara haimo kwenye mipango na kwamba hata siyo *trunk road*. Kwa hiyo, naomba nimpe hiyo taarifa na kwamba asije akawakatisha tamaa wananchi wa Mwibara ambao wanaamini safari hii itajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Habari njema.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba tu nisikubaliane na taarifa yake. Mimi ni Waziri Kivuli wa Ujenzi, kwa hiyo, *data* ninazotoa nina uhakika nazo, nimeshazifanyia uchunguzi wa kina. Ni kwamba barabara ya Bunda - Mwibara kuja Kisyla – Rugezi - Nansio mpaka Masonga, haimo kwenye Ilani ya Uchaguzi na kwenye bajeti ya 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ni ahadi ya Mheshimiwa Rais lakini si ya leo wala ya kesho. Mimi ni Waziri Kivuli, nimemwuliza Waziri Magufuli aniambie kama barabara imo kwenye bajeti yake, akasema haimo kwa sababu siyo *trunk road* ni barabara ya Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Tunapokwenda katika hali kama hii ndiyo maana leo mashirika yote ya umma yanapotea na Watanzania tukihoji tunaonekana tunapiga kelele za bure lakini tunasema kelele hizi siyo kelele za chura ambazo hazimzui ng'ombe kunywa maji ni kelele za ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iko wapi *TRA* iko wapi *ATC*, leo tunaposema sisi tunaonekana tunapiga mayowe. Tunapiga mayowe lakini hata wale wanaopingana na sisi wanakubaliana kwa dhati kabisa kwamba hata wao adhabu hii inawatafunu. Inawatafunu kama inavyotaka kumtafunu Mbunge wa Mwibara kwa kudanganya umma kwamba barabara ipo kwenye Ilani wakati haimo, adhabu itamtafunu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zinasema mnapochangia usimtaje Mbunge, Spika, Rais, wewe endelea kuchangia tu.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na madini. Tumepewa hazina kubwa sana Tanzania. Kila sehemu unapozunguka Tanzania hii huenda na Ukerewe ikiwemo, ukichimba tu utakutana na madini. Cha ajabu ni sawa na watoto waliokaa chini ya mwembe wenye matunda yaliyoiva lakini waanguaji hawaachi hata chembe inayodondoka chini, ndiyo madini yetu yalivyo Tanzania. Inasikitisha hata wale waliotaka kuokota lile alilosahau yule anayeangua, wanachapwa bakora. Wako wapi ndugu zangu wa Nyamongo ambaowalikuwa wanaishi kwa kutegemea madini tena kwa kuchimba kwa mkono, leo wamekula bakora. Wako wapi ndugu zetu wa Buzwagi, wameambiwa watoke maeneo yale. Basi mikataba ile ilenge kumnusuru mwananchi wa Tanzania na maisha mabovu walijonayo kuliko kila siku tuna mlolongo wa machimbo, wanakuja wawekezaji wanachukua, wanaweka, waah, kama zilivyo nyimbo za Chama cha Mapinduzi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wanatuachia mashimo, miaka 50 ya uhuru tunapiga *mark time*, yale mashimo yasije kuwa makaburi ya kutuzika baadaye, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Kengele ya pili?

**SPIKA:** Kengele ya pili, ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Regia Mtema, nadhani yeeye atakuwa wa mwisho.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti ya mwaka 2011/2012, nilikata tamaa lakini kumbe nimepata nafasi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mhashamu Baba Askofu wa Jimbo Kuu la Mahenge, Agapiti Ndorobo na uongozi wa Kanisa Katoliki Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuwa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba, ndani ya Wilaya ya Kilombero ambacho tumekizindua tarehe 12 mwezi huu. Wilaya ya Kilombero imekuwa ni Wilaya ya kwanza Tanzania kupata Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba, nje ya Makao Makuu ya Mkao. Ni fursa Wilayani kwetu na ni fursa vilevile kwa wananchi wa Mkao wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye kujadili bajeti yetu. La kwanza kabisa ambalo napenda nilizungumzie siku ya leo linahusiana na tofauti ya kipato. Kwa mujibu wa Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Binadamu ya Mwaka 2009, tunaambiwa kuna mahusiano ya karibu kabisa kati ya umaskini, ukuaji wa uchumi na tofauti ya kipato. Takwimu hizohizo zinaonesha kwamba Tanzania leo hii, tofauti ya kipato ni 35%; ni tofauti kubwa sana, ndio maana leo hii

wakati kuna watu wana-*surplus* ya *billions of money* kwenye akaunti zao, kuna mwananchi mwingine wa kijiji anakula mlo mmoja au anakula milo miwili au anapata milo mitatu lakini anakula tu ilimradi amekula lakini milo hii sio milo kamili. Wakati leo hii kuna Mtanzania ambaye ana mabilioni ya shilingi kwenye akaunti mpaka nje ya nchi, kuna Watanzania wengine wameshindwa kufanya mitihani kwa kukosa michango ya mitihani. Kuna Watanzania wengine wamekosa huduma muhimu za afya kwa kukosa hela ndogo ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, bajeti hii haijalenga katika kutatua tatizo hili. Ni lazima kama Taifa, tuhakikishe tunapunguza hii asilimia ya utofauti wa kipato, 35% ni kubwa sana. Ni lazima kama Taifa tuwe na uthubutu. Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, alikuwa na uthubutu. Alihakikisha kwamba Tanzania tunasimamia Sera yetu ya Ujamaa ili kusiwe na utofauti wa kipato kati ya Watanzania. Ni lazima kama Taifa katika hali ya sasa, tuweze ku-*control* matajiri wasiendelee kuwa matajiri kupita kiasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu ya sasa hivi, pamoja na kwamba tunaambiwa lengo ni kukuza uchumi na kuhakikisha Mtanzania maskini anakomboka, lakini kiuhalisia, matajiri wataendelea kuwa matajiri. Wafanyabiashara wakubwa wataendelea kuwekeza, wataendelea kuwa matajiri na yule Mtanzania mdogo maskini wa chini, atajikwamua kidogo sana kuhakikisha tu anapata milo mitatu, lakini hatakuwa na *surplus* ya kuweza labda kusomesha watoto wake vizuri. Ndio maana kuna Watanzania wengi leo wanemosha watoto wao kwa kubangaiza, kwa kuombaomba, kwa taabu ili waweze kusomesha watoto wao. Ninapendekeza kama Taifa, ni lazima tuangalie tulipokosea, ni lazima tu-*control*, tuachane na huu uchumi holela, ili Watanzania wa chini na wenyewe tuweze kujikwamua na tofauti ya kipato ya 35% iweze kupungua.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nilipenda kulizungumzia ni suala zima la ajira. Sote tunatambua kwamba nchi yetu ina tatizo kubwa la ajira na takwimu za Mheshimiwa Mkulo, zinatuambia kabisa kwamba, Watanzania milioni 2.2 hawako kwenye ajira lakini ukisoma mkakati wa Mheshimiwa Mkulo, Serikali yetu miaka miwili ijayo imewekeza katika kupanua ajira lakini bado tunatumia mikakati ya kizamani.

**SPIKA:** Sema Mkakati wa Waziri wa Fedha.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Waziri wa Fedha, ndio! Kwenye hotuba yake ameelezea kupanua ajira, lakini karibu ajira zote zimejikita kwenye kilimo, zimejikita kwenye viwanda ambavyo vinashughulika na mazao ya kilimo matokeo yake katika kuongeza huko ajira, kunawalenga wananchi wadogowadogo lakini ikumbukwe kwamba tunao wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu na takwimu zinaonesha kwamba takribani Watanzania 760,000 wanaingia kwenye soko la ajira na wanaopata kazi ni 40,000 peke yao. Sasa mimi ninajiuliza, Mkakati wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambao umewekeza kwenye Kilimo na Viwanda vidogovidogo kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali wadogowadogo, kwa ajili ya kuwasaidia hawa wakulima wadogowadogo, je, hawa wanafunzi wanaomaliza Vyuo Vikuu, wanapelekwa wapi?

Mheshimiwa Spika, kuna mmoja amependekeza kwamba wapewe na wenyewe mikopo ili waweze kufanya shughuli za ujasiriamali, shughuli za kujajiri wenyewe lakini swalii linakuja, *are they ready?* Je, tumewaandaa wawe tayari wakimaliza Vyuo Vikuu wajiajiri? Bado hata ukiangalia mkakati wenyewe wa Serikali, katika kutoa mikopo wanapata mikopo midogomidogo, je, mtu aliyesoma *Sociology*, mtu aliyesoma *Human Nutrition* kutoka SUA, yuko tayari kujajiri kwa kutumia mikopo wa shilingi 300,000/=? Inaonekana kwamba, sio uhalisia. Kwa hiyo, bajeti hii ni lazima ijikite katika kusaidia pia wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanaomaliza, tunawapeleka wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile bado hata huku ambako bajeti hii inaonesha kwamba itakuza ajira kwenye viwanda pamoja na wakulima wadogowadogo, kuna changamoto kubwa. Leo hii tunesikia wafanyakazi wa viwandani wana malalamiko makubwa, wanaajiriwa kama vibarua, wanafanya kazi saa nyingi, kinyume na Sheria za Kazi, wanalipwa mishahara duni, wanafanya kazi katika mazingira magumu, je, Serikali imechukua hatua gani? Sio tunasema tu tunahakikisha kwamba wajasiriamali wadogowadogo na kwenye viwanda wananchi wanakwenda kuajiriwa huko, lakini je, tumewajengea mazingira ili wafanye kazi kwa moyo, vizuri na waweze kufaidika na kile ambacho wanakifanya?

Mheshimiwa Spika, leo hii tumeona wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, wanalamika, leo hii tunesikia wafanyakazi wa Kiwanda cha *Jambo Plastick* cha Dar-es-Salaam wanalamika. Ni lazima kama Taifa, kama Serikali tuangalie upya badala ya kuendelea kutaka kuwekeza huko, tuangalie tatizo liko wapi? Kuna tatizo kubwa la wawekezaji wa nje kuwanyanya Watanzania kwenye maeneo wanayofanyia kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumza ni kuhusiana na wenzangu wenyе ulemavu. Wakati nachangia Mpango, nilizungumzia masuala ya takwimu, lakini leo naomba nijikite kwenye kipengele kimoja tu kinachohusiana na masuala ya elimu. Natambua umuhimu wa elimu na elimu ndio silaha pekee ambayo inaweza kumkomboa mwenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, leo nazungumza hapa nikiwa najiamini, ni kwa sababu elimu imenikomboa, nilipata bahati ya kupata elimu, imeweza kunisaidia nimefika hapa. Kwa hiyo, elimu kwa watu wenyе ulemavu bado imekuwa ni changamoto kubwa. Imekuwa ni tatizo kulingana na mazingira ya shule zetu hasa wa vijijini, shule ziko mbali, shule hazina mazingira rafiki. Serikali imejitahidi, imejenga shule za Kata karibu kwenye kila Kata, lakini shule hizi hazina mazingira rafiki kwa watu wenyе ulemavu. Kwa hiyo, bado ni changamoto kwa watu wenyе ulemavu. Pamoja na wingi wa shule hizi, sio wote ambao wataweza kusoma kwenye shule hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vilevile shule hizi hazina *qualified training Teachers* ambao wamesomea masuala mazima ya watu wenyе ulemavu. Bado ni changamoto kama Taifa na kama Taifa ni lazima tuwekeze kwenye kupata Walimu wa kutosha ili waweze kufundisha kwenye shule hizi na watu wenyе ulemavu waweze kusoma kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile vifaa vya kujifunzia na kufundishia bado havitoshi. Natambua Serikali kwa dhamira njema imetenga 20,000/= mpaka 25,000/= kwa ajili ya kusaidia wenyewe ulemavu, lakini bado ni changamoto. Bado hazitoshi kwa kuwa, vifaa vya watu wenyewe ulemavu vina gharama kubwa. Leo hii, mimi natembelea gongo moja, gongo moja linauzwa shilingi 20,000=/. Mimi naweza ku-*afford* kununua lakini wapo wengine ambao hawawezi kununua gongo kwa shilingi 20,000=/. Wapo wengine ambao wanatumia *wheel chairs*, ambazo ni bei kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mtoa hoja, afikirie kwa mapana yake kuhusiana na masuala haya ya watu wenyewe ulemavu ili tuweze kupata elimu. Hii ndio njia pekee ambayo itaweza kutukomboa, kama tukipata elimu hamtatuona barabarani tukiomba wala hamtatuona popote tukiwa tunahangaika na masuala hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine, naomba nirudi Wilayani Kilombero, ni suala zima la umeme. Nafurahi kwamba Serikali imeweka kipaumbele safari hii kwenye suala la umeme na natambua kwamba mnapoweka kipaumbele kwenye umeme, basi yale maeneo ambayo ni wazalishaji wa umeme na yenye yapewe kipaumbele katika kupata umeme. Wilayani kwetu Kilombero, kuna migodi miwili ya kuzalisha umeme, tuna Kihansi na Kidatu, lakini inasikitisha watu wanaopata umeme Wilayani Kilombero ni chini ya 1% peke yake, karibu shule zote, karibu zahanati zote hazina umeme, haiingii akilini! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *it is very unfair* kwamba, sisi tuzalishe umeme halafu kwenye maeneo muhimu ya kupata huduma, mama mjamzito anakwenda na kibatali kwenye zahanati, wakati kuna wengine hawazalishi umeme, wana umeme mpaka kwenye *swimming pools!* Tunaomba Serikali iliangalie hili kwa mapana yake ndani ya mwaka huu wa bajeti tuhakikishe Wilaya ya Kilombero inapata umeme kwenye maeneo mengi na hasa maeneo nyeti.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusiana na Wilaya ya Kilombero na napenda nitoe taarifa kwa Bunge lako Tukufu, kwamba Wilaya yetu ilikumbwa na mafuriko katika Kata za Bafu, Mbingu, Idete pamoja na Mgeta. Mpaka hivi leo, kuna watu wanaishi kwenye makambi, hawana chakula, wanalala vibaya, naomba nitoe ombi maalum kama utaona inafaa ili tuweze kama Wabunge kuwachangia watu waliopatwa na maafa haya ili waondokane na suala la njaa na suala zima la kupata malazi kama wanadamu wengine ambavyo wanastahili kupata.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuzungumzia, bado nalia na bei ya sukari. Wilayani kwetu Kilombero, tunazalisha sukari nyote mnafahamu, nafurahi Serikali ililiona hilo na ikaonesha nia, baadhi ya maeneo bei ya sukari imeshuka, lakini bado kuna maeneo bei ya sukari haijashuka. Naomba liangaliwe hili kwa mapana yake, nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Regia.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (URATIBU, SERA NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (URATIBU, SERA NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Taarifa ya ufahamisho tu Dada yangu huyo, nampenda.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu nimfahamishe kutokana na mafuriko haya yaliyotokea Kilombero, Serikali imeshawapa pole wananchi akiwemo Mheshimiwa Mbunge. Serikali, ilisha-*respond*, tumepeleka tani 239 za mahindi na tulijua kwamba hawawezi kusafirisha, tukapeleka shilingi 32,982,000/= kwa ajili ya kusafirishia lakini pia tumepeleka shilingi 60,000,000/= kwa ajili ya kununulia maharagwe tani 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile tumepeleka shilingi 66,000,000/= kwa ajili ya kununulia mafuta ya kupikia. Tumepeleka shilingi 1,400,000/= kwa ajili ya kununulia chumvi kilo 1,400. Tumepeleka shilingi 46,000,000/= kwa ajili ya kununulia sukari kilo 23,000. Tumepeleka shilingi 210,000,000/= kwa ajili ya matengenezo ya madaraja sita kama walivyoomba na tumepeleka shilingi 340,000,000/= kwa ajili ya matengenezo ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliomba wenyewe na tulipeleka kama walivyoomba kwa 100%. Nilikuwa nataka kutoa taarifa hiyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmefurahia kwamba hamtakiwi kuchanga! (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tukirudi saa 11:00 wataanza Manaibu Waziri, kujibu baadhi ya hoja halafu atahitimisha Mheshimiwa Waziri. Kama nilivyosema, naomba wote mje, hata kama afya sio njema sana lakini kwa shughuli hii uje kusudi tuweze kukamilisha suala hili. (*Kicheko*)

Wiki hii yote mmeona Naibu Spika, hayupo, Naibu Spika, amepelekwa safari Uingereza pamoja na Wabunge wengine watatu, watarudi baada ya wiki ijayo.

Mheshimiwa Anne Kilango, yeye hayupo toka mwanzo hapa, Mzee Samuel Malecela, amepata *operation* kubwa ya moyo.

Tuna mwenzetu Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, ameondoka leo, kafiwa na kaka yake huko Pemba. Kwa hiyo, hawa ni watu ambao najua hawapo kwa sababu hizo.

Waheshimiwa Wabunge, pia nina tangazo lingine. Katibu wa Wabunge wa *CHADEMA*, Mheshimiwa Mnyika, ameniomba niwatangazie Wabunge wa *CHADEMA* kuwa leo hii tarehe 21, saa 10.00 alasiri, kutakuwa na kikao katika jengo la Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Mimi sina matangazo mengine, nasisitiza Waheshimiwa Wabunge kuja katika suala moja kubwa katika kazi yetu na ni la Kikatiba, ni hili la kupitisha bajeti. Usije ukasema aah, nitafika au nitafanya nini, maana inawezekana kabisa huko uliko huko, ukaona sio jambo muhimu, nawaombeni wote mfike, ahsante.

Baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.55 mchana, Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri walioifanya ya kuandaa bajeti nzuri ambayo imerudisha matumaini mapya kwa wananchi wetu hasa wale wa kada ya chini.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya mwaka 2011/2012, imezingatia vipaumbele vitano kama viliyvoainishwa katika ukurasa wa tano (5) katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambavyo ni (i) Umeme; (ii) Maji; (iii) Miundombinu ya usafirishajji (reli, bandari, barabara, viwanja vya ndege, mkongo wa Taifa; (iv) Kilimo na umwagiliaji; na (v) kupanua ajira kwa sekta binafsi na ya umma.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na vipaumbele kwani ni vizuri na kama vitatekelezwa kama ilivyokusudiwa tutakuwa tumepiga hatua moja mbele kutoka tulipo sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya utangulizi, sasa napenda kuelekeza mchango wangu kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu mfumo wa Bajeti. Mfumo wa bajeti na uandaaji wake una matatizo ya kimsingi. Ili kusimamia sera za uchumi mpanga Serikali inatekeleza mpango wa uchumi ambao imekubaliana na *IMF*. Mpango huu pamoja na mambo mengine una malengo yanayopimika ikiwa ni pamoja na fedha ambayo Serikali itakopa toka katika mabenki. Ili programu ya *IMF* ikamilike Serikali inakubalina na shirika hili mfumo wa bajeti ambao una tofauti na mfumo wa bajeti unaotewa kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka wa fedha 2010/2011, bajeti iliyoletwa Bungeni na kupitishwa ilikadiriwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo jumla ya Shilingi Trilioni 11.6 lakini katika programu ya *IMF* Serikali

ilipanga kutumia Trilioni 10.1 tofauti ya 1.5 na Shilingi Trilioni 10.4 kuwa matumizi yanayotarajiwa na Serikali ambayo yanakaribiana na program ya *IMF* kuliko bajeti iliyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha Serikali imeleta bajeti ya Shilingi Trilioni 13.53 lakini katika programu ambayo Serikali imekubaliana na *IMF* matumizi yote katika mwaka wa fedha 2011/2012, ni Shilingi Trilioni 11.26 tofauti ya Shilingi Trilioni 2.27 na kwa hali hii lazima Serikali itatekeleza mfumo wa bajeti uliokubaliwa na *IMF*.

Mheshimiwa Spika, pia katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali inaonesha matarajio ya kukusanya Shilingi Trilioni 7.126 mapato ya ndani na *IMF* inaonesha Shilingi Trilioni 6.397. Hivyo, Serikali itahakikisha kuwa programu ya *IMF* inatekelezwa kwa kutumia mfumo wa kuhusu matumizi kwa kadri ya mapato yaliyopo yaani *Cash Budget*. Hivyo, bajeti inayopitishwa na Bunge na hasa ya maendeleo haiheshimiwi, huku ni kulidhalilisha Bunge, kuliletea makadirio ya mapato na matumizi ambayo Serikali inajua haitayazingatia ukilinganisha na program ya *IMF* ya *Policy Support Instrument*.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia juu ya ukusanyaji wa mapato na misamaha ya kodi. Misamaha holela ya kodi inapunguza mapato ya Serikali. Utafiti unaonesha kuwa misamaha hii inalipotezea Taifa wastani wa asilimia sita ya pato la Taifa sawa na Shilingi Trilioni 2.1 kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011. Kwa mfano, nchi yetu ya Tanzania inauza dhahabu nchi za nje yenye thamani ya zaidi ya dola bilioni 1.5 lakini Serikali inapata mrahaba wa dola milioni 45 tu. Zaidi ya hapo makampuni yanaidai Serikali mabilioni ya shilingi iyazidishie kodi walizolipa katika uagizaji wa mafuta ya Petroli.

Mheshimiwa Spika, tunaachiwa mashimo mali yote inakwenda nje. Sasa wakati umefika wa kuchukua hatua za kimapinduzi ya au za kuyatoza makampuni kodi ya maliasili (*Resource tax*) ya asilimia ishirini mpaka thelathini ili angalau Serikali na Watanzania tunufaika na mali asili yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza kueleza kuwa sina tatizo na vipaumbele vya bajeti, kama kweli Serikali itaamua kwa makusudi kusimamia vizuri utekelezaji wa mambo tuliyoyaainisha basi nasi Watanzania tutatoka katika hali ya maisha tuliyonayo sasa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kueleza maoni yangu. Naomba kuwasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara, Waziri, Wataalam na Serikali kwa kuleta bajeti nzuri inayomjali na kumsaidia Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, pili, mkakati wa kukusanya mapato na kuongeza wigo uimarishwe na mianya ya kupoteza mapato izibwe.

Mheshimiwa Spika, tatu, misamaha ya kodi ifanyiwe ukarabati na ishushwe kufikia asilimia moja ya makusanyo. Hii itatoa nafasi kwa Serikali kuongeza mapato yake na kuongeza uwezo wa kugharamia maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nne, Sekta ya Mifugo na Uvuvi ipatiwe fedha zaidi ili fedha iliyotengwa ionyeshe kuwa mifugo na uvuvi vimo kwenye kipaumbele kama Mpango unavyotaja.

Mheshimiwa Spika, jitihada zifanyike za kutolewa fedha ili shughuli zilizotengewa fedha husika zifanyike kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa bajeti katika ngazi ya Halmashauri viwekewe mkazo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu itazamwe na mwongozo, taratibu, usimamizi na utendaji bora wa kazi vikazaniwe ili kuleta tija na kupunguza malalamiko ya wanafunzi vyuoni.

Mheshimiwa Spika, vifungashio vya maziwa vinavyoagizwa kutoka nje ya Afrika Mashariki viondolewe kodi na tozo viwe (*zero rating*) ili kukuza uzalishaji na uuzaaji wa maziwa yaliyosindikwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, muda wangu wa kuchangia haukutosha, hivyo naona nichangie kwa maandishi.

Mheshimiwa Waziri bajeti yako ni nzuri na imeandaliwa kitaalamu. Tatizo kubwa siku zote ni utekelezaji wa mikakati iliyowekwa. Naomba Wizara yako isimamie kikamilifu *TRA* pamoja na Taasisi zingine zinazoshughulikia makusanyo ya mapato. Wizara ya TAMISEMI izisimamie Halmashauri zote katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia muda haukutosha kuzungumzia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kupunguza utegemezi wa bajeti na kufikia asilimia kumi ifikapo 2015. Naomba tuziige nchi za China, Singapore, Malaysia, South Korea na Hong Kong ambazo hazikuendelea kwa kutegemea misaada bali kwa kuwekeza zaidi hasa kwa kutumia utaratibu wa *FDI* pamoja na kuuza nje zaidi (*Emphasis on Exports*).

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeza Serikali kwa kutambua tena umuhimu wa kuwa na *Industrial Base* kuwa na viwanda mama na viwanda mbalimbali. Nakumbuka viwanda vyetu vya nguo vilivyokufa *Mwatex*, *Kiltex*, *Sunguratex*, *Urafiki*, *Mutex*, *Morogoro Textiles*, viwanda hivyo vifufuliwe.

Mheshimiwa Spika, tatu, bajeti inazungumzia umuhimu wa umeme katika kuchochea ukuaji wa uchumi. Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Ngara haina umeme ingawa Ngara ina maporomoko makubwa ya maji yajulikanayo kama Rusumo *Falls*. Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo *Falls* ni mradi wa nchi tatu Tanzania, Rwanda na Burundi. Ni mradi wa siku nyingi. Ombi langu kwa Serikali ni kuharakisha utekelezaji wa mradi huo kwa kushirikiana na hizo nchi mbili ili Wilaya ya Ngara na Wilaya ya Biharamulo tuweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, nne, mradi wa Kabanga *Nickel* ambao uko Ngara unahitaji umeme wa *Megawatt* 45. Mgodi huu ni mkubwa sana na ni wa pili duniani baada ya ule wa Canada. Ombi kwa Serikali ni kuiwezesha *TANESCO* iweze kuipatia umeme Kabanga *Nickel*. *Megawatt* 10 zinaweza kutoka mradi wa Rusumo *Falls*. Mradi huu ni muhimu sana ni vizuri kwa Serikali kuipatia umeme kabla ya wawekezaji (*Barrick*) hawajakata tamaa.

Mheshimiwa Spika, tano, mradi wa Kabanga *Nickel* unahitaji pia Reli ya Isaka kwenda Rwanda na Burundi. *Branch* ya Reli ya kwenda Burundi (Msongati) ndiyo itakayopita Kabanga *Nickel*. Naishauri Serikali iharakishe ujenzi wa Reli hii kwa sababu mradi huu ni mkubwa sana na ni muhimu kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, sita, sekta ya Elimu na Afya siyo vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, lugha inayotumika ni “kuendelea kulinda mafanikio yaliyokwishapatikana katika elimu na afya”. Nionavyo mimi, bado tuna changamoto nyingi katika sekta hizo mbili za elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, kwenye elimu bado walimu hawatoshi, vitabu ni matatizo, walimu wa Sayansi ni tatizo kubwa, walimu wengi hawana nyumba, hosteli kwa wasichana ni tatizo. Walimu hawatoshi kiidadi na kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, Mpango wa MMAM bado utekelezaji wake unaendelea. Kwa mfano, wakati Mpango wa MMAM unazungumzia ujenzi wa Zahanati kila Kijiji na Kituo cha Afya, kila Kata katika Jimbo au Wilaya ya Ngara kuna Kata 20 lakini Vituo vya Afya ni vinne tu na wakati Ngara ina Vijiji 72 tunazo Zahanati 43 tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Serikali kuvalia njuga mambo ambayo ni *Comparative Advantage* kwetu ukilinganisha na nchi zinazotuzunguka, mambo hayo ni Bandari iboreshwe, Maliasili, wanyama na misitu, Utalii na amani (*peace and Security*). Hizo ni *strengths*, zifuatazo ni *weaknesses*, bado hatuna wataalam wa kutosha, bado rushwa ni tatizo, hatuna umakini (*lack of seriousness and commitment*), tuna tatizo la kigugumizi cha kufanya maamuzi (*procrastination*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi hoja hii ya Mapato na Matumizi ya Serikali pamoja na Hali ya Uchumi wa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuweka vipaumbele ambavyo vinagusa kwa karibu zaidi maisha ya Watanzania walio wengi. Hakika vipaumbele hivi vikitekelezwa kikamilifu vitaongeza uchumi wa Taifa na kupunguza tofauti kubwa ya kipato mionganoni mwa Watanzania, kitu ambacho ndicho kilio kikubwa cha wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo kadhaa ya msingi katika utekelezaji wa bajeti hii tunahitaji rasilimali watu pamoja na mapato ya kutoka Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Inatia faraja kusikia kwamba Serikali imepanga kuwajengea uwezo Madiwani wa kusimamia Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwajengea uwezo kielimu, ningeshauri Serikali iangalie pia suala la maslahi ya Madiwani ili wasiweze kushawishiwa na wenye fedha na kukiuka misingi ya utendaji kazi wao. Maslahi haya ni pamoja na kukopeshwa vyombo vya usafiri, kuvezeshwa kupata mikopo ya benki, pia kuboresha posho ya mwezi. Ni vema Serikali ikatambua kuwa, pamoja na kwamba mapato ya Halmashauri ni kidogo lakini matumizi yake ni makubwa kiasi cha kuathiri maendeleo ya Taifa endapo matumizi haya hayatasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo hili la Serikali za mitaa tunadhani kwamba vyanzo vya mapato ni vichache. Lakini hata hivyo, utaratibu wa makusanyo unahitaji kuboreshwa zaidi ili kuepuka mianya ya upotevu. Kwa mfano, Mzabuni anaweza kupewa kazi ya ukusanyaji wa mapato katika eneo ambalo Halmashauri haijalifanya utafiti vizuri kujua mapato halisi yanayotarajiwa ni kiasi gani, hivyo Mzabuni anaweza kuwa akiwasilisha shilingi 2,000,000/= ambapo yeye pengine anakusanya shilingi 20,000,000/= kwa mwezi. Hivyo, naishauri Serikali ifuatilie kwa makini ni maeneo gani yanayolalamikiwa kimapato na iagize wataalam kufanya utafiti wa kiasi tarajiwa ili iweze kuzisaidia Halmashauri kuhusu vigezo vya kuwapa makampuni zabuni za ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuishauri Serikali ni kuhusu msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani. Serikali imetaja kupunguza kodi hii kwenye zana za kilimo pamoja na vifungashio vya *juice* na maziwa. Ni vema Serikali pia ikatamka vifungashio vya bidhaa zote za mazao ya chakula ya hapa nchini ili kuhamasisha uongezaji thamani wa mazao yetu yote ya chakula ikiwemo korosho. Vile vile hizo zana za kilimo ingebidi zioneshe kwamba ni tangu mazao hayajapandwa, kuvuna hadi usindikaji. Pendekezo hili linatokana na utata unaojitokeza kwa Maafisa wa Forodha wakati wa kulipia vifaa vya usindikaji vyakula kama vile *Vaccum Sealer* kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya chakula yasiharibike. Ukiwaeleza Maafisa hawa kwamba hiki kifaa ni zana ya kilimo hawalewi, wanachukua muda mrefu kuitia sheria bila mafanikio. Hivyo basi, zana za kilimo ni lazima zihusishe zile za kuhifadhi mazao na si kulimia tu kwani bila hifadhi bora ya mazao, kilimo hakina tija.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameahidi kwamba bajeti italinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta za elimu na afya pamoja na kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa. Hili ni jambo jema kabisa. Mafanikio ya elimu yanaonekana wazi katika ongezeko la idadi ya shule za Sekondari pamoja na idadi ya walimu walioko vyuoni. Lakini kama tunavyojua ipo changamoto kubwa ya kushuka kwa ufaulu wa wahitimu wa kidato cha nne. Moja ya sababu ni wanafunzi kufanya mitihani kwa baadhi ya masomo ambayo hawakujifunza hasa yale ya Sayansi kutokana na uhaba wa walimu na maabara. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali iharakishe ukamilishaji wa mkongo wa mawasiliano ili shule zisizo na walimu zipate mafunzo kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya bado lipo tatizo la baadhi ya wataalam wasio waadilifu katika Vituo vya Afya ambao hufanya hujuma kwa vifaa tiba hasa vile vya kujifungulia. Tatizo hili huchangia uchelewashaji wa akinamama kujifungua kwani wanapofika katika kituo cha afya huambiwa wakatafute kwanza vifaa. Hivyo, naishauri Serikali iharakishe uundaji wa Kamati ya Kitaifa kwa ajili ya ufuutiliaji wa afya ya Mama na Mtoto kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta Bajeti yenye kulenga kumkomboa Mtanzania. Ni Bajeti ya kila Mtanzania hadi walalahoi wanaipenda.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni nzuri kwa kuwa vipaumbele vikubwa ikiwemo Kilimo, Elimu, Afya. Maji, Miundombinu, Nishati na Madini vimezingatiwa katika Bajeti hii. Bajeti hii imejikita katika kilimo kwanza kwa maana ya kilimo na mifugo. Naiomba Serikali safari hii Serikali itilie mkazo wa kutosha katika ufugaji mkazo wa kutosha katika ufugaji na uvuvi. Bajeti hii haionyeshi nia thabiti ya kuwaendeleza wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Spika, shughuli ya ufugaji nchini humu inatakiwa izingatie mambo muhimu yafuatayo:-

Kwanza, ardhi, kama wote tujuavyo mfugaji yejote anahitaji ardhi ya kutosha. Wafugaji wengi hawana ardhi ya kutosha kwa ajili ya mifugo yao.

Pili, maji, Bajeti ilenge kuwapatia wafugaji maji ya kutosha. Malambo ya maji yajengwe kwenye maeneo ya wafugaji.

Tatu, madawa ya kuogesha mifugo, katika hili naipongeza Serikali kutoa dawa za ruzuku lakini zinaishia mikononi mwa wachache, hazifiki kwa wafugaji wa vijijini.

Nne, mikopo kwa ajili ya mifugo iwaendee hata wafugaji wa chini kwa maana ya walio kule vijijini, wasio na makampuni au ranchi.

Tano, soko la mazao ya mifugo ni muhimu. Katika hili Serikali lazima ijenge Viwanda vya Vyama, Maziwa na Ngozi. Wafugaji wa Tanzania hawana soko la mifugo yao, maziwa na ngozi. Nazidi kusisitiza Serikali iache utani katika suala la ufugaji, ufugaji ndio njia pekee ya kumkomboa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga Bajeti nzuri kwa sekta ya maji. Lakini ni kwa nini Serikali haipeleki miundombinu mikubwa ya maji mfano ule wa Mto Wami katika maeneo ya miinuko Jimboni na Wilayani Karagwe hata Mkoa mzima wa Kagera. Wilaya ya Karagwe inavyo vyanzo vingi vya maji kuanzia Mto kagera, Ziwa Rwakajunju, Ziwa Songambele na kadhalika lakini ajabu wananchi wa maeneno haya hawana maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo na umwagiliaji. Serikali ifanye juhudi za makusudi kuwapelekea wananchi wa Karagwe maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nimevutiwa na Serikali kuiongezea fedha Bodi ya Mikopo ya Vyuo Vikuu. Hapa namaanisha asilimia nne ya *Skills levy* kwenda vyuo vikuu. Ni hatua nzuri sana. Ombi langu, Serikali itoe mikopo kwa wanafunzi kwa wakati na bila ubaguzi wowote. Hatutaki kuona migomo ya vyuo vikuu na taasisi nyinginezo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kupiga vita ununuzi wa samani toka nje ya nchi, tuendelee kununua samani zilizotengenezwa hapa nchini kwa kutumia mbao zinazozalishwa hapa nchini ambazo ni nzuri na ngumu mfano mninga, mpodo, mkangazi na kadhalika. Sambamba na hili Serikali iache kununua nguzo za umeme kutoka nje ya nchi kwani nchi yetu tunayo miti mingi ya nguzo, ni kwa nini tusitumie miti hii kwa kuiongeza kipato kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, leseni za biashara, hili ni jambo zuri kwa Serikali kurudisha tozo ya leseni za biashara. Kodi ya leseni itaiiongezea Serikali mapato ya uhakika. Muhimu watendaji wasiwe na urasimu katika kutoza kodi ya leseni. *Notification* (faini ya *traffic* barabarani, kiwango kinachopendekezwa cha kutoka shilingi 20,000/= hadi 50,000/= ni kikubwa sana kitamuumiza mwananchi wa kawaida. Pia fedha faini za barabarani zisilipwe kwa Afisa wa Polisi wa barabarani na badala yake fedha hizo (faini) zilipwe *TRA*. Mtenda kosa apewe *notification* (tiketi) na muda wa kutosha ili akalipie *TRA*.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais ni amri, hivyo, Bajeti iziangalie na kuzifanya kazi ahadi za Mheshimiwa Rais, mfano, ahadi za umeme vijijini Jimboni Karagwe wa kutoka Begene–Rwabwere–Kiruruma hadi Nyakaiga na umeme wa Kayanga–Runyaga–Rwambaizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwanza upande wa ukusanyaji kodi yaani *TRA*. *TRA* ipewe wazo vitu vyote vinavyoingizwa toka nje bei za kulipia ushuru. Kama magari, vyombo, nguo, *spears* na kadhalika ili muagizaji ajuwe anapoagiza bidhaa fulani basi ajuwe ushuru wake kabla ya kuagiza. Kwa kufanya hivyo kutapunguza mianya ya rushwa na *TRA* itakusanya mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, pia *TRA* iwaorodheshe wafanyabiashara ndogo ndogo wote ili walipe kodi sababu wanamitaji mikubwa iliyofichikana. Wana uwezo wa kununua magari na kujenga nyumba kwa nini wasilipe kodi? Ili kuliongezea Taifa mapato? Pia *TRA* naiomba ifuatiliye kwa makini sana katika kampuni zote za uchimbaji madini kuhusu makato ya mishahara ya wafanyakazi, sina imani kama pesa hizo zote zinawasilishwa *TRA*. Iwapo zitakusanya basi pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, pia *TRA* iangalie upya misamaha ya kodi ni mingi sana hasa kwa wachimbaji wa madini hasa upande wa mafuta na vipuri pia kwa makampuni na Taasisi mbalimbali. Kwa kufanya hivyo Taifa litakusanya mapato mengi. Pia *TRA* ichukuwe hatua kali kwa wote ambao wanakwepa kulipa kodi za Serikali. *TRA* iwachukulie hatua kali watendaji wake wote wanaoshiriki kuchangia kupoteza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa tena shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi na pengine nitapata nafasi ya kuchangia kwa kuongea. Bado naliona tatizo kubwa sana katika nidhamu na vipaumbele pale ambapo tayari fedha za Bajeti zinapelekwa, hata tukipeleka fedha na kutenga nguvu kubwa ya fedha ni bure (*power without control is nothing*).

Mheshimiwa Spika, zipo fedha zilizotolewa na Serikali kupitia Bajeti hasa kwenye maji kutoka bilioni 391.6 hadi 621.6 ikilinganishwa na Bajeti ya 2010/2011. Ni hatua kubwa sana na ya kupongezwa na kwa kweli kama itazingatiwa basi hali ya maji italeta mabadiliko. Fedha hizi zielekezwu katika kusambaza maji vijijini kuliko kuzitumia katika matumizi ya kuitawala na kununua magari.

Mheshimiwa Spika, maji hayana mbadala, kiu ya maji haimalizwi na gari, ni aibu kuliona gari la programu ya maji likipita katika kijiji kisicho na maji. Wananchi wanataka maji sio magari. Uwepo wa maji unapunguza sana bajeti ya afya na kupunguza mzigo kwa Serikali. Katika vijiji vyenye maji safi na salama kuna idadi ndogo sana ya magonjwa ya milipuko kama, kipindupindu, kuhara damu, homa ya matumbo (*typhoid*) na magonjwa mengine yakiwemo ya ngozi na macho.

Mheshimiwa Spika, vijiji vyenye maji vina wagonjwa wachache, hii itapelekea vijiji vingi kuipunguzia sana Serikali fedha inayotumika kupata na kuagiza madawa toka nje ambayo ni ya gharama kubwa. Pia tafiti zinaonyesha vijiji vyenye shida ya maji vina ufaulu mdogo wa wanafunzi kwani muda mwangi watoto wanautumia kutafuta maji umbali mrefu kuliko kuhudhuria darasani.

Mheshimiwa Spika, ndoa nyingi sana huvunjika na pia ukosekanaji wa maji unachangia sana migogoro ya kifamilia kwa kuwa mama na wake zetu hutumia muda mrefu kufuata maji umbali mrefu kuliko kukaa na watoto na hii huchangia malezi duni na kusababisha watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, watoto wengine wamekimbia familia zao na kukimbia mjini ili kuepukana na adha ya kusomba maji. Maji ni kila kitu ni katika maisha ya binaadamu, kukosa maji ni kitu kibaya sana katika maisha. Napenda sana kuona kuna usimamizi mzuri wa fedha za maji zinafanya kazi kamili itakayokusudiwa hasa katika kuweka vyanzo vypya vya maji na kuvisambaza.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema sekta ya elimu kwa kweli kulingana na ongezeka la 12% ya bajeti kutoka bilioni 2,045.4 mwaka 2010/2011 na kufikia 2,283.0 pia ni vizuri sana na matokeo ya ufaulu yataonekana kama fedha zitalenga ufaulu zaidi wa wanafunzi hasa wanaotoka vijijini. Elimu ndio uwekezaji pekee wa mzazi maskini. Hakuna hazina ya maskini zaidi ya kumsomesha mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwa fedha inayotumika katika elimu haipotei ila itatoa riba kubwa baada ya ufaulu wa mtoto na itaonekana wazi baada ya ufaulu wa mtoto na itaonekana wazi pale, mtoto atakapokuwa analitumikia Taifa. Elimu bora ni Walimu bora na vifaa bora vya kufundishia vikiambatana na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kila Kata katika nchi tayari inayo Sekondari basi fedha zitumike kujenga maabara, maktaba, pia kutoa motisha kwa Walimu wa vijijini kwani Walimu wengi hujakimbia maeneo ya vijiji na kukimbilia mjini na hii imeleta tofauti kubwa ya ufaulu kati ya shule za mijini na vijijini. Ujenzi wa mabweni na kujenga maabara uendane sambamba kabisa na ubadilishanaji wa wanafunzi kutoka mkoja mmoja na kwenda mwingine kwa kurudisha *warrant* za safari hii, itajenga utafiti kwa watoto wetu na kuondoa ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, yawezekana utaratibu huu ukaonekana ghali ila kupoteza Utaifa ni ghali zaidi. Natumaini mengi niliyoyasema yakizingatiwa basi tofauti kubwa sana itaonekana na tutasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Wizara ya Fedha kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imelenga kumsaidia mwananchi wa kawaida. Tendo la Wizara yako kupunguza bei ya mafuta kwa kweli unastahili kupongezwa sana kwa sababu hata sisi wananchi wa Tabora tuna imani gharama za usafirishaji zitapungua.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la kilimo, Mkoa wa Tabora unalima sana zao la tumbaku, hata ukiangalia rekodi za *BOT* utaona tumbaku inaongoza kwa kuingiza fedha za kigeni kuliko zao lolote la biashara hasa Tanzania, tatizo la sasa ni ukosefu wa soko la uhakika na bei ya soko kwa sasa sio zuri.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la reli ya kati, nina imani sana na Wizara yako kuwa itasaidia kuimarisha reli ya kati kwa sababu nina imani uchumi wa Mikoa ya Kigoma na Tabora utakuwa kwa haraka sana. Napenda kukumbusha kuwa, Mji wa Tabora ndio kitovu cha reli ya kati kwa Mwanza, Kigoma, Mpanda, Dodoma mpaka Dar es Salaam. Usafiri wa reli ndio njia nafuu kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, suala la riba ni kero kubwa kwa wananchi wa kawaida. Riba ya 15% ni kubwa sana, napenda kumnukuu Hayati Baba wa Taifa alisema ukikopa Benki za Tanzania labda uwe unaiza Bangi ndio utaweza kulipa deni pamoja na riba? Kisingizio cha *Risk* sielewi inatoka wapi, naomba Wizara yako ilifanyie utafiti pamoja na *BOT* ili kuwezesha wananchi wa kawaida kukopa ili kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, *TRA* wanafanya kazi nzuri ila wanaopiga kelele ni wale watu wanaoshirikiana na wanaokwepa kodi. Naomba *TRA* waendelee na kazi nzuri na sisi tutaendelea kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Maji, Tabora tuna matatizo sana ya maji lakini kwa bajeti hii na kwa Mpango wa miaka mitano, Tabora tuna imani ya kupata maji toka Ziwa Victoria kuititia Kahama.

Mheshimiwa Spika, hali ya maji ya upatikanaji katika Manispaa ya Tabora ni mbaya sana. Mahitaji ya maji kwa sasa ni lita 24,000,000 kwa siku. Mahitaji ya maji ifikapo mwaka 2020/2025 itakuwa lita 35,000,000 kwa siku. Uwezo wa uzalishaji wa mamlaka ya maji (*TUWASA*) kutokana na miundombinu ya maji iliyopo ni lita 17,000,000 kwa siku. Vyanzo vya maji katika Mji wa Tabora ni Igombe lita 15,000,000 na Kazima lita 2,000,000. Uzalishaji wa maji kwa sasa ni wastani wa lita 9,500,000, hali inayopelekea wananchi kupata maji kwa mgao mkali. Bwawa la Igombe kwa sasa linatoa lita 9,500,000 na Bwawa la Kazima limekauka.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Tabora ina uwezo wa kupunguza tofauti hiyo kwa kuzalisha maji lita 15,000,000 kwa siku kwa kutumia Bwawa la Igombe ambalo bado lina maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, hatua za dharura zinazohitajika ni kununua pampu za kuchota maji Bwawani kupeleka kwenye chuji kwa kipindi cha mpito wakati wananchi wakisubiri mpango kabambe toka Ziwa Victoria utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka inadai malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji kutoka kwenye Taasisi za Ulinzi na Usalama yamefikia kiasi kikubwa na kukwamisha shughuli za mamlaka. Jumla ya madeni hayo Tsh. 411,591,837/= ambapo JWTZ

inadaiwa Tsh. 312,861,185/= na Polisi inadaiwa Tsh. 98,730,652=/. Madeni haya yamekwisha kuhakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uwasilishaji wa Bajeti Waziri wa Fedha katika kitabu cha Bajeti cha Lugha ya Kiingereza Ukurasa 26 (53) ameeleza nanukuu: “*Madam Speaker, on the expenditure side, Government continued to realize funds depending on the availability of resources by taking into consideration planned priorities. The trend is showing that total expenditure will be less than the target of 2010/2011 Budget, due to shortfall in revenue collection. Also, before the end of 2010/11 the Government will have paid all verified claims of the State Security Forces, house allowance for Lecturers of Public Universities and house rents for Judges.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nahitaji maelezo ya Mheshimiwa Waziri, je, kwa maelezo niliyoyaeleza hapo juu Wizara haioni ni wakati muafaka kulipa deni la TUWASA ili waendelee kutoa huduma kwa wananchi wa Tabora Mjini? Endapo Hazina watailipa mamlaka, nina imani kuwa, watapata uwezo wa kununua *pump* za kusukuma maji na hatimaye wananchi wa Tabora watapata nafuu ya adha ya maji. Mamlaka haitahitaji msaada wa Serikali kwani uwezo wa kujiangezia mapato toka milioni 100,000,000 mpaka 150,000,000 unaweza kupatikana katika Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili lipewe kipaumbele kwa maendeleo ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja ya Wizara ya fedha kwa asilimia mia moja.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja moja kwa moja Bajeti ya Serikali. Kadhalika niwapongeze wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini kwa imani yao kwangu, kwa Serikali yao na kadhalika kwa Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Aidha, imani yao kwa Serikali na ufuutiliaji wao wa mambo yanayoendelea katika Bunge hili Tukufu nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuipongeza Bajeti kwa vipaumbele vilivyoanishwa. Ambavyo ni Umeme, Maji, Miundombinu, Kilimo na Ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la Nishati hasa hasa umeme limekuwa sugu nchini na hakika jitihada nyingi zimekuwa zikielekezwa. Aidha, nchi imeshuhudia ni jinsi gani siasa zimechangia kunyima wananchi fursa ya kupata umeme pale suala la DOWANS lilipochukua nafasi. Nchi yetu imejaliwa gesi asilia nyingi na hakika hata nchi za mbali zimeanza kuita eneo la Kusini mwa Tanzania kuwa ni *Qatar* mpya. Hii ni bahati kubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza ni jinsi gani pamoja na rasilimali hii Watanzania wamekuwa pembeni. Miradi yote ya gesi na mafuta iliyoko nchini kwa

mujibu wa (*PSA*) mkataba husimamiwa na makampuni ya nje na ushirika wetu ni mdogo sana. Asilimia iliyonayo Serikali kwenye mkataba ni ndogo na hivyo kutufanya Watanzania kuwa wanyonge kwa rasilimali yetu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ijielekeze kulisaidia Shirika la Maendeleo ya Petrol (*TPDC*) iandae vijana (*successors*) washiriki kikamilifu kwa mujibu wa sheria za nchi au *PSA* kwenye utafiti na uzalishaji wa gesi baharini na nchi kavu. Ni vema Serikali sasa itoe sapoti kwa kutenga fungu mahususi kwenye miradi ya gesi iliyoandalliwa na *TPDC*, kama ile ya gesi ya majumbani, ya magari na hata viwanda ili nchi yetu ipate maendeleo kupitia rasilimali nishati tulionyayo.

Mheshimiwa Spika, bajeti pia itoe fursa kama si mwaka huu basi mwakani kupitia Wizara. Waunde *National Drilling Company* kwa ajili ya tafiti na uzalishaji wa gesi na mafuta ili kuanzisha Taifa lenye kujitegemea zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kilimo. Mabilioni ya JK sasa yatolewe kila Kata kwa mfumo wa zana za kilimo kusaidia Watanzania hasa wakulima. Kadhalika sasa wakati umefika wa kuangalia upya waliohodhi ardhi zilizokuwa mashamba ya mkonge ili yapewe wananchi. Aidha, Dirisha la Kilimo ni taa ya mkulima ya kumletea mafanikio.

Mheshimiwa Spika, barabara ni chombo muhimu, ujenzi wa miundombinu, utaibadili sura ya nchi, naipongeza bajeti. Ila zana ya ujenzi wa Bandari ya Mbegani uangalie upya kwani Mbegani na Dar *port* ni karibu na pia uwepo wa meli waweza tishia viumbe walio eneo la Saadani. Badala yake Bandari ya Tanga ipanuliwe na kupokea mizigo mikubwa. Hii itasaidia kugawa *gateways* kwenda nchi jirani na kuongeza njia kwenye ukanda huu wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la teknolojia na uwepo wa mahitaji ya kilimo, rasilimali watu, ardhi na ari ya kujiletea maendeleo, akinamama na watoto ni muhimu kwa uchumi wetu. Hii itasaidia kupunguza makali ya maisha na kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo la Korogwe ni miongoni mwa maeneo maarufu kwa matunda na mazao mengine, hivyo Bajeti kutoa kipaumbele kwa sekta ya viwanda ni ukombozi kwa wakulima na wafugaji kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la maji limechukua sura mpya na uhaba mkubwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi. Pamoja na kutajwa katika Bajeti ningependa kutoa ushauri ufuataao, kuwa Serikali au Bajeti ianzishe Kitengo cha *Water Drilling* kila Mkoa, na kuchimba visima virefu na vifupi.

Mheshimiwa Spika, hapa tutakuwa tumetekeleza kwa dhati mpango wa Serikali. Kadhalika tutakuwa tumetoa ajira, na kusogeza kitengo hiki karibu zaidi na tija za huduma zake zitaonekana haraka ikiwa ni pamoja na kupunguza kero ya maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme naunga mkono bajeti na pale panapostahili wazingatie ushauri.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba nitoe rambirambi zangu kwako wewe, kwa msiba kubwa uliokupata wa kuondokewa na mama yako mpenzi. Ninaungana na wenzangu wote walio tangulia kuchangia, kumwombea Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya mama yetu mpendwa mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia hoja iliyoko mezani kwetu, ninaomba nichukue nafasi hii, niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini, kwa imani kubwa waliyonayo kwangu, kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa mara ya tatu mfululizo. Nami ninawaahidi tena kuwa, nitaitunza na kuiheshimu imani yenu kwangu, kuendelea kushirikiana nanyi siku hadi siku ili kuharakisha kuleta mapinduzi halisi ya kimaendeleo Musoma Vijijini.

Mheshimiwa Spika, mimi nililelewa na wazazi wangu kwamba, mama akileta chakula mezani kiwe kidogo ama kingi onja usikiteme. Mshukuru mpishi, usimbeze mpishi wala chakula chake. Kama pengine mpishi hakuunga nyama au samaki vizuri, mwombe akuletee chumvi kidogo uongeze ili uendelee kukila.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge walio tangulia kuchangia, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kundi lake zima, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuletea Mezani Bajeti hii ili tuone kama inahitaji kuboreshwa hapa na pale kabla haijaanza kumegwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba niwaambie Wananchi wangu wa Musoma Vijijini haya yafuatayo:-

Bajeti hii haina lolote jipya la kimaendeleo Musoma Vijijini. Kero zetu kubwa tulizokwishaomba Serikali itusaidie kuzimaliza katika Bajeti hii, hazitaguswa hata kidogo. Kero hizi sugu ambazo zimeachwa pemberi ni kama zifuatazo:-

1. Barabara ya kutoka Musoma hadi Busekela, yenyе urefu wa kilometra 93 itakuwa ikikarabatiwa hapa na pale lakini haikuwa kwenye mpango wa kujengwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa wakati wa kampeni.
2. Uwanja wa ndege ambaa tumekuwa tukiahidiwa kila mwaka kujengwa Nyansurura hauonekani katika Bajeti ya mwaka huu.
3. Tatizo sugu la Buhemba litabaki hivyo hivyo na kwamba, wale wachimbaji wakubwa kutoka Afrika Kusini na majirani zetu watabaki.
4. Malambo ya maji tulioahidiwa kwa kipindi chote cha Ubunge wangu, hayapo kwenye Bajeti hii tena! Malambo hayo ni haya yafuatayo: Kiagata Marambo mawili

yaliyoko Wegero na Buswahili; na Lambo la Kyarano, Butuguri (Shulen Oswald Man'gombe, Rwamkoma, Busegwe, Muhoji na kadhalika.

5. Mradi chakavu wa maji kutoka Mugango kwenda Butiama, Muryagu/Bumagi kuitia Kyabakari (*Buturu Trunk Route*) haumo kwenye Bajeti.
6. Barabara ya kutoka Musoma – Butiama, Ikizu Fort Ikoma, kilomita 164, haimo tena kwenye Bajeti hii.
7. Barabara ya kutoka Suguti hadi Kiwasi karibu na Bunda haipo ndani ya Bajeti hii tena.
8. Hospitali ya Kwangwa ambayo ilikusudiwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Mara, haipo tena kwenye mpango bali itazidi kubaki gofu tu.
9. Barabara ya kutoka Kirumi hadi Mugumu kuitia Kiagata Sir Simba, ambayo imekuwa kero kubwa tangu enzi za ukoloni, bado haijapata ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato: Nimesikitishwa sana kuona eti Serikali inapendekeza kufanya mabadiliko madogo madogo ya kwenye Sheria ya Kodi mbalimbali ili ipate kiasi kidogo kama shilingi 71.6 milioni. Ndugu yangu na rafiki yangu wa siku nyingi tokea tukiwa Uingereza tukisomea mambo ya fedha na uchumi; hapa umeeleza hizi fedha za reja reja hazitasaidia Tanzania, hazitatupa fedha za kutosha kunijengea barabara ya kutoka Musoma hadi Busekela Jimboni kwangu Musoma Vijijini. *Overhaul Structurer* nzima ya Kodi ya Income Tax na VAT.

Ninapendekeza, kwanza upunguze *rate* ya Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 hadi 26 na badala yake ongeza *rate* ya Kodi ya Ongezeko la Thamani hadi kufikia asilimia 21.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, mapato ya Serikali yataongezeka kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninasema hivyo? Hapa nitamnukuu mtaalamu mmoja aliyebolea katika Sheria ya Kodi, Bwana Hugh Mason wa *Pricewaterws Coopers* anasema:-

*“Countries with large informal sectors usually are characterized by both low rates of tax revenue in relation to gross domestic product, yaani GDP and a very large proportion of government tax revenue being provided by only a very few large tax payers..... there is a general correlation between poor countries with large informal sectors and low proportions of tax revenues, Tanzania shows both of the features. Some large 400 large tax payers contribute almost 80% of the domestic tax revenue and the tax revenue of Tanzania Government is relatively low in relation to GDP.” Tax And The Informal Sector A Paper For Discussion Hugh Mason.”*

Mheshimiwa Spika, tunajifunza nini katika somo hilo? Mimi ninashauri ili kuinua Pato la Serikali ni lazima tujikite katika Kodi ya Ongezeko la Thamani, yaani VAT, ambayo kwa jina lingine kiutaalam huitwa *Consumption Tax*; ni lazima *rate* ya VAT ipandishwe kufikia asilimia 21 na *rate* ya *Income Tax* ipunguzwe hadi asilimia angalau 26. Mataifa mengi kote duniani hufanya hivyo; Uingereza, Ufaransa, *most EU Countries* zinafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda maslahi ya Wananchi wetu walio na kipato kidogo, ninashauri ile *Tax Rate* ya VAT isiwe *flat rate* 21%, bali iwe *Graduated VAT TAX Rate*. Ninaambiwa hata jirani zetu Kenya, hawana *flat VAT rate* katika *supplies* zote. Kama Ufaransa, nchi iliyobuni VAT mwaka 1954 na sasa inatumiwa karibu nchi zote duniani; kwa nini Tanzania isiige ukusanyaji wa Kodi ya VAT kinamna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kutunga Sheria ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2010, maarufu kama *The Public Private Partnership Act, 2010*.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kipekee ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana ndugu yangu Mizengo Pinda, Waziri Mkuu, alivyonisikiliza kilio changu cha kuharakisha utungaji wa Kanuni za Kutekeleza Sheria mpya kabisa ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, pengine Waziri Mkuu asingeingilia kati kwenye jambo hili leo, Sheria hii isingekuwa tayari kuanza kutumika. Ninaomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Kigoda, kwa kuniruhusu kuingia katika Kamati yake ili nichangie nguvu zangu zote, umuhimu wa kuharakisha urekebishaji wa Sheria ya *Public Procurement Act*, yaani Sheria kuhusu Manunuvi ya Umma, ambayo bila kuwepo Sheria ya *PPP*, isingeweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ni lazima ieleteke kwamba, msingi wa *PPP* ni Sheria ya *Public Procurement*. Kwa umuhimu huo basi, Sheria zote hizo mbili ni lazima zioane; vinginevyo, itakuwa vigumu kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kila mwaka huwa inatenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara, reli, miradi ya uzalishaji na usambazaji wa umeme, ujenzi wa viwanja vya ndege, bandari na miundombinu mbalimbali, bila shaka sasa kasi ya maendeleo nchini itaongezeka kutohana ushirikishwaji wa watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi kubwa ya Serikali kuleta Bungeni Miswada hii miwili, yaani Sheria ya *PPP* na *Public Procurement Act*, bado kuna changamoto kubwa zitakazoikabili Serikali.

*Regulations* zilizotungwa na Waziri zinazohusu PPP zimechakachuliwa katika uanzishwaji vitengo vile viwili: Kitengo kimoja kilichowekwa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania, yaani *TIC*; na Kitengo cha pili ambacho kimewekwa Wizara ya Fedha eti ambacho kitahusika kuifanya tathmini Miradi ya Ubia eti kuhakikisha kuwa,

Miradi inayoanzishwa hapa nchini, inajiendelesha kibiashara na kwa misingi ya thamini ya fedha na haisababishi mzigoto kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, *this is nonsense*. Tangu lini Serikali ikajishughulisha na uendeshaji wa biashara; Serikali hii ilishindwa kuendesha Mabenki, Hoteli, Bima, ATC, Shule na kadhalika. Wizara ya Fedha ipo hoi katika usimamizi wa hata kulipa mafao ya wastaafu wa zilizokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi uko hoi; kila siku ni migomo ya wanafunzi kuhusu kushindwa kwa Wizara ya Fedha kufanya tathmini kuhusu mahitaji ya wanafunzi, walimu mashulenii, Idara ya Polisi na sehemu nyinezo.

Sasa mnaomba tena kupokea *your noise* kwenye *sensitive issue* kama PPP. Je, kweli Wizara ya Fedha italiweza jukumu hili jipya na *complicated* kama PPP?

Mheshimiwa Spika, huu ni usanii wa hali ya juu. PPP ni kama aina ya ubinafishwaji (*Privatization*). Chombo maalum cha ubinafsishwaji kipo PSRC, ambayo inafanya kazi nzuri sana na kumaliza kazi hiyo. Mashirika yote ya Umma yalikwisha binafishwa, *common sense* inaonesha wazi kwamba, hiyo *unit* inayokusudiwa kuwekwa Treasury inastahili moja kwa moja kwenda *Holding Company*, chombo kilichokuwa kinaitwa PSRC.

Mheshimiwa Spika, ninashauri *unit* ya pili iende *former PSRC* au isichanganywe na *bureaucracy* ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja hii kwa kweli inawapa Watanzania nafasi ya kujionea wenyewe ni jinsi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi inavyowajali katika Awamu hii ya Nne. Pia nachukua nafasi hii adimu kuipongeza Serikali kwa juhudhi inazozifanya kuleta maendeleo ya kiuchumi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri wa Fedha aliyoisoma leo ina lengo la kuonesha mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha kuanzia 2011 hadi 2015. Ukisoma kwa haraka haraka utadhani mwelekeo huo una matumaini. Ukisoma kiundani utaanza kuona kwamba kwa mwelekeo huo sioni jinsi gani tutafika tunakotarajia. Ninazo sababu kubwa tano kwa nini nina wasiwasi kuhusu malengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kukuza uchumi wetu hauwezi kuendelea kama Serikali inavyotarajia iwapo mageuzi makubwa hayatafanyika katika miundombinu ya kutisha iliyoko katika Jiji la Dar es Salaam, bila *major reforms* za barabara zote za Dar es Salaam hakuna tegemeo lolote la uchumi nchini. Dar es Salaam ndio mdomo ambao uchumi unapoanzia. Bandari ya Dar es Salaam inapaswa kupanuliwa mara tatu *at the very minimum*, ni lazima tuichukue Dar es Salaam Kama ilivyo *Suez Canal*. Meli kubwa ziletazo bidhaa Tanzania na zile ziendazo DRC, Rwanda, Burundi na kadhalika lazima ziweze kushusha na kupakua mizigo sio zaidi ya siku tatu *at the maximum*, siku tatu ndizo *International Standard*. Mombasa, Beira na Bandari kubwa zote duniani zimeweka siku tatu kama *acceptable efficiency bench mark*. Kwa mantiki hii ni lazima usitishwe na badala yake upanuzi wa Bandari uanze haraka sana. Ni lazima (kwa maoni ya wataalam

wengi wa kiuchumi duniani) nusu ya Kigamboni ichimbwe ili kuweza kuruhusu meli nyingi kutia nanga na kupakua na kubeba mizigo haraka sana.

Mheshimiwa Spika, tuisahau Dar es Salaam *Port* hadi wakati wa kupata uhuru ilikuwa bandari ya Congo (i.e DRC) chini ya King Leopard wa Ubeligiji. Siamini kama ingelikuwa bado chini ya Ubelgiji Bandari hii ingelikuwa katika hali mbaya kama ilivyo sasa. Ni lazima *container* zote ziwe ndani ya miundombinu ya Bandari na sio usanii wa kufanya *dry ports* kama jinsi Serikali inavyokusudia kufanya.

Mheshimiwa Spika, fedha za kuweza kufanya mageuzi makubwa kama haya zipo, nasema zipo maana mradi kama huo pamoja na kuonekana kuwa *ambitious* ni *bankable*. Wachina wanaweza kutoa fedha kama hizo kama mkopo. Dhamana tuliyonayo ni madini yetu, gesi nyingi iliyopatikana na *potential* ya Mchuchuma na kadhalika. Angalia nchi ndogo kama Djibouti, Msumbiji na kadhalika wanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, mageuzi makubwa yakifanya umuhimu wa barabarabara zitokazo Dar es salaam kwenda bara ni lazima zipanuliwe kuwa *five lane* na sio usanii wa kujenga *fly over* ninazozisikia. Je, ni kipi rahisi kubomoa nyumba zote zilizoko kando kando ya barabara hizi na kupanua barabara hizi kufikia *lane* tano au kujenga *fly over* ambazo hazitakuwa wala na *parking places*?

Mheshimiwa Spika, barabara zitokazo Dar es Salaam kwenda Bara lazima zipanuliwe kokote zipitapo nchini Tanzania sio kuishia Dar es Salaam. Ni muhimu Serikali iwe na *vision* sahihi kama hii vinginevyo tunajiua sisi wenyewe. Wenzetu Kenya sasa wameanza kufanya hivyo, sisi tuko wapi!

Mheshimiwa Spika, mapinduzi ya miundombinu yasikomee Dar es Salaam pekee bali yaguse miji yetu yote mikubwa hususan Morogoro, Dodoma, Tabora, Mwanza, Tanga, Arusha, Kigoma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri inazungumzia kilimo, mifugo, misitu na kadhalika. Sera ya Kilimo Kwanza imekuwa ikisemwa mara kwa mara. Siamini kama sera hii itafanikiwa iwapo shule zetu hususan Vyuo Vikuu vya Kilimo vitaanzishwa ili kufanya mapinduzi madhubuti ya kilimo. Ilani ya CCM inazungumzia uzalishaji wa ujenzi wa Chuo cha Mwalimu Nyerere hapo Butiama. La kushangaza ni kwamba pamoja na *World Bank* kupitia Shirika lake la Kiuchumi *ITC* kukubali kuchangia fedha ili kujengwa sioni juhudzi zozote za Serikali kuhusu chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, nimesoma Hotuba ya Waziri Mkulo pamoja na ile ya Tanzania *Five Year Development Plan 2011/2015-2016* kwa makini. Kinachojitokeza ni kwamba, Chuo Kikuu cha Kilimo kwanza hakitajwi. Je, kwa kuwa lengo la sera ya *Public Private Partnership (PPP)* ni kuongeza nguvu za Serikali kuchangia ucharaka wa ujenzi wa Chuo Kikuu kama hiki na kwa kuwa Serikali haioni umuhimu wa kutenga fedha kwenye Bajeti hii au hapo usoni Serikali haioni ni aibu kwa Watanzania kuendelea kikitaja mara kwa mara? Je, maandalizi yote yaliyokwishafanyika hadi sasa kwa

kushirikiana na *IFC* hatma yake ni nini katika mwelekeo huo wa kiuchumi 2015 hadi 2025?

Mheshimiwa Spika, pamoja na wasiwasi nilionao kuhusu ujenzi wa Chuo Kikuu chini ya mwelekeo huu, naunga kwa shingo upande Hotuba ya Waziri wa Fedha.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hali ya kupanda kwa gharama ya maisha. Hali ya maisha hasa kwa vijiji imezidi kuwafanya wananchi kutokuwa kabisa na imani na maisha yao, wengi wao hawawezi kupata hata au hawana uhakika wa kupata milo miwili ya siku. Wengi wao wakiwa wanasahau hata matumizi ya sukari sababu zimepanda bei. Pamoja na Serikali kusisitiza sukari kilo moja iuzwe Sh. 1,700/= lakini hadi sasa bei ya kilo moja ya sukari bado ni Sh. 2,000/= mpaka Sh. 2,100/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wanaosafirisha sukari na vitu vingine vyote kufikia wateja lazima watumie usafiri na bei ya mafuta imezidi kupanda hivyo kuwalazimu kuongeza ziada hiyo kwenye bidhaa hizo. Hivyo Serikali ina ulazima wa kupunguza utitiri wa tozo wanazolipa wauzaji wa mafuta kama vile *TRA*, *SUMATRA*, *TPA*, *TBS*, *TIPPER*, *EWURA*. Kwa kuwa Taasisi hizi tayari zinapata ruzuku hivyo hakuna sababu ya kupata fedha zaidi na kufanya bei ya *Petrol*, *Diesel* na kadhalika kuwa ya hali ya juu kiasi hicho. Haja ya bei ya mafuta ya taa iwe bei sawa na *Petrol* na *Diesel* ili kuondoa uchakachuaji ambao hupelekea magari mengi kuharibika.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu kushuka kwa thamani ya shilingi. Kwa kuanzia ni vizuri Serikali kuangalia hili kwa uangalifu mkubwa. Hapa Tanzania tumekuwa na kawaida ya sasa kuthamini dola za Kimarekani kuliko fedha yetu. Kwa mfano, malipo yote ya kutembelea mbuga za wanyama, wawindaji, kulala mahotelini wanalipa kwa kutumia dola (*USD*) lakini wenzetu wa Afrika Mashariki huwezi kufanya malipo yoyote kwa fedha za kigeni, lazima uende maduka ya kubadilisha fedha ili uweze kulipa unachodaiwa. Je, tusipothamini fedha yetu wenyewe nani ataithamini?

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika usafiri wa anga. Inabidi Serikali ichukue hatua za haraka kuhakisha Shirika letu la *ATC* linafanya kazi yake ya biashara. Tumeshindwa hata kufaidi soko la *AGOA* kama wenzetu wa Kenya sababu tu wao wanazo ndege zao wenyeza za kusafirisha mizigo kwa bei ya unafuu. Sio hivyo tu Serikali imekuwa ikisisitiza na kutoa matangazo wawekezaji au ndege nyingi zije Tanzania kuwaleta watalii. Je, watalii hao wakishafika uwanja wa Dar es Salaam au *KIA* wataruka na ndege gani kwenda kwenye *final destination*? Sio hilo tu kwa kutokuwa na Shirika letu la Ndege inafanya watalii kuona Tanzania kuwa ya ghali sana. Naungana na Kambi ya Upinzani, Serikali kutenga bilioni 200 ili kulifufua upya shirika hili.

Mheshimiwa Spika, pia niongelee kuhusu riba katika mabenki. Wananchi wengine wanashindwa kukopa katika mabenki yetu sababu riba ni kubwa sana, zinaanzia 18% mpaka 25%. Hii inapelekea watu wengi kushindwa. Kuna haja *BOT* kuliangalia vizuri kwa sababu wateja wakiweka (*Saving Account*) wanapata faida ndogo sana haifiki 3%. Wakati wenzetu wa nchi za nje zinawasaidia wananchi wake kukopa kwa bei nafuu,

wengi wao wanaishi kwa mikopo. Unakuta nyumba analipia *mortgage*, gari mkopo, anakwenda likizo mkopo, mpaka chakula cha kula ndani ni mkopo. Lakini yote haya yanawezekana, kwanza, wananchi wote wanajulikana wanakaa wapi na anuani zinajulikana ikiwa ni pamoja na Vitambulisho vya Taifa vinavyoonyesha makazi yao. Je, hapa Tanzania mchakato wa Vitambulisho vya Taifa umefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, nichangie vile vile katika suala la ubora wa noti mpya. Naipongeza Serikali kwa kubadilisha noti zetu za fedha, lakini noti hizi zina matatizo makubwa, baadhi ya benki bado machine zao hazisomi kama ni feki au nzuri. Sio hilo tu bado zinachakaa mapema sana na wananchi hasa wafanyabiashara wadogo wadogo bado wanazikataa kuzitumia. Naomba Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania kuhusu noti hizi kama hazina matatizo ili wafanyabiashara wazipokee. Pia dola za Kimarekani zile zenye vichwa vidogo kuanzia 2001 nyumba na maduka ya kubadilishia fedha hapa nchini hata baadhi ya mabenki wanakataa kuzipokea, lakini noti hizi zinatumika katika nchi zao. Hivyo watalii wakija Tanzania wanakuja nazo sababu kwao hazina shida, zikikataliwa kwetu zinaleta usumbufu mkubwa sana. Je, nini tamko la Serikali kuhusu noti hizi?

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, hoja ya kupunguza matumizi kutoka katika fedha za Serikali. Pamoja na kupendekeza kutokuwa na magari ya kifahari kwa viongozi wa Serikali na badala yake kununua magari ya bei nafuu ili kuokoa fedha za Serikali yetu. Vilevile kupunguza gharama hizo kwa kufanya mambo yafuatayo:-

Kutonunua vifaa vya kutendea kazi maofisini kutoka kwa mfanyabiashara hapa nchini na badala yake Serikali kuagiza makontena ya vifaa hivyo kutoka nje bila kupitia kwa mfanyabiashara yeyote. Mfano, wa vifaa hivyo ni *Computer*, samani za maofisini, vifaa vya kufundishia mashulen na kadhalika. Kufanya hivyo kutasaidia kupunguza matumizi makubwa ya Serikali kwa kutokununua vifaa hivyo kwa bei kubwa ukilinganisha na ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha elimu inakuwa ya kukidhi mahitaji yenye ubora wa elimu anayostahiki kupewa. Hivyo basi, Serikali iwe na mpango au mkakati wa kuweka vitabu yaani kuwe na maktaba (*library*) katika kila shule au katika kila Wilaya. Vile vile kuwe na vifaa vya kufundishia elimu kwa vitendo. Kuifanya hiyo kutaiwezesha nchi yetu kupata rasilimali watu ambao hutegemewa zaidi katika jamii na maendeleo kwa ujumla na sio rasilimali watu ambao ni tegemezi kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo vijiji, kuna Mikoa ambayo ina vijiji ambavyo huingiza pesa nyingi kupitia watalii na kilimo na huwa ni vya mbele katika kutoa kodi na kuongeza pato la Serikali. Lakini bado katika maendeleo mbalimbali kama elimu bado hawana shule na pia shule chache zilizopo hazina walimu na vifaa vya kufundishia. Kwa kuwa huleta sehemu ya pato la Serikali, basi Serikali nayo iwaangalie kwa kuboresha shule zao na huduma mbalimbali ili kuleta maendeleo zaidi ya pato la Taifa na hata katika vijiji husika katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nichangie katika suala la miundombinu. Pamoja na kuwa suala hili la miundombinu kupewa kipaumbele, tunaiomba Serikali kuangalia zaidi barabara mbovu zilizopo katika maeneo ya mikoa ambayo inazalisha au ina wakulima ambao hutoa mazao yenye kuleta pato la Taifa. Ili kutopoteza thamani ya mazao yao na pia kuboresha barabara ili mazao yafike kiwandani kwa wakati na kuongeza thamani ya bidhaa na vile vile kuongeza pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, hususan viwanda vilivyopo jirani na maeneo ya mashamba vifufuliwe ama virudi mikononi mwa Serikali (kuchukuliwa na Serikali) ili kuwapunguzia adha wakulima wetu. Mfano, wakulima wa chai (Njombe – Iringa) na hususan kwa wakulima wa Lupembe.

Mheshimiwa Spika, mwisho nizungumzie suala la Muungano. Kwa kuwa Serikali yetu ni ya Jamhuri ya Muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika. Tunaiomba Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kujenga Ofisi zote za sekta ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Kwani kuna sekta mbalimbali za Muungano ambazo hazina Ofisi kwa Zanzibar. Mfano, sayansi na teknolojia na kadhalika hazina Ofisi kwa Zanzibar. Suala hili pia huleta kero mionganoni mwa kero za Muungano.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi. Napenda kuchangia Bajeti ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huduma za afya ni muhimu popote hasa kijijini kwa upande wa uzazi salama naishauri Wizara iangalie kwa kina pia ifanye jitihada za makusudi kuchagua vijana wenyewe uwezo wanaoishi katika kijiji husika halafu kila kijiji kichague watu watatu ili kuweza kusaidia kwa kutoa huduma ya uzazi salama. Naomba vijana hao wapatiwe mafunzo, wapewe vifaa vya kuzalishia (*KIT*) *Deliver Kit* pia wapewe buku ili kuweka kumbukumbu zao. Hili litasaidia sana wakati itakapotokea dharura kusaidia uzazi huo pia itapunguza idadi za vifo vya mama na mtoto wakati wa uzazi pia itasaidia upatikanaji wa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuelekea sehemu ya umeme. Kwa kuwa tatizo la umeme limekuwa gumzo katika nchi yetu, ningependa Serikali ifanye utafiti wa kina ili tuweze kuliondoa tatizo hili kwa kuwa baadhi ya mikoa katika nchi yetu kuna milima kama mlima iliyoko Mkoani Arusha Oldonyo Lengai. Naiomba Serikali ifanye utafiti ili milima hiyo tuitumie kwa ajili ya kuzalisha umeme, hii pia itasaidia kupunguza kutokea kwa *volcano* mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nichangie katika suala la madawa ya kulevya. Kuna kundi la vijana wetu wengi kuingia katika madawa ya kulevya, hii inadhoofisha sana uchumi wetu sababu vijana wanapoelekea huko nguvu kazi inapungua kwa sababu huwa hawawezi tena kufanya kazi, hubakia kupita wakizurura ovyo. Hii pia inasababisha vijana wetu wa kike kukosa kuolewa kwa muda kwa sababu wengi wanaopotoka na madawa ya kulevya ni vijana wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kutafuta mbinu mbadala ili madawa haya yapungue na baadaye tuwaelimishe, wao ndio watakuwa walimu kwa wengine watakaobakia. Naiomba Serikali ijithidi kwa hili maana vijana wetu wanaangamia na vijana ndio nguvu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri wa Fedha kwa Bajeti nzuri. Naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara ya fedha, hususan Waziri wake Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Manaibu wake pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii. Aidha, niwapongeze Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa Bajeti hii ambayo inalenga kuboresha maisha ya Watanzania na kukidhi Ilani ya Uchaguzi ya CCM, niseme tu kwanza kuna maeneo ambayo yanatakiwa kupewa pesa za kutosha na kwa wakati bila kuchelewa ili kuendana na wakati. Suala la umeme ni muhimu sana, hivyo miradi yake ni vema ipewe pesa kwa wakati, suala la mradi wa Mchuchuma, Liganga na Ngake, Serikali ione kuwa ule ni urithi wa Watanzania amba Mungu aliwapa ili utoe umaskini wao kwani kila nchi ameigawia rasilimali zake kwa faida ya watu wake. Hivyo ni vema Serikali iwekeze ili kupata mgao mzuri katika uwekezaji unaofanyika badala ya kuwaachia wageni peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *NDC*, *malaria* upewe pesa mara moja ili tuepuke kuendelea kutumia pesa nyingi katika kuagiza dawa za *malaria* nje. *EPZ* - Bagamoyo ipewe pesa za kutosha na maeneo mengine fidia zilipwe kwa wakati, bila kuwasahau *SIDO* na mitaa ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi kulikuwa na suala linalohusu wakimbizi na kwenye mchangwo wangu wa awali katika mpango wa miaka mitano nilichangia juu ya suala hilo nikihusisha na Vitambulisho vya Taifa. Kwa upande wangu, nikiri kuwa nami ni mionganoni mwa anayewaonea huruma wakimbizi kama binadamu wenzangu. Lakini huruma hiyo isithiri watu wengine, inaweza kusababisha vita za ndani kwa ndani kati ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba wanapoingia nchini wakae kwenye maeneo yale ambayo angalau mila zao zinapanana, kuliko kuwasambaza nchi nzima. Mfano, Mtwara walipokea wakimbizi wengi sana toka Msumbiji, hali kadhalika Ruvuma. Hivyo na hao ni vema wakabaki maeneo waliyokuwa wakiishi kwani wameshaanza kuzoeana. Lakini hata hivyo, huo umoja wa Kimataifa unaingia nini kwa watu hao? Maana kama hawatachangia angalau makazi, basi ina maana ni sawa na kuongeza umaskini nchini. Hivyo ni bora kwanza tukakamilisha suala la vitambulisho. Pili *UNHCR* kama iliweza kuwatunza watu hao kwa muda mrefu, basi pia iwaache katika mikono salama kimaisha kwa kuwasaidia *shelter and training* angalau kwa theluthi moja of the population ili pia waweze kujiajiri kwa namna moja au nyingine. “Wema usizidi uwezo.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kambi ya Upinzani ya kupunguza ada kwa shule za sekondari ambazo ni za Kata, sio la lazima sana kwa sasa kwani watoto wanakuwa kwa wazazi wao na ni vema pia wao kuchangia kidogo. Tatizo kubwa lipo kwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu, kwani gharama za masomo ni kubwa sana. Katika eneo hilo, walimu au wakufunzi wanadai pesa nyingi za posho zao, hali hiyo Mwalimu ataacha kukinung'unikia chama na Serikali yake darasani? Kwani hiyo inagusa maslahi binafsi na ndio mategemeo ya maslahi binafsi na ndio mategemeo ya maisha yake. Lakini pia nao ndio watu wenyewe akili sana pamoja na ushawishi mkubwa kwenye jamii na ukweli ni kwamba mwanafunzi yejote anamsikiliza sana Mwalimu wake kwa karibu kila kitu anachomfundisha na ndio maana migomo haiishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni vizuri kuangalia juu ya posho za wanafunzi waliopo chuoni kwa sasa na ikibidi tusiongeze idadi ya udahili katika kipindi hiki ili kuepuka ukuaji wa mikopo ambayo kwa mikakati ya Taifa ya kuangalia kwanza vipaumbele vichache ili kukuza uzalishaji na pato la Taifa. Hata hivyo ni vema mkopo wa posho hizo uongezwe kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya elimu yaboreshwe mpaka vijijini kwani kutokana na *passmark levels* na *division* zinazochukuliwa kama vigezo, unakuta kwamba watoto wanaobahatika na mikopo hii sio watoto wa maskini (wengi wao) kwani wao wapo vijijini na wamepata elimu duni hivyo ni wachache sana wanapata division one na two. Kwa kweli pengine hata kijiografia kuna maeneo mgao wao ni mdogo sana. Ni vema sasa uboreshwaji wa mazingira ya elimu uangalie sana maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Nyasa na fukwe zake halijatumika vizuri kiuvuvi, kiutalii na hata katika kuunganisha wananchi na biashara za Tanzania, Msumbiji na Malawi. Hata barabara ya mpakani Mbambabay–Lituhi inapewa Bajeti ndogo mno Milioni mia moja tu km 110 hivi kweli ni sahihi? Hivi kuzaliwa huko ni laana? Barabara nyingine zipo mjini na zinapiiwa *Land Cruiser* lakini zinawekwa lami na kuchimbiliwa tena kila siku, hao wanahitaji changarawe tu, jamani hata kusema hadharani haifai.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na wataalam wengine wote wa hotuba nzuri sana ambayo imejifafanua kwa kina.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuipongeza Serikali kwa namna ilivyozingatia kwa umakini mkubwa, Malengo ya *Millenium* lakini vile vile kwa namna ya kipekee ilivyozingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015. Naipongeza Serikali pia kwa namna ambayo Bajeti ya 2011/2012 ilivyozingatia hali halisi ya maisha ya Mtanzania hii inaonesha namna ambavyo Serikali yetu ni sikivu na inawajali wananchi wake na hasa wale wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa zaidi kwa namna ambavyo Serikali imeweka mkazo wa utekelezaji kwa kuainisha vipaumbele ambavyo mimi binafsi naamini kama utekelezaji wake utakamilika basi ni dhahiri kwamba ile kauli mbiu isemayo, “Maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana” ili mradi tu na wananchi wenywewe wanafanya

bidii katika kuyafikia hayo maisha bora. Vipaumbele hivyo pia vitategemea namna ambavyo Wizara husika zimejipanga kuvitekeleza vipaumbele hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala la kuongeza ajira kwa sekta binafsi na ile ya umma litategemeana zaidi na namna tulivyoziaandaan kanuni zetu za *PPP* na kuziruhusu zianze kutumika mapema kama Hotuba inavyojieleza. Ningombaa Mheshimiwa Waziri atueleze kanuni hizi sasa zimefikia hatua gani na ni lini hasa kanuni hizi zitaanza kutumika na tayari zimekuwa *gazetted* kwenye gazeti la Serikali?

Mheshimiwa Spika, naipongeza pia Serikali kwa namna ambavyo imejipanga kuzikabili changamoto mbalimbali ambapo utekelezaji wake utaleta unafuu mkubwa katika maisha ya wananchi wetu. Kasi ya kupanda kwa bei bidhaa mbalimbali ni dhahiri kwamba imesababishwa na kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia lakini pia kutopatikana kwa umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana na namna ambavyo Serikali imedhamiria kuzingatia upya tozo mbalimbali za mafuta na kuona namna ambavyo itazipunguza baadhi ya kodi ili kuleta unafuu wa bidhaa hii. Naishauri Serikali ifanye haraka katika kulitekeleza suala hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza pia namna ambavyo itatekeleza miradi ya umeme. Naiomba Wizara husika itakapowasilisha Bajeti yake basi ije na maelezo kamili ya utekelezaji wa miradi yote kama ilivyoainishwa kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha. Baada ya kuelezwaa maneno kama mchakato unaendelea, tupo mbioni, tunajipanga na kadhalika, basi tuelezwe uhalisia wa utekelezaji wa mradi wenywewe.

Mheshimiwa Spika, katika mikakati ya utekelezaji wa sera ya uwezeshaji limezungumziwa suala la Vitambulisho vya Taifa. Katika hili kila leo tumeelezwa mchakato unaendelea! Ukiangalia kwa namna suala zima lilivyozungumziwa kwenye Hotuba, bado sioni kama kuna *any definitive statement* kwenye hili suala. Namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze suala hili hasa linategemewa kumalizika lini?

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya 2011/2012, jumla ya mapato yote yaliyoainishwa kwenye Hotuba ni Sh. 13.5 trilioni, lakini kati ya fedha hizo *TRA* pekee tunategemea kukusanya Sh. 6.2 trilioni.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana *TRA* kwa kazi nzuri kwa mwaka uliopita, lakini binafsi naamini wanao uwezo wa kupanua wigo wa ukusanyaji mapato. Nashauri yafuatayo yafanyike:-

- (1) Kampuni zote *formal/ informal* zilizopo mikoani zinazojiendesha kibiashara zipangiwe mkakati wa kufikiwa na kuwekwa katika mtandao wa kodi.
- (2) Ukaguzi wa magari nje ya nchi usitishwe na badala yake magari hayo yakaguliwe humu humu nchini ili mapato yabakie humu nchini.

(3) *Yard* zote za magari/*Showroom* zitengewe eneo moja maalum ili iwe rahisi kuzitoza kodi badala ya utaratibu wa sasa kwani ni vigumu *TRA* kuzibaini *yard* hizi/*Showroom* za magari.

(4) *Propert tax* iangaliwe upya kwani majengo mengi hayalipiwi kodi.

(5) Nyumba zinazopangishwa zibainishwe na wenye nyumba hizo walipe kodi toka kwenye kodi za pango kwa mwaka.

(6) Misamaha ya kodi iangaliwe upya hasa kupitia *TIC* kwani waombaji wengi wa misamaha hiyo huishia kuitumia vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza mapato katika Halmashauri zetu, nashauri yafuatayo yaangaliwe:-

(a) Hoteli zote za kitalii zilipe asilimia tano ya fedha inayomtoza mgeni kwa chumba kwa siku (*Bed fee*). Hii itaongeza mapato makubwa kwenye zile Halmashauri zenye fukwe, mbuga za wanyama na vivutio vingine.

(b) Miradi yote ya sekta ya madini ipitiwe upya kuona endapo mapato yatolewayo na migodi yanakidhi hali halisi ya leo (yanaendana na usasa).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naipongeza sana Serikali. Ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha Bajeti nzuri, ambayo inajali wanyonge wa Taifa letu. Bajeti hii ina vipaumbele vitano ambavyo vyote ni muhimu kwa kuleta maendeleo ya Taifa letu, lakini nitachangia kipaumbele cha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, barabara ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu, msisitizo wangu katika barabara za mijini, tunapoamua kuzifanyia matengenezo barabara za mijini, tutengeneze barabara za kisasa ambazo zinahusisha njia maalum wanazopita walemvu pamoja na watu wanaokwenda kwa miguu. Sasa Serikali inabidi kutafuta wajenzi wageni ambayo wanaweza kufanya njia zetu ziwe za kisasa, maana jambo hili litasaidia kuiweka nchi yetu kuwa na barabara bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kusisitiza zaidi, kila mmoja wetu ni mlemavu mtarajiwa, kwa hivyo, tunao uwezo wa kuifanya kazi ili kuwawekea mazingira mazuri watu wenye ulemavu. Pamoja na waenda kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mia kwa mia Bajeti yetu ambayo itawapunguzia makali ya maisha Watanzania wote. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Bajeti kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na wadau wote walioandaa Bajeti. Hongereni sana, Bajeti ni nzuri, ni Bajeti ya wanyonge na imewalenga Watanzania wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hizo posho ziyaangalie makundi kama Walimu, Madaktari, Manesi na watumishi wengine kama wanajeshi na Polisi. Pamoja na mambo mazuri ya Serikali yaliyopo katika Mpango tuangalie kundi hili ni muhimu katika maisha ya binadamu na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi hayo yanafanya kazi bila kujali muda. Ni vema tukawatia moyo kwa kuwaandalia malipo ya ziada kulingana na ugumu wa kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu awabariki.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa Bajeti nzuri ya 2011/2012 ambayo imelenga na kukusudia kutatua kero za maisha ya Watanzania. Pia naunga mkono vipaumbele viliyoainishwa na Serikali. Ni ukweli usiopingika kwamba Taifa changa kama Tanzania ni lazima liwekeze katika vitu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, upatikanaji wa nishati ya uhakika. Mchango wa nishati katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ni muhimu sana. Tunahitaji nishati ya uhakika katika maisha yetu ya kila siku hasa katika Hospitali zetu na Vituo vya Afya vyote, viwandani, mashulen, na kadhalika. Nishati ya umeme ni kichochea katika uzalishaji na maendeleo ya jamii. Tunahitaji nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, pili, kilimo na umwagiliaji. Taifa letu linahitaji kuwa na uhakika wa chakula. Maji ni muhimu katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Naishauri Serikali itekeleze kipaumbele hiki cha kilimo na umwagiliaji kwa vitendo. Nasisitiza hivyo kwa sababu urari wa biashara ya bidhaa kati ya nchi yetu na jumuiya mbalimbali siyo mzuri, takribani maeneo yote tunayofanya biashara urari wetu una nakisi. Taifa letu haliwezi kuendelea kama linaagiza bidhaa zaidi kuliko tunavyouza. Nchi yetu imejaliwa kuwa na rutuba, maziwa, mito na wananchi wenye ari ya kufanya kazi. Nashauri tubadilike, tukiamua tunaweza na wakati wa kuamua ni sasa. Naomba kama Taifa tuamue kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tukipanua kilimo cha umwagiliaji, tutajenga ajira nyingi kwa makundi mengi hasi ya vijana na wanawake. Nashauri huduma za utafiti katika kilimo zipatiwe fedha za kutosha. Utafiti uelekezwe katika kutafuta aina ya mbegu zinazofaa na zinazostahimili na kuhitaji maji kidogo, kukomaa kwa muda mfupi na kutoa mavuno mengi. Huduma za utafiti zisaidie kudhibiti maradhi mbalimbali yanayoathiri maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi, Serikali iwekeze zaidi katika kusaidia wananchi kwa kuwapatia zana za kisasa ili sekta ya uvuvi ipanuke. Serikali pia iwekeze katika kujenga viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuamua kuwekeza katika miundombinu. Uwekezaji katika miundombinu utaimarisha sekta hii. Wananchi wanahitaji barabara ili waweze kusafirisha mazao yao kutoka sehemu za uzalishaji hadi kwenye masoko. Hili limeainishwa hata kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 – 2015. Hivyo kulifanikisha hili ni kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya Reli na Bandari ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu hasa kwa sababu nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia na DRC hazina Bandari, hivyo kuingiza mizigo yao kutoka nje kwenda katika nchi hizo watatumia reli zetu na Bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali yetu kuainisha ukosefu wa ajira kama kipaumbele cha kupambana nacho ni uamuzi wa kimapinduzi. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo. Wananchi wenge umri wa miaka 15 -24 na 25-64 wengi hawana ajira. Hali hii ikiendelea, nchi yetu itakuwa na wimbi kubwa la uhalifu. Watu hawa wanahitaji kuishi. Lazima Serikali iwaongoze wananchi wapambane na kutokomeza ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kutokomeza ukosefu wa ajira, nashauri Serikalii iipitie upya mitaala ya elimu (*education curricula*) ili itoe taaluma ambayo itawaandaa vijana kuweza kujiajiri mara wamalizapo masomo yao badala ya mtindo wa sasa ambao unawaandaa vijana kwa ajili ya ajira za maofisini tu.

Mheshimiwa Spika, naishauri pia Serikali kwamba, iyaelekeze mabenki kupunguza masharti ya mikopo na vile vile pawe na Mifuko ya kusaidia vijana na makundi mengine ili wapate kuajajiri.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nizungumzie kuhusu rushwa. TAKUKURU imeshindwa kupambana na tatizo la rushwa. Nashauri wa Taifa ishiriki katika kutokomeza Rushwa na kudhibiti mafisadi. Idara ya Usalama wa Taifa imefanikiwa sana katika majukumu yake. Hivyo, nina imani na idara hii kama itapewa jukumu la kupambana na rushwa katika mikakati na mafisadi, miaka mitano ijayo rushwa haitakuwepo tena au itapungua sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwe wazi katika kupambana na rushwa na wahusika watangazwe hadharani ili liwe fundisho kwa Watanzania wenge tabia chafu kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niongelee kuhusu mfumko wa bei. Nchi nyingi zimepatwa na misukosuko ya kisiasa kutokana na shida za maisha ambazo zimesababishwa na mfumko wa bei. Maisha ya wananchi huwa magumu sana kutokana

na mfumko wa bei. Naipongeza Serikali yetu kwa kuwa mwajibikaji kwa watu wake. Uamuzi wa kudhibiti bei za mafuta, vyakula unafaa kuungwa mkono na wananchi wote. Ombi langu ni kwamba, uamuzi huu uwe wa vitendo na siyo maneno matupu. Zama hizi ni za ushindani. ili tuendelee kuungwa mkono na umma wa Watanzania Serikali yetu na hasa wenzetu Mawaziri na watendaji mbalimbali ni lazima wawajibike ipasavyo. Pia pale Mtendaji anaposhindwa kufanya kazi ambayo Taifa limemkabidhi ni vema akawajibika ili asikilettee balaa Chama cha Mapinduzi kuja kukataliwa na Watanzania 2015.

Mheshimiwa Spika, ili mipango yetu na bajeti yetu iweze kutekelezeka, naomba tupunguze kutegemea misaada au mikopo kutoka nje. Sekta za madini na utalii zikitumika vizuri zinatosha kuisaidia nchi yetu kuachana na utegemezi wa nje. Mikakati ya uchimbaji madini ni mbovu sana. Haiwezekani baada ya uwekezaji mkubwa katika sekta ya madini, mchango wa sekta hii ni 2.4% katika *GDP*. Pia sekta ya utalii bado haijachangia ipasavyo. Nashauri Mikataba katika sekta hii ipitiwe upya.

Mheshimiwa Spika, upande wa matumizi ya fedha za umma, nashauri Serikali iwe kali na wanaohusika na utumiaji mbovu wa fedha za umma. Nidhamu ya matumizi ya fedha za umma isimamiwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri Serikali yetu iache kujenga majengo mapya au kukarabati majengo yaliyoko Dar es Salaam. Msisitizo uwekwe katika kujenga majengo ya Serikali Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kimsingi, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu, Mawaziri na Watendaji wote kwa mpango elekevu kwa mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwanza natambua na kupongeza hoja ya muda mrefu ya kupunguza idadi ya akaunti za fedha katika Halmashauri zetu kutoka 34 hadi 06. Hii ni changamoto nzuri ya kuongeza ufanisi wa usimamizi wa fedha. Kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuimarisha Halmashauri zetu ambazo zinazidi kudhoofika na kupata hati chafu, hati ya mashaka badala ya kuongeza uwezo wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, nchi haiwezi kuendeleza viwanda katika hali mbaya ya upatikanaji wa umeme, maji, barabara na reli. Wengi wa wawekezaji ambao wamejaribu kuingia Tanzania ili kuwekeza, wameshindwa kufanya hivyo. Kwa kuwa tumeweka dhamira yetu ya vipaumbele, sasa katika maeneo hayo muhimu lazima tuyatekeleze ili kuinua uchumi kwa kuongeza viwanda na pia kuongeza ajira. Katika Sekta ya Nishati na Madini lazima tujiulize yafuatayo:-

Nini kimekwamisha miradi ya umeme ifuatayo ambayo ilikuwepo katika mipango ya utekelezaji tangu mwaka 2000:-

- Miradi ya Kiwira na Mchuchuma;
- Mradi wa Mnazi Bay;
- Kuongeza mradi wa gesi na umeme kutoka Songosongo;
- Kutoanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa Steeglers Gorge;
- Kutotumia gesi ya Mkuranga; na
- Kuchelewa kutekelezwa miradi ya Ubungo na Morogoro.

Tunapoweka dhamira ya kweli katika mpango wa mwaka 2011/2012 na kushirikisha sekta binafsi ndani na nje ya nchi, basi tutashindwa tena katika utekelezaji wa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami na hati kwa kiwango cha changarawe ni gharama kubwa, lakini ni sehemu ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2011/2012 lazima sasa tupunguze gharama za utengenezaji wa barabara kwa kiwango cha changarawe kwa kutumia teknolojia mpya ya lami nyepesi ambayo imefanyiwa majaribio mwaka 2010 katika eneo dogo la barabara ya Muheza – Amani na kuonyesha mafanikio makubwa na kupunguza gharama za sasa kwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa kodi ya mapato unatakiwa kuangaliwa upya na hasa kuepuka kuongeza viwango katika mwaka 2011/2012 hasa baada ya kurejesha ada za kodi za leseni za biashara kwa kiwango cha Sh. 50,000/= na Sh. 30,000/= kati ya Halmashauri za Jiji/Manispaa na Halmashauri za Wilaya. Ongezeko hili linasogezza viwango kwa wale wanaolipa mapato ya Sh. 90,000/= kufikia Sh. 120,000=/. Halmashauri za Wilaya, Sh. 140,000/= katika jiji/Manispaa na kundi la pili kutoka Sh. 291,000/= hadi Sh. 321,000/= katika Halmashauri za Wilaya na Sh. 341,000/= katika Jiji. Kutokuwepo kwa viwango vikubwa vya kodi za mapato na leseni za biashara kumewezesa leo kuwepo kwa vibanda vingi vya kudumu vya biashara vilivyojengwa nchi nzima na hata katika maeneo ya nyumba binafsi. Hii ni picha ya dhamira ya wananchi kutaka kuhalalisha biashara ndogo ndogo kwa lengo la kujitegemea na kuongeza kipato. Tuboreshe mfumo wa kuzitambua biashara hizo kwa kuziandikisha kwa mpango wa *Tin Number* ili uwepo mtaji wa kundi kubwa la walipa kodi hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha Hazina imekwishapeleka fedha za miradi ya VTTP na LGCDG katika Halmashauri za Wilaya ya Muheza mwaka 2010/2011 kwa kiasi cha Sh. 420,602,682=/. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imeandika barua Kumb. Na. HW/MUH/F.60/29/107 ya tarehe 13 Juni, 2011 kuomba mafungu hayo.

Mheshimiwa Spika, adhari za kukosa fedha hizo kumesababisha kushindwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

- Ujenzi wa Kituo cha Afya Mhamba.....Sh. 61,078,000/=
  - Ujenzi wa madarasa saba ya Sekondari.....Sh. 21,500,000/=
  - Ujenzi wa nyumba tano za walimu wa  
Sekondari.....Sh. 35,000,000/=
  - Ujenzi wa vyoo matundu 18 kwa Sekondari.....Sh. 12,600,000/=
  - Ununuzi wa madawati 148 Sekondari.....Sh. 4,440,000/=
  - Ujenzi wa madarasa mawili Shule za Msingi.....Sh. 18,000,000/=
  - Ujenzi wa nyumba nne za walimu, Shule  
za Msingi.....Sh. 520,000,000/=
  - Ujenzi wa vyoo matundu 24, Shule za Msingi.....Sh. 16,800,000/=
  - Ununuzi wa madawati 104, Shule za Msingi.....Sh. 5,200,000/=
  - Ukarabati mradi wa maji - Misaki.....Sh. 24,000,000/=
  - Ujenzi wa kisima kirefu - Masiguru.....Sh. 20,000,000/=
  - Ujenzi wa kisima kirefu - Majengo.....Sh. 20,000,000/=
  - Ujenzi wa kisima kirefu - Mtindiro.....Sh. 20,000,000/=
  - Ruzuku Vijijini.....Sh. 109,984,682/=
- Jumla.....Sh. 420,602,682/=**

Mheshimiwa Spika, ni wazi fursa kubwa za maendeleo ya Wilaya ya Muheza zimekwamishwa kwa kukosa fedha hizo toka Hazina. Tunaomba maelezo kamilifu. Licha ya mapungufu niliyoinisha na kwa kuwa dhamira ya bajeti ya mwaka 2011/2012 ni nzuri, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja, lakini kwa sababu sikupata nafasi ya kuchangia kwa kusema, naomba mchango wangu wa maandishi upokelewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya maji katika bajeti hii, bado wasiwasi wangu ni utekelezaji. Mfano mradi wa maji wa “*World Bank*” haujaanza kutekelezwa hadi leo kitu ambacho ni suala la utekelezaji tu unaokwamisha mradi huu katika Wilaya ya Kondoaa.

Pili, mradi wa maji wa Ntomoko, ulioasisiwa na Baba wa Taifa mwaka 1974 hadi leo haujakarabatiwa na maji hayafikii wananchi katika maeneo karibu yote na hakuna mtu anayejali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itupatie majibu wananchi wa Kondoaa tunaotegemea mradi huu wa maji ambaa hata Rais alipokuja kwenye ziara ya kampeni alitoa ahadi ya kukarabatiwa kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali, imekuwa ikikusanya kodi na kutafuta vyanzo vingine vya mapato. Naishauri Serikali ianzishe vyanzo vingine vya mapato mfano *TV license*, naamini kama Serikali itaanzisha kodi ya televisheni, itapata kiwango kikubwa cha fedha ambazo sehemu yake ingeweza kutumika kuendesha Shirika la

Utangazaji Tanzania, *TBC*. Kwa mfano, nchini Uingereza *BBC* inaendeshwa kwa sehemu kubwa na kodi za televisheni.

Pili, kumekuwa na kodi nyingi sana za vitu vidogo vidogo sana mfano leo ukiangalia kwenye magari, hususan daladala, mbele ya kioo kuna vikaratasi vingi sana vy a kodi mfano, *fire, road license*, bima, usalama barabarani na kadhalika, hali ambayo inaonyesha wazi kuwa pesa hizi huenda hazifiki Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuondoa ushuru wa zana za kilimo. Wasiwasi wangu ni: Je, zana hizi itawafikia wakulima? Pili, naishauri Serikali kwa kutafuta suluhu ya migogoro ya ardhi na mipaka katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo ambalo Serikali imelipa kisogo ni suala la michezo. Michezo ni eneo linaloweza kutoa nafasi ya ajira kwa vijana, lakini katika Mpango wa Maendeleo na bajeti ya mwaka 2011/2012, Serikali haikuligusa kabisa. Ushauri wangu ni kwamba naiomba Serikali iondoe, ama ipunguze kodi ya vifaa vy a michezo ili viwasaidie vijana kujingiza zaidi katika michezo na kupata ajira. Leo vijana wengi wanashinda vijiweni kubishana kuhusu siasa kwa sababu hawana vifaa vy a michezo vinavyoweza kuwasaidia kufanya mazoezi. Michezo ni afya na michezo ni umoja. Tukiondoa ama kupunguza kodi tutafanikiwa. Ahsante.

**MHE. NASIB S. OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016 na hotuba ya bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wa Zanzibar wamekuwa wakipata matatizo makubwa wanapopitisha mizigo yao katika Bandari ya Dar es Salaam, miezi michache iliyopita, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitembelea Bandari ya Dar es Salaam, akapewa malalamiko haya na wafanyabiashara na Wakala wa utoaji mizigo bandarini. Rais alikubali kulishughulikia suala hili. Lakini inasikitisha hadi leo bado wafanyabiashara hawa wananyanyaswa na *TRA* bandarini na baadhi ya matatizo yao ni:-

- (i) Kutozwa ushuru mara mbili;
- (ii) Kucheleweshwa kwa makusudi kutoa mizigo; na
- (iii) Kuna rushwa iliyokithiri, huwezi kutoa mizigo bila kutoa chochote.

Mheshimiwa Spika, suala hili limekuwa likijadiliwa kila mwaka bila kuchukuliwa hatua ya kurekebisha matatizo haya. Matatizo haya yanaondoa imani ya wananchi wa Zanzibar kwa Serikali yao. Kila Mzanzibar analijua na analilalamikia. Maofisa hawa wa *TRA* wana kiburi, hawakubali kuonana na wadau ili kutatua matatizo mizigo unapozuiwa bila ya sababu. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aeleze katika majumuisho, atachukua hatua gani kurekebisha hali hii?

Mheshimiwa Spika, kodi inayotokana na mitandao ya simu inayo-operate Zanzibar, mitandao mitano ina-operate Zanzibar, nayo ni *Tigo*, *Vodacom*, *Zantel*, *Airtel* na *TTCL*, isipokuwa *Zantel*. Mashirika yaliyobaki hayapeleki fungu la kodi kwa simu zinazopigwa Zanzibar kwa Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Fedha ahakikishe kodi hiyo inalipwa kwa Serikali ya Zanzibar kwani kutokupeleka kodi hiyo kwa Serikali ya Zanzibar kunapunguza uwezo wa Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono na kupendekeza yafuatayo:-

Kwa kuwa ripoti ya mwaka 2009 inaonyesha kuwa Sekta ya Uchukuzi haikufanya vizuri kwenye miundombinu ya reli, anga na usafiri wa majini. Serikali ingetoa kipaumbele kwenye sekta hii muhimu katika kufufua urchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itafute wawekezaji wa ndani na nje ili wafufue reli ya kati, reli ya Dar es Salaam – Tanga – Moshi – Arusha na reli ya *TAZARA*. Takwimu zinaonyesha kuwa usafirishaji wa mizigo na abiria kwa reli zote ulishuka sana mwaka 2009. Hatuwezi kujenga urchumi imara bila miundombinu imara.

Mheshimiwa Spika, ni jambo linaloshangaza kuona kwamba Tanzania hatuna Shirika la Ndege baada ya *ATCL* kufa. Serikali ikaribishe wawekezaji wa ndani wafufue shirika hili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ikaribishe wawekezaji wa usafiri wa majini ili kutoa huduma kwenye jiji la Dar es Salaam ili kuondoa msongamano kwa shabaha ya kuokoa muda ili wananchi wafanye kazi za uzalishaji na maofisini kwa ufanisi zaidi ili kuleta tija.

Pia Serikali ibane matumizi yaliyo lazima kama vile manunuzi ya samani kutoka nje, manunuzi ya magari ya kifahari, safari zisizo lazima na semina na warsha nyingi. Vile vile, Serikali ipunguze pia idadi ya maadhisho/sherehe ili kupunguza ghamama na kuongeza muda wa kufanya kazi. Sherehe nyingine zifanyeke kila baada ya miaka miwili au hata mitano.

Katika kuwaongezea kipato wakulima, wapewe fursa/uhuru wa kuuza mazao yao popote kulingana na mahitaji ya soko. Wakulima na wafugaji wapewe ruzuku ya pembejeo na madawa ya mifugo mapema na kwa kiwango nafuu. Aidha, kujengwe mabwawa na malambo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji pamoja na maji kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza kuwe na sheria ya kuvuna tembo au wanyamapori wanaozidi na mazao yatokanayo na mavuno hayo yauzwe ili kutunisha

pato la Taifa badala ya kunufaisha pato la Taifa badala ya kunufaisha watalii tu. Aidha, Serikali ije na Mpango wa kuendeleza utalii wa utamaduni badala ya kuwa na utalii wa kuona wanyama tu. Hii itasaidia watalii kutembelea vijiji na kuongeza mapato ya vijiji husika na kuboresha maisha ya wananchi wa vijiji husika.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha Shule za Kata na Msingi, mikopo itolewe kwa wanafunzi wanaosoma Vyuo vya Umma tu na wale wanaosoma taaluma muhimu kama udaktari na ualimu ili kutoa fursa kwa Serikali kuhudumia maeneo mengine vizuri kama uimarishaji wa Shule za Sekondari za Kata na Shule za Msingi. Wengi wanaopeleka wanafunzi Vyuo vya binafsi wana uwezo wa kuwasomesha.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi ya kipekee kumpongeza Waziri wa fedha kwa bajeti yake ambayo ina dhamira ya kweli ya kumkomboa Mtanzania. Mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Najua ndugu zangu wa CHADEMA hawapendi kuona CCM inafanya vizuri, lakini wapinzani wa kweli huwa wanakosoa penye mapungufu kwa lengo la kuisaidia Serikali iliyopo madarakani, ijisafishe na kupongeza pale wanapoona Chama Tawala kinafanya vizuri. Hii ndiyo demokrasia ya kweli. Sio kupinga kwenye mabaya na kudai wanaigwa pale wanapoona Chama Tawala kinafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa dhamira ya kweli ambayo imeamua kuchukua kwa ajili ya kukabiliana na hali ngumu ya maisha yanayowakabili Watanzania kwa kudhibiti upandaji wa bei ya petroli kwa kuondoa tozo zisizo na tija.

Mheshimiwa Spika, nimeridhishwa sana na bajeti hii hasa Serikali ilipoamua kutoa vipaumbele vya nishati, maji na miundombinu. Angalizo ni kwamba Serikali iwe makini na kuhakikisha kwamba kuna gawiwo sawa la vipaumbele, kuna baadhi ya maeneo yanathaminiwa kuliko mengine. Hili ni tatizo. Mfano, kuna baadhi ya maeneo katika Jimbo la Mufindi Kaskazini hayajawahi kupata maji tangu uhuru. Kuna baadhi ya maeneo yapo katika vyanzo vya umeme, lakini umeme unapita juu, haupitii kwenye vijiji vinavyozunguka vyanzo hivyo, mfano, bwawa la Kihansi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa bajeti ya Waziri wa Fedha, naomba kuweka angalizo katika maeneo yafuatayo: Bajeti ya mwaka 2009/2010, 2010/2011, 2011/2012 zimeonyesha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni nyingi kuliko fedha inayotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Itakuwa ngumu sana kuondoa umaskini kama hatutaongeza fedha za maendeleo (*proverty reduction*).

**2009    2010/2011    2011/2012**

Matumizi ya Kawaida	70%	67%	62%
Matumizi ya Maendeleo	30%	33	38%

Mheshimiwa Spika, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha aondoe matumizi yasiyo muhimu ili aje aboreshe bajeti ya maendeleo. Serikali haina umuhimu wa kutumia *Land Cruiser Vx*. Serikali itapunguza matumizi ya matufa na pia

matengenezo ya magari hayo ambayo ni ghali mno. Serikali iweke angalizo la utumiaji wa mafuta hasa siku za *week end* na unakuta magari kwenye maeneo ya starehe.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yetu hasa Waziri wa Fedha ajitahidi katika mwaka huu wa fedha tupate 50% matumizi ya kawaida na 50% pesa za maendeleo. Kwa kukata maeneo yasiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajue kuwa kuna sheria ya leseni ya mwaka 2007 inayotumia leseni bure, lakini katika bajeti yake ya mwaka huu, leseni zinatakiwa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kuu, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa kuandaa bajeti nzuri na yenye kupangwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kudhibiti na kusimamia matumizi. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, lakini pia napongeza Mpango wa kuwa na *Supreme Internal Auditor* akiwa na Idara yake na sasa uteuzi wake. Tunaomba afanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu riba za mabenki, bado ziko juu sana. Riba iliyio juu haisaidii shughuli za uwekezaji na hufanya uchumi kudumaa. Serikali iangalie njia za kutazama suala la riba. Riba kubwa katika miradi yenye *gestation period* ndefu kama katika kilimo, mwekezaji hupata gharama kubwa na mara nyingi hasara.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Usalama barabarani, nyongeza ya adhabu toka Sh. 20,000/= kwenda Sh. 50,000/=, itakuwa kichocheo cha rushwa. Napendekeza ibaki hiyo hiyo Sh. 20,000/=.

Mheshimiwa Spika, napongeza urejeshwaji wa leseni. Itasaidia hasa, siyo kukusanya mapato, lakini hasa kusaidia kudhibiti au kuweka utaratibu kuhusu ni nani aruhusiwe kufanya biashara na ni nani asiruhusiwe. Leo kila kitu ni holela.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpanda Vijijini kwa kuniamini na kuniwezesha kufika Bunge Tukufu. Nami nawaahidi sitawaangusha kuhakikisha nawawakilisha ipasavyo kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi wa ngazi ya Taifa na Wilaya, Mkoa hadi matawini kwa kunipa ushirikiano mkubwa walionipa na wanaonipa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia bajeti hii. Hotuba ya bajeti ni nzuri iwapo itatekelezwa ipasavyo, kwani tumekuwa na utaratibu usiokuwa na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nianze kuishauri Serikali juu ya nishati. Pamoja na mipango mizuri ya kuboresha nishati ya umeme, bado umeme wa uhakika ni mdogo sana. Ni kwanini tunashindwa kutumia vyanzo vyetu nya makaa ya mawe yasitumike kuwezesha nishati hii itumike vizuri ili tatizo la umeme liishe katika chini hii? Lakini bado ninaiomba Serikali, nishati hii ielekezwe vijijini kwani umeme ukielekezwa vijijini utasaidia kukuza uchumi wa nchi, kwani wananchi walio wengi wanaishi vijijini na ndio wazalishaji wakubwa wa mazao mbalimbali. Umeme ukifika huko, thamani ya mazao itapanda kwa sababu kutakuwa na uwezekano wa mazao haya kusindikwa pamoja na matunda mbalimbali yanayopotea bure.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo bado halijapewa msukumo mkubwa, kwani ukitaka wakulima hawa wazalishe kwa kiwango kikubwa, Serikali iwawezeshe kwa kuwapa mikopo ya matrekta ili yaweze kuwasaidia wakulima hawa. Wakulima wakiwezesha, wataboresha maisha yao na kukuza uchumi wa Taifa. Lakini pamoja na Serikali kuandaa mpango mzuri wa kutoa ruzuku za pembejeo kwa wakulima, bado dhamira ya Serikali hajjatekelezwa ipasavyo, kwani pembejeo nyingi zinazotolewa na Serikali haziwafikii walenga. Pembejeo nyingi zinachakachuliwa na watendajji wa Serikali hasa Idara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili tuendelee, tunahitaji miundombinu mizuri ambayo itasaida wakulima walio wengi wanaishi kwa kutegemea kilimo, barabara ni muhimu sana. Ukiboresha barabara, mazao yanayozalishwa na wakulima yatapanda thamani, kwani eneo hili likiboresha tutafaulu sana kuondoa umaskini wa Watanzania. Bado katika Jimbo langu kuna tatizo kubwa sana la barabara ya Mpanda – Karema. Barabara hii ni muhimu sana ukizingatia kuwa ni barabara iendayo mpakani na kuna shughuli za uvuvi katika ziwa Tanganyika na ukiangalia, eneo hili ni la mpakani, kuna askari jeshi wanaolinda mpakani jambo ambalo tunahitaji miundombinu bora ambayo itatusaidia kuboresha huduma za wananchi waishio eneo hili. Lakini kuna barabara ya Mpanda – Mwese kuunganisha Mkoa wa Kigoma kuitia vijiji nya Lubalisi mpaka Lukoma. Barabara hii ni muhimu sana kwa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Ardhi, naiomba Serikali iharakishe mpango wa kuwamilikisha ardhi wananchi wa vijijini. Wananchi wakimilikishwa ardhi watakuwa na nafasi ya kupata mikopo ya Taasisi ya Fedha (mabenki) ili iweze kusaidia kuinua kipato cha mwananchi wa kawaida na pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo kubwa sana hasa katika Jimbo langu la Mpanda Vijijini, kuna vijiji ambavyo havijapata maji toka uhuru. Vvijiji hivyo ni Igagala, Kasekese, Vikonge, Isenga, Kasinde, Kapalamsenga, Itunya, Ikoo na Kasangatongwe. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma hii katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iboreshe Idara ya Elimu kwani kuna matatizo makubwa ya walimu kuwa na mishahara isiyokidhi mahitaji. Serikali iangalie

katika bajeti hii iwaongezee mishahara walimu, kwani wanafanya kazi kubwa ukilinganisha na kazi wanayoifanya. Pili, mazingira ya kazi siyo mazuri. Nyumba wanazoishi hazifai kwa watumishi (waalimu); tatu, madai mbalimbali wanayodai walimu walipwe haraka iwezekanavyo; nne, tutengeneze vyuo vya VETA na kuviboresha vilivyopo ili kuharakisha kutoa ajira kwa vijana ambao wanashindwa kuendelea na masomo ya juu.

Mheshimiwa Spika, uvuvi ni eneo ambalo halijafanyiwa kazi kabisa hasa katika Ziwa Tanganyika ambalo lina samaki wengi na dagaa wengi, lakini wanaovuliwa kwa uvuvi uliopitwa na wakati. Ninaiomba Serikali iangalie kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo ambao ni wengi na wakiwezesha watazalisha kwa kiwango kikubwa na kutoa mchango mkubwa kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni suala la ufugaji. Wafugaji walio wengi hawajafaidika na zao lao la ufugaji. Niiombe Serikali iwasaidie kwa kuwachimbia malambo, majosho na kuwatrafutia soko la mazao ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, makundi ya vijana na akina mama hayajaboreshwu ipasavyo kwani hawa wakiwezesha watafuta umaskini Tanzania. Nashauri Serikali iandae mpango mahsuswi wa kuwaandalia mpango mkakati na kuwapa mikopo kupitia *SACCOS* mbalimbali au vikundi watakavyoviunda.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa kusaidia wakulima wadogo wadogo hasa katika suala zima la mikopo, Serikali iboreshe utaratibu wa namna ya kuwapata walengwa wa mpango huu. Imebainishwa kuwa mikopo mingi haiwafikii walengwa, badala yake wanafaidika watu wasiokuwa na tatizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya namna ya ugawaji wa pembejeo za kilimo hasa mbolea ya ruzuku kwa wananchi. Kumekuwa na kilio kikubwa kwa wananchi kuhusiana na ugawaji wa mbolea na mbegu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza wenyewe ulemavu waanze kupata huduma za afya bure.

Mheshimiwa Spika, kwenye mpango wa umeme, Wilaya ya Kilombero isisahaulike kwa kuwa yenyewe ina migodi miwili ya kuzalisha umeme, mgodi wa Kidatu na Kihansi.

Mheshimiwa Spika, naomba tatizo la migogoro ya ardhi iondolewe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri inayotia matumaini kwa

Watanzania walio wengi. Nawapongeza vile vile Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa maandalizi mazuri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2010/2011. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mikakati mizuri iliyowekwa, ikawezesha pato la Taifa kuendelea kukua hadi kufikia 7%, pamoja na changamoto kubwa za ukosefu wa umeme wa uhakika, upandaji wa bei za mafuta na uhaba wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa uchumi mkuu umeendelea kukua, lakini haujitafsiri katika kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja. Umaskini wa kipato unaendelea kuwatesa wananchi walio wengi. Ni tatizo gani linalosababisha haya? Je, ili ukuaji wa uchumi ukue na kuwanufaisha Watanzania wa hali ya kawaida walio wengi, ni kitu gani kinabidi kifanyike?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa, inabidi tuziangalie upya na kuboresha sekta zinazobeba watu wengi. Mfano, Sekta ya Kilimo inaa jiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania, lakini mchango wake katika pato la Taifa umeendelea kuwa mdogo sana, kwani kwa sasa kilimo kinachangia pato la Taifa kwa asilimia 4.2 tu. Tunaweza kuondoa umaskini wa kipato kama mikakati iliyowekwa ya kuboresha kilimo itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mafanikio iliyoyapata katika kukusanya mapato kutoka shilingi bilioni 390 kwa mwaka 2009/2010 hadi shilingi bilioni 473 mwaka 2010/2011. Makusanyo hayo yametuwezesha kuendelea kupunguza utegemezi wa bajeti kwa wafadhili. Ninashauri na kukubaliana na mapendekezo ya Waziri kuwa wigo wa kodi inabidi uongezwe na upanuliwe. Bado kuna watu wengi wanaofanya shughuli za kibiasara lakini hawalipi kodi. Kuna vitega uchumi vingi kama majumba havilipi kodi husika.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iweke mikakati ya makusudi ya kutambua walipa kodi wapya ili mapato ya Taifa yaongezeke.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuipongeza bajeti hii, ni nzuri na naunga mkono hoja.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2011/2012. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla juu ya kuleta mapinduzi katika raslimali muda. Nchi yetu imekumbwa na kasoro kubwa ya kutojali muda. Hili ni tatizo kubwa sana na ningeshauri Serikali itengeneze mkakati wa kufanya mapinduzi katika kujali muda katika kufanya kila jambo katika jamii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia katika suala la migomo vyuoni. Naiomba Serikali ijitahidi kutekeleza ahadi zake na pale ambapo kuna tatizo, uongozi wa Serikali uende kukutana nao kabla ya kusababisha migomo. Pili, ninashauri Serikali kusitisha shughuli za siasa vyuoni. Inawezekana kule katika miaka ya nyuma wakati wa chama kimoja hali iliruhusu. Lakini kwa sasa ni hatari sana kuwahuksika wanachuo na siasa, maana iko hatari kuwa ipo siku wanachuo hawa watauana kutokana na tofauti zao za kiitikadi. Tafadhali Serikali itoe tamko la kutoruhusu siasa vyuoni na mashulenii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu na Watanzania tumepoteza mwelekeo katika suala la uzalendo. Ninashauri suala la kuanzisha masomo yenye lengo la kuelimisha kizazi chetu kijacho. Pia turudishe jeshi letu la kujenga Taifa (JKT) ili vijana wetu wajunge kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, suala la Kilimo Kwanza ni muhimu sana. Ningeshauri suala la kutafuta masoko ya mazao ya wananchi, kama kule kwenye Jimbo langu, wananchi wanalima sana mazao aina ya kunde, lakini yamekosa soko lenye bei inayofanana na gharama za uzalishaji. Moja ya mazao hayo ni choroko zao ambalo lina soko kubwa sana kwenye nchi za Asia na bei kule ni nzuri sana. Ninashauri mazao haya aina ya kunde yaingie kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani, mfumo ulioonekana kuwa ni mzuri kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono bajeti ya mwaka 2011/2012.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mungu kwa kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2011/2012 kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustapha Mkulo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza wale wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii kwa kuanzia na Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Watendaji mbalimbali waliohusika, Kamati za Bunge za kisekta kwa kuititia bajeti hii na kushauri kadri walivyoona inafaa na wadau mbalimbali walioshiriki katika kutoa maoni yao kuhusu bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2011/2012 ni sikivu na inayojibu changamoto za ukali wa maisha iwapo utekelezaji utakuwa ni wa vitendo. Bajeti hii imechukua hatua kadhaa za kupunguza makali ya maisha kwa kutangaza kupunguzwa kwa kodi katika maeneo mbalimbali na kuongezwa katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika bajeti hii ya mwaka 2011/2012 utajielekeza katika maeneo ya mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, natambua Serikali imejipanga vizuri katika kukusanya mapato ambapo kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imejipanga kukusanya karibu

shilingi trilioni 13.5, na kati ya hizo, kiasi cha shilingi trilioni 6.77 ni mapato ya ndani (mapato ya kodi – *TRA* na mapato yasiyo ya kodi) pamoja na mapato ya Halmashauri ya shilingi bilioni 350.4. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na mawakala wa mapato (*TRA*) ya kuongeza kiwango cha makusanyo ya mapato kutoka wastani wa shilingi bilioni 390 kwa mwezi mwaka 2009/2010 hadi shilingi bilioni 473 mwaka 2010/2011, bado lengo la kukusanya mapato ya ndani halifikiwi.

Mheshimiwa Spika, tatizo linalohusiana na upungufu katika makusanyo ya mapato ya ndani, ni kutoongezeka kwa wigo wa walipa kodi, kwani takwimu zinaonyesha, zaidi ya asilimia 80 ya mapato ya ndani yanayokusanywa yanatokana na asilimia 20 ya Watanzania wote wenye shughuli zinazoingiza kipato.

Mheshimiwa Spika, *TRA* imewafikia tariban walipa kodi waliosajiliwa na Tin 686,098. Idadi hii ni ndogo sana. Sheria ya kodi inatamka kuwa, kila mmoja wetu anawajibika kulipa kodi, lakini ukusanyaji kodi kutoka sekta isiyo rasmi (*informal sector*) hauridhishi. Wapo wafanyabiashara ndogo ndogo amba wanakodisha kumbi za starehe, wapo wamiliki wa nyumba wanazozipangisha kwa bei ya juu, wapo washereheshaji (*MC*) katika sherehe mbalimbali wanaopata kipato kila wiki, wapo wanaotoa huduma za vyakula (*catering services*) kwenye sherehe na matukio mbalimbali na kadhalika. Hawa wote kipato chao kinazidi hata kipato cha mfanyakazi, lakini hawalipi kodi. Hivyo naomba, *TRA* iijipange vizuri kuwafikia walipa kodi wengi wakiwemo makundi niliyoyataja kwenye mchango wangu. Katika hili la kuongeza wigo wa walipaji kodi, Serikali ihakikishe zoezi la utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya Taifa na uanzishaji wa anuani za makazi kama ilivyoelezwa kwenye hotuba ya bajeti. Zoezi hili likikamilika litawezesha *TRA* kuwafikia walipa kodi wengi.

Mheshimiwa Spika, licha ya wigo wa walipa kodi kuwa mdogo, lipo tatizo la mapato ambayo vyando vyake vimeainisha na ni vya uhakika, lakini mapato hayo hayakusanywi kwa mfano kwa mwaka 2009/2010 kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* kiasi cha Sh. 116,320,437,347/= hazikukusanywa kutoka Serikali kuu/wakala na Taasisi mbalimbali za Serikali. Kwa upande wa Serikali za Mitaa, kiasi cha Sh. 2,608,924,620/= zilizokusanywa na mawakala hazikuwasilishwa kwenye Halmashauri husika. Naiomba Serikali iwachukulie hatua kali wale wote waliohusika na kadha hiyo, na pia Serikali katika utaratibu wa kupima utendaji wa Maafisa wake. Kigezo cha kufikia lengo la ukusanyaji mapato kiwe moja ya vigezo vitakavyotumika pamoja na vigezo vingine hasa wakati wa kupandishwa cheo au uteuzi wa maafisa katika ngazi za juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imerejesha ada ya leseni kwenye Serikali za Mitaa na naipongeza sana kwa uamuzi huu, lakini nashauri Serikali Kuu kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa pamoja na Mamlaka ya Mapato (*TRA*) iandae utaratibu wa kuwezesha malipo ya kodi yaende sambamba na ulipaji wa ada za leseni ili irahisishe namna ya kuwafikia walipa kodi wengi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kushauri, linahusu misamaha ya kodi (*Tax exemption*). Natambua Serikali imejipanga kupunguza misamaha hiyo na imependekeza kuondoa misamaha kwa mashirika yasiyo ya kiserikali (*NGOs*)

isipokuwa misamaha kwa mashirika ya kidini. Hata hivyo, kwa mwaka 2009/2010 misamaha ya kodi ilikuwa karibu shilingi bilioni 680 kati ya hizo *NGOs* zilipewa shilingi bilioni 22. Mashirika ya kidini yalipata misamaha shilingi bilioni 28, Sekta ya Madini ilipata misamaha ya shilingi bilioni 48, taasisi za kiserikali shilingi bilioni 52 na kadhalika. Hivyo kuondoa misamaha ya kodi kwa *NGOs* ambazo ni karibu shilingi bilioni 22 tu, nadhani haina mchango mkubwa sana. Naiomba Serikali iangalie upya misamaha hiyo ya kodi hasa katika Sekta ya Madini. Mchango wa madini katika pato la Taifa ni mdogo sana, na ukweli unabaki pale pale kwamba madini haya yatakwisha. Kwanini Serikali isianzishe kodi ya raslimali (*resource tax*) katika madini yetu?

Mheshimiwa Spika, sioni sababu ya Makampuni ya madini kupewa misamaha ya kodi kwenye mafuta ambapo kuna tetesi misamaha hiyo itatumia vibaya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi wa busara wa kurudisha ada ya leseni kwenye Serikali za Mitaa, hatua ambayo itaongeza mapato kama inavyojidhihirisha kwenye makadirio ya makusanyo ya mapato kutoka shilingi bilioni 172.6 kwa mwaka 201/2011 mpaka shilingi bilioni 350.4 mwaka 2011/2012. Hivyo, nashauri Serikali kuangalia upya viwango vilivyopewa, kwani viwango vilivyowekwa ni *flat rate*, havizingatii uwezo wa kila mfanyakishara. Mfano, mamlaka za miji kiwango cha Sh. 50,000/= kwa wafanyakishara wa aina zote (wakubwa na wadogo) inaweza isisaidie sana katika dhana ya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, suala la kuboresha viwango vya kubakiza maduhuli (*retention*) kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kama inavyoelezwa kwenye ukurasa 45 wa kitabu cha bajeti mwaka 2011/2012 linahitaji kuangaliwa upya kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kifungu 11 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 ambayo inashurutisha mapato yote yanayokusanya na Serikali kuu yanatakiwa kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sera ya kubakiza maduhuli (*retention scheme*) ni kinyume cha matakwa ya Katiba, na inachangia sana kuwa na matumizi mabaya ya pesa hizo na ongezeko kubwa la matumizi kwa mafungu husika hasa pale sera ya kubakiza maduhuli inakuwa na asilimia 100. Nashauri Serikali izingatie matakwa ya ibara ya 135 ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ijitahidi kubuni vyanzo vingine vya mapato, kuendelea kutegemea vyanzo vya vinywaji baridi, vileo vikali, sigara kama vyanzo vya kuongeza mapato upo wakati Serikali yetu itakwama hasa watumiaji wa vileo/sigara wakiamua kupunguza utumiaji wa bidhaa hizo. Natambua Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliopitishwa na Bunge hivi karibuni, umejitetahidi kuainisha vyanzo vipyta/mbadala vya mapato kati ukurasa 79 – 82 wa kitabu cha Mpango. Naiomba Serikali iharakishe mchakato wa majaribio ya vyanzo hivyo hasa katika kuangalia namna gani Watanzania wanaoishi nje ya nchi watakavyoweza kuchangia pato la Taifa kuitia shughuli zao zinazowaletea mapato (*Tanzanians in the diaspora*).

Mheshimiwa Spika, napongeza mikakati yote iliyowekwa na Serikali juu ya kudhibiti matumizi katika kitabu cha bajeti ya mwaka 2011/2012 kuanzia ukurasa wa 50 mpaka 55, hatua hizo ni pamoja na kuimarisha ukaguzi wa mishahara (*payroll audit*) na kupanga kufanya sensa ya watumishi wote wa Serikali na taasisi (*national pay day*) na kuwawajibisha Wakuu wa Idara na Maafisa Wahasibu kwa malipo ya mishahara hewa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Ndani, na kwa uteuzi wa Mkuu wa Idara hiyo. Sambamba na hilo, naipongeza Serikali kwa kuunda nafasi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Msaidizi. Hawa wote watashughulikia usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa (Mhasibu Mkuu Msaidizi) na kusimamia masuala ya ukaguzi wa ndani katika Serikali za Mitaa (Mkaguzi Mkuu wa Ndani).

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa uamuvi wake wa kupunguza idadi ya akaunti za benki katika Halmashauri hadi zifiki sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 katika jitihada za kudhibiti matumizi ya fedha, kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuboresha utoaji wa taarifa za mapato na matumzi.

Mheshimiwa Spika, napongeza uamuvi wa Serikali wa kusitisha ununuvi wa magari ya aina zote, ununuvi wa samani za ofisi hususan zile zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, kupunguza malipo ya posho mbalimbali yasiyokuwa na tija na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali ihakikishe bajeti hii inasimamiwa vizuri ili iwe bajeti inayotekelzeza. Serikali iimarishe kitengo cha ufuatiliaji na tathmini ili kuona bajeti hii na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano inatekelezwa kwa ufanisi. Tukithubutu inawezekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2011/2012.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika ripoti ya *Global Financial Integrity 2008* yenye mada ya *Illicit Financial Outflows from Africa*, ripoti hiyo inaonyesha kuwa kwa kipindi cha miaka 39 tangu mwaka 1970 mpaka 2008, ripoti hiyo inasema Tanzania imepoteza shilingi trilioni 11.6 na ni nchi ya 13 kati ya nchi 20 za kwanza Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hesabu ya shilingi trilioni 11.6 ilifikiwa kwa kuitia akaunti ya majina ya wahusika: Je, Serikali imetekeliza vipi taarifa zilizopo kwenye ripoti hiyo (*global financial integrity – 2008*)?

Mheshimiwa Spika, kuhusu leseni za biashara, kwa kuwa Halmashauri za Wilaya zitakusanya katika maeneo ya miji midogo na vituo vya biashara na Halmashauri za vijiji katika maeneo yake: Je, vijiji vilivyopo kwenye miji midogo na vituo vya biashara zitapataje mapato?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSA KHAMIS SILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kupongeza wadau wote wa Wizara ya Fedha kwa kuandaa bajeti nzuri sana yenye kutenga maslahi ya wanyonge.

Pia naishukuru Serikali kwa kuweka kipaumbele katika suala la umeme. Suala la umeme ni tatizo katika ukuaji wa uchumi wetu kwani kutokana na tatizo la umeme viwanda vinashindwa kufanya kazi zake za uzalishaji. Pato la Taifa linaanguka kutokana na kuyumba kwa uchumi wa Taifa letu unaotokana na viwanda na biashara. Ushauri wangu ni kwamba *TANESCO* iongeze nguvu kwa kukaribisha wawekezaji katika suala zima la umeme. Hiyo itasidia kupunguza lawama nyingi kwa Serikali. Tukiangalia mfano wa *TTCL*, simu zilikuwa tatizo, lakini baada ya kukaribisha wawekezaji, huduma za simu zimeenea nchini kote.

Pia eneo la ushuru katika mafuta, naomba ushuru upunguzwe kodi ili kushusha bei ya mafuta. Kupanda kwa bei ya mafuta kunasababisha bei za vyakula kupanda na bidhaa zote zinazosafirishwa zinapanda bei. Pia *EWURA* wawe makini katika kuzilinda bei za mafuta kuwa zinapoanza kupanda, zinapanda haraka sana, lakini kushuka ni tatizo.

Ushauri wangu ni kwamba, kukinga hali hiyo, boyo la *SBM* bandarini lifanyiwe haraka na mfumo wa *bulk procurement* uanze haraka, labda itasaidia kudhibiti upandishaji wa bei za mafuta kwa kasi sana. Lakini hiyo pia haitoshi, ni vyema tukaanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta. Tukiwa na Hifadhi yetu kubwa ya mafuta, hata bei zikipanda katika Soko la Duniani, hifadhi itasaidia kulinda soko la ndani japo kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Bajeti ya Mapato na matumizi ya mwaka 2011/2012.

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na uchukuzi katika hotuba yake nzuri ya bajeti. Pamoja na hayo, napenda kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote waliowezesha kufanikisha maandalizi ya bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ambayo ipo mbele yetu. Hata hivyo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali kupunguza umaskini nchini, bado hali siyo nzuri katika Mkoa wa Mtwara na hasa Wilaya ya Nanyumbu. Hivyo, naiomba Serikali iweke mazingira mazuri yanayoweza kuwaondolea umaskini uliokithiri kwa wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Maeneo kama Sekta ya Kilimo yakiimariswa, yataweza kuwakomboa wananchi wa Nanyumbu. Tukiwapatia zana nzuri za kilimo, tukiwapatia wakulima huduma za ugani, tutaweza kuwainua na kuwaondolea umaskini. Bei nzuri za mazao ndiyo eneo moja linaloweza kuwaondelea umaskini wananchi wa Nanyumbu. Kwa mfano, mwaka huu wakulima wa Nanyumbu walilima sana zao la choroko. Walivuna choroko nyingi, lakini ufinyu wa bei umewaacha

wakulima hawa wabaki na umaskinini wao. Hivyo, naiomba Serikali isimamie bei za mazao mchanganyiko ili wakulima wasidhulumiwe.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la kuboresha na kujenga miundombinu imara ndani ya Wilaya ya Nanyumbu. Nanyumbu haina barabara nzuri Ndani ya Wilaya, hivyo, ili wakulima wa Nanyumbu waweze kusafirisha mazao yao kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji, hali ni mbaya sana Wilayani Nanyumbu, kuna shida kubwa ya maji na hivyo kuwafanya akina mama ambao ndio wakulima wakubwa kutumia muda mrefu na kutembea umbali mrefu kutafuta ndoo moja tu ya maji. Hivyo, ninaiomba Serikali kuitopia Wizara ya Maji kutupatia au kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi. Kero ya maji ni kubwa mno Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eimu, hali ni mbaya sana Wilayani Nanyumbu. Kuna uhaba mkubwa sana wa vyumba vya madarasa, matundu ya choo, uhaba wa walimu pamoja na uhaba wa madawati. Naomba bajeti hii itoe ufumbuzi wa matatizo haya Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima, naomba kuwasilisha mchango wangu kuhusu Bajeti ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Bajeti na uandaaji wake una matatizo ya kimsingi. Ili kusimamia sera za uchumi mpana, Serikali inatekeleza mpango wa uchumi (*Policy support instrument*) ambao umekubaliana na *IMF*, mpango huu pamoja na mambo mengine una malengo yanayopimika ikiwa ni pamoja na fedha ambayo Serikali itakopa kutoka katika mabenki ili *program* ya *IMF* ikamilike Serikalini, inaonekana kukubaliana na shirika hili, mfumo wa kibajeti.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa bajeti ambao Serikali imekubaliana na *IMF* ni tofauti na mfumo wa bajeti unaotolewa kwa mfano mwaka wa fedha wa 2010/2011, bajeti iliyotolewa Bungeni na kuitishwa ilikadiria kutumia kwa ajili ya matumizi ya kawaide na maendeleo jumla ya shilingi trilioni 11.6, lakini katika *program* ya *IMF* Serikali ilipanga kutumia shilingi trilioni 10.1 tofauti ya shilingi trilioni 1.5. Matumizi halisi ya Serikali yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 10.4. Matumizi haya yako karibu sawa na *program* ya *IMF* kuliko bajeti iliyotolewa na Serikali na kuitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwanini Serikali haiwi wazi inapoleta bajeti Bungeni kuwa inafuata mpango wa *IMF*?

Kwa upande wa mapato ya ndani, Serikali ilikadiria kukusanya shilingi trilioni 6.176 ikijumuisha mapato yanayokusanywa na Halmashauri. *Program* ya *IMF* mapato ya Serikali yatakuwa shilingi trilioni 5.652. Serikali inatarajiwa kukusanya shilingi trilioni 5,726 ambayo imezidi kidogo tu mapato yaliyokadiriwa katika *program* ya *IMF*.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu wa fedha, Serikali imeleta bajeti yenyе jumla ya matumizi ya shilingi trilioni 13.53, lakini katika *program* ambayo Serikali imekubaliana na *IMF* matumizi yote katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 ni shilingi trilioni 11.26 tofauti ya shilingi trilioni 7.126 (ukijumlisha mapato yanayokusanywa na Halmashauri) *program* ya *IMF* inaonyesha mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 6.397. Kwa maana hiyo, Serikali inahakikisha kuwa makini sana kuwa program ya *IMF* inatekelezwa mfumo huu wa kuruhusu matumizi kwa kadri ya mapato yaliyopo, yaani *Cash budget*. Kwa maana hiyo, bajeti ambayo inapitishwa na Bunge ambayo ndiyo maamuzi ya Watanzania wote haiheshimiwi hata kidogo. Hivyo huku ni kuiburuza Tanzania isijitegemee (Hii ni hatari).

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanaelewa hivi na hii baadaye inaweza kuleta mzozo mkubwa kiuchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, bajeti yenyе kujitegemea hata kama malengo hayakufikiwa ni muhimu sana tuache kutegemea *IMF policy*.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha inaonekana ni kubwa na tegemezi zaidi kuliko ya mwaka wa fedha uliopita kitu ambacho ni hatari sana. Jambo hili tungweza kulidhibiti endapo tutakuwa macho na vyanzo vya mapato yetu mfano *TRA*, madini, utalii, viwanda, reli pamoja na miundombinu mingine bila kusahau umeme. Vitu hivyo kama vikisimamiwa vizuri na kwa kumaanisha, bajeti yetu isingekuwa tegemezi kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei na kuperomoka kwa thamani ya shilingi yetu ni vitu ambavyo vinaathiri uchumi wetu sambamba na maisha ya Watanzania wengi walio masikini. Pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kuboresha maisha ya wananchi, bado kunatakiwa juhudhi za makusudi za Serikali kuhakikisha kuwa wananchi hawaumizwi sana na hali hii, Serikali idhibiti mfumuko huu wa bei za bidhaa muhimu kama vile Sukari, Unga, Mahindi, Maherage na Mazao yale ambayo wananchi wanayazalisha kuhakikisha yanapata bei nzuri katika masoko ya dunia, sambamba na kuimarisha masoko ya ndani.

Mheshimiwa Spika, aidha, suala la kuboresha Vyuo mbalimbali vya Ufundii hususani *VETA* ili vijana wetu waweze kupata ajira, basi katika hili Serikali imaanishe ili tatizo la ajira lipungue. Katika Mikoa ambayo inazalisha matunda kwa wingi kama vile Tanga, viwanda vya kusindika matunda vijengwe ili kuongeza ajira kwa vijana. Benki zetu zisimamiwe katika kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya wanawake na vijana kuhakikisha kuwa riba inayotozwa isiwaumize sana au isiwe kubwa. Katika hali hii tatizo la umasikini na ajira pia litakuwa limetatuliwa kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya utalii yaboreshwe kwa kutengenezewa ama kujenga barabara nzuri ili mbuga zetu zifikike kwa urahisi na hivyo kuongeza pato la Taifa, kodi za magari kwa wale wanaowapeleka watalii ipunguzwe ili vijana/wananchi wetu wafaidi jasho lao.

Mheshimiwa Spika, aidha, suala la utawala bora ni muhimu sana. Serikali iwe macho inapofanya manunuzi ya vitu isiletetatu vitu visivyofaa na wanaokwenda kujadili manunuzi hayo wawe ni waaminifu. Serikali isisite kuwachukulia hatua wale viongozi wote wanajihusisha na vitendo vya rushwa, kwani hao ndio hasa wanaolisababishia Taifa hasara kubwa na hivyo kusababisha uchumi wa nchi kuperomoka. Miradi yote isimamiwe vizuri, uaminifu iwe ni sifa mojawapo kubwa ya kiongozi kupewa heshima ya kusimamia miradi mikubwa ya Serikali au kufanya manunuzi ya vifaa, mitambo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia watumishi Serikalini wapewe mishahara mizuri ambayo pengine itawafanya wafanyakazi kutoa huduma kwa moyo mkunjufu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kinachotakiwa ni vitendo, ili Taifa letu liweze kujikwamua na utegemezi usio wa lazima. Sehemu kubwa tujitegemee wenyewe. Kila mtu akitimiza wajibu wake, Tanzania yenye neema inawezekana. Vianzishwe Vyuo muhimu maalum vya maadili kwa ajili ya kuwanoa viongozi amba watakuwa ndio wasimamizi wakuu wa raslimali za Taifa kwa sababu inaonyesha Watendaji wengi wamekuwa wakihujumu juhudini za Serikali.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naanza kwa kuipongeza hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha ambayo imetoa dira ya kuinua hali ya maisha ya Watanzania na hasa wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali katika maelezo yake, imeainisha jinsi ya kupunguza tozo mbalimbali za mafuta na hiyo itapelekeea kupunguza makali ya gharama mbalimbali katika maisha ya kila siku na hasa kwa wananchi wa vijiji, ili kuwa na uhakika wa azma hii ni lazima kutengeneza mazingira ambayo wananchi watapatiwa ujuzi katika kilimo, uvuvi, mifugo na kazi mbalimbali za mikono Hili liwe kwa wanawake na vijana. Kwa hivi sasa vijana wengi wanaomaliza shule au vyuo hawana cha kufanya hii itawasaidia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina uwezo mkubwa sana wa kuwatafutia soko wajasiriamali hao kwa kutumia Wizara na Idara husika. Natoa mfano, nchi mbalimbali za Asia na hata mabara ya Ulaya tunaona ni jinsi gani bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo na wakati wa nchi hizo kuuza nje ya nchi na hata hapa Tanzania tunazona. Je, Serikali imejipanga vipi katika uendelezaji wa utaratibu huu amba ukifanikiwa tutatokana na kuwa katika kiwango cha 15% ya pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, ili kuinua kipato cha wananchi ni lazima kuangalia ni vipi tunatengeneza mazingira mazuri ya wananchi amba ndiyo mtaji wa kufufua uchumi amba watakuwa endelevu. Nchi yetu ina neema ya utajiri wa kutosha katika raslimali za misitu, bahari/maziwa, mito, mifugo na kilimo, ambapo pia na Serikali itakusanya mapato yake badala ya kusubiri kodi za vileo na sigara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ukatekelezwa kwa ukaribu, umakini na uadilifu zaidi utaongeza pato la Taifa kwa asilimia zisizopungua 45% au zaidi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema, hayo yakitekelezwa, hali ya umasikini nchini itapungua. Naipongeza tena hotuba hii na naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa hotuba nzuri na yenye kutia matumaini, iliyosomwa Bungeni wiki iliyopita.

Mheshimiwa Spika, naamini bajeti hii itasaidia sana katika kusukuma maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania na hususan Jimbo langu la Siha. Wakati utakapofika wa kupitisha bajeti hii, uwe na hakika kuwa wananchi wa Siha tutakuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, hongera sana.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufikia siku hii na wakati kama huu kuweza kuichangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, bajeti husika siyo ya chama kimoja, yaani siyo ya upinzani wala tawala bali ni ya Watanzania wote. Kwa mantiki hii, ningeshauri kuwa tutakapofika kutoa uamuza wa bajeti ya kutumika mwaka ule wa 2011/2012, Serikali isiwe na ajizi ya kuchukua mapendekezo mazuri kutoka bajeti iliyopendekezwa na wapinzani kupitia Mheshimiwa Zitto Kabwe na kuitumia katika kuboresha bajeti ya Serikali ya Mheshimiwa Waziri Mkulo na Mheshimiwa Kigoda.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe angalizo na msisitizo wa kuwapatia bajeti nzuri wananchi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

Serikali kutoka na mikakati mahususi ya kuwa na ujasiri wa kuwatambua mafisadi, yaani wale wanaosababisha kupanda kwa bei ya petroli ambayo ndicho chanzo cha kupanda bei karibuni kwa vitu vyote muhimu kama chakula na vifaa vya kufanya kazi kama pembejeo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya wafanyabiashara wa mafuta ambaو wanataka kuipotosha Serikali kuwa bei ya mafuta ya taa, ipandishwe bei ifanane na petroli, hoja hii haifai kabisa kwani kufanya hivyo ni kutaka kuwakandamiza wanyonge wote wa vijijini na mijini ambaو hutumia majiko ya mafuta ya taa kwa kupikia na kutumia vibatari na taa kwa kuwasha. Tatizo kubwa ni lile lile la kuacha kutumia mafuta ya taa na kutumia mkaa. Sasa hili nikirudi kwenye jambo bayu zaidi la kuharibu mazingira, maana tutakuwa tumeongeza mahitaji ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la Serikali, kuna mikakati yake. Ni jambo la kuzuia utoroshaji wa fedha kupitia njia za kiujanja ujanja mfano, bila kufikiria kuwa ni

ubaguzi wa rangi hawa wenzetu wenye asili ya Asia/Kihindi wanapaswa kufanyiwa mkakati wa kujua kwa uhalisi kutokana na biashara zao wanahifadhi kiasi gani kwenye mabenki ya hapa ndani na kiasi gani wanatoa nje ya nchi kwa njia zipi? Ama ni kiasi gani wanatunza ndani ya nyumba zao? Siyo hilo tu, wenzetu hawa mara nyingi wanakuwa na uraia zaidi ya mmoja. Hivi wengi wao wana akaunti India kwao, Uingereza, Canada na kadhalika. Hawa pia ni wenye maduka ya fedha nayo huyafanya hivi hivi kutorosha fedha kwenda nje.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la kutilia mkazo ni kukomesha wizi wa mali ya umma kwa makusudi na kwa kupanga. Ni tabia zimejengeka za watu kuwaibia watu mamilioni ya fedha kama siyo mabilioni na watu hao kuachia tu hata wakati mwingine kupewa adhabu kidogo isiyofanana na thamani ya kile walichoiba au kupoteza. Ushauri mzuri ni kuifanyia kazi Sheria ya Uhujumu Uchumi. Sheria hii inaruhusu kumfilisi mtu yejote atakayebainika kuwa ameneemeka kwa mali ya ujisadi. Hili likitekelezwa, litazuia ujisadi. Mfano, sasa hivi wafanyakazi wengi wafanyao katika mashirika yatoayo huduma zinazohusiana na kodi au kukamata wahalifu kama *TRA* na *Jeshi la Polisi*, wengi wao wana mali zisizolingana na vipato vyao hata ungezidisha mara tano kupato hicho kisingefikia mali walizonazo. Jambo hili lifanyiwe kazi mapema, itasaidia sana pia katika kuwezesha sheria za ulaji rushwa kufanikiwa. Siyo hivyo tu, bali tutakuwa tunasaidia kizazi kisichopenda mapato yasiyolewaka na hivyo kuimarisha uadilifu katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu pia wa kufanya hima kuwezesha baadhi ya *NGO's* zetu ziwe na uwezo wa kufanya shughuli ambazo Serikali inashindwa kuzifanya kuititia idadi ndogo ya wafanyakazi wake. Mfano, siyo vibaya kutenga mafungu ya kuzipa *NGO* zifanyazo vizuri ziweze kufanya kazi za utoaji wa elimu ya uraia, kilimo, ufundi, Teknohama, afya kwani wenzetu hawa wana uzoefu na mitandao yao ni *well organized*, yaani imepangiliwa vizuri. Siyo vibaya kwa Serikali kuchukua nafasi ya kuyajengea uwezo baadhi ya mashirika yetu na kuyapandisha hadhi kuwa kama mashirika ya nchi zilizoendelea ambayo yana mashirika kama *MSAID*, *NORAD*, *GTZ*, *NIMD* na kadhalika na huyatumia hata nje ya nchi zao kuendeleza ajira za watu wao na utamaduni wao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Naomba nihitimishe kwa kusema nitaunga mkono iwapo bajeti hii itazingatia kutumia baadhi ya mapendelekezo muhimu yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani, Kamati ya Fedha na Uchumi kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Abdallah O. Kigoda, pia na maoni yangu niliyotoa katika dokezo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi na wataalamu, wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha, lakini pia naunga mkono bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2011/2012 imekuja na vipaumbele vitano, umeme ukichukua kipaumbele cha kwanza. Kwa mujibu wa mipango ya *Tanesco*,

Wilaya ya Ngorongoro/Loliondo ilikuwa ipate umeme mwaka 2015. Lakini sasa umeme wa Jenereta utawashwa kati ya mwezi Julai na Agosti mwaka huu, miaka minne mbele ya mpango wa *Tanesco*. Naishukuru sana Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Spika, katika suala la miundombinu, hiki ni kipaumbele cha tatu katika bajeti ya mwaka huu. Naipongeza sana Serikali ya CCM kwa kukubali kujenga barabara hii ya Mto wa Mbu – Engavesero – Loliondo kwa kiwango cha lami licha ya upinzani mkubwa kutoka kwa wana mazingira na mashirika ya kimataifa ya wanyamapori kwa hoja kuwa barabara hiyo itaathiri mfumo mzima wa ikolojia ya hifadhi ya Serengeti ambayo ni urithi wa ulimwengu. Ujenzi wa barabara hii, siyo tu umewekwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2010/2015 bali pia imetengewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.6 katika mwaka huu wa fedha. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kutetea kwa nguvu ujenzi wa barabara hii kwa manufaa ya wananchi wa Ngorongoro/Loliondo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro hususani Tarafa ya Ngorongoro inakabiliwa na tatizo la njaa, kutokana na mambo yafuatayo:-

- (1) Ukame wa miaka mitatu mfululizo;
- (2) Kudhoofika na hatimaye kufa kwa wingi kwa mifugo inayotegemewa na wafugaji kwa asilimia mia moja kwa chakula na mahitaji mengineyo;
- (3) Volcano ya mlima Lengai imechangia pia kwa kiwango kikubwa kukausha majani, uoto wa asili na vyanzo vya maji na hivyo kuathiri malisho ya mifugo na wanyamapori; na
- (4) Kupigwa marufuku na Serikali, kilimo cha kujikimu (Bustani) katika Tarafa ya Ngorongoro ambayo pia ni hifadhi mseto (*A multiple land use Area*).

Mheshimiwa Spika, Ngorongoro tunaomba chakula.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Micheweni, naomba nichangie kwa maandishi hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hotuba hii kimaelezo ni nzuri sana kiasi ambacho wananchi walio wengi walipoisikia ikisomwa iliwapatia matumaini makubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini kinyume na maelezo ya bajeti hii, mimi niseme bajeti hii kwa kiasi kikubwa haiwezi kumsaidia mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika nianze kuchangia kwenye kilimo. Serikali ya awamu ya nne ilitangaza Sera ya kilimo kama ni sekta iliyopewa kipaumbele katika kauli mbiu yake “Kilimo Kwanza” lakini bado bajeti ya Wizara hii haioneshi umuhimu huo kivitendo kutokana na fedha zilizotengwa ili kukabili mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa kilimo unatarajiwa kukua na kufikia wastani wa 5.5%. Watanzania wengi walipata matumaini mara baada ya kutangazwa kwa sera ya Kilimo Kwanza kuwa sasa wataondokana na matatizo mengi ambayo wanayakabili katika kujiondolea umasikini kupertia sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huo ambao kilimo kimepewa, lakini mchango wa kilimo katika pato la Taifa unatarajiwa kupungua kutoka 21% mwaka 2010 hadi 18.7% mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, wakati tunapotangaza mipango mbalimbali yenyе kuleta matumaini kwa wananchi, ni lazima tuwe makini kusimamia ili wananchi waone kweli Serikali ipo kuwasaidia na sio kufanya siasa.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu. Vilevile kama ilivyo Sekta ya Kilimo, elimu ni Sekta inayotarajiwa kutimiza matarajio mengi ya Watanzania. Serikali imetoe vitabu vya kiada na ziada kwa wanafunzi Shule za Msingi ili kuwapunguzia wananchi wanyonge wa Taifa hili mzigo wa kununua vitabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010 inaonyesha kuwa hadi kufikia Desemba, 2010 Shule nyingi za Msingi zimepokea fedha zisizozidi Sh. 60,000/= hadi Sh. 30,000/= kwa kazi hiyo kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, hii ni kuelewa kuwa wananchi wetu wengi hawana uwezo wa kununua vitabu, lakini jambo la kushangaza 40% ya ruzuku maalum inayotolewa na Serikali kwa lengo hili. Hapa ni lazima tuijulize, hiki kiasi kingine cha fedha kinakwenda wapi? Kama fedha hizi za umma zinatengwa kwa ajili ya shughuli hizi na zimetolewa, lakini bado tunazungumzia tatizo hili kwa ukubwa ule ule kila siku. Hii sio hali ya kuipuuzia, ni lazima tufikirie upya ili kuwajengea imani wananchi kuwa kweli tupo Serikalini kuwapunguzia kero na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wake, Makatibu wakuu na timu yake yote kwa kuwasilisha bajeti inayojali kupunguza makali ya maisha ya wananchi kukuza uchumi na kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeza Wizara/Serikali kwa kuja na vipaumbele muafaka na vinavyowajali wananchi wote. Iwapo bajeti hii itatekelezwa na kusimamiwa kwa umakini, italeta tija kubwa kwa maendeleo ya nchi na watu wake.

Mheshimiwa Spika, msingi wa bajeti ni mapato. Hivyo kuna umuhimu wa kupanua vyanzo vya mapato yetu badala ya kutumia vyanzo vile vile. Kuna haja ya kuangalia eneo hili kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza umaskini, kuna umuhimu wa kuelekeza nguvu vijijini ambako ndiko kwenye uzalishaji mkubwa. Nishati vijijini ni muhimu ili kufungua fursa nyingi zaidi ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa viwanda vya mazao. Viwanda vidogo vidogo na kadhalika. Hata hivyo, bajeti ya umeme iliyowekwa ni kidogo mno kwa kukuza uchumi vijijini.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa ardhi vijijini upewe kipaumbele na kwa gharama nafuu ili wananchi waweze kutumia raslimali ardhi kama dhamana ya mikopo kutoka Benki kama mtaji wa maendeleo na hususan uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuongeza uzalishaji uende sambamba na uongezaji thamani ya mazao na kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpungeza Mheshimiwa Dk. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa alioifanya kuhakikisha bajeti ya mwaka huu 2011/2012 inakuwa ya historia, kwani imewajali Watanzania wa kada zote, yaani wanawake, vijana, wazee, watu wenye ulemavu, wajane, yatima, wafanyakazi, wakulima, wafugaji, wajasiriamali na masikini.

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kutokana na simu au ujumbe (*message*) kutoka kwa wananchi mbalimbali hasa wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Mustafa Mkullo - Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Gregory George Teu - Naibu Waziri, Mheshimiwa Pareira Ame Silima - Naibu Waziri wa fedha, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imekonga nafasi za Watanzania. Ninawaombea Mwenyezi Mungu awape afya, maisha marefu na mshikamano ili waweze kutekeleza azma yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Wanawake na Watoto ninaipongeza sana Serikali kwa kuwajali wanawake kwa njia ya kuwatengea mfuko wao, wanawake ili waweze kukopeshwa fedha za kuwasaidia kukuza mitaji yao ya kuendeshea miradi yao midogo midogo. Serikali bado haijawafikia wanawake walio wengi kuwapa elimu ya kuendesha miradi na namna ya kutunza fedha; Halmashauri nyingi hazitekelezi agizo la kutenga fedha za asilimia kumi kwenye mfuko wa wanawake na Serikali haikemei wala kutoa adhabu; Halmashauri hazifuatili marejesho ya mikopo hiyo kwa wanawake; Serikali inatenga fedha ndogo kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto ndio maana hata Wizara inapeleka fedha ndogo kwenye akaunti ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali sasa iweke mikakati madhubuti ya kusimamia mfuko huu pamoja na kuuboresha.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu kodi ndogo kwenye Halmashauri na Kata, napenda kuishukuru Serikali kwa ubunifu wake wa kuibua vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwa ni pamoja na kurejesha kodi ndogo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninatoa angalizo kwa Serikali kuwa makini katika kupeleka maelekezo kwenye Halmashauri zetu, kwani wasije wakaanza kuomba ushuru wa nyanya na biashara nyingine ambazo wananchi masikini wanafanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa angalizo kwa Serikali kuwa makini na taarifa mbalimbali zinazowasilishwa na Watendaji wetu. Uzoefu wangu unaniambia kuwa Watendaji wengi wanakusanya takwimu Mezani, hawaendi vijijini kutafuta taarifa (*data*).

Mheshimiwa Spika, ninapata wasiwasi kuwa hata takwimu za kipato cha kila mwananchi kwenye Mikoa yetu, mfano Singida siyo sahihi. Ninampongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Singida Dk. Parseko Kone, tatizo hili ameliona na amekemea.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali itafute takwimu upya za uzalishaji kwenye Mikoa yetu ili tupate takwimu zilizo sahihi. Hii itasaidia kuweza kutoa mgawo unaotosheleza walengwa wa kila Mkoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kuwajali wananchi wa Mkoa wa Singida kwa kuwaunga mkono katika ujenzi wa Hospitali ya Rufaa, wazo ambalo alilianzisha Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Dk. Parseko Kone na akaanza ujenzi kwa fedha alizotafuta kwa wahisani yeye mwenyewe. Nimeipongeza Serikali kwani tulipoomba msaada ilikubali na ilianza kutenga shilingi bilioni mbili kila bajeti pamoja na bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuijulisha Serikali kuwa, kwa kutenga shilingi bilioni mbili kila bajeti, hospitali itajengwa kwa miaka mingi sana. Hivyo, ninaiomba Serikali kuongeza kiwango cha fedha ili tuweze kumaliza ujenzi huu mapema. Hospitali ambayo itatoa huduma hata Mikoa jirani. Ninasubiri kauli ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Hii itasaidia sana wachimbaji wadogo wadogo ambao wote ni wazawa na itapunguza migogoro kati ya wachimbaji wadogo wadogo na wawekezaji. Vilevile itawasaidia kununua vifaa, kwani wengi wao huwa hawana na itasaidia kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vifaa vya uchimbaji ni ghali sana na vingi hutoka nje, ninaiomba Serikali kupunguza kodi ili kusaidia wachimbaji wadogo wadogo kumudu bei zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za *TACAIDS* ninaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Mfuko wa Ukimwi. Nina matumaini mfuko huu utasaidia sana kuongeza nguvu ya kuwa na mfuko wa kudumu ambao utakuwa endelevu kwa zoezi zima la kupambana na Ukimwi. Hivyo ninaiomba Serikali kuusimamia mfuko huu

pamoja na Serikali kutenga fedha za kutosha ili kupunguza utegemezi kwa wahisani. Ni ukweli usiojificha kwamba Serikali inatenga fedha ndogo sana, fedha nyingi tunategemea za wahisani.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali kwa kupokea ombi la wananchi wa Singida kujenga Mahakama kuu Singida. Napenda kujua kuitia bajeti hii ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono bajeti hii nikitegemea kuwa mchango wangu utapewa kipaumbele na maeneo ninayohitaji majibu nitapewa wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ina maeneo mawili muhimu. Kwanza, eneo la ukusanyaji mapato na pili, ni lile la matumizi. Mchango wangu utajikita kwenye eneo la ukusanyaji wa mapato.

(a) Misamaha ya Kodi inatupotazea fedha nyingi sana ambazo kama zingeingia kwenye Mfuko wa Taifa, zingesaidia sana kuboresha maisha ya Watanzania: Mheshimiwa Spika, ninatambua kuwa zipo Sheria mbalimbali za Misamaha ya Kodi ikiwa ni pamoja na ile ya Uwekezaji, chini ya (*TIC*), Misamaha ya Kodi inayotokana na *Government Notice, GN No. 479 (2002), GN. No. 55 na 113 za mwaka 2004, IPTL, GN. No. 247 ya 2001*, pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Hesabu za Serikali, tarehe 15 Aprili, 2009, *TRA* waliahidi kuchukua hatua za kupunguza misamaha ya kodi ili kuongeza Pato la Taifa. Leo taarifa zinaonesha kuna misamaha ya kodi imefikia asilimia 2.5 ya Pato la Taifa mwaka 2010/11, kiasi cha Sh. 869.6 bilioni hadi Machi, 2011. Kiasi hiki ni kikubwa kuliko hata msaada wa Wafadhili katika Bajeti ya Taifa kwa mwaka. Hii ni aibu, tunatembeza bakuli kuomba misaada, huku tunasamehe zaidi ya kiwango hicho. Ningependa kujua ni hatua zipe zilizochukuliwa toka mwaka 2009, *TRA* walipoahidi Bunge kuchukua hatua kupunguza misamaha?

Mfano msamaha wa mafuta ya petroli kwa Makampuni ya Migodi ya Madini ni takriban 27 bilioni; hii ni Bajeti ya Halmashauri 27 ya Road Fund. Hii ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama hili linafanyika kwa nia ya kuwavutia wawekezaji, huko siyo kuwavutia ila ni kuliwa mchana mchana, wawekezaji watavutiwa na mazingira bora ya uwekezaji ikiwemo, miundombinu, kuondoa urasimu, amani, utulivu na kadhalika. Ninaungana na Kamati ya Fedha na Uchumi, kupendekeza misamaha ya kodi isizidi asilimia ya Pato la Taifa.

(b) Ukusanyaji wa mapato katika maeneo yasiyo ya kodi (*Non Tax Revenue*): Bado upo udhaifu mkubwa katika eneo hili na kwa kiasi kikubwa, baadhi ya maeneo hata makadirio yaliyowekwa ni ya chini sana kuliko hali halisi.

Mheshimiwa Spika, eneo hili likitiliwa mkazo, litafidia pale ambapo Wananchi wanachangia katika Miradi ya Maendeleo. Sote tunajua kuwa, hali ya maisha ya Wananchi ni ngumu na Wananchi ni maskini sana; kama huo ndiyo ukweli, basi jitihada ziwepo kuwawezesha na siyo kuwakomoa kwa kuwataka wachangie fedha katika Miradi ya Maendeleo. Watu hawa maskini, wanalipa Mfuko wa Elimu shilingi 5,000 au 10,000 kwa mwaka, Bima ya Afya shilingi 5,000 hadi 10,000 kwa familia na hususan kila familia baada ya mafanikio ya elimu nchini na kuwepo kwa Sekondari za Kata, ina mwanafunzi mmoja au zaidi ambaye anasomeshwa! Ninashauri Serikali ilione jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuandaa Bajeti nzuri na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako, kwa ajili ya kuijadili na hatimaye kuipitisha. Pamoja na hayo, ningependa nichangie Bajeti katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo linalowaumiza Watanzania wengi na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi ni kupanda kwa bei ya mafuta ya aina mbalimbali yakiwemo, *diesel, petrol*, mafuta ya taa na kadhalika. Pamoja na ukweli kwamba bei ya mafuta imepanda sana duniani kutokana na machafuko/vita katika nchi zinazozalisha mafuta duniani, lakini ukweli mwingine ni mafuta hayo kutozwa kodi nyingi sana zaidi ya 20; hali hiyo imechangia sana ongezeko la bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ahadi ya Serikali ya kuzipitia upya kodi hizo ili kupunguza au kuzifuta, bado Serikali haikuweka jambo hili wazi kwa maana ya kiasi gani cha kodi na fedha kinatarajiwa kupunguzwa. Bado Wananchi hawaelewi. Ninaishauri Serikali ilifanyie kazi jambo hili mapema inavyowezekana ili bei ya mafuta ipungue na kutoa nafuu ya maisha kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Watanzania wengi wanamiliki pikipiki, hasa za Kichina, kwa matumizi ya kawaida na zaidi kwa biashara. Hata hivyo, pikipiki hizo ambazo nyingi zina cc kati ya 125 – 200, hutozwa kodi ya mwaka ya Sh. 95,000, sawa na gari (taxi) zenye cc kati ya 900 – 2000. Sidhani hii kama ni sawa; kutoza kodi sawa kwa vitu viwili tofauti, gari na pikipiki; ni kuwaonea Wananchi wenye uwezo mdogo unaowafanya wamiliki pikipiki na siyo gari.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iliangularie suala hili upya ili wafanyabiashara wa pikipiki wapunguziwe kodi hiyo. Ikumbukwe kwamba, wamiliki walio wengi wa pikipiki hizo ni vijana; ninachelea kusema kwamba, wasiposikilizwa wanaweza kuichukia Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kama kuna kundi kubwa la Wananchi ambao hawatendewi haki, basi ni wastaafu na wasimamizi wa mirathi kwa watumishi waliofariki. Ninasema hawatendewi haki kwa sababu hawalipwi mafao yao mara tu baada ya kumaliza utumishi wao Serikalini au baada ya kufariki dunia. Watumishi wengi wametoa mchango mkubwa kwa Taifa hili, hakuna sababu ya kuendelea kutowalipa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe mfano; hadi mwaka 2008/2009, wastaafu na wasimamizi wa mirathi kwa watumishi waliokuwa watumishi wa *TAZARA*, walikuwa wanadai zaidi ya shilingi bilioni 40, hivi ninavyoandika kiasi hicho kitakuwa kimeongekeza. *TAZARA* kama Shirika, lilishaiomba Serikali iingile kati ili kulipa deni hilo. Ninafurahi kwamba, Serikali ilishakubali kuubeba mzigo huo na ndiyo sababu *CAG* aliingizwa afanye tathmini ya deni la wastaafu na wasimamizi wa mirathi wa *TAZARA*, kazi ambayo ilishakamilika. Sasa ninataka kujua ni kiasi gani (fedha halisi), kinadaiwa na Serikali ina mpango gani wa kulipa deni hilo kwa wastaafu na wasimamizi wa mirathi wa *TAZARA*?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe wastaafu hao hawajalipwa kuanzia mwaka 2006/2007; inashangaza na kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali imekuja na Mpango mzuri kwa Sekta ya Kilimo, lakini upatikanaji wa mikopo kwa wakulima siyo wa kuridhisha, hasa kwa wakulima wadogo, bado masharti ya mikopo kupitia Dirisha la Kilimo (TIB) ni magumu sana. Dirisha hili linaonekana kama kufaidisha zaidi wakulima wakubwa. Bado riba za mabenki ni kubwa sana, kwa ujumla zinakatisha tamaa wakulima.

Ninashauri upatikanaji wa mikopo uwe mkubwa kwa wakulima wadogo sanjari na upunguzaji riba kwenye mikopo hiyo. Benki ya Kilimo inayokusudiwa kuanzishwa na ambapo tayari fedha zimetengwa, iwe na matawi Mikoani au Kanda, kwa kuanzia kuweka huduma hizi Dar es Salaam ni kuwapa mzigo usio wa lazima wakopaji. Aidha, Mfuko wa Pembejeo uongezewe pesa ili Wananchi/Wakulima wengi wafaidike.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali imeahidi kuangalia upya suala la posho, basi ninashauri ifanye hivyo mapema ili zile posho zisizo na tija kwa watumishi wote wakiwepo Wabunge ziondolewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, ninachangia kupitia maandishi katika Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2011/2012. Bajeti hii kwa kadiri nilivyoipitia ni ya kisanii, ambayo haitoi majibu ya hali ngumu na mfumko wa bei, inayowakabili Watanzania maskini.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bei ya petroli duniani, ambayo inatumika kama sababu ya kupanda wa gharama za maisha ni ndogo mara dufu, ukilinganisha na bei ya petroli hapa nchini. Hii inatokana na kodi kubwa ya Serikali na tozo nyingi kwenye

bidhaa hiyo muhimu nchini. Ninashauri Serikali kama kweli inataka kumsaidia Mtanzania maskini wa vijijini na mjini, waondoe kabisa kodi kwenye bidhaa ya mafuta ya petroli na kufuta tozo nyingi zilizojaa kwenye bidhaa hiyo ili Watanzania waweze kufaidi uhuru wao walioupigania kwa trakriban miaka 50 sasa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu bado inaendelea kukumbatia aibu ya Wananchi wake kuishi katika nyumba za makuti katika maeneo mengi ya Tanzania, nchi iliyojaa kila aina ya rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu hakufanya makosa kuziweka Tanzania. Ninaishauri Serikali isimamie kwa uadilifu matumizi bora ya rasilimali zetu na kuzuia hongo na rushwa ndani ya mikataba na kwenye sekta zilizozunguka rasilimali zetu. Rasilimali zilizojaa ndani ya nchi yetu zikitumika vyema, hatutahitaji kukopa mikopo ya aibu, iliyojaa kila aina ya dhuluma kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali iache mpango wa kukopa ovyo kwenye mabenki ya kibishara na ijielekeze katika kusimamia matumizi bora ya rasilimali zetu ili kutoa unafuu kwa maisha ya Watanzania. Bajeti hii bado imekuwa ni tegemezi, kwa kiasi kikubwa tukiwategemea wahisani kwa masuala yote ya maendeleo na kiasi kikubwa cha fedha kikipelekwa katika masuala ya utawala na uendeshaji wa nchi. Huduma za kilimo, pamoja na misamiati ya muda mrefu kwamba, kilimo ndiyo utu wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, imetengewa kiasi kidogo sana cha fedha.

Mheshimiwa Spika, bado kwa bajeti hii Tanzania itaendelea kushikilia mkia kwa kuendelea kuongoza kuwa mionganoni mwa nchi maskini Duniani. Utatengeneza barabara na kuweka miundombinu, lakini kama wananchi hawapati maji safi na salama, wataendelea kutumia maji yaliyochanganywa na kinyesi kwa matumizi ya nyumbani huku tukiendelea kuzika Watanzania wasio na hatia kutoptana na maradhi ya kipindupindu, malaria na *typhoid*.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mchango wangu katika Bajeti hii ya Mwaka 2011/2012. Ninaomba kuwasilisha ila mambo mazuri hayataki haraka, lakini chelewa chelewa utakuta mtoto si wako.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, nami NInachukua nafasi hii kuchangia katika Bajeti ya Serikali ya 2011/2012.

Kwa mtazamo wangu ninaona kuwa, Bajeti hii haijajitosheleza, kwani imemfanya Mtanzania acae mkao wa kula huku chakula hakijaiva.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, Bajeti ina sura mbili kwa jinsi inavyojonesha: Kuongeza madeni nchini; na kuwapa Watanzania matumaini yasiyoteklezeka kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia pato la ndani litokanalo na kodi ni *almost six trillion* wakati matumizi yaliyoainishwa ni trilioni 13; sasa je; kama hizi fedha nyingine,

yaani mikopo ya ndani, mikopo ya misaada ya nje na mikopo ya masharti ya kibashara, zisipopatikana matumizi haya yatafanikiwa?

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, ichukue hatua madhubuti za kusimamia uchumi wa nchi ukue, ukizingatia kuwa kikwazo kikubwa ni uwezo wake wa kuongeza mapato yatakayokidhi matumizi. Serikali isimamie vipaumbele vyote vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano ili kupunguza upandaji wa gharama za maisha, mfumko wa bei za bidhaa mbalimbali mfano mafuta, umeme na kadhalika; isimamie maboresho ya reli, barabara zipitike vijijini kwa wakulima ili wapate urahisi wa kusafirisha mazao yao kutafuta masoko.

Serikali pia isimamie uchimbaji wa visima hasa vijijini ili wapate maji salama kwa afya zao, kwani afya ni muhimu sana katika maisha ya wazalishaji hao wa kilimo, ambao wengi wapo vijijini. Tuahidi kwa vitendo na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Watendaji wake Wakuu wote. Pia ninampongeza Waziri wa Fedha, kwa Hotuba yake nzuri, inayotia moyo kwa Watanzania wengi na tuna matumaini makubwa kuwa Bajeti hii itasidia kuongeza kasi ya kuwapatia maendeleo ya kuondokana na umaskini wa kipato unaowakabili Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ninataka kugusia Halmashauri zetu zenyet matatizo mengi ya kukosa maendeleo, hii inatokana na Serikali Kuu kuchelewesha kupeleka fedha kwa wakati na hivyo, Miradi mingi kudumaa au kuchelewa na hata fedha hizo zinapofika zinakuwa siyo kama zilivyopangwa katika Bajeti husika. Hivyo ninaishauri Serikali kujitahidi sana kupeleka fedha kwa wakati wa kuhakikisha kwamba tatizo hili linatatuliwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, imetangazwa kuwa mwaka huu wa fedha, samani zote zinatengenezwa na kununuliwa humu nchini, kwa maana hiyo Serikali haitoagiza kutoka nje. Hili ni jambo zuri kwani Tanzania tunayo miti mingi na mizuri, pia tunavyo viwanda vingi vya kutengenezea samani; ninapongeza hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kuwa; je, Serikali imechukua hatua gani ya kuhakikisha samani zitakazotengenezwa zitakuwa na ubora mzuri (*quality*) kama zile zinazoagizwa kutoka nje ili kuondoa kile cha kujivunia baadaye kununua au kuagiza nje?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPHINA T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa Hotuba yake nzuri sana.

Ninaipongeza Kamati husika. Pia ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine, kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nichangie katika Bajeti hii. Bajeti hii ni nzuri sana na imetulia, kwani imegusa makundi yote; vijana, akina mama, watoto na akina baba.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 20118/2012, ina vipaumbele vifuatavyo:-

kwanza ni umeme, mishati ya umeme ni muhimu sana katika maisha ya Mtanzania wa kawaida. Umeme unarahisisha maisha yetu. Niiombe Serikali ijitahidi sana kutimiza ahadi zake inazozitoa kwa Wananchi wake. Umeme siyo starehe au anasa, bali ni maendeleo.

pili, ni maji, maji ni muhimu sana katika maisha ya Mtanzania; hivyo, ninaomba Serikali iliangalie tatizo hili kwa macho mawili; kwa mfano, tatizo la ukosefu wa maji Mkoani Geita limekuwa likichangia kwa kiasi Fulani, kukua kwa umaskini, kwani akina mama wengi wamekuwa wakitumia muda mwangi sana na nguvu nyingi katika kutafuta maji badala ya kufanya kazi zao za kila siku za ujenzi wa Taifa.

Tatu, miundombinu, miundombinu kwa Taifa letu ni tatizo; ninaishukuru sana Serikali kwa kuliona hilo. Mkoa wa Geita ni Mkoa mpya, kwa maana hiyo unakabiliwa na changamoto nyingi; barabara mbovu, kwa mfano, barabara inayotoka Geita – Msalala kupitia Nyang'wale ni mbaya sana, ninaomba Serikali iifikirie.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kwa kuipongeza sana Serikali inayoongozwa na chama chetu cha Mapinduzi, Chama Dume, kwa umakini wake katika kujali na kusikia vilio vya wanyonge na Wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Kwanza Mwanamke nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa Hotuba yake nzuri, aliyoiwasilisha Bungeni hapa kuhusu Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja (2011/2012).

Mheshimiwa Spika, ninapenda nianze na suala la riba zinazotozwa na taasisi zinazohusika na utoaji mikopo nchini. Kutokana na nchi yetu kuwa na Wananchi walio wengi maskini na wafanyakishara walio wengi huonesha kushindwa kuendeleza biashara zao kutokana na ukubwa wa riba inayotakiwa kulipwa kwa kipindi fulani kutokana na mkopo waliochukua, ninaomba Serikali iangalie upya namna ya kuzitaka taasisi hizo kupunguza riba wanazotoa. Nchi yetu inaandaa mikakati mbalimbali ya kuondokana na umaskini, lakini umaskini hautaondoka kama hatukuzingatia namna

mbalimbali zinazosababisha umaskini huo. Tutaondokana vipi na umaskini wakati biashara ni moja kati ya mwendelezo wa maisha bora ya binadamu kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKUKUTA, Mkakati huu ni mzuri sana, bila shaka Serikali haikuwa na maana kwamba, kuletwa kwa Mkakati huu tufikie kiwango kilichopo sasa. Ninaiomba Serikali izingatie changamoto zilizojitokeza Kipindi cha Pili cha MKUKUTA. Serikali ihmize ufuatiliaji na usimamizi wa hali ya juu, kwa mantiki ya kumwendeleza Mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezwaji wa Sekta ya Elimu Nchini, ninaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi trilioni 2.283 katika Sekta hii, ikiwa ni ongezeko la 12 la kiasi kilichotengwa mwaka uliopita. Ushauri kwa Serikali katika Sekta hii na nyinginezo:-

- Walimu walioajiriwa kufanya kazi eneo fulani iweke mkakati wa miaka kumi bila kuhama, baada ya kipindi hicho kama anataka kuhama anaweza akajibowi kufikiriwa.
- Wengine walimu hawakai maeneo waliyopangia kufanya kazi.
- Shule zilizojengwa kila Kata zipate walimu wa kutosha.
- Serikali iweke MKAKATI wa kuweka Maabara kila shule moja ya sekondari ili mtaala wa sayansi uweze kukua nchini.
- Serikali ihmize Wananchi kuhusu kuchangia chakula cha mchana mashulenii ili wanafunzi wapate nafasi ya kuwa shulenii kwa muda mrefu bila kuondoka.
- Kuhimiza ufuatiliaji katika kila sekta na utendaji ulio bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, ninaunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, NIaunga mkono hoja iliyopo mbele yetu na ninakubaliana na Vipaumbele Mkakati vitano vilivyoainishwa kwenye Bajeti hii kama ifuatavyo: Nishati; Miundombinu; Kilimo (mifugo na uvuvi); Maji na Raslimali Watu.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa fika kuwa, kila moja ya vipaumbele hivi kimebeba majukumu mahususi mfano: Kilimo kimebeba dhana ya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji; maji yamebeba dhana ya maji safi ya kunywa kwa matumizi ya binadamu, wanyama, umwagiliaji (kilimo cha kisasa) na kadhalika; rasilimali watu nayo ina dhana pana zaidi, kwa maana ya elimu (taaluma yenyewe mashulenii, vyuoni, weledi na kadhalika); na afya kwa maana ya ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Bajeti hii kwa kuinua kiwango cha Pato la Taifa kwa asilimia saba. Ninapongeza kwa azma nzuri walionayo ya kupunguza na

kudhibiti ongezeko la bei ya chakula, mafuta, huduma na kadhalika. Ongezeko la ajira kwa Watanzania ni jambo la msingi, kwani itasaidia sana ukali wa maisha, tuwe washauri. Serikali ifanye kila wavezalo hilo lifanyike, vijana ni hazina ya nchi yoyote duniani. Kukosekana kwa ajira ya vijana ni bomu, tujihadhari.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kutoagiza samani (*furniture*) ni jambo la kupongezwa, kwani litapanua ajira nchini na vilevile kuzuia fedha kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na mawazo kuwa Serikali itumie *constructors* wa ndani zaidi, wenye sifa, kuliko wa nje hasa kwa Miradi iliyo na chimbuko la fedha za ndani; na Wananchi waendelee kuwezeshwa kwa kupewa fedha kwa mikopo au ufadhili.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kujishughulisha na kazi za uvuvi hasa wa baharini na kuwekeza kwa vijana, hili nalo ni la msingi. Bahari ni rasilimali kubwa Mungu aliyotupa, unachotakiwa kuwa na *manpower* ya kutosha na vifaa; huhitaji kupanda, kulima, wala kumwagilia, unavyokwenda ndiyo utakavyovuna. Samaki wana soko kubwa ndani na nje ya nchi, la muhimu ni kujipanga.

Mheshimiwa Spika, ninaona sasa umefika wakati wa kuinua Zao la Ngozi kwa kuhakikisha Tanzania tunatumia ngozi kwenye viwanda vyetu kikamilifu. Tujiipange ngozi yetu yote itumike ndani kwa matengenezo ya vitu mbalimbali kama vile viatu, mikoba, mabegi mikanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, inasemekana Tanzania tunaagiza viatu kutoka nje zaidi ya shilingi bilioni 90 kwa mwaka, viatu ambavyo ni makaratas; kwa nini basi Serikali haijipangi na kuanzisha uzalishaji wa viatu kwa matumizi ya vikosi vyetu hapa nchini, viatu kwa matumizi ya wanafunzi mashulenii kuanzia sekondari na vyuo kwa *spirit* ya tutukuze vyetu? Dhana hii itakuza ajira kubwa kwa vijana nchini. *Product* zetu ni nzuri, hata mabegi yanayozalishwa ni mazuri, kubwa hapa ni kupanga na kujiamini tu.

Mheshimiwa Spika, inawezekana, tutimize wajibu wetu.

**MHE. MONSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninampongeza Waziri wa Fedha, kwa Bajeti nzuri, inayolenga kuleta maisha bora zaidi kwa kila Mtanzania. Ningependa kuchangia yafuatayo:-

Njaa: Jimbo la Kwimba, kuna njaa kubwa, ninaomba Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, ifuatilie hilo tatizo kwa karibu.

Sera ya Mapato: Ningeshauri dhahabu inayozalishwa kwenye migodi mikubwa, iuzwe kupitia Benki ya Tanzania na pia iuzwe kwa pesa zetu za Tanzania, yaani wanunuza walipe dola zaidi ya 60 halafu wachukue TSh. wapeleke kila mgodi na mgodi ubakie na TSh.; hii itafanya pesa zetu zipande thamani. Mwekezaji alitaka anunue kwa dola zaidi ya 60, siyo kama ilivyo hivi sasa wanaauza dhahabu pesa zinabaki nje haziletwi hapa kwenye uchumi wetu.

Misamaha ya kodi ya forodha ihamie kwenye *income tax*, maana yake a-declare faida ili aweze kurudisha *investment* yake, siyo kama ilivyo hivi sasa.

Kilimo Kwanza, nashauri wananchi wanaomiliki mashamba ya miwa wapate hati miliki; hii itakuwa mtaji mkubwa kwao na watakuwa wamejiandaa vizuri, siku Benki ya Kilimo ikifunguliwa, basi wakulima watakuwa tayari kupata mikono ili waweze kuboresha maisha yao.

Matrekta ya JKT yangesambazwa Halmashauri zote nchini na yauzwe huko huko. Wakulima wa Kwimba wanataka kununua matrekta lakini yapo Dar es Salaam.

Miundombinu, Mheshimiwa Rais, aliahidi barabara ya lami kutoka Magu – Ngudu – Hungumarwa, ninaomba Waziri wa Miundombinu alifuatilie suala hili.

Umeme, Jimbo la Kwimba lina kata 15 lakini umeme upo kwenye Kata moja tu na katika Kata ya Hungumarwa kuna Programu ambayo ni zaidi ya miaka kumi; ninaomba Serikali iangalie hili suala angalau lipate majibu. Tuna *Ginnery* ya Pamba ya Mwalujo na Sangu nazo zinaomba zipate umeme. Hizi *ginnery* zina mchango mkubwa kwa Wakulima wa Pamba.

Pamba, napongeza mwaka huu bei imeboreshwa kutoka Sh. 600 – 1,100, bado ninaomba Serikali ipandishe bei, bei ya chini iwe Sh. 1,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii kushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Bajeti ilioletwa mbele yetu ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia Bajeti hii katika maeneo yatuatayo:-

Viwanda, nchi yoyote inayoendelea, suala la viwanda ni jambo ambalo linapewa msukumo maalum ili kuwezesha bidhaa zinazozalishwa ziweze kusaidia Taifa kuuza nje na kupata fedha za kigeni na pia kusaidia kuleta ajira zaidi katika nchi. Hivyo basi, ninaishauri Serikali ivipatie msukumo maalum, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutoka ili kuvisaidia viwanda vyetu.

*TRA*, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya wafanyabiashara kuhusu utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), baadhi ya malalamiko ni kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa TRA wamekuwa na mtindo wa kukataa *invoice* halali zinazopelekwa na wafanyabiashara na badala yake wanapandisha bei kwa matakwa yao. Mfano, ukiagiza gari Japani, ukipeleka *invoice* uliyonunulia inakataliwa halafu wanapandisha mara tatu zaidi ya bei iliyonunulia. Hivyo, ninaomba Serikali ipeleke mawakala wao katika nchi ambazo zinauzwa magari zaidi, yaani Japani, Dubai na

kwagineko, wafanye uhakiki mara tu mtu anaponunua gari, litakapofika hapa itaondoa mkanganyiko wa bei kama inavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali na hili linatokana na ushirikiano mkubwa kati ya Maofisa wa *TRA* wasiokuwa waaminifu. Maeneo mawili yanayoongoza katika ufujaji huo ni Mafuta ya *Transit* na Mizigo ya *Transit*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipoteza pesa nyingi kwa mafuta ambayo hupitia Dar es Salaam kwenda nchi jirani, lakini idadi kubwa ya mafuta hayo huishia kuuzwa hapa hapa ndani ya nchi yetu. Hivyo hivyo na kwa bidhaa za kontena; hivyo basi, ninaiomba Serikali ifuutilie kwa karibu kadhia hii ili ifikie malengo yake ya ukusanyaji wa mapato na mkazo zaidi uelekezwe katika mipaka ya Kasumulu – Tunduma, kwani haya ni maeneo ambayo yakidhibitiwa vilivyo, nina hakika mapato ya Serikali yataongezeka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012, kama ilivyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuongelea juu ya matumizi makubwa ya Serikali hususan katika ununuzi wa magari ya Viongozi wa Serikali na Taasisi zake, gharama kubwa ya mafuta na dizeli na petroli kwa magari hayo na hata uendeshaji juu ya matengenezo.

Mheshimiwa Spika, haiingi akilini hata kidogo kwa nchi maskini kama Tanzania, Watendaji wake kutumia magari ya kifahari na ya gharama kubwa, namna hiyo ambapo hata wale wanaotupa misaada Viongozi wao wa Serikali, hawatumii magari kama hayo. Ninapenda kuishuri Serikali kuwa, magari yote ya Watendaji wa Serikali, maarufu kama mashangingi, yauzwe na badala yake wanunuliwe magari ya bei nafuu ili kuwapunguzia mzigo Wananchi. Aidha, ninaitaka Serikali ibadili utaratibu wake wa kuwakopesha fedha za kununulia magari Mawaziri amba pia ni Wabunge. Mawaziri hao amba ni zaidi ya 50, wamekopeshwa kila mmoja shilingi milioni 90 kwa ajili ya kununua magari ilhali wao wanatumia magari ya Uwaziri na hivyo, milioni 90 hizo hawanunulii magari na badala yake wanafanya shughuli zao binafsi. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi, ambazo zingeweza kupelekwa katika Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la Mifuko mbalimbali, ambayo ilianzishwa na Serikali kimantiki kwa ajili ya kuviwezesha Vikundi Maalum katika jamii kama vile Wanawake na Vijana. Kipekee, nizungumzie Mfuko maarufu kama Mabilioni ya JK. Serikali imekuwa ikitoa mabilioni ya fedha kila mwaka kwa ajili ya makundi hayo, lakini kutokana na utaratibu mbovu uliowekwa, fedha hizo zimekuwa haziwafikii walengwa na wala hawana taarifa kuwa Serikali inatoa fedha hizo kwa ajili

yao. Fedha hizo zainatolewa kuitia katika mabenki ambayo yako mijini ilhali Wananchi wengi wanaozihitaji wako vijiji na hata nauli ya kuwafikisha mjini hawana.

Mheshimiwa Spika, ninaitaka Serikali iangalie namna nyingine ya kufikisha fedha hizo kwa walengwa kama vile SACCOS, VICOBA au vikundi vingine vilivvopo katika jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi ni eneo lingine ambalo linaikosesha Serikali mapato. Taarifa ya *TRA* inaonesha kuwa, misamaha ya kodi kwa mwaka 2010/2011, ilikadiriwa kuwa ni asilimia 2.5 ya Pato la Taifa, wakati jirani zetu Kenya na Uganda wakitoza wastani wa asilimia moja ya misamaha ya kodi. Cha kusikitisha zaidi ni kwamba, wanaosamehewa kodi kwa kiwango cha juu ni watu binafsi na Makampuni ya Madini, ambayo yanafanya biashara kubwa na kwa faida kubwa. Ninakubaliana na Hotuba ya Bajeti ya Kambi ya Upinzani kuwa, misamaha yote ya kodi sasa isizidi asilimia moja ya Pato la Taifa. Katika mwaka 2010/11 pekee, jumla ya Sh. 869,575.37 milioni zilisamehewa.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa kasi kwa bei za mafuta ni eneo muhimu, ambalo Serikali imeshindwa kulidhibiti. Pamoja na ukweli kuwa, bei ya mafuta ni kubwa katika soko duniani, Serikali bado ina nafasi ya kuangalia upya ukokotoaji wa bei ya mafuta hapa nchini, ambapo bei za mafuta ni za juu sana na hivyo kupandisha kwa kasi mfumko wa bei za bidhaa muhimu.

Pamoja na kwamba, Serikali imekubali kupunguza tozo mbalimbali zinazotozwa na baadhi ya taasisi kama vile *TRA*, *TBS*, *TIPPER*, *EWURA* na kadhalika, bado Serikali haijasema tozo hizo zitapunguzwa kwa kiasi gani ili hatimaye ziweze kupunguza bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika tozo hizo, zipo Taasisi za Serikali ambazo huzitoza bila hata kufanya kazi iliyokusudiwa. Mfano, *TRA* hutoza *Destination Inspection Fee* 1.2 % ya *FOB*, wakati *Destination Inspection* inafanywa na wenye mzigo wenyewe na siyo *TRA*. *TRA* imekuwa ikikusanya pesa hii nyingi kwa kuwaibia walaji/wanunuzi wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, katika ukokotoaji wa bei za mafuta, zipo tozo ambazo hutozwa kwa Dola ya Marekani badala ya Shilingi ya Tanzania. Mfano, gharama za kuweka vinasaba kwenye mafuta (*marking fees*), ambayo hutozwa kwa Dola ya Marekani ilhali mafuta yanakuwa tayari yapo nchini. Hali hii hufanya bei ya mafuta kwa mtumiaji wa mwisho kuwa ya juu sana. *TBS* nayo hujinufaisha kwa kuwa na tozo mbili katika lita hiyo hiyo ya mafuta. *TBS batch certification fee 0.2% of C & F* na *TBS application and testing fee U\$D 0.38/MT*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Serikali kupanua wigo wa mapato na makusanyo ya kodi. Njia zifuatazo zinaweza kutumika:-

Kwanza, kunyanya Sekta ya Uvuvi ambayo kwa sasa inachangia asilimia 1.4 tu. Kwa kufanya hivi, kutaongeza mchango wa Sekta hii kwa Pato la Taifa na vilevile kutoa ajira kwa vijana.

Pili, mchango wa Sekta ya Mifugo bado ni mdogo. Serikali itengeneze mazingira ya wafugaji kunufaika na Sekta hii. Serikali iwekeze katika kutoa mbinu bora za ufugaji, kutengeneza masoko ya ndani na nje kwa ajili ya nyama, jibini na ngozi.

Tatu, wigo wa walipa kodi bado ni mdogo, kuna haja ya Serikali kuingia katika Sekta Isiyo Rasmi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kufanya *assessment* ya kodi inayotakiwa kulipwa kwenye uingizaji wa magari, ufanywe kwa utaratibu uliopo kwenye sheria; ina maana, kufuata *stages* za *options (1) to (3)* na asiachiwe mtu mmoja kufanya tathmini jinsi yeye anavyoona, hii italeta mianya ya rushwa na hivyo Serikali kupoteza mapato.

Mfano, wafanyabiashara wanaouza spea na vyombo mbalimbali, hawatou risiti na hasa Wahindi. Pia wale wanaouza nguo au kushona, wanakusanya fedha nyingi lakini hawalipi kodi.

*Traffic Offences:* Ninashauri faini hiyo ya Sh. 50,000 iwe kwa mtu ye yeyote anayevunja Sheria za Usalama Barabarani, zikiwemo za madereva wa pikipiki. Ajali zinazoongezeka sasa ni za pikipiki, tusiachie hili, lazima tukazie faini maana hawa madereva hasa wa pikipiki, wengi wao hawana hata leseni. Tusilet siasa kwenye hili.

Bei ya mafuta, ili kuzuia uchakachuaji wa mafuta ya dizeli na mafuta ya taa, bei za mafuta ya taa na dizeli ziwe sawa au tofauti iwe kidogo sana. Hili lina athari sana kwa uchumi kwa kuwa uchakachuaji unaharibu sana magari na hivyo kutumia fedha nyingi kwenye matengenezo ya magari hayo.

Kiwepo kipengele kwenye Mikataba kuwa muwekezaji asifanye *transfer* ya *ownership* au kuuza kwa makusudi ili kukwepa kulipa kodi ya Serikali kama Hoteli ya Movenpick, Mohilel *et cetera* ili muda ule uliotolewa kwa yule mwanzilishi ukiisha, wale watakaofuata tuhakikishe hiyo kodi inalipwa *in full*.

Ushuru wa Mazao, Halmashauri nyingi zinatumia mawakala kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri, lakini usoefu unaonesha mwisho wa siku ni fedha kidogo inawasilishwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kulipa faini/ushuru/tozo fedha zinazokusanya kwenye mizani (*weighbridges*), feri au vivuko, ushuru wa mazao na kadhalika, nyingi hazifiki Serikalini na maeneo mengine wanazo risiti feki. Utaratibu wa kulipa benki tozo hizo utasaidia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kutangaza kuunga mkono Hotuba ya Waziri wa Fedha. Pamoja na kuunga mkono, vipaumbele vilivyowekwa na Serikali ni muhimu sana, miaka iliyopita vilikuwa tofauti, jambo ambalo ni kawaida kwa mahitaji ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali ya maisha magumu inasababishwa na umaskini mkubwa inayowakabili Wananchi. Umaskini huu ni lazima upigwe vita na Serikali, pamoja na Wananchi wenyewe. Hatuwezi kuwa na maisha mazuri kama hatufanyi kazi. Kilimo ni sehemu ya kupunguza umaskini, Serikali inajitahidi kutoa matrekta, mbolea na pembejeo zote kwa juhudii za kusaidia kilimo kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, uchumi unategemea vitu vingi; kilimo, mifugo, uvuvi, biashara, utalii na kadhalika. Ninapenda kuelezea hali ya Wananchi wa Wilaya ya Longido, ambaa ni wafanyabiashara. Namanga ni Mji Mdogo ulioko mpakani, Wananchi walioko ni wafanyabiashara, lakini wanapopeleka bidhaa zao kwenda Kenya, wanapata shida sana hasa Serikali wanapoweke utaratibu wa kuvuka mipaka. Kwa sasa Serikali imepiga marufuku mahindi yasivushwe kwenda Kenya. Tatizo ni kwamba, tupo kwenye Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wenzetu wanafanya biashara kwetu bila kikomo, Wananchi hawa wamekopa mikopo benki na hawawezi kulipa kama watazuliwa kufanya biashara. Namanga ni eneo la biashara, siyo wakulima na wala siyo wafugaji.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atembelee eneo la mpaka wa Namanga, kwa ajili ya kuona kero ya Wananchi ya kunyimwa kufanya biashara huku wenzao wa Kenya, ambaa wao wanafanya biashara, wakisaidiwa na Serikali yao hata kufuta baadhi ya ushuru ili waweze kuleta hali nzuri kwa Wananchi wao.

Jambo lingine ni biashara ya mifugo, ambayo hakuna utaratibu wa kuvusha kwenda Kenya, lakini wakishavushwa Serikali ya Kenya wanalipisha ushuru. Hali hii siyo nzuri, kwani inaonekana kwamba, sisi hatuna namna ya kuwalipisha ushuru, kwani hatuna sehemu ya kutoza ushuru. Inafaa sasa kuweka minada mipakani kwa ajili ya kupata ushuru.

Mheshimiwa Spika, Watalii wanaokuja kutembelea mbuga zetu wanatua Uwanja wa Kenya, Afrika Kusini na maeneo mengine; tunakosa mapato kutokana na viwanja vyetu. Pamoja na hayo, Hazina nayo iwape fedha Wizara ya Maliasili ili iweze kutangaza utalii katika nchi yetu. Tanzania ina vivutio vingi sana, hatuwezi kupata utalii bila kutangaza na matangazo nayo ni gharama.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali imeweka umeme, kipaumbele ni afadhali umeme usambazwe sana vijijini kama tulivyoweka Mfuko wa Kusambaza Umeme.

Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaunga mkono Hotuba ya Waziri wa Fedha.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake, pamoja na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri ya kutengeneza Bajeti nzuri ya mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2011/2012, imetupa matumaini makubwa kutokana hatua zilizochukuliwa za kuleta unafuu wa maisha kwa Wananchi. Hatua ambayo hata wapiga kura wangu wameipongeza ni ile ya kupunguza kodi na tozo mbalimbali kwa mafuta ya petroli. Hatua hii italeta afueni katika huduma zote ambazo zilitegemea mafuta ya petroli hususan usafiri na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

Hatua nyingine inayostahili pongezi ni ile ya kuboresha kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa nishati ya umeme. Ninaomba sambamba na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme, pia uwepo mkakati wa kuongeza usambazaji umeme vijijini ili kuweka mazingira mazuri ya kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao kama matunda na nafaka.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Wizara kwa kuahidi kuharakisha maboresho yanayoendelea katika Sekta ya Fedha na utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji, ambazo zitasaidia upatikanaji wa mikopo kwa Wananchi ili waweze kupata mitaji, pamoja na kujajiri. Hatua hii itasaidia kupunguza matatizo ya ajira kwa vijana. Ninaomba hatua hii iharakishwe kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kusaidia uboreshaji wa upatikanaji wa pembejeo hususan matrekta ili tuweze kufanikisha Kilimo Kwanza hususan katika maeneo yenye rutuba kama yalivyoainishwa kwenye Hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri anayoifanya. Ninaomba waongeze kasi ya kukagua Hesabu za Serikali za Mitaa na ikiwezekana waangalie hali ilivyo kwenye Miradi ya Vijijini. Huko vijijini matumizi ya hela za Serikali pamoja na michango ya Wananchi ni mbaya sana. Hali hii inakatisha tamaa Wananchi katika kuchangia shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba, mikakati yote ya kuboresha maisha ya Watanzania inayohidiwa katika Bajeti ya 2011/2011, itakelelezwa kwa wakati kufuatana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ninaitakia Wizara kila la kheri katika kutekeleza Bajeti hii kwa mafanikio. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuongoza nchi kwa misingi ya Kidemokrasia, Utawala wa Sheria na kuhakikisha amani na utulivu inadumu nchini. Hata hivyo, ninaomba Serikali isiwavumilie watu wanaosababisha fujo na maandamano ya mara kwa mara hata kama ni Viongozi.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuwasilisha Bajeti nzuri, ambayo ina lengo la kumkomboa Mwananchi, kupunguza ukali wa maisha kwa Wananchi na kuondoa kero za Wananchi. Bajeti hii pia ni nzuri kwa sababu inalenga kusimamia vyema matumizi ya Serikali, kwa kupunguza ununuzi wa magari ya Serikali (mashangingi) na kupiga marufuku ununuzi wa samani kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imeeleza bayana kuwa, itaangalia tozo zinazohusiana na mafuta kwa shabaha ya kuziondoa ili kupunguza bei ya mafuta. Ninaunga mkono hoja hiyo kwani ikitekelezwa, bei ya mafuta itashuka na hivyo gharama za undeshaji hasa wa viwanda zitapungua na kwa maana hiyo, bei ya mabati, sementi na nondo zitashuka. Hata hivyo, tozo peke yake haitapunguza bei ya diseli/petrol, ninashauri Serikali ipunguze pia kodi nyinginezo zinazohusiana na mafuta kama *excise duty* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Rais, kwa kuigawa Wilaya ya Singida na Iramba na kuanzisha Wilaya Mpya ya Ikungi na Mkalama. Tatizo langu, sijaona bajeti ya Wilaya hizi Mpya na kwamba; je, zitaanza rasmi lini?

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu, Wananchi wengi wamekuwa wakilalamika kuwa, Tanzania hatujafaidika na rasilimali za madini. Kinachopatikana sasa bado ni kidogo; hivyo ili tuongeze mapato ya kuridhisha, kuna haja ya kusikiliza kilio cha watu kuititia upya Mikataba ya Madini ili kuongeza asilimia ya mrabaha. Ninashauri Mikataba Mipy ya Madini izingatie kilio hiki cha Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita, Serikali ilisitisha zoezi la *DECI*, ambapo pamoja na mambo mengine, ilikamata au ilichukua zaidi ya shilingi bilioni 14 za Wanachama husika, pamoja na kuwafungulia mashtaka Viongozi wa Taasisi husika. Hata hivyo, muda mrefu umepita, hatima ya mahakama haileweki, lakini Wananchi wamekuwa wakilalamika na hoja yao ya msingi ni kwamba, Serikali inawapora fedha zao. Nini hatima ya fedha za Wananchi? Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya makusudi ya kutoa suluhu ya kudumu ya tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni *TRA* imeanzisha utaratibu mpya wa kutoza kodi hasa kwenye magari ambapo makadirio ya kodi hayazingatii thamani ya gari husika kwa kuangalia *invoice* au kwa utaratibu mwengine wowote wa kuthibitisha thamani halisi ya gari husika, bali *TRA* wamekuwa wakikadiria thamani husika kwa viwango

wanavyovipanga wao. Matokeo yake, kodi imekuwa mzigo mkubwa kwa raia wa kawaida na vijana wetu wanaofanya biashara ya magari.

*TRA* wametengeneza mfumo wao wa kushusha thamani (*depreciate*), kulingana na miaka ya magari yalivytengenezwa. Sasa tatizo kubwa ni wapi wamezipata hizo bei? Kwa mfano, kuna magari kama *Toyota Mark II* ya cc chini 2000 yamepewa bei ambayo ni US\$ 32,660 na yenyecce juu ya 2000 yamepewa bei yao ambayo ni US\$ 28,200, lakini *Toyota Mark II* zipo za aina nyingi; kuna *Toyota Mark II 90, GX 100 and GX 110*; hizo zote zimepewa bei sawa. Sasa wakishazipa bei ndiyo wanakwenda ku-*depreciate* kama asilimia walizojiwekea! Je, ni kweli magari haya yana bei sawa hata kiwandani? Siyo kweli, hayana bei sawa!

Mheshimiwa Spika, hata kama wanataka kutumia *depreciation* basi siyo hivyo wanavyofanya, kwani *depreciation* ya gari ya mwaka 2000 inatakiwa ipewe bei ambayo iliuzwa mwaka huo na kisha ku-*depreciate* kwa kutumia thamani ya mwaka 2000. Sasa wao wanatumia thamani ya mwaka huu likiwa kiwandani, kisha wana-*depreciate* wakati magari mengi yanayokuja hapa Tanzania, hayatengenezwi tena huko viwandani; sasa bei wanapata wapi ya mwaka huu? Utaratibu huu unakinzana na Mikataba ya *WTO*. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, anipatie majibu tafadhali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa mchango wangu mfupi kwa maandishi. Nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, kwa kuandaa Bajeti nzuri, inayotoa matumaini kwa Watanzania. Ninapenda nitamke kuwa, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ya Mwaka 2011/2012, imelenga katika kuchukua hatua mbalimbali zitakazosaidia kupunguza kwa kiwango fulani makali ya maisha kwa Wananchi wetu. Imeahidi kudhibiti ongezeko la bei ya mafuta, ongezeko la bei za bidhaa na huduma, kudhibiti matumizi ya Serikali na azma ya Serikali ya kuongeza ajira; ninaipongeza.

Mheshimiwa Spika, kuititia Sera ya Serikali ya Mapato na Matumizi, Bajeti hii inaonesha wazi kuwa, uchumi wetu (Tanzania), una changamoto kubwa katika eneo la kukuza mapato ili kugharimia matumizi ya Serikali ambayo yanaongezeka kila mwaka. Ninashauri Serikali ifanye kila lililo chini ya uwezo wake, kuongeza mapato ya ndani (ya kodi na yasiyo ya kodi). Yapo maeneo mengi ambayo hatujayatumia vizuri; mfano mzuri ni suala la uvuvi hasa katika ukanda wetu wa uchumi. Tunaweza kuongeza mapato maradufu iwapo Serikali itawekeza katika kudhibiti uvuvi (uporaji wa rasilimali za nchi yetu) haramu.

Mheshimiwa Spika, pili, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TRA*, bado inaweza kufanya vizuri zaidi siyo tu katika kuongeza ukusanyaji wa mapato, lakini pia katika kuhakikisha kuwa, mapato yanakusanywa hayavuji, tuzibe mianya inayotumiwa na wajanahache kuipinguzia Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, tatu, ninaipongeza Serikali kwa kuweka vipaumbele vikuu vya jumla vitano vikijumuisha nishati hasa umeme. Serikali ichukue haraka uamuzi kuhusu *TANESCO* ili Sekta Binafsi ijue kwa uhakika kama Serikali/*TANESCO* iendelee kuwekeza kwenye uzalishaji, usafirishaji na usambazaji kama ilivyo sasa au Serikali ijielekeze katika kuwekeza kwenye kuboresha na kupanua usafirishaji na usambazaji wa umeme na kuachia Sekta Binafsi shughuli za uzalishaji peke yake au kwa ubia na *TANESCO*. Ninarudia, Serikali itoe maamuzi haraka.

Mheshimiwa Spika, Serikali tangu mwaka 2007 imekuwa ikiangalia uwezekano wa kukopa kutoka nje kwa kutumia *sovereign bonds*. Mbali na tatizo la mtikisiko wa uchumi duniani (2008/2009), ambapo haikuwezekana kuendelea na mpango huo, hali ya sasa katika soko la fedha ni tulivu na zipo fedha nyingi zinazotafuta maeneo mazuri ya uwekezaji. Ninashauri Serikali ilichangamkie kwa dhati eneo hili. Wenzetu wa Zambia, ambao nao walikumbwa na tatizo hilo hilo mwaka 2008/2009, Serikali yao imetangaza kuwa, wamekamilisha hatua muhimu ya *sovereign rating* ambapo wamepata alama ya B+ na watakwenda sokoni mwezi Oktoba mwaka huu kusaka mkopo wa *Euro 500*, ambazo zitaelekezwa katika kuboresha na kupanua miundombinu. Sisi hapa bado ni wimbo ule uele tupo mbioni.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Waziri wa Fedha wakati atakapokuwa akihitimisha hoja yake, alieleze Bunge na Taifa lini zoezi la *Rating* litakamilika na zoezi hilo linafanywa na nani; *Fitch* au *Standard & Poors*.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, awali, ninaomba nikupongeze kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge letu. Ninakuahidi ushirikiano. Aidha, ninakupa pole kwa kufiwa na mama yetu mpandwa. Mwenyezi Mungu, amrehemu mama yetu mpandwa; *amen*.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia Bajeti, ninaomba nizungumzie hali mbaya ya hewa na njaa Mkoa wa Shinyanga. Hali ya hewa ya mwaka huu ilikuwa mbaya sana; sijawahi kuona hali mbaya kiasi kile. Mipango ya kawaida ya Serikali kupeleka chakula cha msaada (*sporadically*), haiendani/haioani kabisa na tatizo lililopo sasa. Miaka mingine, njaa tunapata kwa miezi michache ya Agosti – Januari. Mwaka huu wa Bajeti, njaa ni kwa watu wote na kwa mwaka mzima; ni muhimu sana Serikali itenye Bajeti Maalum ya Njaa Mkoa wa Shinyanga na ifanye yafuatayo:-

1. Itangaze Mkoa wa Shinyanga hasa Jimbo la Msalala kwamba ni eneo la maafa. Familia zote zipatiwe chakula cha msaada kwa mwaka mzima kuanzia sasa (Juni) hadi msimu wa mavuno Aprili/Mei 2012.

2. Kwa kuwa watu wote wana njaa inayotishia uhai, ninaomba Serikali itenge bajeti kubwa kwenye miradi yote ya mandeleo kama elimu, afya, maji, mifugo kilimo na kadhalika, bila kutegemea mchango wa fedha toka kwa Wananchi.
3. Ili kupunguza gharama na kutekeleza Miradi mingi zaidi, Serikali ianzishe Mpango wa Chakula cha Kazi kwa wenyewe uwezo wa kufanya kazi. Ninajua Serikali inaweza ikapata tabu kutoa chakula cha bure kwa wote, basi wapewe kazi kisha walipwe chakula. *WFP* wamefanya Miradi kadhaa kwa njia hii na kupata mafanikio makubwa.
4. Ili kuondokana na njaa ya kila wakati Shinyanga, Serikali ianzishe Mpango Maalum wa Usalama wa Chakula Shinyanga. Tunaomba uwepo Mpango Maalum wa Umwagiliaji kwenye mabonde yote yanayofaa kwa kilimo hiki. Mabonde kama ya Chela, Segese, Ngogwa, Bulige, Kabondo, Nganya na mengineyo, yawe na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali izingiatie hayo ili kuepuka aibu ya watu wetu kufa kwa njaa, hali ambayo inaoneka dhahiri inaweza kutokea Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RACHEL R. MASHISHANGA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2011/12 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba niainishe mambo machache, ambayo ningependa kujikita nayo kwenye kuchangia Bajeti iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kuchangia kwenye kipaumbele namba mbili, yaani maji. Kiasi cha shilingi bilioni 621.6 zilizotengwa kwa ajili ya maji ni kidogo sana, ukilinganisha na mahitaji ya maji katika Nchi yetu Tanzania. Tunavyosema “Maji ni Uhai” tunamaanisha kwa vitendo. Ninachelea kuona inawezekana kabisa hata hizo asilimia zinazotakiwa zipate maji kwa mwaka huu, zisipate hata kile kidogo.

Mheshimiwa Spika, wanawake wanapata tabu sana kufuata maji mbali na maeneo wanayoishi; hivyo, kuwafanya muda mwingi kupotea katika kutafuta maji, ambapo maji yangekuwa karibu na maeneo, wangeweza pia kufanya shughuli zingine za kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa kuwaona Wakazi wa Mkoa wa Shinyanga, kwa kuweka Mradi mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Victoria. Naishukuru na kuipongeza Serikali kwa asilimia 200.

Mheshimiwa Spika, kasoro zilizoko kwenye Mradi huu ni kwamba, Mradi umelenga kuwasaidia Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, lakini ninaona ni Mradi wa kuwanyonya Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. Ninasema hivyo kwa sababu kuna

mamlaka mbili za maji ambazo zote ni mali ya Serikali, yaani KASHUWASA na SHUWASA, maana KASHUWASA ni Mradi ambao unatoa maji Ziwa Victoria na kuleta Shinyanga huku msambazaji ni SHUWASA. Kwa nini Serikali isiipe mamlaka moja tu kufanya kazi zote ili kupunguza gharama?

Mheshimiwa Spika, suala la maji liangaliwe kwa mapana yake na hasa tukiangalia mwanamke ndiye mhanga wa suala hili pande zote za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Nina wasiwasi na mfumo mzima wa ulipaji wa *VAT* hasa kwa Mwananchi mmoja mmoja. Wengi wa Wananchi hawajui umuhimu wa kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Ninasema hivyo kwa sababu wafanyabiashara wengi wamekuwa wakisaidia wanunuzi wasilipe Kodi ya Ongozeko la Thamani (*VAT*). Utakuta mfanyabiashara anamwambia mnunuzi kuwa, bei hii ukitaka risiti na bei hii kama hutahitaji risiti. Hii maana yake ni nini? Ni watu wangapi nchini wanacheza huu mchezo na kukosesha nchi mapato? Ningependekeza wafanyabiashara waelezwe umuhimu wa kodi kwa Taifa na wasiangalie faida zao tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kuongelea kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168. Sheria hii ikipita, *traffic* wote watapiga makofi kwa kucha. Sheria hii itaongeza kwa kiwango kikubwa sana; hakuna mwananchi au dereva atakayeweza kulipa shilingi 50,000 kama *traffic notification fee*, wakati walikuwa wanashindwa shilingi 20,000 na kuwfanya wawe wanatoa shilingi 5000 – 10000 kwa *traffic* ili waachiwe.

Mheshimiwa Spika, shilingi 50,000 ni kubwa mno, hapa *traffic* atapata Sh 10,000 – 15,000 kwa kosa moja; hili hakuna asiyejua.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ibatilishe Sheria hii ili kunusuru mianya ya rushwa ambayo inaweza kulichafua Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue fursa hii, kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa bajeti nzuri ya Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 katika Sekta ya Madini, Serikali imepangwa kutenga maeneo ya uchimbaji mdogo pamoja na kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo, jambo ambalo linafurahisha. Changamoto kubwa ipo katika utekelezaji. Ninaiomba Serikali itekeleze kama ilivyo katika Mpango. Ninasema hivyo kutohana na Bajeti iliyopita, ambayo ilikusudia kutoa mtaji kwa wachimbaji wadogo. Katika Wilaya ya Geita, wachimbaji wadogo wa Rwamgasa, Nyarugusu na Kaseme, hawakufanikiwa kupata mtaji huo. Ninapenda kutoa ushauri kwa Serikali kwamba, tuwajali wachimbaji wadogo kwa kuwekeza katika kuwaelemisha na kuwapa mitaji,

tuwajengee uwezo, watazalisha kwa kiwango kikubwa na mwisho wa siku watachangia pato la kaya na Pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuwapatia maeneo ya Buziba Nyarugusu. Eneo la Tembomine, Kaseme na eneo la Bingwaleaf na Kata ya Rwangasa. Kwa kufanya hivyo, tutainua hadhi ya wachimbaji wadogo hawa na kuwa wachimbaji wanaotambulika na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara; kuna ahadi ya Rais ya kujenga barabara ya lami kutoka Geita – Kahama kuititia Bukoli halafu Bukoli – Nyarugusu, pia barabara ya kutoka Katoro – Bukombe kuititia Kaseme. Kwa kuwa ahadi ilitolewa na Rais wa Serikali hii hii, ninaomba Serikali iangalie namna ya utekelezaji wa barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Afya, Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kupeleka dawa za kutosha katika vituo vya afya na zahanati vijijini. Mara nyingi Wananchi wanateseka sana na tatizo la upungufu wa dawa ya malaria nayo haipo. Ninaomba katika Bajeti hii, tuangalie uwezekano wa kuhakikisha upatikanaji wa dawa unakuwa kipaumbele. Ule utaratibu wa *MSD* wa kusambaza dawa kila baada ya miezi mitatu na hata wanapoleta dawa hizi zinakuwa ni chache na baadhi ya dawa zinakuwa hazipo kabisa, Serikali ingalie utaratibu mpya wa usambazaji dawa hata kwa kuongeza makampuni ya usambazaji ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, suala la Kilimo Kwanza ni muhimu sana kwa kuzingatia kuwa, Watanzania zaidi ya asilimia 70 wanategemea kilimo. Bajeti kubwa sana inalenga katika kuwekeza katika kilimo Nyanda za Kusini na kuacha mikoa mingine bila kuwezeshewa pamoja na kwamba, uzalishaji katika kilimo uko katika hali ya chini katika mikoa hii. Ninaomba Serikali iunde Programu Maalum kwa ajili ya kunadi kilimo katika mikoa hii. Mfano, Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Serikali iangalie namna ya kuendesha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria. Hii itainua uchumi wa kaya kwa Wananchi waliozunguka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema ili niweze kuendelea kuwawakilisha Wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kwa moyo wa dhati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, asilimia kubwa ya Wananchi wetu wanategemea sana kilimo na kilimo chenyewe ni cha kujikimu tu na wala siyo kilimo endelevu kwa ajili ya biashara. Watu hawa kipato chao ni kidogo mno, kwa sababu kwanza, mazao yanayozalishwa ni kidogo mno na mara nyingi hali ya hewa, ukosefu wa pembejeo na mbolea na kukosekana kwa soko la uhakika ni baadhi ya sababu ambazo zinapelekea kuwa na kipato kidogo. Suala la utumiaji wa wanyama kazi na matrekti, lingepewa msukumo mkubwa, lingechangia sana kuinua kilimo. Leo hii msisitizo

unawekwa kupunguza kodi kwenye matrekta madogo (*power tillers*), ambazo hata sehemu nyingine hazifai kabisa kutokana na umuhimu wa ardhi. Ningeshauri Serikali ipunguze kodi kwenye matrekta makubwa na vifaa vya kilimo ili kuongeza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la ajira kwa vijana limekuwa likijadiliwa mara nyingi, lakini linapewa umuhimu mdogo na Serikali. Vijana ndani ya nchi hii ni asilimia 60 na hawa hawana ajira iliyo rasmi. Sehemu nyingi, Vituo vya VETA vimekufa au haviendelezwi na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii navyo viro hoi. Ningependa kuishauri Serikali, ili kuwasaidia vijana katika Taifa hili, ni vyema sana kutenga fedha nyingi katika kufufua vituo hivi vya VETA na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika Wilaya zote ili kuwasaidia vijana hawa wapate stadi za kazi na hatimaye waweze kujiajiri wenyewe. Pia ningeshauri wapunguziwe ada za leseni ili kwa wale wanaojajiri wenyewe wapate unafuu katika kupata leseni hizo.

Mheshimiwa Spika, suala la ununuvi wa samani; vijana wetu wamekosa ajira kwa sababu ya kutojali mali zinazozalishwa hapa nchini. Tanzania imejaliwa kupata misitu ya asili yenye miti mizuri na ya kutengeneza samani nzuri, lakini magogo haya yanauzwa nje ya nchi pasipo kuiingizia Serikali mapato ya kweli na hatimaye Serikali hii kwenda kununua samani hizo za mninga uliotoka Tanzania kwa bei kubwa. Ninaishauri Serikali ijenge utamaduni na kudhamini bidhaa zetu za ndani ili kulinda soko letu na pia kuinua kipato cha Wananchi hususan wazalishaji wa samani hizo. Mfano, vikundi vya mafundi seremala wa Nyantakara na Nyakanazi, hawa ni mafundi wazuri sana na sioni sababu hata ya Halmashauri zetu kwenda kununua samani toka sehemu za mbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, Bajeti hii haijatoa kipaumbele au umuhimu wowote wa wachimbaji madini hasa wachimbaji wadogo wadogo. Kundi hili ni muhimu sana katika kuchangia Pato la Taifa hususan pale Serikali inapokuwa imewatengea maeneo maalum ya uchimbaji; kundi hili haliwezeshi wala halitambuliwi na ndiyo maana ya machafuko sehemu mbalimbali; mfano, Marota na Tarime. Kuna eneo la Busiri ndani ya Jimbo la Biharamulo Magharibi, watu hawa hawana lolote ambalo Serikali imelifanya kuwasaidia.

Ninaishauri Serikali iwapatie wachimbaji hawa maeneo ili wachimbe kwa uhakika na waweze kuchangia katika Pato la Taifa na wao waondokane na wimbi hili la umaskini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia 100 kwa 100.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni nzuri sana, hongera sana. Nigusie suala la Utalii, tunaomba pesa zitengwe kwa ajili ya kurudisha Mjusi “Dinosaur” kule Ujerumani ili kukuza utalii nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Lindi, naomba ifufuliwe ili kukuza ajira Lindi na uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Hospitali ya Ruangwa ipewe vifaa vya Hospitali kama *X-ray*, *Ultrasound*, dawa, *Operation set* na vitanda vya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, umeme Mkoa wa Lindi hakuna. Tunaomba tusaidiwe umeme. Tangu tupate uhuru hatujawekwa katika umeme wa grid. Mkoa una gesi lakini hatujui matumizi ya gesi hiyo?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nachingwea na Lindi hakuna maji. Ule mradi wa Nachingwea - Mbwinji unasuasua tu na Lindi Mjini, *World Bank* hakuna.

Mheshimiwa Spika, bajeti inasema Madereva wakikosa watatozwa faini Tshs.50,000/=, tunaomba adhabu hiyo ipunguzwe kwani ni hatari zaidi kwani Madereva wengi ni Waheshimiwa Wabunge, viongozi mbalimbali na wananchi. Adhabu hii itawagusa sana viongozi na wananchi wataathirika. Pesa hakuna, tupunguziwe.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, hatuna Walimu wa kutosha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pembejeo za kilimo hususan *Sulphur* ya kupulizia mikorosho, hadi sasa hajaletwa Mkoani Lindi kwani pesa hazijapelekwa kwa tajiri na wakati wa kupulizia umefika, je, Serikali inafahamu hilo? Pelelezeni kwanza hilo. Tunaomba *Sulphur* iende Lindi.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri ambayo imeja matumaini kwa Watanzania amba wanashubiri maendeleo kutoka kwa Serikali yao ambayo iko madarakani.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Bumbwini kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie bajeti hii katika sehemu ya Nishati (Umeme). Ili tuweze kupata maendeleo katika nchi yetu, basi umeme ni kipaumbele kama ilivyoainishwa katika bajeti. Kinachoonekana hapa katika eneo hili ni utendaji mbaya wa sekta hii, naiomba Serikali itupie macho sana sekta hii ya umeme, kwani ndio roho ya mafanikio ya nchi yetu pamoja na maendeleo ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nijikite katika sekta ya kilimo. Bado hatujaweza kujipanga vizuri katika sekta hiyo pia hatujaweza kutumia mito, mabwawa, kwa ajili ya

umwagiliaji. Naishauri Serikali kwamba tujikite zaidi katika kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kulima bila kusubiri msimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa upande wa madini, bado madini yetu yanapotea bila sisi wenyewe kujua, wachimbaji wanahamisha mpaka mchanga wa sehemu husika. Napendekeza Serikali ipitie vizuri mikataba hiyo ili tuweze kudhibiti mali zetu na tuweze kuingiza mapato kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mosi katika taarifa ya utekelezaji wa bajeti, Serikali imepanga kuendeleza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya na Tiba cha Muhimbili (*MUHAS*) eneo la Mloganzila. Wananchi wa Ubungo tunaunga mkono ujenzi husika kwa maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, Serikali inapaswa kutoa kauli ya haraka kuhusu fidia ya wananchi wa eneo husika. Serikali isipotoa tamko kwa hatua ambayo mgogoro umefikia kunaweza kutokea uvunjifu wa amani kwani hatua zimeanza kutekelezwa za kuwataka wananchi waondoke wakati wapo ambao hawajalipwa fidia na hawataki kuondoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na taarifa potofu mionganii mwa uongozi wa Serikali kuhusu mipaka ya eneo husika na mchakato wa tathmini ambao umefanyika. Aidha taarifa potofu zimekuwa zikitolewa kuwa hakuna kesi Mahakamani kuhusu eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali irejee barua yangu ya tarehe 13 Mei 2011 kwa Waziri wa Ardhi ambayo imeeleza kuhusu suala husika baada ya kukutana na wananchi hao na kupatiwa nyaraka zao (Rejea barua yenye Kumb. *OMU/AR/005/2011*). Hivyo Waziri wa fedha atoe tamko kuhusu fidia ya wananchi wa eneo husika kama italipwa kwa ukamilifu katika mwaka huu wa fedha kabla ya kuanza ujenzi wa majengo ya MUHAS eneo la Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, pili katika hotuba na bajeti limeelezwa kusudio la ujenzi wa barabara za kupunguza foleni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kati ya barabara ambazo ni vizuri zikawekwa kwenye kipaumbele cha kujengwa kwa kiwango cha lami ni barabara fupi ya kutoka Ubungo Maziwa mpaka Mabibo External yenye urefu takribani kilomita mbili tu (2 Km). Barabara hii itasaidia magari ya kutoka barabara za Morogoro na Kigogo kupita kwenda barabara ya Mandela bila kulazimika kupitia mataa ya Ubungo. Barabara hii ni muhimu sana katika kupunguza foleni wakati ujenzi wa barabara ya magari ya haraka (*DARTS*) na *Flyover* utakapoanza eneo la Ubungo. Barabara hii ilikuwa ni ahadi ya Waziri Bungeni kwenye hotuba za miaka ya fedha iliyotangulia lakini mpaka sasa haijatekelezwa. Barabara hiyo iko chini ya Manispaa ya Kinondoni, lakini kutokana na Halmashauri kuwa na rasilimali chache za kuihudumia na umuhimu wake kwa Jiji la Dar es Salaam, *TANROADS* imeiweka katika orodha yake na Mkoa umeomba ipandishwe hadhi.

Mheshimiwa Spika, tatu, pamoja na kauli ambayo Waziri wa Fedha aliitoa Bungeni kuhusu fedha za *DECI*, kutokana na malalamiko yanayoendelea mionganoni mwa wananchi kuhusu hatma ya fedha zao pamoja na kuwa kesi inaendelea Mahakamani. Serikali inapaswa kulieleza Taifa zilipo fedha za *DECI* na kuwahakikishia watusika fedha ziko salama na hazijatumika kwenye matumizi mengine. Pia ileze kwa nini fedha hizo ambazo zinaweza kutolewa kwa asilimia 40 kwa wananchi waliopanda mbegu hazirejeshwi kwa wenyewe.

**MHE. AUGUSTINO MANYANDA MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hasa kwa kuweza kubaini vipaumbele vya barabara, reli, bandari na Mkonga wa Taifa. Mwelekeo wa bajeti hii ni kuboresha huduma ya mawasiliano kwa watu na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa. Sote tu mashahidi kufanikisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nchi nzima na maendeleo yanaonekana.

Mheshimiwa Spika, sekta ya biashara imepanuka kwa kiwango kikubwa, wafanyabiashara wamefanya biashara na mataifa ya nje ya China, Japan, Thailand, Singapore, Dubai, India n.k. Bidhaa toka nchi hizi nyingi zinasafirishwa kwa meli na kwa mantiki hii meli zinahitaji kutia nanga katika bandari ya Dar es Salaam kwa hiyo, miundombinu na huduma katika bandari hii iboreshwe na kuondoa urasimu usiokuwa na sababu bandarini.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kama bajeti inavyosema, reli na barabara ziboreshwe ili kuwezesha usafirishaji wa mizigo toka bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mkonga wa Taifa nao una mchango mkubwa kwa vile gharama za mawasiliano ya simu zitapungua na kuzifanya gharama za kibiashara kupungua pia kwa vile wafanyabiashara watapata taarifa za kibiashara na za bei ya bidhaa kwa gharama nafuu na kwa mantiki hiyo bidhaa zitasafirishwa kwa gharama nafuu na hata bei kwa mlaji wa mwisho itakuwa nafuu.

Mheshimiwa Spika, nishati ni kiungo muhimu katika kuleta maendeleo kwa vile uzalishaji wa bidhaa viwandani utaongezeka na kwa maana hiyo Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi ya kweli nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya kilimo na umwagiliaji pia imezingatiwa, tunayo imani kwamba mbolea itaongezewa ruzuku na kwamba wakulima wataweza kuzalisha mazao ya biashara na yale ya chakula kwa upana mkubwa na hivyo kubadili hali ya maisha kutoka uduni hadi kufikia maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Spika, suala la maji ni la kufa na kupona kwa vile maji ni uhai, bila maji safi na salama maisha hayawezi kuwepo lakini Serikali imeliona hilo na kuongeza bajeti.

Mheshimiwa Spika, elimu ni msingi wa Taifa, Serikali imeliona hili na kuitengea fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, tunaweza, kinachotakiwa ni kuwa na nia njema, hakika tutafanikiwa kwa kusimamia mipango yote iliyotengewa fedha hizi.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza bajeti hii kwa namna ilivyoandaliwa kwa lengo la kumjali Mtanzania wa tabaka lolote hivyo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha umeme ni cha muhimu sana kwa sababu karibu kila sekta hutegemea chanzo hiki kama viwanda, kilimo n.k. Umeme ukifika vijijini wananchi watatumia kwenye biashara zao ndogondogo hivyo kumuinua mwananchi kutokana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, njaa, Tanzania ni ya wakulima na wafanyakazi. Wananchi wa Kanda ya Ziwa kwa ujumla wao ni wakulima. Mwaka wa 2010/2011 majira ya mvua hayakuwa mazuri, msimu wote ulikuwa na ukame wa hali ya juu sana hivyo kuathiri mavuno na kuwa chini sana hasa mavuno yatokanayo na chakula.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina maeneo mazuri sana yanayozalisha chakula kama vile Mikoa ya Mtwara, Rukwa, Ruvuma n.k. Naishauri Serikali kuwa karibu na Mikoa hiyo ili tuweze kuhifadhi chakula cha kutosha katika maghala yetu ya Taifa kwa manufaa ya nchi nzima hasa Mikoa ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, fedha vyuo vikuu, kumekuwa na maandamano ya mara kwa mara kwa sababu kubwa tu ya kutokulipwa pesa zao za posho kwa wakati. Nashauri na kupendekeza katika bajeti zetu tutenge pesa hizi aidha kwa robo mwaka, nusu mwaka, kama hatuwezi kilitenga fungu hili la mkopo kwa mwaka. Nasema hili ili kuondoa kelele hizi za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, utalii kama chanzo cha mapato. Tanzania tuna maeneo mengi sana ya kuvutia kitalii. Kwa mfano Ukerewe, Mwanza kuna utalii wa Jiwe linalocheza. Hii ni kweli kwa sababu nimeshuhudia. Mwanza ina mapango mengi sana ambayo yanaweza yakawa kivutio kikubwa sana kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu bajeti hii. Awali ya yote, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa ukiwa mwanamke wa kwanza kuongoza Bunge katika Afrika Mashariki.

Pili, natoa pongezi kwa viongozi wote wa Bunge waliochaguliwa katika nyadhifa tofauti. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuchaguliwa kuingia katika Bunge lako Tukufu. Pongezi kwa Waziri wa Fedha, Naibu na wafanyakazi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Mkuu na viongozi wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee ni kwa wanawake wa Morogoro, hususani UWT, Wilaya zote Mkoa wa Morogoro walioniwezesha kuingia kwenye Bunge lako Tukufu. Nawapenda kina mama, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika bajeti yetu ni nzuri, kwani imelenga kupunguza makali ya mwananchi na mwananchi huyu ni Mtanzania. Kwanza, tukiangalia vipaumbele vimezingatia na vimeridhia kutoa huduma bora na kupunguza maisha makali kwa wananchi yaani kupunguza umaskini wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, habari ya umeme kila Mtanzania nina imani anafurahi kusikia umeme umepewa kipaumbele cha juu. Wananchi wengi hasa wanaishi vijijini 80% wanaishi gizani, hawana umeme. Tukiwa na umeme wa uhakika, maendeleo yataongezeka hasa vijijini na mijini. Viwanda vidogo na vikubwa vitaanzishwa. Akina mama na vijana wataweza kujajiri kwa urahisi. Usindikaji wa vyakula utaendeshwa hivyo kupunguza umaskini kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, binadamu yejote hawesi kuishi bila ya chakula na maji. Kwa hiyo wananchi wakipata maji safi na salama maisha ya wananchi yatazidi kuneemeka.

Mheshimiwa Spika, miundombinu safi ndio maendeleo ya Mtanzania. Kwa mfano, mpaka sasa barabara zinaendelea kutengenezwa. Barabara za mijini na vijijini zinatengenezwa. Muhimu ni Halmashauri zetu zizidi kuangalia barabara za vijijini hasa wakati wa mvua, matengenezo ya mara kwa mara ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Morogoro, barabara pia zinaendelea kutengenezwa kwa mfano, barabara ya Handeni – Mvomero – Kilosa - Mikumi inaendelea vizuri. *Mtwara Corridor*, barabara ya lami inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Tanzania unategemea kilimo. Bajeti ambayo imelenga kuboresha kilimo na kilimo cha umwagiliaji imelenga maisha ya Mtanzania. Watanzania asilimia 80% wanategemea kilimo. Kwa sasa hivi, baadhi ya Wilaya wamepata ukame mkali kwa hiyo matokeo yake ni njaa. Mikoa ambayo imepata mvua ya kutosha hasa Mikoa ya Kusini Ruvuma, Rukwa, Mbeya wana chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kilimo Kwanza, kanuni bora za kilimo, wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanaomba vocha ziongezwe, zifike mapema na idadi iongezeke. Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanashukuru kwa mpango huu wa ruzuku.

Ruzuku itaongezeka ila mpango utakuwa mzuri kwa kila mkulima kama ukisimamiwa vizuri. Kwa hiyo, kila mdau afanye kazi kwa kujituma.

Mheshimiwa Spika, tutaishi vizuri tukidumisha kilimo cha umwagiliaji. Mabonde mazuri ya Kilombero, Mvomero, Kilosa yaktumika, Mkoa utakuwa na chakula cha kutosha na wananchi watainua maisha yao. Cha msingi tufanye kazi.

Mheshimiwa Spika, kupanua ajira kwa sekta binafsi na ya umma. Vijana wengi wanaomaliza shule wanatafuta ajira, ni taabu. Vijana hawa wakikubali elimu ya ujasiriamali wanayopata vyuoni na kuitumia, hapatakuwepo tatizo la ajira. Vijana hawa watakuwa tayari kuanzisha sekta binafsi na kujaajiri.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kilimo kwa Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*) utasaidia wananchi hasa vijana na wanawake, kwa kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, mkopo, dirisha la kukopesha miradi ya kilimo la TIB na Benki ya Wakulima, ni maendeleo makubwa kwa kupunguza makali ya gharama kwa mkulima. Jambo muhimu ni kuwapatia elimu wananchi hawa ya jinsi ya kupata mikopo hii. Uanzishaji wa SACCOS imara, VIKOBA, DUNDULIZA na vikundi imara, ni muhimu kwa maendeleo ya mwananchi.

Mheshimiwa Spika, ujasiriamali ni muhimu hasa kuinua maisha ya Mtanzania hasa wanawake. Ni muhimu sana wapewe mwelekeo namna ya kuendeleza mitaji yao.

Mheshimiwa Spika, bajeti itapunguza mfumuko wa bei, mafuta, tozo, kutoa baadhi ya kodi na mishahara kupanda. Bajeti ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti hii kwa moyo wote.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze sana hotuba ya Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012. Hotuba hii inalenga kutekeleza kwa dhati Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba yake, napenda kuchangia katika maeneo kadhaa ambayo naona iwapo yanetiliwa nguvu zaidi ingeharakisha zaidi watu wetu kujikombua kiuchumi. Kilimo cha umwagiliaji kinapaswa kisifanywe kwa miradi midogo tu bali kuwe na mpango mkubwa hususani katika mabonde yetu makubwa ya Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa ili nchi ijitosheleze kwa chakula na kupata ziada ya kuuza nje. Vituo vya umwagiliaji vya Kanda kama vile kilichopo Nyakato – Mwanza lazima kiimarishe na kiwekewe malengo makubwa.

Mheshimiwa Spika, mji wa Mwanza umekaa vizuri sana kijiografia katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Hivyo iwapo ungewekwa mkakati maalum wa kuuendeleza kibashara, ungeweza kuliingizia pato kubwa Taifa letu. Hivyo, nashauri mpango wa

Serikali wa kuujenga Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa hadhi ya Kimataifa utekelezwe haraka ili kuruhusu watu wengi hususani wafanyabiashara kuja kuchukua bidhaa hapo. Hii ni njia muhimu ya kufanya Tanzania itawale uchumi wa nchi za Ukanda huu.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango wa Serikali wa kujielekeza zaidi kwenye ujenzi wa miundombinu. Hata hivyo, iko barabara moja kuu ambayo ingefungua haraka Ukanda wa Mashariki (Tanga) na kuunganisha na nchi za Maziwa Makuu. Barabara ya Arusha, kupitia Karatu, Meatu, Bariadi hadi Lamadi ingeleta ushindani mzuri sana kibiashara kwa bandari ya Tanga. Fursa hii tunayo Tanzania pekee, ni vema tukaitumia na kuacha malumbano juu ya barabara hii muhimu. Wapo washirika wa maendeleo ambao wapo tayari kutuunga mkono kwa barabara hii, ni vema tukaidaka fursa hiyo ya pekee.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta kasi ya maendeleo ni pamoja na kushirikisha jamii kubwa katika uzalishaji kwa ubora. Taasisi za VETA na *SIDO* ni vyombo muhimu sana kwa kutoa utaalim kwa wananchi wa kawaida ili waweze kufanya shughuli zao za uzalishaji kwa ubora zaidi. Ni vema *SIDO* na VETA zikajengewa uwezo wa kuwafikia wananchi wengi zaidi hususani vijana ili waweze kushiriki kuzalisha mali au kufanya biashara kwa tija zaidi. Bila maarifa katika uzalishaji, nchi yetu itachukua muda mrefu zaidi kuweza kushindana na nchi jirani kama vile Kenya na Uganda katika uzalishaji na biashara. Tuimarishe *SIDO* na VETA.

Mheshimiwa Spika, maarifa ya uzalishaji na tija vitapatikana pia iwapo tutaimarisha Ushirika, *SACCOS* na *VICOBA*, vina mchango mkubwa katika kuongeza tija na hata kubadilisha tabia ya watu “*attitude*” kuhusu ushindani wa kibiashara. Idara ya Ushirika katika Halmashauri za Wilaya ziimarishwe kwa kuongezewa Watendaji na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza mapato ya Serikali, ni muhimu sana kudhibiti matumizi katika Halmashauri za Wilaya ndipo kwenye upotevu mkubwa wa fedha ya Serikali, pasimamiwe vema. Napongeza Serikali kwa kuweka Idara Maalum ya kufuatilia fedha kwenye Serikali za Mitaa, lakini ni muhimu Idara hiyo ifanye kazi kweli na isije ikatumbukia kwenye mfumo wa rushwa kama ilivyo kwenye Halmashauri nyingine nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, najikita kwenye sekta ya afya. Kwa kuwa wanawake wengi Tanzania wamekuwa wakipoteza maisha yao kila lisaa limoja wakati wa kujifungua, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, naomba itenye fedha za kutosha katika mwaka huu wa bajeti kuhakikisha Zahanati za Kata na Hospitali za Mikoa zinaboreshw na Madaktari na Manesi wanaopelekwa katika vituo husika wanaandaliwa mazingira mazuri na wapatiwe vitendea kazi. Tatizo hili limekuwa sugu katika Vituo vya Afya. Hospitali nyingi hazina

dawa, maabara na vipimo mbalimbali muhimu vya kukidhi mahitaji ya akina mama wajawazito wanaofika kujifungua pamoja na wagonjwa wengine wanaosumbuliwa na maradhi mbalimbali. Kwa hiyo, kama Serikali itatenga bajeti nzuri katika Vituo vya Afya, tutaokoa vifo vya Watanzania wengi wakiwemo wamama wajawazito wanaoenda kujifungua.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika suala zima la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Tatizo hili ni janga la Taifa. Serikali kupitia bajeti hii ya mwaka wa fedha 2011/2012 ihakikishe Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto inatengewa fedha za kutosha ili kutatua matatizo yanayowakabili watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto inahakiki vituo vyote vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu kupatiwa mahitaji muhimu kama vile elimu, afya n.k. Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto ihakiki vituo vyote vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu kama vimesajiliwa ili kuepuka makundi ya watu wachache wanaoanzisha vituo hivi kwa maslahi yao binafsi na misaada inayotolewa na wafadhili kutowafikia walengwa. Kwa kuwa watoto hawa hawatoki Mkoa wa Dodoma tu, wanatoka Mikoa mbalimbali ya Tanzania, Serikali na Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto ihakikishe Mikoa yote inapatiwa semina endelevu kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu Magereza. Kwa kuwa wafungwa wengi hawatendewi haki na kesi nyingi zinachukua muda mrefu, Mahakama za Mwanzo na za Wilaya kupitia mwaka wa fedha 2011/2012 zitengewe fedha ya kutosha ili kuendesha shughuli za Kimahakama. Wakiptiwa fungu la kutosha wataweza kuendesha kazi zao kiuadilifu na kuondosha msongamano wa kesi. Kwa kuwa wafungwa wengi wanawake hawatendewi haki magerezani, hawapewi mahitaji muhimu kama vile pedi wakiwa katika siku zao za hedhi na mavazi yao kutokidhi haja. Serikali kupitia mwaka wa fedha 2011/2012 ihakikishe wanawake hawa wafungwa nao wanapatiwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, naomba Vyuo vikuu vya Zanzibar vitatuliwe matatizo yanayohusiana na Bodi ya Mikopo. Hili limekuwa ni tatizo sugu la wanafunzi wa Vyuo Vikuu na sekta zote zinazohusu Muungano. Naomba na sisi Wazanzibar tukumbukwe katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu suala zima la Watanzania wanaoishi vijijini katika mazingira magumu katika nyumba za nyasi zisizokidhi mahitaji. Kupitia mwaka huu wa fedha wa Serikali 2011/2012 iwatengee Watanzania hawa mkopo wa fedha wa kujengea nyumba za kisasa na Serikali ihakikishe vifaa vya ujenzi vinashushwa bei ili Watanzania wasio na uwezo nao wanufaikie katika vifaa hivyo ili waweze kujenga nyumba za kisasa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kutumia nafasi hii kuipongeza Serikali, bajeti yake ni nzuri, bajeti yenye matumaini, bajeti yenye kujali maskini, bajeti iliyojaa vipengele muhimu vya kuifikisha Tanzania kwenye neema

kwa kutenga shilingi trilioni 13.5 kukomboa Watanzania yenyе vipaumbele vya umeme, miundombinu, kilimo, ajira kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mapato, *TRA* imekuwa na uhuru mkubwa kwa watumishi wake wa kutoa makadirio ya mlipa kodi. Makadirio ya mapato kwa mlipa kodi yanakuwa katika sura mbili zilizojificha ndani yake. Kutoa kadirio la kodi kwa kumkomoa mlipa kodi kwa kuzidisha kiwango badala ya kiwango kinachotakiwa hadi kumfanya mlipa kodi (Mfanyabiashara) kutafuta njia nyingine ya kuomba kupunguziwa kadirio hilo njia yenyewe ni (Rushwa) kwa kupewa fedha, (HONGOs) matokeo yake Serikali inapata pato dogo. Hivyo kwa mtindo huo athari zifuatazo zinaweza kutokea, Serikali kupata hasara, kupunguza morali na hamasa ya watu wenye nia ya kuanzisha biashara na wananchi kuilaumu Serikali ya CCM kutokana na vitendo hivyo. Hivyo, Serikali itafute njia nyingine ya kumkadiria mfanyabiashara kwani njia inayotumika sasa inanufaisha baadhi wa watumishi wa *TRA* badala ya Serikali kunufaika.

Mheshimiwa Spika, pili, viwanda, Serikali ifikirie kuanzisha viwanda maeneo yaliyo karibu na malighafi badala ya kuanzishwa mbali na Mkoaa unaotoa malighafi hiyo. Inakuwa ni upendeleo Mkoaa mmoja unakuwa na viwanda vingi hata kama hauna malighafi husika, huo ni upendeleo. Mfano, viwanda vya kusindika matunda viwepo Mikoa inayolima matunda kwa wingi, viwanda vya nguo, kwa Mikoa inayolima pamba, katani n.k na katika viwanda vya ngozi na maziwa vijengwe Mikoa yenyе mifugo mingi n.k. Serikali ikifanya hivyo itakuwa imeongeza ajira katika maeneo husika, itainua uchumi, itapunguza umaskini na itakuwa imeondoa upendeleo wa kuanzisha viwanda eneo moja. Serikali itakuwa imehamasisha kilimo, ufugaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatu, Benki ya Mkulima, tunapozungumzia kuanzishwa kwa Benki ya Mkulima, ni jambo zuri sana lakini ni lazima benki hii itolewe tafsiri nzuri kwa madhumuni thabiti ya kumsaidia mkulima, lazima tutoe maelekezo ni wakulima wa namna gani? Kwa sababu mkulima anaweza kuwa ni mtu ye yeyote anayeweza kuamua kulima. Tafsiri ikieleweka benki hiyo inaweza kugeuka kuwa benki ya matajiri wakubwa waliohodhi ardhi kubwa, badala ya nia ya Serikali ya kusaidia wakulima wadogowadogo. Kwa maana hiyo, Serikali iandae mpango mahsusи wenye nia ya kumsaidia mkulima mdogo.

Mheshimiwa Spika, nne, kilimo, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali za kuinua na kupanua sekta ya kilimo lakini bado Serikali haijafanya utafiti wa kutosha katika kuyafahamu vyema baadhi ya maeneo katika nchi hii ambayo ni mazuri kwa kilimo na maeneo ambayo yana ardhi yenyе rutuba na yenyе hali ya hewa isiyotetereka hadi sasa na ina mvua za kutosha, ina mito mingi ya isiyokauka na inafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ina mabonde mazuri yanayoweza kustawisha mazao mengi yakiwepo mazao ya chakula, biashara au matunda mbalimbali. Serikali ikiyatumbia maeneo hayo vizuri inaweza kuongeza uchumi wa nchi yetu na kuwakomboa wakulima wadogowadogo na kuweza kuondoa umaskini. Baadhi ya maeneo ambayo Serikali imeyasahau ni Ukanda wa Ziwa Rukwa yaani Bonde la Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, tano, Vyuo vya Mafunzo mbalimbali, ili kupanua uwezo wa ujuzi katika mafunzo mbalimbali kwa kuongeza ujuzi na ukuzaji wa uzalishaji wa vitu mbalimbali ni vyema ikawa inajenga vyuo hivyo kulingana na malighafi iliyopo katika eneo husika. Kwa kufanya hivyo, uzalishaji utakuwa na gharama nafuu sana, hivyo utakuwa umeongeza ujuzi wa vijana katika kupata ajira, hivyo utakuwa umeondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kuanzisha Chuo cha Kilimo, Mkoa wa Rukwa kwani Mkoa unatoa mchango mkubwa sana wa chakula katika nchi hii. Vilevile kipo Chuo kidogo cha Kilimo kilichoanzishwa na *Mission* ya *RC* katika Mji Mdogo wa Laela, tunaomba Serikali ikipanue kiwe Chuo cha Kilimo katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia pia kwa maandishi ingawa nilipata fursa kuchangia kwa kuongea lakini bado nina mengi ambayo ningependa kuishauri Serikali na kwa kuwa Serikali ni sikivu ninaimani ushauri wangu utazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kupambana na umaskini hususani Mkoani Kigoma na kuinua pato la Taifa na nchi kwa ujumla, pale tuna bandari ya Kigoma, bandari ambayo ina shehena ya watu na mizigo japokuwa meli si imara vya kutosha jambo ambalo kama tahadhari haitachukuliwa yanaweza tokea kama yale yaliyotokea MV. Bukoba.

Mheshimiwa Spika, Kigoma tumekuwa na kituo au bandari ndogo (Forodha) ijulikanayo kama Kibirizi. Eneo hili limekuwa na wafanyabiashara takribani mia nane (800) wakifanya shughuli za kupakia chumvi ya Uvinza na bidhaa nyingine kuzipeleka Burundi na Kongo. Sasa ni takribani wiki tatu maboti hayo yamezuiwa kwa kuwa Sheria ya *Export of Goods* inazuiwa *Wooden boat* kusafirisha bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, hivyo, wananchi wale ni maskini sana na hawana shughuli tegemezi isipokuwa biashara na uvuvi, ni matumaini ya wana-Kigoma. Kwa kuwa meli hiyo ni moja na inabeba mizigo na watu kwa pamoja, wanaomba Serikali ipeleke meli nyingine ili zitenganishwe kwa ajili ya abiria na mizigo au Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma wenye maboti hayo kwa kuwa wamepoteza ajira nyingi ili waendelee na usafirishaji wa bidhaa hizo ili Halmashauri zetu zipate mapato na kipato cha mwananchi mmoja mmoja kiongezeke.

Mheshimiwa Spika, toka shughuli hizo za Forodha zianze, kumekuwa na upungufu wa matukio ya ujambazi katika eneo la Kigoma Mjini kwa kuwa vijana wengi walikuwa wamejishikiza pale. Sasa ni hofu kwa wananchi kuwa shughuli hii kusitishwa maisha yao yanaweza kuwa hatarini wakizingatia kule wapo mpakani.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweze kuliangalia hili kwa jicho la huruma, ahsante nawasilisha.

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Spika, bajeti kuu imeweza kuzungumzia mambo mengi yenye kutaka kuleta maendeleo katika nchi yetu, kati ya hayo ni suala la Uvuvi. Sekta hii hatujaitumia ipasavyo katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Wizara imeondoa kodi katika nyavu na kwa wanaotaka kusafirisha samaki nje ya nchi. Kwa kweli bado hatujanufaika na sekta hii ya uvuvi. Kwa nini Serikali haiwawezeshi wavuvi wadogowadogo wakapewa vyombo vyaya kisasa ili waweze kuvua katika Bahari Kuu. Nchi yetu ingenufaika kwa kupata mambo mawili makubwa kwa wakati mmoja. Tutafaidika kwa kupata samaki wa kutosha kwa ajili ya chakula na biashara na pia wanetumika wavuvi hawa kama walinzi kwa kutoa taarifa kwa Serikali pale wanapozikuta meli za nje zinazokuja kuvua na kuiba rasilimali katika bahari yetu. Watanzania tunahitaji tutafakari hali halisi tuliyonayo na tubuni sera na mikakati ya pamoja ya kujikwamua toka dimbwi la umaskini.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mungu aliye asili ya mema yote, kwani bila yeye hatuwezi kitu. Namwomba Mungu abariki Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge wote wa vyama vyote ili waweze kufanya kazi kwa faida ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla. Kwa kupendana, kuheshimiana, kuthaminiana na mwisho kufikia amani ya kweli, kwani amani bila haki si kitu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa upande wa bajeti. Bajeti hii si mbaya lakini nina wasiwasi kama itatekelezeka kwa sababu kwanza, bajeti inaonesha kuongezeka kwa deni na pili, tukiangalia pato la ndani litokanalo na kodi ni takribani shilingi trilioni sita wakati matumizi yaliyoainishwa ni Shs.Trilioni 13 hivyo matumizi ni makubwa kuliko mapato. Kwa kuwa penye nia pana njia basi tuombe Mungu. Hivyo napenda kuishauri Serikali ilekeze nguvu katika vipaumbele vyote muhimu ili tujikwamue kiuchumi na kumuweka mwananchi katika unafuu.

Mheshimiwa Spika, reli, tukumbukwe Wilaya ya Mpanda tuna wakati mgumu sana kiusafiri. Reli ni mbovu na imechoka. Tumekuwa tukinusurika ajali mara kwa mara kuanzia kilometra 90 kwenda Kaliua. Mabehewa ni chakavu yamejaa kunguni na panya. Ni aibu sana Daraja la I na II hakuna ni shida tupu, Serikali ilione hili.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege, kwa hapo naipongeza Serikali uwanja unaonekana, ahsante.

Mheshimiwa Spika, barabara, Serikali ijithidi kujenga barabara hasa za kwenda vijijini ili wananchi wapate kusafirisha mazao yao kutafuta masoko. Barabara vijijini ni shida.

Mheshimiwa Spika, maji ndiyo kabisa, wananchi wa Mpanda hasa Vijijini wanapata shida sana, wanachangia maji na wanyamapor (Ngiri) katika madimbwi ambayo mvua zikikatika hukauka. Naiomba Serikali iwakumbuke wananchi wa Mpanda, kwa Mjini Kata ya Nsemulwa, Mpanda Hoteli, Kawajense – Kazima. Kwa Vijiji, Ikaka, Iloba, Sibwesa, Kakese na Chamalendi, Tarafa ya Usevya. Hawa wanachangia maji na ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, kilimo, hii ndiyo sekta mama. Mpanda tumejaliwa sana kwa rutuba nzuri na tuna mabonde ya kulima zao la mpunga vilevile mbogamboga na miwa kwa biashara, lakini wakulima hawana uwezo wa pembejeo pia wakulima wengi hawana utaalamu wa kuitumia ardhi. Serikali isimamie hili.

Mheshimiwa Spika, afya, Hospitali yetu ya Wilaya ambayo muda si mrefu itakuwa ya Mkoa, Serikali ituongezee watumishi, Madaktari na Wauguzi hawatoshi. Pia kipimo cha *X-ray* ni kibovu na mtaalamu hakuna. Pia kwa Zahanati za Vijijini watumishi vituo vingi hakuna.

Mheshimiwa Spika, elimu, tuongezewe Walimu na vifaa vya kufundishia. Kwa VETA, tunaishukuru Serikali watoto wetu wanapata ujuzi mbalimbali. Serikali iwawezeshe mikopo vijana ili wajajiri kwa ufundi wanaopata katika vyuo hivi vya VETA bila kuwasahau akina mama mikopo kwani ndiyo walezi wa familia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kuhusu bajeti hii pamoja na wataalam wake. Pia naunga mkono hoja hii na kukubaliana na vipaumbele vyote vilivyoolezwa na Mheshimiwa Waziri, sina pingamizi navyo.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii, katika vipaumbele vilivyopo, mimi nakubaliana na kilimo, kwani kilimo ndio uti wa mgongo kwa Watanzania. Kilimo ndio kinachoibua uchumi wa Mtanzania na kumwondoshea umaskini. Kilimo kimeajiri 75% ya wananchi na hivyo mafanikio yake yatawafikia Watanzania wengi popote walipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyabiashara kutoka Zanzibar ambaa tayari wananyanyasika wakati wakitoa biashara Zanzibar kuleta Tanzania Bara na kutozwa kodi mara mbili, ukiangalia eti tatizo hilo msingi wake ni '*harmonisation*' ya kodi ambayo ilifanywa mwishoni mwa miaka ya tisini ili kuondoa kitu kinachoitwa kupitia njia za uchororoni (Zanzibar). Jambo hili pia limesababisha sio tu kubomoa lakini hata *Tax-base* kwa Wazanzibar kuwa mbaya. Ingawa ahadi ni nyingi na za muda mrefu za kusawazisha suala hilo lakini bila ya mafanikio na kila uchao malalamiko yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ukurasa wa 53 imeelezwa kubana matumizi, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri lakini bado, kwanza ukiangalia Sheria ya Manunuzi ina mwanya wa kuruhusu mapato kutoka. Serikali inapoteza, asilimia 70% ya fedha zinaliwa au kuingia mikononi mwa Maafisa Manunuzi, hata bajeti ya maendeleo

inapokwenda kwenye manunuzi fedha zinapotea mikononi mwa wajanja. Ili tufanikiwe ‘Muswada na Manunuzi’ uletwe Bunge kunusuru fedha za Serikali. Vilevile tuzisaidie Halmashauri, Serikali za Mitaa kwa kuwapelekea wataalam ambao wana elimu ya manunuzi ili waweze kukomesha manunuzi hewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na wataalamu na wafanyakazi wa Wizara kwa kazi wanayofanya kwa kuhusisha wadau wengi zaidi katika kuandaa bajeti hii na mimi naunga mkono. Maoni yangu ni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, uwiano wa riba kwa ajili ya amana na mikopo ni tofauti sana. Mikopo bado riba yake ni ndogo na hivyo watu hawashawishiki kuweka fedha kwa ajili ya akiba. “*Risk*” inayosemwa na mabenki si kubwa kiasi ambacho benki za biashara wanataka tuelewe. *Balance Sheet* za benki hizo zinazochapishwa haionyeshi hivyo.

Mheshimiwa Spika, pili, wafanyakazi walioko vijijini wanapata shida sana kufuata mishahara Makao Makuu ya Wilaya. Inabidi kulipa nauli na kulala nyumba za wageni. Wafanyakazi wa mjini hawapati adha hii. Wizara inaweza kuangalia utaratibu wa kuanzisha ‘*Agencies*’ kwa kushirikiana na mabenki ili kuhakikisha wafanyakazi walio vijijini wanapata mshahara wao bila gharama nyingine zaidi, inawezekana.

Mheshimiwa Spika, tatu, *Tanzania Investment Bank (Agriculture Window)*, nia ya Serikali ni kuwawezesha wakulima kupata mikopo kwa masharti nafuu. Nimetembelea shirika hilo masharti niliyopewa ni lazima kuwa na *Limited Company* yenye mwaka mmoja na zaidi na *Title Deed* za nyumba na shamba, Hati za Kimila zinazotolewa na Halmashauri hazitambuliki. *TIB* wameingia katika ugonjwa uleule wa *Big Commercial Banks*. Wasomi wanaotaka kuingia katika kilimo si rahisi kufanikiwa kupata mikopo. Napendekeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Gavana waliangalie vema jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nne, mwaka 2006 aliyejewa Waziri wa Fedha katika hoja yangu ya *PPF* na *NHC* kujenga Wilayani na hasa Mbinga aliniomba nizungumzie na *PPF* kuhusu kutekeleza ujenzi wa makazi Mbinga. Nasikitika kwamba mpaka leo hii nia hii haijatekelezwa. Napenda kuomba basi angalau mwaka huu Shirika la *PPF* lijenge angaliu jengo moja la ghorofa tatu pale Mbinga Mjini kupunguza tatizo la makazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ipewe nguvu zaidi za kweli ili ituongoze katika kusimamia vipaumbele vyetu kiuchumi na si kila Wizara kupanga kivyake lakini pia kuwe na ufuatiliaji wa kila mwezi kuona Wizara zinavyotekeliza mpango wake.

Mheshimiwa Spika, naitakia Wizara mafanikio makubwa katika utekelezaji wa bajeti hii.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kuleta bajeti yenye mwelekeo, matumaini kwa wananchi wetu ili waweze kupata maendeleo ya haraka. Maeneo yafuatayo yatiliwe mkazo katika utekelezaji wa bajeti. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kupeleka fedha kwa wakati, miradi mingi ya maendeleo inatumia fedha nyingi. Hivyo fedha zipelekwe kwa wakati ili kukwepa kupanda kwa gharama mara fedha zinapochelewa.

Mheshimiwa Spika, miradi isimamiwe, miradi mikubwa inapotekelezwa itekelezwe kwa viwango ili kupata thamani ya fedha inayolipwa. Majengo yajengwa kwa viwango. Barabara ambazo zinajengwa kwa fedha nyingi “*almost 10% of the budget, we must be keep on follow up on implementation.*”

Mheshimiwa Spika, kupunguza misamaha ya kodi kwa makampuni ya Mafuta na Madini. Misamaha itolewa pale ambao miradi hiyo italeta tija ya haraka kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuongeza Mrabaha wa sekta ya Dhahabu. Asilimia 3% ya mrahaba wa Dhahabu ni mdogo. Serikali ianze majadiliano na wawekezaji angalau ifikie asilimia 5% ya bei ya dhahabu. Wakati makampuni haya ya migodi yanaanza kuwekeza bei ya wakia moja ya dhahabu ilikuwa US\$ 1200 kwa wakia. Hivyo makampuni hayo yanapata faida kubwa na wana “*Offset*” gharama zao kutokana na faida kubwa wanayopata, sasa ni wakati wao kuendelea kufungua migodi mipyä.

Mheshimiwa Spika, kujinyima kwa ajili ya Maendeleo. Asilimia 70% ya bajeti ni “*Recurrent*” na asilimia 30% ni kwa ajili ya maendeleo. Tunakula zaidi kuliko kijiwekea kwa maendeleo. “*Consumptive Budget*.” Yapo maeneo katika “*Recurrent Budget*” ambapo Serikali inaweza kupunguza matumizi mfano *Discretionary* na *Non-Discretionary Allowances*; matumizi ya magari, mafuta, *maintenance*; semina; warsha, kongamano na mafunzo ya nje ya nchi. Bajeti ya *Recurrent* ikipungua kwa asilimia 20% kwenye maeneo hayo inaweza ku-save Shs.800 bilioni ambazo zinaweza kuwekwa katika bajeti ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawatakieni kheri katika utekelezaji wa bajeti.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri, uliotukuka wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa sera zake makini zinazojali maendeleo, umoja, amani na ustawi wa wananchi wake.

Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa bajeti ya mwaka 2011/2012 ambayo imetayarishwa kwa utaalamu na umahiri mkubwa uliozingatia matakwa ya Taifa. Bajeti hii imegusa kila nyanja ikizingatia vipaumbele katika kuendeleza kilimo, nishati,

umeme, miundombinu, fursa za biashara, huduma za jamii, elimu na afya tatizo la ukosefu wa ajira na kuthibiti mfumuko wa bei za bidhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya mwaka 2011/2012 imelenga kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Napenda nianze kuchangia hoja kwa kushauri kwamba pamoja na uzuri wa yaliyopangwa katika bajeti, kila mmoja wetu anahitaji kushiriki kikamilifu katika uwajibikaji na kutimiza wajibu wake pale alipo. Ikiwa ni pamoja na matumizi mazuri ya rasilimali zetu, uadilifu, weledi na kuona kwamba bajeti hii inalenga kukomboa wananchi hasa wale wanaoishi vijijini. Sekta ya miundombinu ikiwa ni pamoja na reli na bandari ni vyanzo vizuri vya mapato ya Taifa. Hivyo inatakiwa sekta hii ipate fedha za kutosha ili tuweze kupata mapato zaidi (huwezi kutegemea maziwa kutoka kwa ng'ombe ambaye hujamtunza na kumlisha vizuri).

Mheshimiwa Spika, reli ya Tanzania inapita katika Jimbo la Kibaha Vijijini na inategemewa na wananchi katika usafiri, ajira na biashara kwa maana katika stesheni za Soga, Ruvu, Kwala na Magindu. Stesheni ya Ruvu, treni huunganisha mabehewa ya kwenda Kigoma, Mwanza, Tanga na Moshi kutoka na kwenda Dar es Salaam. Kuboresha reli hii itafungua mwanya wa mapato zaidi kwa Mikoa inayopita kwani wananchi watapata fursa ya kuongeza kipato lakini pia upatikanaji wa pembejeo za kilimo bora na pia mazao yao yatafika sokoni kwa wakati. Taifa litakuwa na uhakika wa kupata fedha za ndani na za kigeni kwani reli hii inatumwa kusafirisha mizigo ya nchi za jirani hasa zile za maziwa makuu kama Uganda, Burundi, Rwanda, Malawi, Zambia na DRC. Kama reli yetu itaboreshwa na kutumiwa ipasavyo, itapunguza uharibifu wa barabara na kuokoa fedha za ukarabati wa mara kwa mara kwa mizigo itasafirishwa kwa reli badala ya barabara.

Mheshimiwa Spika, bandari ni sekta nyingine inayotegemewa na Taifa kwa mapato yake. Kwa sasa hivi bandari ya Dar es Salaam inaelekea kuelemewa na mizigo wakati bandari zetu zingine mfano Tanga na Mtwara hazitumiwi kikamilifu. Katika hili lazima Serikali ione na inapanga mikakati ya kupunguza msongamano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na kutoa fursa kwa bandari ya Tanga na Mtwara hutumika kikamilifu. Kwa mfano, Serikali inaweza kuamua magari yote yanayopitia bandari ya Dar es Salaam yapite bandari ya Tanga au Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji Mdogo wa Mlandizi kuna maeneo makubwa ya ardhi, Serikali ingefikiria kujenga bandari kavu ya kuegeshea magari yote yanayoingizwa hapa nchini, yawe ya *transit* au ya kuuza hapa hapa nchini kama ilivyo katika mji wa Sharjah kule Dubai. Kwa kufanya hivi, Serikali itasaidia kukuza maendeleo ya Mkoa wa Pwani, itapunguza msongamano wa sehemu za kuegesha magari zilizoko kila mtaa wa Dar es Salaam, itaongeza huduma ya kutoa mizigo kwa haraka zaidi na pia kupunguza msongamano wa mizigo bandari ya Dar es Salaam, kukuza uchumi wa Mkoa pamoja na kutoa ajira kwa vijana wa Mkoa wa Pwani na hata Mikoa ya jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa bandari kavu, Serikali inaweza kujenga stendi kubwa na ya kisasa kwa ajili ya magari ya mizigo na abiria yaendayo na yatokayo

Mikoani na nchi za jirani pale Mlandizi. *Stand* hii itaharakisha maendeleo ya Jimbo lile kwani jinsi watu watakavyotumia *stand* ile basi majengo yataongezeka, hoteli za kulala wageni, maduka na mzunguko wa pesa utakuwepo kwani huduma mbalimbali zitaboreshwani.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi yetu unategemea Wakulima na Wafugaji. Nafarijika kuona bajeti imejali pia sekta hii. Napenda kuchangia kwamba kuna haja ya kuboresha huduma na kutoa elimu kwa wananchi vijijini na kupunguza makongamano ya wataalamu, sasa waende vijijini waliko wakulima na wafugaji. Mfano katika Jimbo la Kibaha Vijijini kuna shamba kubwa la mfano la malisho ya mifugo Vikuge. Nachelea kusema kwamba pamoja na nia njema ya kuanzisha shamba hili lakini halitumiki kikamilifu. Kuna haja ya kufungua mashamba mengine kama haya pamoja na kubuni mbinu za kuvuna maji ya mvua ili msimu wa ukame mifugo ipate malisho bora pamoja na maji. Hii itasaidia pia kuondoa tatizo la ugomvi wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme ni sekta nyingine itakayotuletea maendeleo ya haraka katika karne hii ya utandawazi. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuliona tatizo la ukosefu wa umeme linavyoathiri maendeleo ya Jimbo la Kibaha Vijijini. Wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu aliahidi kulitatua tatizo hili hasa katika Kata ya Ruu. Nipende kukiri kwamba ufuatiliaji wa utekelezaji wa ahadi hii ulishaanza na Naibu Waziri wa Nishati na Madini amekwishafanya ziara katika Jimbo kuona ukubwa wa tatizo. Ni matumaini yangu kwamba bajeti ya mwaka huu itaipa uwezo Wizara kuweza kutekeleza ahadi hii na kuondoa kero ya umeme katika Kata ya Ruu.

Mheshimiwa Spika, mtu ni afya, bajeti hii imetambua hilo na kwamba Hospitali zetu zitakuwa na dawa na vifaa vya kutosha, wataalamu wa maabara, Madaktari, Manesi na watoa huduma mbalimbali katika hospitali na zahanati zetu. Ni matumaini ya wananchi kwamba huduma hii itaboreshwana Zahanati zitajengwa kila Kijiji na Kata. Aidha, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kukipandisha daraja Kituo cha Afya cha Mlandizi kuwa Hospitali ya Wilaya itatekelezwa katika bajeti hii kwani kituo kile kinabeba majukumu mengi ya kuhudumia jamii kubwa kuliko malengo yake ya awali.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini lilitokana na Jimbo la Kibaha Mjini, hivyo maendeleo yake kiuchumi liko nyuma. Huduma za afya, biashara, elimu nazo ni duni. Naomba basi katika bajeti hii Serikali isaidie kwa makusudi kabisa kuinua maendeleo ya wananchi wa Jimbo hili ambao wanajitahidi sana katika kilimo cha mbogamboga, uvuvi na ufugaji kwa kujenga soko la kisasa katika Mji Mdogo wa Mlandizi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuishauri Serikali katika athari za kuruhusu baadhi ya wafanyabiashara kutumia fedha za kigeni kama fedha halali ya kufanya manunuzi hapa nchini. Ni jambo la kawaida kabisa kusoma matangazo ya mauzo ya bidhaa na huduma katika magazeti au maduka fulani kutaka zilipwe kwa fedha ya dola ya kimarekani badala ya fedha halisi ya Tanzania. Suala hili kwa mtazamo wangu

linashusha heshima ya fedha yetu. Ukienda nchi nyingine kama Afrika Kusini, Uingereza na hata Marekani kwenyewe huwezi kununua chochote kwa kutumia fedha zaidi ya zile za nchi hizo. Ifike wakati sasa Serikali ikemee jambo hili ili fedha za Taifa letu zipewe heshima stahiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, napenda kuunga mkono hoja ya bajeti ya mwaka huu 2011/2012.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa hotuba yake nzuri, naomba niwapongeze Manaibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuanza kuufungua Mkoa wa Kigoma, tayari barabara zimeanza kufunguka, Mwandiga - Manyovu imekamilika, Kigoma – Kidawe – Uvinza - Molagasi inaendelea kujengwa na tunaishukuru Serikali kwa kuitengea fedha mwaka huu barabara ya Kigoma – Kasulu - Kibondo mpaka Nyakanazi, naomba sasa pesa hizo zilizotengwa ziweze kutumika kama zilivyopangiwa kwa sababu bajeti ya mwaka 2010-2011 barabara ya Kigoma – Kasulu - Kibondo mpaka Nyakanazi pesa zilitengwa mpaka sasa kazi hiyo haikuwa imeanza.

Mheshimiwa Spika, reli, tunaomba Serikali iangalie kilio cha watu wa Kigoma kwa sababu reli ndio mkombozi wa usafiri wa watu wa Kigoma. Wao wenye hewaze kusafiri kwa gharama nafuu, hweza kusafirisha mizigo na bidhaa nyingine kwa urahisi zaidi lakini pia uchumi wao pamoja na uchumi wa nchi uweze kukua iwapo usafiri wa reli utakamilika.

Mheshimiwa Spika, umeme katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005-2010 ilisema kuwa kila Makao Makuu ya Wilaya yatapatiwa umeme, tunashukuru kazi inaendelea kufanyika lakini sasa ni lini umeme utawaka katika Wilaya za Kasulu na Kibondo? Wananchi wana hamu kuona umeme unawaka ili waweze kujielekeza kwenye ukuzaji wa uchumi wao kwa sababu umeme ukipatikana viwanda vitaanzishwa na ajira zitapatikana. Wanawake na vijana wataweza kupata soko la kuuza matunda kama Nanasi, Maembe na matunda mengi mengi kwa ajili ya kutengeneza *juice*.

Mheshimiwa Spika, uwezeshejji wa wananchi kiuchumi. Napenda kuchangia hoja hii kwa kusema tumeweza kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi na VIKOBA, wananchi wameitikia vizuri lakini hawajaweza kukopeshwa kwa sababu hawajaweza kupata elimu ya kutosha ya kuweka na kukopa. Naomba Serikali iweze kupanga fedha kwa ajili ya kwenda kutoa elimu ya ujasiriamali, ili wananchi waweze kuelimika hatimaye waweze kukopa kwenye vyombo vyaya fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kila nchi huwa na bajeti yake kulingana na matakwa ya nchi juu ya namna gani ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia, naomba kujikita katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato, kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kupitia benki na kuanza kutumia mfumo wa M-PESA kwa malipo ya kodi yasiyo zidi Tshs.500,000/= ili kuondoa kero ya walipa kodi hususani katika hali hii ya sasa ya ukuaji wa mifumo ya kibenki itumiayo simu za mikononi na makampuni ya simu yanayotoa huduma za fedha. Ni vyema tukatumia makampuni ambayo Serikali ina hisa kubwa kama *TTCL, Zantel, Shirika la Posta au Kampuni za kibenki kama NMB* ambayo ina mifumo mingi ya huduma kupitia simu.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado haikusanyi mapato stahiki toka sekta ya misitu. Vitabu vya uwindaji vinapaswa kuipatia Serikali mapato zaidi kuliko ilivyo sasa. Wakati umefika wa kufanya mapinduzi wa kuyatoza makampuni kodi za maliasili kwa asilimia 20-30 ili angalau Serikali inufaikie na maliasili ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, stadi za ujasiriamali, kufanya tafiti zenyе lengo la kuendeleza stadi za ujasiriamali kwa kuanzisha na kuboresha shughuli za uchumi, Serikali imezitumiaje au imejishirikisha vipi katika tafiti zilizofanywa na mashirika yasiyo ya Kiserikali kama ESRF, REPOA na taasisi za elimu ya juu katika eneo hili. Ni vizuri kuangalia tafiti hizi ili ziweze kusaidia Serikali na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji, ni nzuri kwani wananchi watapata mikopo ili waweze kupata mitaji na kujajiri lakini kuna mikakati gani imewekwa kukabiliana na riba kubwa ambazo zinatozw na taasisi nyingi za kifedha zitoazo mikopo ambazo kwa kiasi kikubwa zinarudisha nyuma juhudzi za wanaojajiri. Ni vizuri Wizara ikapanga vyema shughuli hii ili waweze kuwasaidia vijana na wanawake ambaao wanajajiri wenyewe na kuwapunguzia mzigo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kupunguza malipo ya posho, kupunguza malipo mbalimbali yasiyokuwa na tija, kupunguza matumizi ya mafuta kwa magari ya Serikali, kupunguza safari za ndani na nje. Upunguzaji huu unatakiwa kuwa vipi? Kwani vitabu vya bajeti hasa kwa Wizara bado posho, matumizi ya mafuta na safari za ndani na nje zimeainishwa na kutengewa fedha nyingi. Ni vyema bajeti ikaainisha kwa asilimia ngapi punguzo hizi zitakuwa.

Mheshimiwa Spika, fedha za miradi ya maendeleo, bado fedha za miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa ni tegemezi kwa wahisani. Fedha za ndani ni milioni 1,871,471 wakati fedha za nje ni milioni 3,054,137. Serikali inapaswa iweke mikakati ya kujikwamua katika utegemezi huu hasa wa miradi ya maendeleo. Serikali inapaswa iweke mikakati siku za usoni, matumizi ya kimaendeleo katika bajeti yawe na gawio kubwa kuliko matumizi ya kawaida kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa Katiba Mpya, je, bado Serikali ina dhamira ya kutekeleza mchakato wa Katiba Mpya? Kwani katika mpangilio wa bajeti haijaainisha kabisa pia hata katika hotuba ya Waziri wa Fedha hajaligusia, licha ya uzito na unyeti wake.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze na kiwango cha malipo ya makosa barabarani kutoka Shs.20,000/= hadi Sh.300,000/= kama inavyosomeka kwenye kitabu cha bajeti ingawa Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitamka Shs.50,000/=. Kwanza atuambie (*Traffic Notification Fee*) ni kiasi gani kati ya Shs.50,000/= au Shs.300,000/=. Kama ni Shs.300,000/= ni pesa nyingi itakayochochea rushwa kwani Watanzania kipato chao ni kidogo hawawezi lipa hiyo shilingi laki tatu. Matokeo yake Askari wa Barabarani watageuza mradi na rushwa itazidi, makosa yatatafutwa kilazima ili mradi tu Askari apate chochote kutoka kwa Dereva, anapoonesha hawezি kulipa pesa hiyo ya (*Traffic Notification Fee*).

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya maisha ya Mtanzania ni ngumu kwani gharama za maisha zimepanda. Nashauri Serikali isikie kilio cha Watanzania walio wengi kwani bei ya bidhaa za matumizi ya kila siku mfano chakula; Unga, Mcchele, Maharage n.k bei ni kubwa mno hasa kwa walaji wa kipato cha chini hasa waishio vijijini. Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha mkakati wa makusudi wa kupunguza ukali wa maisha kwa kuangalia jinsi gani mtapunguza bei za mafuta ya *petrol*, *diesel* na mafuta ya taa na Serikali isisitize katika uinuaji wa uchumi vijijini (*rural economic growth*).

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana Serikali ising'ang'anie tu katika kufuta tozo, maana tozo zenyewe ni sita tu kati ya maeneo 21. Ipo haja ya Serikali kuangalia pia *Excise Duty* na *Import Duty* ili punguzo la gharama za mafuta liwe endelevu hata bei zikipanda. Aidha *Road Toll* isipunguzwe. Kwani utekelezaji wa hatua hiyo muhimu na ufuutiliaji wake utapunguza kwa kiwango kikubwa ukali wa maisha ya Mtanzania mwenye kipato cha chini ambaye huathiriwa sana na bei ya mafuta kupanda kwani wenyе uwezo huwa wanakabiliana na hali hiyo kwa urahisi kidogo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia *TPDC* pamoja na kuwa na mamlaka ya udhibiti katika kutafuta na kuchimba mafuta na gesi, nashauri Serikali iiwezeshe *TPDC* iweze kununua hisa asilimia 50 zilizobaki za BP (T) Limited na kuipa mtaji wa kutosha ili ifanye biashara ya mafuta kwani nchi nyingi duniani hutumia mashirika yake ya umma kwenye sekta ya umma ili kudhibiti upandaji bei wa mafuta bila mpangilio.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napendekeza kuwa makampuni ya uchimbaji madini yasipewe misamaha ya kodi kwenye mafuta pia makampuni ya ujenzi, sababu ni kwamba imethibitika kuwa makampuni hayo yanaposamehewa kodi nchi yetu inapoteza mapato makubwa na mafuta mengi yanayoingia kuitia msamaha huu hurudi kwenye soko na kuuzwa rejareja, ambapo lita 133m za *diesel* sawa na 20 ya mafuta yote ya *diesel* yanayoingizwa nchini, ziliingizwa na makampuni matano tu ya migodi ya dhahabu na kampuni hizo zililipa dola laki mbili tu kama ushuru. Hivyo bora tufute misamaha yote ili

nchi ipate mapato zaidi kwani hali halisi inaonesha mafuta hayo hurejeshwa sokoni na kuuzwa rejareja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake pamoja na Watendaji wake wa Wizara kwa maandalizi ya bajeti nzuri na muhimu kwa Taifa na ya matumaini ya Watanzania hasa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimefarijika kwa maandalizi haya bali hofu yangu ni utekelezaji kwani ukilinganisha bajeti ya mwaka 2010/2011 na hii ya mwaka 2011/2012 haina tofauti pamoja na nyongeza ya fedha inayoonekana kwenye maandishi, kwani jinsi gharama za maisha na ongezeko la matumizi ya fedha yalivyo leo yamepanda kupindukia. Shs.1,000/= ya mwaka 2008/2010 matumizi yake na Shs.1,000/= ya leo ni tofauti hivyo hakujaongezeka kitu. Hata kama Wizara imeongezewa fungu basi bado hali ni ileile kwa mfano bei uliyonunulia *cement* mwaka 2010 na leo hii tofauti na hata pembejeo za kilimo ni hivyo hivyo. Maana yangu ni kwamba hata hivyo vipaumbele hatuwezi kuvifiki kulingana na kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Biashara na Viwanda bajeti iliyopita, fedha waliyopewa safari hii imepunguzwa na hiyo ya mwaka jana haikupatikana kama ilivyopangwa. Je, tutafikia malengo au tunadanganyana tu?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ya Elimu tuiongezee bajeti kwani mahitaji ni makubwa zaidi mfano upungufu wa Walimu, nyumba za Walimu, maabara na hata mishahara ya Walimu hairidhishi ukilinganisha na ugumu wa kazi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Elimu na Afya ni Wizara za kuziangalia kwa umakini mkubwa. Bila Walimu wenye uwezo, hatuna wataalamu na Taifa lisilo na wataalamu ni Taifa duni, lakini pia bila afya hatuna nguvu kazi. Naomba sana tutoe kipaumbele kwa vitendo na sio kwa maneno.

Mheshimiwa Spika, bado tuna matatizo ya mapato ya Serikali kuwa madogo na hivyo kutokidhi kuchangia kwenye miradi ya maendeleo. Pia huwezi kupunguza bajeti tegemezi kwa mapato ya ndani kuzidi matumizi ya kawaida. Ukiangalia bajeti iliyopita 2010/2011 na hii ya mwaka 2011/2012, utaona kwamba bajeti ya maendeleo haiheshimiwi na huku ni kulidhalilisha Bunge kuleta bajeti ambayo haitekelezeki na hicho ndicho kilichotokea bajeti zilizopita.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Mpango wa Maendeleo, Tume imepanga kukuza uchumi kwa 8%, lakini kwenye bajeti inazungumzia kukuza uchumi kwa 6% tu. Je, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatuambiaje hapa Bungeni ili wananchi wajue kiwango halisi cha ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, MPAMITA ambao ulizinduliwa tangu mwaka 2006 na ulitarajiwa kuupatia misaada Tanzania toka nje, lakini inaonekana umaskini umeongezeka ukilinganisha na matumizi ya kimataifa ambayo ni dola moja lakini watu

wanaotumia chini ya dola moja ni 68% na kusababisha Watanzania 34% kuwa na utapiamlo.

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tulipokuwa tunasitisha shughuli mchana nilisema tutaanza na Waheshimiwa Mawaziri kuanza kujibu hoja au kufafanua hoja mlizokuwa mmezitoa katika muda wa siku tano. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri mmojawapo na atatumia muda wa dakika kumi na tano zinazobaki Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili la bajeti, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo. Vile vile, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu kwa kipindi cha miaka mingine mitano. Aidha, namshukuru sana Rais kwa imani yake kwangu na kunateua kuwa Naibu Waziri wa Fedha, kazi ambayo naahidi nitaifanya kwa nguvu zangu zote. Nampongeza pia Mheshimiwa Mizengo Kayaza Pinda, Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo tena kwa kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano. Nampongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya Naibu Spika, niwapongeze vile vile Wenyeiti wa Bunge, Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Sylvester Mabumba kwa kuteuliwa kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpwapwa kwa imani waliyoonyesha kwangu kwa kunichagua na kunipa ridhaa ya kuingia Bungeni, nawaahidi kuwatumikia kwa moyo wangu wote.

Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja mbili zilizowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, kwanza aliwasilisha kuhusu hali ya uchumi na vilevile aliwasilisha bajeti ya Serikali. Napenda kuunga mkono hoja zote mbili ambazo zimelenga kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Bajeti hii imezingatia masuala muhimu ya Kitaifa ambayo ni nyezo muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa mwaka 2025. Aidha, bajeti hii ni ya mwaka wa kwanza wa mpito wa kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano unaozingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 na awamu ya pili ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili Hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 pamoja na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo watu wengi walichangia ilikuwa ni sera ya magari ya Serikali. Serikali inatarajia kukamilisha Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kukamilika kwa sera hiyo kutatoa miongozo yote ya jumla inayohusu ununuzi wa umma ikiwa ni pamoja na suala la magari ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ilikuwa ni kuongeza huduma za kibenki vijijini. Katika hotuba ya Hali ya Uchumi iliyowasilishwa hapa Bungeni, Waziri wa Fedha alieleza kwa kina katika aya ya 29, aya ya 32 maboresho yaliyofanyika katika sekta ya fedha hususan kuongeza huduma za kibenki vijijini. Serikali inaendeleza juhudzi za kupanua wigo wa utoaji huduma za kibenki ili kufikia asilimia 50 ya Watanzania ifikapo mwaka 2016. Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zikiwemo kufungua milango ya kuanzisha huduma za benki mbalimbali nchini na kulegeza masharti ili asasi na taasisi za aina mbalimbali nchini zenye mwelekeo na uwezo wa kutoa huduma hizo ziweze kufanya hivyo. Matokeo ya utafiti wa upanuko wa huduma za kifedha uliofanyika mwaka 2009 yalionyesha kwamba asilimia 12.4 ya Watanzania wanapata huduma za kifedha kutoka sekta rasmi ya fedha yaani mabenki. Asilimia 4.3 hupata huduma kuitia *SACCOS*, vilevile hupata huduma kuitia *NGOs* na Makampuni ya Mikopo kama vile *PRIDE*, *VICOBA* na *ROSCA* na asilimia 56 walikuwa hawapati huduma za kifedha kabisa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zilizochangia hali hii ni pamoja na ukosefu wa elimu kuhusu masuala ya kifedha, imani ya kutohifadhi fedha benki, urasimu wa taratibu za kibenki, umbali na mahali benki ilipo, umaskini wa kipato na miundombinu dhaifu. Katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha vijijini, yafuatayo yamefanyika:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mkakati wa huduma za kifedha vijijini, yaani *rural financial services strategy* pia nia ni kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa mtu mmoja mmoja, kaya na wajasiriamali wadogo na wale wa kati. Benki ya Dunia imetoea mkopo wa dola za Kimarekani zipatazo milioni 40 kwa ajili ya kuanzisha mfuko au chombo cha kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba, ikiwemo mikopo midogo midogo ya muda mrefu ya ujenzi wa nyumba kwa wananchi wa kipato cha chini yaani *microfinance housing facility*. Vile vile ni kuweka mazingira bora ya kutoa elimu ya kifedha vijijini na kutengeneza mfumo wa kumlinda mtumiaji wa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushindani mkubwa wa taasisi za kifedha vijijini au mijini, taasisi za kifedha zimeendelea kufungua matawi katika maeneo yaliyo nje ya miji mikubwa, taasisi nyingine kama vile Vyama vya Kuweka na Kukopa yaani *SACCOS* na Benki za Wananchi zimeendelea kusogea huduma kwenye miji midogo zaidi. Aidha, huduma zinazotolewa kwa njia ya kiteknolojia ya mawasiliano ya simu yaani *mobile banking* na *ATMs* zinakuwa kwa haraka zaidi. Inatarajiwa kuwa kukamilika kwa hatua hizo, kutaboresha zaidi upatikanaji wa huduma za kifedha vijijini na hivyo kuboresha zaidi maisha ya Mtanzania anayeishi kijijini.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ilikuwa mifuko ya *SELF* au *VICOBA* na *SACCOS* iwezeshwe ili ikopeshe Watanzania wengi. Kama ilivyoelezwa na wachangiaji wengi ni vigumu kwa wananchi wa kawaida kupata mikopo toka mabenki ya biashara. Taarifa zitokanazo na tafiti *Free scope* Tanzania za mwaka 2006 na 2009 zimebaini kwamba takriban asilimia 54 ya Watanzania kwa mwaka 2006 na asilimia 56 kwa mwaka 2009 hawajafikiwa na huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na mikopo. Serikali imeandaa sera na programu mbalimbali ambazo zinalenga kupanua wigo wa kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kupata huduma za kifedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *SELF*, umeendelea kuwezesewa ambapo hivi sasa unatekeleza awamu ya pili inayofadhiliwa na Serikali pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika katika awamu ya kwanza kilitumika kiasi cha shilingi bilioni 13 ambapo shilingi bilioni nane zilitumika kukopesha asasi ndogo ndogo za kifedha, hususan katika sekta ya uvuvi. Aidha, mpango huu unakusudia kutoa mikopo ya shilingi bilioni 30 katika kipindi cha 2010/2015 na kuwafikia walengwa karibuni 840,000. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa JK, ulioanzishwa mwaka 2005 umehamasisha kwa kiasi kikubwa uanzishwaji wa *SACCOS* hapa nchini. Serikali itaendelea kuimarisha *SACCOS* kuitia Idara ya Ushirika ili iweze kutoa huduma bora za kifedha kwa wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne, ni ujenzi wa ofisi za Wizara zinazohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar. Suala la ujenzi wa ofisi zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Muungano limekuwa likipewa kipaumbele na Serikali zote mbili. Wizara za Muungano zimekuwa zikijenga ofisi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kwa upande wa Zanzibar kulingana na mahitaji kwa mfano, Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania tayari wana majengo ya ofisi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano, ilikuwa inalenga kutotengwa fedha katika bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa ajili ya uanzishwaji wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri mpya. Kama alivyofafanua Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni, mchakato wa kuanzisha Mkoa, Wilaya na Halmashauri mpya unapitia hatua mbalimbali za kisheria ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni ya wananchi na hatimaye kutangaza rasmi maeneo hayo ya kiutawala katika Gazeti la Serikali. Mchakato huo unaendelea kukamilishwa na mamlaka husika. Aidha, ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imetenga fedha chini ya Fungu 21 yaani Hazina ambapo fedha hizo zitahamishiwa kwenye Mafungu husika mara baada ya taratibu hizo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inahu kurudishwa kwa ada za leseni katika Halmashauri za Miji, Manispaa, Wilaya kutazuia uanzishwaji wa biashara ndogo. Serikali imeamua kurejesha leseni za biashara kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa kanuni za biashara...

**SPIKA:** Naomba tumsikilize acheni kunong'ona sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. GREGORY G. TEU:** Kurahisisha utambuzi wa biashara mpya na hatimaye kupanua wigo wa kodi. Aidha, napendekeza kwamba badala ya Serikali kupanga viwango vya leseni ya biashara kwa Serikali za Mitaa, viwango hivyo vitapangwa na wao wenyewe. Kadhalika Halmashauri zitatakiwa kuweka kanuni na taratibu za kusimamia utoaji wa leseni ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba haiwi kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba, Mamlaka ya Mapato Tanzania iwachukulie hatua watendaji wake wanaoshiriki kupoteza mapato ya Serikali. Tunakubaliana na hoja kuwa hatua hazina budi kuchukuliwa kwa watendaji wote wanaoshiriki kupoteza mapato ya Serikali. Katika kuhakikisha kuwa mapato yote ya Serikali yanakusanywa ipasavyo, *TRA* inasimamia kwa makini taaluma, uadilifu na uwajibikaji wa watumishi wake, kwa upande wa taaluma, *TRA* inaendelea kuboresha Chuo cha Usimamizi wa Kodi ambako watumishi hupata mafunzo ya taaluma mbalimbali mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine inahusu Makampuni ya Madini hayalipi kodi na kuwe na *specialized training* ili kugundua wanaodanganya. Baadhi ya Makampuni ya Madini ambayo katika siku za nyuma yalikuwa hayalipi kodi ya makampuni sasa yameanza kulipa kodi hiyo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali imekusanya kodi ya makampuni shilingi bilioni 32.1. Uchimbaji wa madini hutumia mitaji mikubwa katika ununuzi wa mitambo inayofanya uanzishwaji wa gharama za uwekezaji kuchukua muda mrefu na hivyo kufanya baadhi yao wasilipe kodi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kwamba, Serikali inakosa mapato kwa kutotumia vizuri bahati nasibu. Katika jitihada za kuongeza mapato, Serikali imeweza kuboresha mfumo wa bahati nasibu kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kumpata mwendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa. Mwendeshaji huyo ataanza rasmi uendeshaji wa bahati nasibu tarehe 15 Agosti, 2011, hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni nyumba zinazopangishwa zibainishwe na wenye nyumba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri anayefuata!

**NAIBU WA WAZIRI WA FEDHA - MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia, naomba

niziunge mkono hoja zote mbili zilizowasilishwa kwa kuamini kwamba zina nia nzuri kwa jamii ya Watanzania katika kuondoa umaskini na kuinua uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa tena kwa kishindo na kunipa imani ili nifanye kazi kama Naibu Waziri wa Fedha. Nashukuru kwa umahiri wako Mheshimiwa Spika pamoja na wenyeviti katika kuendesha vikao hivi. Nawashukuru kwa kipekee wapiga kura wangu wa Jimbo la Chumbuni, nawaahidi sitowaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba nichukue nafasi nami kufafanua baadhi ya hoja ambazo zilitolewa kwenye hoja hizi mbili zilizowasilishwa. La kwanza, kuhusu Benki Kuu na kuweka akiba ya dhahabu. Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya *BOT*, kinatoa ruhusa ya kutumia dhahabu kama akiba ya Taifa. Hadi mwaka 2003, *BOT* ilikuwa imekusanya trilioni elfu themani na hamsini na saba kama akiba, pamoja na hayo, *BOT* ilikuwa inapata hasara wakati ambapo bei ya dhahabu kwenye soko la dunia ilikuwa inashuka. Hii ilikuwa ina matatizo kulinganisha na sera za *BOT* kwamba lazima akiba zihakikishwe zina usalama wa kutosha ili kulinda thamani ya shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia kuhusu kukamilisha zoezi la *sovereign rating*. Katika suala hili, Mshauri Mwelekezi ameshapatikana na taratibu zinaendelea na atatangazwa hivi karibuni. Hoja nyingine ilikuwa ushauri kwamba, mikopo inayochukuliwa isitumike kwa matumizi ya kawaida. Katika hili nakubaliana na Sheria ya Mkopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 na kanuni zake ambayo ndiyo nguzo kuu ya masuala haya. Serikali inakubaliana na hoja na itakopa ndani na nje kwa kugharimia shughuli za maendeleo kama ilivyofanya katika 2010/2011 ilipokopa kwa ajili ya ujenzi wa barabara na mitambo ya umeme wa Dar es Salaam na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali haitakopa kugharamia matumizi yetu ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuharakisha utekelezaji wa shughuli za ubia au *PPP* baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Baada ya kupitisha sheria, kanuni pia zimeshachapishwa na zimetangwazwa kwa tangazo namba 165 la tarehe 3 Juni, 2011. Kinachoendelea ni kuainisha miradi ambayo itashughulikiwa katika mwaka huu wa fedha. Serikali inakubali ushauri wa kutangaza miradi inayoonekana inafaa kwenye tovuti za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya Mbunge kuhusu ujenzi wa Chuo cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere na kwamba je, kuna uwezekano wa kuanzishwa chuo hicho kwa kutumia *PPP*? Jibu ni ndiyo! Maombi yanaweza yakafanywa kwa kutazama kwamba chuo hicho kinaweza kikafikia masharti yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba siku 18 kuondoa mizigo bandarini ni nyingi. Naomba nitoe maelezo kwamba uondoaji wa mizigo unategemea wadau wengi wakiwemo Shirika la Meli, *TRA*, *TPA* na wengine wengi. Kwa hiyo, ili mizigo itoke bandarini kwa wakati, ni lazima wote washirikiane na kila mmoja afanye kazi kwa kadri

ya uwezo wake. Mwaka 2009 kulikuwa na utafiti ulioonyesha kwamba kwa wakati ule kuondoa mzigizo ilikuwa inachukua wiki mbili, wadau walikutana wakakubaliana kwamba zisizidi siku tano. Katika kulitekeleza hili waliomba kibali kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Sheria ya *East African Customs Law* na wakaruhusiwa kwamba *at least papers* za Wizara zipelekwe kabla meli haijafikia yaani *24 hours* na hili limesaidia na inaonekana kama malengo yanaweza yakafikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo au taarifa kwamba *sub millers* wanatumia njia na mikakati ya kukwepa kodi. Naomba nitoe taarifa kwamba jambo hili ni kweli liligunduliwa wakati *TRA* walipokuwa wanafanya ukaguzi wa kawaida na pia taarifa za ziada zilipatikana kwenye mtandao wa *Action Aid*. *TRA* inashirikiana na nchi nyingine katika kulifuatilia hili, wale ambao wana makampuni ya *sub miller* na taarifa tutaitoa pale ambapo taarifa zaidi zitajitomoza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba tupige marufuku kama vivutio vya misamaha ya kodi kwa vifaa ambavyo vinapatikana nchini. Kwa mujibu wa Sura namba 38 ya Sheria ya Uwekezaji ni kweli misamaha inatolewa, lakini unafuu huo hautolewi kwa bidhaa kutoka nje kama za ndani zipo, bidhaa hizo ni kama *cement*, nondo na kadhalika. Msamaha unaweza kutolewa pale tu ambapo bidhaa za ndani hazitakidhi mahitaji ya kazi maalum inayotaka kufanywa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni ushauri kwamba *income tax returns* zizazwe na kila mtu kwa mujibu wa Sheria. Nathitibisha kwamba Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 332, inataka kila mtu ajaze *returns* hizi isipokuwa mtu ambaye mapato yake yote yanatokana na ajira tu. Utekelezaji utakuwa rahisi pale ambapo Watanzania wote watakuwa na vitambulisho kwa sababu itakuwa rahisi kutambuana.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya *income tax* kushushwa kwa viwango vya chini hadi 9%. Serikali inatambua ugumu wa maisha unawakumba wananchi na kwa sababu hiyo mwaka 2006/2007 tayari iliteremsha *income tax* kutoka 18.5% mpaka 14% mwaka 2010. Pia kuongeza kiwango cha chini ambacho *income tax* inaanza kukusanywa. Kwa hiyo, hili ni wazo zuri na Serikali itaendelea kulifanyia kazi pale hali ya bajeti inaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni tatizo la magari yaliyotolewa msamaha wa kodi kutoruhusiwa kufanya biashara. Naomba nilithibitishe hili kwamba Sheria ya Usajili wa Magari, Sura Namba 124, inaruhusu magari kufanya biashara yale tu ambayo yalisajiliwa kwa ajili hiyo. Iwapo gari lilipata msamaha haliruhusiwi kufanya biashara mpaka lisajiliwe kwa kazi mpya ambayo linataka ifanye.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya kutaka kutoza *freight rate* kwa *container* yenye bidhaa zinazofanana. Naomba nitoe taarifa kwamba Tanzania ni mwanachama wa *WTO* na pia *WCO* ambayo ni Shirika la Forodha la Dunia. Hawa ndiyo wanatupa kanuni za kukadiria mzigizo na kutohana na kanuni zao inasisitiza kwamba thamani au kodi izingatie thamani ya mzigizo halisi ya bidhaa zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ya kuboresha utaratibu wa kukadiria ushuru wa magari. Ni kweli kwamba *TRA* imeanzisha utaratibu mpya tunaouita *BORA* wa kutathmini magari hasa makuu kuu ambao umeanza tarehe 1/6/2011. Utaratibu huu uko kwenye tovuti na mtu yejote anaweza kuupata kwa taarifa na pia anaweza kuutumia kwa ajili ya kukadiria, angeweza kutozwa kodi ya kiasi gani. Utaratibu huu umeshatumika kwa ufanisi kwenye nchi za Kenya, Mauritius, Ghana na Sri Lanka na mpaka sasa unaonekana unaweza kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ilikuwa ni uwasilishaji wa kodi za mapato kwa mishahara ya wafanyakazi wa Makampuni ya Wachimbaji Madini. Kulikuwa na wasiwasni kwamba kunawenza kuwa na ujanja, *TRA* imejizatiti kukusanya kodi ya mapato popote pale ilipo na kwa hili kama Waheshimiwa Wabunge wapo ambao wana taarifa za viashiria basi tunawakaribisha ili tuweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kukusanya kodi ya Ongezeko la Mitaji yaani *Capital Gains* kwenye mauzo ya kampuni ambazo mali zake ziko nchini. Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura Namba 332, hairuhusu yaani sheria yetu ya sasa hairuhusu kukusanya ongezeko la thamani unaotokana na hisa ambazo si za Kitanzania *off show shares transfers*. Hata hivyo, utatafutwa uzoefu au *best practice* na tunaweza tukafikiria kubadilisha sheria ili tusiendelee kukosa faida yake.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuanzisha utaratibu wa kushughulikia kadhia na nyaraka ya mizigo kwa saa 24. *TRA* imekuwa inaongeza muda kuhakikisha kwamba mizigo haikai na imeongeza muda wa kufanya kazi katika siku za kawaida kwenye maeneo ya kuzishughulikia kadhia mpaka saa mbili kwa siku za kawaida na saa saba mchana siku za Jumamosi, lengo ni kufanya kazi saa 24. Hili litawezekana tu ikiwa wadau wote wanaofanya kazi na *TRA* wanaweza wakabadilisha mwenendo wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja kuhusu mapato ya uvuvi. Kitabu *Volume I* kilisemekana kwamba hakikuonyesha mapato yanayopatikana kutockana na uvuvi. Kuna mapato ya uvuvi ambayo yalikusanywa na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu jumla ya milioni 2.1 *dollars* mpaka Juni 15, 2011. Mapato haya hugawanywa kwa 50% kubaki mamlaka, 30% kubaki SMT na 20% kwenda SMZ. Katika hili SMT ilikusanya 632,454.26 *dollars* katika mwaka 2010/2011. Mamlaka ndiyo kwanza imeanza, kwa hiyo, kusingkuwa na *figures* katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu ukubwa wa riba. Toka mwaka 1991, Serikali iliaachia soko kupanga riba, mahitaji na *supply* yanatakiwa yatupe riba. Pamoja na hivyo Serikali imekuwa inapitia sera zake za bajeti na fedha kujaribu kupunguza ugumu wa riba kwa kupitia kwenye ujazi wa fedha na hatua nyingine za kibenki. Pamoja na hivyo, riba zimeendelea kubaki juu lakini Benki Kuu inaendelea kulisimamia suala hili na linawashauri *bankers* kuendelea kuwaelimisha wateja wao pamoja na kuhakikisha kwamba vyombo vinavyohusika katika kupunguza riba kubwa vinakuwepo nchini. Kulikuwa na hoja ya ukusanyaji wa mapato yasiyokadiriwa yaani mapato ambayo si ya kodi.

Mheshimiwa Spika, mapato haya hukusanywa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – MHE. PEREIRA AME SILIMA:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri na sasa nitamwita mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mbunge wa Peramaho; Mheshimiwa George Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Mheshimiwa Sylvester M. Mabumba, Mbunge wa Dole kwa jinsi mlivyosimamia na kuongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja za Serikali nilizotoa tarehe 8 Juni, 2011 kuhusu taarifa ya hali ya uchumi kwa mwaka 2010 pamoja na mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012. Aidha, nawashukuru kipekee Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dokta Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kuwasilisha kwa ufasaha maoni ya Kamati yake. Kadhalika namshukuru Waziri Kivuli wa Fedha na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika masuala ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini kwa maoni ambayo kwa sehemu kubwa yanaunga mkono bajeti ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kuwashukuru Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Gregory G. Teu na Mheshimiwa Pereira Silima kwa kuchangia na kutoa ufanuzi kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na waliota maoni yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, hoja zangu zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 227. Kama ilivyo ada itabidi niwataje na nakuomba kwamba muda nitakaoutumia kuwataja Waheshimiwa Wabunge uongezwe, maana yake...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri muda huo hatutauhesabu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza ni Waheshimiwa Wabunge 92 na ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Dokta Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni; Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini; Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando; Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mbunge wa Sumve; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na Mheshimiwa Kidawa H. Salehe Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Zungu Mussa Azzan, Mbunge wa Ilala; Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga; Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mbunge wa Kawe; Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa; Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa; Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga; Mheshimiwa Khamis Seif Ali, Mbunge wa Mkoani; Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri, Mbunge wa Babati na Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mbunge wa Solwa; Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Mbunge wa Kikwajuni; Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga; Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo; Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni; Mheshimiwa Godbless J. Lema Mbunge wa Arusha; Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini; Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu;; Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi na Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, Mbunge wa Mwibara; Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mbunge wa Chonga; Mheshimiwa Stephen J. Maselle, Mbunge wa Shinyanga; Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Deogratias Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara; Mheshimiwa Munde T. Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime; Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini na Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ali Kheir Khamis, Mbunge wa Kwamtipura; Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo; Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini; Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo; Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu; Mheshimiwa Haji Kombo Mussa, Mbunge wa Chakechake na Mheshimiwa Tundu A. Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba; Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mbunge wa Gairo; Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, Mbunge wa Kishapu; Mheshimiwa Charles J.P. Mwijage,

Mbunge wa Muleba Kaskazini; Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini; Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini; Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Joseph Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani; Mheshimiwa Mwigulu L. M. Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi; Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia wapo Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rita Louise Mlaki, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela; Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Njombe Kaskazini; Mheshimiwa Zainab Rashid Mfaume Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni; Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mbunge wa Lushoto; Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa; Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge na Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mbunge wa Rombo; Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini; Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mbunge wa Masasi; Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mbunge wa Babati Vijijini; Mheshimiwa Ramo M. Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini; Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mbunge wa Dole; Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mbunge wa Hai; Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni; Mheshimiwa Said R. Bwanamdogo, Mbunge wa Chalinze; Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile; Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mbunge wa Mbogwe; Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mbunge Ukerewe; Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mbunge wa Viti Maalum; Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mbunge wa Mpwapwa na Mheshimiwa Pereira A. Silima, Mbunge wa Chumbuni na Naibu wa Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha Waheshimiwa 135 walichangia kwa maandishi. Nao ni hawa wafuataao:-

Mheshimiwa George B. Shimbachawene, Mbunge wa Kibakwe; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa AnnaMaryStella J. Mallac, Mbunge wa

Viti Maalum; Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe; Mheshimiwa Ismail A. Rage, Mbunge wa Tabora Mjini; Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Zaynabu M. Vullu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe; Mheshimiwa Hussein N. Amar, Mbunge wa Nyang'hwale na Mheshimiwa Vincent J. Nyerere – Mbunge wa Musoma Mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Yusuph A. Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini; Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini; Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Koani; Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe; Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mbunge wa Dole; Mheshimiwa Maua Abeid Daftari, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa; Mheshimiwa Dokta Militon M. Mahanga, Mbunge wa Segerea na Mheshimiwa David N. Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Christina G. Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Titus M. Kamani, Mbunge wa Busega; Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mbunge wa Kwela; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mbunge wa Kiembe Samaki; Mheshimiwa Josephine T. Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mbunge wa Matemwe; Mheshimiwa Mansoor S. Hiran, Mbunge wa Kwimba; Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde; Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Faustine E. Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni; Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mbunge wa Njombe Magharibi na Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mbunge wa Longido.

Mheshimiwa Spika, wengine waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dokta Lucy S. Nkya, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki; Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi; Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mbunge wa Kawe; Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi; Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala; Mheshimiwa Rachel Mashishanga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Lolesia M. Bukwimba, Mbunge wa Busanda; Mheshimiwa Dokta Anthony G. Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi; Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, Mbunge wa Sihia; Mheshimiwa Naomi M. Kaihula, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mbunge wa Ngorongoro; Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni; Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla, Mbunge wa Kilolo na Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini; Mheshimiwa John J. Mnyika, Mbunge wa Ubungo; Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mbunge wa Mbogwe; Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa

Rukia K. Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Fakaria Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki; Mheshimiwa Saleh A. Pamba, Mbunge wa Pangani; Mheshimiwa Abuu H. Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini na Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile wapo Mheshimiwa Thuwayba Idrissa Muhammed, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto; Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mbunge wa Ngara; Mhe, Annastazia J. Wambura, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini; Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mbunge wa Kibiti; Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni na Mheshimiwa Dokta Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Joseph J. Mukya, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mbunge wa Dimani; Mheshimiwa Rose K. Sukum, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu; Mheshimiwa Maida Hamadi Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Aliko N. Kibona, Mbunge wa Illeje; Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi; Mheshimiwa Innocent E. Kalogeris, Mbunge Morogoro Kusini; Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mbunge wa Muheza; Mheshimiwa Juma S. Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini; Mheshimiwa Suleiman Nassibu Omar, Mbunge wa Mfenesini; Mhe, John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi; Mheshimiwa Mahmoud H. Mugimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini; Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mbunge wa Kyerwa; Mheshimiwa Moshi S.Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini; Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni pamoja na Jerome D. Bwanausi, Mbunge wa Lulindi; Mheshimiwa Subira Hamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa; Mheshimiwa Mussa Khamis Silima, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi; Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu; Mheshimiwa Salum Khalifan Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini na Mheshimiwa John Z. Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wengine ni pamoja na Mheshimiwa Christopher O. Ole – Sendeka, Mbunge wa Simanjiro; Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Nyambari C.M. Nyangwine, Mbunge wa Tarime; Mheshimiwa Shawana Bukheri Hassan, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole; Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Abdallah Juma Abdallah Saadala, Mbunge wa Raha Leo; Mheshimiwa Devotha M.

Likokola, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Binilith S. Mahenge, Mbunge wa Makete na Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe; Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni; Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki; Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, Mbunge wa Bukombe; Mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Rebeca M. Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Seif S. Rashid, Mbunge wa Rufiji; Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Namelok E.M. Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dokta Mary M. Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Shaffin A. Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini; Mheshimiwa Dokta Kebwe S. Kebwe, Mbunge wa Serengeti; Mheshimiwa Mohammed G. Dewji, Mbunge wa Singida Mjini; Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mbunge wa Kiwani na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Uchumi na Fedha, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge yataisaidia sana Serikali katika utekelezaji wa bajeti hii na katika kuandaa bajeti za miaka iijayo. Kukamilisha bajeti moja ndiyo mwanzo wa maandalizi ya bajeti nyingine, nawashukuruni nyote kwa michango yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwa kuunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti iliyowasilishwa. Kuunga mkono huku ni ushahidi tosha kwamba bajeti niliyowasilisha imezingatia masuala muhimu ya Kitaifa ya kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha. Bajeti hii ni bajeti ya matumaini na ni imani yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote tutashirikiana kwa karibu kutekeleza bajeti ya Serikali niliyowasilisha ili kuwaaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya bajeti ya Kambi ya Upinzani imekubaliana na makadirio ya mapato na matumizi niliyowasilisha katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mapato ya Halmashauri kukusanya shilingi bilioni 351, mikopo ya misaada inayotegemewa kutoka nje shilingi trilioni 3. 924, mikopo ya ndani shilingi trilioni 1.204 na matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje shilingi trilioni 3.54.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo tumetofautiana ni pamoja na sera inayohusu mauzo ya mbao na magogo, kurejesha ada za leseni ya biashara katika Halmashauri, mauzo ya hisa za Serikali ili kupata shilingi bilioni 550 na ongezeko la kima cha chini cha mshahara kuwa sh. 315,000/=.. Napenda kueleza hapa kuwa mapendekezo haya hayawezi kutekelezeka kwa sasa kutokana na athari ambazo zinaweza kujitokeza. Hata hivyo, napenda niwahakikishie wenzetu wa Upinzani kwamba, tumeyachukua na tutayafanyia kazi ili yale yanayoonekana kutekelezeka yaweze kuzingatiwa na ikiwezekana kuingizwa katika bajeti zijazo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo ya baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nirejee kusisitiza maneno muhimu katika hotuba yangu ya bajeti. Lengo la kufanya hivi ni kwamba, Serikali inadhamiria kwa dhati kupambana na changamoto za kiuchumi na kijamii ambazo Watanzania wanakabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na ongezeko la bei za mafuta ya petroli, upungufu wa nishati ya umeme, upungufu wa chakula na upungufu wa ajira na hasa hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza pia katika hotuba yangu kwamba bajeti hii imezingatia vipaumbele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umeme, maji, miundombinu na usafirishaji na hasa reli, bandari, barabara, viwanja vya ndege, mkongo wa Taifa, kilimo na umwagiliaji na kupanua ajira kwa sekta ya umma. Ni dhamira ya Serikali kwamba kwa kushirikiana na sekta binafsi tutatumia rasilimali zote ikiwemo fedha na rasilimali watu ili kuhakikisha maeneo hayo ya kipaumbele yanatekelezwa ipasavyo ili kuwaletea wananchi maendeleo na kuondokana na hasa umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilihu makali ya bei za bidhaa na huduma. Vyanzo vikuu vya mfumuko wa bei ni pamoja na kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia, kupanda kwa mfumuko wa bei katika nchi tunazoshirikiana kibiashara (*imported inflation*), kutopatikana kwa umeme wa uhakika pamoja na upungufu wa chakula hapa nchini na nchi jirani. Katika mizania fahirisi ya bei, chakula na vinywaji baridi hubeba 47.8% ya fahirisi ya bei za bidhaa na huduma katika kapu la walaji, ikifuatiwa na usafirishaji 9.5% na nishati 9.2%. Hivyo, upungufu wa chakula unachangia kwa kiasi kikubwa katika kasi ya upandaji bei na kuongeza gharama za maisha kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti, nchi yetu inakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa umeme wa uhakika kutokana na kiwango kidogo cha uzalishaji usiokidhi mahitaji. Kukosekana kwa umeme wa uhakika kuna athari nyingi ikiwemo kushuka kwa uzalishaji na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji. Hali hiyo husababisha kupungua kwa bidhaa sokoni na hivyo kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma. Kupanda kwa mfumuko wa bei katika nchi ambazo tunashirikiana nazo katika

biashara husababisha bei nchini kupanda, pia kwa kuwa bidhaa tunazoagiza huathiriwa na mfumuko wa bei wa nchi ambako tunaagiza bidhaa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuongezeka kwa bei za mafuta ya petroli nako kunaongeza gherama za uzalishaji pale ambapo viwanda vyetu vinapolazimika kutumia mafuta ambayo ni ghali ikilinganishwa na nishati ya umeme utokanao na nguvu za maji, kuendesha mitambo yake na pia kuongezeka kwa gherama za usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo moja kwenda lingine na yote haya kwa pamoja husababisha kupanda kwa bei za bidhaa na huduma kwa walaji.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwa kina katika hotuba yangu ya bajeti hatua zitakazochukuliwa na Serikali kupunguza makali ya maisha kwa wananchi hususan kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa na huduma mbalimbali. Mionganoni mwa maeneo ya kimkakati yatakayozingatiwa kwa lengo la kupunguza mfumuko wa bei kama ilivyoanishwa katika hotuba ya hali ya uchumi na bajeti ni pamoja na yafuatayo:-

- (i) Kuongeza uzalishaji wa umeme;
- (ii) Kupanua na kuimarisha miundombinu;
- (iii)Kupunguza ongezeko la bei ya mafuta;
- (iv)Kusambaza na kuuza sehemu ya chakula kutoka katika hifadhi ya nafaka ya Taifa;
- (v) Kuongeza upatikanaji wa chakula kwa kuhimiza kilimo cha umwagiliaji;
- (vi)Kuimarisha hifadhi ya chakula kwa kuongeza ununuzi wa mazao ya chakula katika wakala wa hifadhi ya chakula; na
- (vii) Kuendelea kuimarisha miundombinu hususan ya barabara na reli.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu kushuka kwa thamani ya shilingi na kupanga bei kwa *dollars* za Kimarekani kwa bidhaa na huduma zitolewazo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kushuka kwa thamani ya shilingi; thamani ya shilingi ya Tanzania huamriwa katika soko huru na hivyo inatarajiwa kupanda na kushuka kulingana na nguvu za mahitaji na ugavi sokoni. Benki Kuu huingilia kati mabadiliko ya thamani ya shilingi yasiyo ya kawaida ambayo huwa ni ya muda mfupi na yanayobainika kuwa hayaendani na hali halisi ya kiuchumi. Endapo mabadiliko ya thamani ya shilingi yanatokana na sababu za kimsingi za uchumi (*economical fundamentals*), Benki Kuu haiwezi kuingilia kwani kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na nguvu halisi ya soko na tunaweza kumaliza hazina yote ya fedha za kigeni bila mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Spika, katika robo ya mwisho ya mwaka 2010 thamani ya shilingi ikilinganishwa na *dollar* ya Kimarekani iliimarika kutoka shilingi 1,483.80/= kwa *dollar*

tarehe 2 Novemba, 2010 na kufikia shilingi 1415.90/= kwa *dollar* tarehe 22 Desemba, 2010. Kuimarika huku kulitokana na mahitaji makubwa ya shilingi ambayo yalichangiwa na msimu wa mazao wa mwaka 2009/2010 kuwa mzuri. Kwa vile sababu za kuimarika kwa shilingi zilikuwa ni za msingi, thamani ya shilingi ilipungua tena baada ya msimu na kufika mwishoni mwa mwezi Januari 2011 ilikuwa imefikia sawa na ilivyokuwa Novemba, mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kutokea kipindi hicho thamani ya shilingi imekuwa ikipungua kidogo kidogo hadi kufikia sh. 1,518/=, mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu. Upunguaji huu ni wa kawaida ambao kwa kiwango kikubwa unatokana na tofauti ya mfumuko wa bei katika Tanzania na nchi tunazofanya nazo biashara. Hata hivyo, upunguaji wa thamani ya shilingi uliongezeka kwa kasi kutoka sh. 1,519.70/= tarehe 1 mwezi huu hadi kufikia shilingi 1,548.80/= tarehe 16 mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa *dollar* ni mionganini mwa sababu zilizochangia kupungua kwa thamani ya shilingi. Vile vile, kuimarika huko kumeathiri sarafu nyingine duniani. Kwa mfano, katika kipindi hicho thamani ya shilingi ikilinganishwa na *dollar* ilishuka kwa 1.7% na thamani ya Paundi ya Uingereza ililinganishwa na *dollar* ilishuka kwa kiwango hicho hicho cha 1.7%, wakati thamani ya shilingi ya Kenya ilishuka kwa 4.6% na *Euro* ilishuka kwa 1.2%.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya mikakati ya Kibenki ya kutumia hazina ya fedha za kigeni ili kupandisha thamani ya shilingi haiwezi kuwa endelevu na kufanya hivyo kunaweza kumaliza akiba ya fedha za kigeni bila kutatua tatizo kama iliviyowahi kutokea Uingereza mwaka 1992 na pia Nigeria na Uganda katika vipindi tofauti. Hata hivyo tatizo hili linatarajiwaa kumalizika uchumi wa dunia utakapoimariika hususan katika nchi za Ulaya. Vilevile Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza mfumuko wa bei na kuhimiza uzalishaji wa bidhaa na huduma tunazouza nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kupanda bei za bidhaa na huduma zitolewazo nchini kwa kutumia dola za Kimarekani, pamekuwepo dhana ya kuwa *dollarisation* inaweza kuwa moja ya sababu za kupungua kwa thamani ya shilingi. Kwanza ningependa ifahamike kwamba *dollarisation* hutokea tu pale ambapo thamani ya fedha yako inakuwa inaanguka. Kwa hiyo, *dollarisation* ni matokeo na sio sababu. Kama maelezo hayo hapo juu yanavyoainisha sababu kubwa ya kushuka kwa thamani ya shilingi hivi karibuni ni kuongezeka kwa thamani ya dola duniani na mahitaji makubwa ya dola kutohakana na kuongezeka kwa bei ya mafuta na sio *dollarisation*. Aidha, napenda ifahamike *dollarisation* ikiangaliwa kwa kipindi cha miaka mingi imekuwa aidha, ikishuka au tulivu

kwa ujumla. Kwa mfano, kiwango cha amana na dola katika ujazo wa fedha ambacho ndicho kipimo cha *dollarisation* kilikuwa takribani asilimia 32 mwaka 2002 ikapanda hadi asilimia 34 mwaka 2003 na kushuka taratibu hadi kufikia asilimia 27 mwezi Aprili, mwaka huu. Hii inaonyesha wazi kuwa hakuna ushahidi wa kuongezeka *dollarisation* kama inavyodhaniwa na hii ni kukua kwa thamani ya shilingi inaendelea kuwa tulivu kwa ujumla katika miaka ya hivi karibuni ikilinganishwa na miaka ya nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameongelea pia suala la wafanyabiashara na wenye mahoteli au nyumba za kupangisha wageni kuonyesha bei zao kwa dola. Kwanza napenda ifahamike kuwa tatizo hili linatoka pale ambapo wafanyabiashara wanakuwa na hisia kuwa thamani ya shilingi itashuka, hivyo hutaja bei hizo kwa dola ili kulinda biashara zao dhidi ya hasara inayoweza kutokana na kuanguka kwa shilingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kifungu namba 26 cha Sheria ya Benki Kuu sura ya 197 kinatoa mamlaka kwa Benki Kuu kutoa sarafu ya fedha ya Tanzania ambayo lazima ikubaliwe kwa malipo yote hapa nchini yaani *legal tender*. Hii ina maana kwamba ni kinyume cha sheria kwa mtu ye yeyote kukataa kupokea shilingi kama fedha ya malipo ya bidhaa au huduma inayotolewa hapa nchini. Kwa hivyo, mtu ye yeyote anayekukatalia kupokea shilingi ni vyema ama ukatoa taarifa polisi au ukatoa taarifa pale Hazina ili tumchukulie hatua. Serikali itaangalia upya sheria hii na sheria nyingine zinazohusiana ili tuweze kuchukua hatua muafaka ikibidi kubadilisha sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilihu su uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na kupungua kwa umaskini. Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia saba mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia sita mwaka 2009. Licha ya Serikali kufanikiwa kukuza uchumi kasi ya ongezeko na idadi ya watu ni kubwa ikilinganishwa na ongezeko la Pato la Taifa. Hali hii inaathiri juhudhi za Serikali kuwafikishia wananchi huduma za msingi kama vile maji, elimu na afya kwa sababu badala ya kutumia fedha za Bajeti kuboresha miundombinu ya kiuchumi fedha zinaelekezwa katika kupanua huduma za jamii kukidhi ongezeko la idadi ya watu kwa maana ya kutoa huduma za msingi wa jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa Pato la Taifa kuna maana ya kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika nchi. Aidha, pato hili huzalishwa na Watanzania wenyewe kuitia shughuli mbalimbali za kiuchumi wanazozifanya kwa mfano, katika kilimo, ujenzi, mawasiliano na huduma mbalimbali. Kadhalika ili ukuaji wa uchumi jumla uweze kupunguza umaskini ni muhimu sekta zinazokuwa haraka ziwe zile zinazoajiri watu wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo inategemewa na asilimia takriban 75 ya Watanzania ambao wanaishi vijiji kwa maana ya ajira na usalama wa chakula. Sekta hii imekuwa ikikua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia nne kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo. Sekta nyingine za kiuchumi kwa mfano sekta ya mawasiliano, ujenzi na uchukuzi japo zinakuwa kwa kasi, lakini mchango wake katika kupunguza umaskini wa kipato ni mdogo kwa vile sekta hizi zinaajiri sehemu ndogo tu kwa Watanzania wote.

Serikali inachukua hatua mbalimbali kuendeleza sekta ya kilimo ikiwemo viwanda vya kusindika mazao ya kilimo kwa lengo la kuongeza ajira na kipato cha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuboresha uzalishaji katika sekta ya kilimo ili kukuza kipato cha walio wengi, Serikali imeendelea kuwajengea wananchi mazingira mazuri na kuwahimiza kupanua wigo wa vipato vyao kwa kufanya shughuli nyingine za kiuchumi nje ya kilimo. Mikakati inayowekwa ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha mijini, kuvutia wawekezaji kwa kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuongeza fursa za ajira na kuwawezesha wananchi kiuchumi kuitia mifuko mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vyema tukafahamu kuwa umaskini haupimwi kwa kuangalia kipato tu bali pia umiliki wa mali na upatikanaji wa huduma za kijamii kama vile elimu, maji na afya ambazo Serikali imeendelea kuziboresha. Kodi na tozo kwenye mafuta zinachangia sana katika ongezeko la bei ya mafuta, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 niliyoisoma tarehe 8 Juni, 2011 kutokana na msukosuko wa uchumi duniani bei ya mafuta katika soko la dunia ilifikia dola za Kimarekani 147 mwezi Julai, 2007 na baadaye ikashuka hadi dola za Kimarekani 40 mwezi Februari, 2009.

Hata hivyo hadi tarehe 1 Juni, 2011 mwaka huu bei ya mafuta ilikuwa imepanda tena na kufikia dola za Kimarekani 116.25 kwa pipa. Ongezeko la bei limechangiwa na kuongezeka kwa gharama za bima ya mizigo kwa meli zinazoleta mizigo nchini kutokana na tishio la maharamia baharini, uagizaji wa mafuta wa kampuni moja moja na migogoro ya kisiasa katika nchi za Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine zinazochangia bei hiyo ya mafuta ni tozo na kodi mbalimbali ambazo zinatozwa kwenye bidhaa hizo za mafuta. Wakati bidhaa za petroli na dizeli hutozwa ushuru wa bidhaa (*excise duty*) na ushuru wa mafuta (*fuel levy*). Mafuta ya taa hutozwa ushuru wa bidhaa yaani *excise duty* peke yake. Pamoja na kodi hizo kuna tozo mbalimbali zinazotozwa na mamlaka zinazotoa huduma katika mfumo wa uagizaji na upokeaji wa mafuta na hivyo kuchangia katika kuongeza bei ya mafuta na makali ya maisha. Aidha, nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itachukua hatua za kupunguza bei ya mafuta kwa kurejea tozo mbalimbali zinazotozwa na mamlaka zinazotoa huduma katika mfumo wa wasindikizaji na upokeaji wa mafuta kwa nia ya kuzipunguza au kuzifuta kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hotuba yangu nimepokea ushauri kutoka kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na hoja kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi ambao walitoa maoni yao na kuishauri Serikali ichukue hatua ya kupunguza bei ya bidhaa za mafuta. Aidha, Kamati ya Fedha na Uchumi walishauri kwamba Serikali ichukue hatua za haraka za kuondoa tatizo la uchakachuaji wa mafuta kwa kulinganisha bei ya bidhaa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi na ushauri mlioutoa Wabunge 227 mliochangia na imeamua kuchukua hatua zifuatazo:-

Moja kufanya marekebisho kwenye viwango vyatayi ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za dizeli na mafuta ya taa na pili, kupunguza viwango vyatayi tozo mbalimbali zinazotozwa kwenye mafuta na mamlaka za udhibiti yaani *EWURA*, *SUMATRA*, *TBS*, *TBA*, *TRA* na *TIBA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunarekebisha ushuru katika mafuta aina ya dizeli kwa maana ya *excise duty*, tunapunguza *excise duty* kutoka shilingi 314 za sasa kwa lita hadi shilingi 256 kwa lita. Punguzo la karibu shilingi 100 kwa lita, ukiongeza punguzo la shilingi 225 kwa lita tulizopunguza kwenye tozo. Kwa hiyo, tunapunguza kodi na pia tumepunguza tozo. Hii ni kwa kufuata vigezo vyatayi bei elekezi ya *EWURA* inayotumika sasa. Hivyo punguzo katika aina ya mafuta ya dizeli itakuwa takribani shilingi 323.5 kwa lita. Kwa hiyo, hii haianzi leo wala haianzi kesho, tutaeleza kwamba *effective date* yake itakuwa lini. Kwa hiyo, wale wanaosikiliza wasianze kufanya maamuzi ambayo Serikali haijafanya. (*Makofi*)

Tozo kwenye mafuta aina ya dizeli, mafuta mazito na mafuta ya taa nako punguzo ni shilingi 224.50 kwa lita ili kuondoa ushawishi wa watu wasio waadilifu kuchanganya mafuta ya taa na dizeli ushuru wa mafuta ya taa utarekebishwa. Lengo ni kuondoa kichocheo cha kukwepa kodi. Tunaomba wenzetu wa *EWURA* watufanyie hesabu za kitaalamu ili Serikali iweze kujua kiasi gani tuweze kuweka ili uchakachuaaji uondoke kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kidogo unyeti wa ugumu uliopo katika kanuni inayotoa bei ya mafuta anayolipa mlaji. Tanzania kama waagizaji wa mafuta hatuna uwezo wa kupanga bei katika soko la dunia. Kwa kawaida bei ya pipa moja la dizeli huuzwa dola za Kimarekani 60 hadi 70, kama hakuna matatizo duniani. Lakini kama nilivyowaambia sasa hivi imefika karibu dola 131 kwa pipa. Lakini kufuatia migogoro katika nchi za Afrika Kaskazini na eneo la nchi za ghuba bei inapanda kila kukicha. Mfano wakati *EWURA* wakitoa bei elekezi wiki moja tu iliyopita bei ya pipa ilikuwa dola za Kimarekani 116 na bei ya pipa mpaka wanafunga soko jana ilikuwa dola za Kimarekani 131 ndani ya wiki moja mafuta duniani yamepanda bei kutoka dola 116 kwa pipa mpaka dola 131. Hii ina maana kwamba Serikali haina mamlaka ya bei katika soko la dunia.

Suala lingine linalotupa shida ni kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa ya dola ya Kimarekani inayotumika kuagizia mafuta. Kwa mfano, leo hii shilingi yetu imefikia kiwango cha shilingi 1,600 kwa dola moja ya Kimarekani. Hii nayo itachangia sana katika kupanda kwa bei ya mafuta. Hata hivyo mtakubaliana nami kwamba ukiacha maeneo ambayo hatuna kishawishi nayo marekebisho katika ushuru na tozo yataleta nafuu kwa mlaji na kuchangamsha uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua hizi pia zitakuwa na manufaa mengi kwa nchi yetu kama ifuatavyo:-

(a) Kuondoa tatizo la uchakachuaji wa mafuta ambalo limekuwa sugu sana kwa muda mrefu kutokana na tofauti kubwa ya viwango vya kodi pamoja na tozo zilizokuwa zinatozwa kwenye mafuta ya dizeli na mafuta ya taa. Aidha, hatua hizi zitasaidia kurejesha imani na ubora wa mafuta na kufufua biashara ya usafirishaji wa mafuta kati ya nchi yetu na nchi jirani na hasa nchi za Burundi, Rwanda, Uganda na *DRC*.

(b) Kuondoa tatizo la uharibifu mkubwa wa vyombo vya usafiri uliokuwa ukisababisha gharama kubwa kwa watumiaji na uchumi kwa ujumla.

(c) Kushuka kwa bei za mafuta ya petroli na dizeli kutapelekea kupunguza kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa mbalimbali na hivyo kupunguza gharama kwa mlaji.

(d) Serikali itaweza kupata mapato yanayostahili ambayo yamekuwa yakivuja kutokana na uchakachuaji wa mafuta ya dizeli na mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, hatua zote hizi kwa ujumla zitaondo vitendo vya kidhalimu vilivyokuwa vikikithiri na kuhujumu uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali imeagiza Mamlaka ya Udhibiti na Huduma za Nishati na Maji yaani *EWURA* kuchukua hatua mbalimbali ambazo pia zitachangia katika kupunguza zaidi bei za mafuta. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Ukokotoaji wa thamani ya shilingi kwa kuioanisha na dola ya Marekani yaani *exchange rate*;

(b) Kuondoa au kupunguza wigo wa asilimia 7.5 ambayo makampuni yaliruhusiwa kuwekwa ili kufidia baadhi ya gharama;

(c) Kupitia upya misingi ya ukokotoaji wa viwango vya tozo mbalimbali za Taasisi za Umma kwa lengo la kubakia na tozo stahili na kwa viwango stahili bila kuathiri majukumu ya udhibiti na usimamizi yanayofanywa na Taasisi hizo.

(d) Kupunguza tozo za Kampuni za mafuta ikiwa ni pamoja na gharama za Kibenki yaani *financing charges*. Upotevu wa mafuta yanayosafirishwa kwenye meli na gharama ya ukaguzi yaani *inspection fees*.

(e) Kuharakisha utekelezaji wa mpango wa uagizaji wa mafuta wa pamoja yaani *Petroleum Bulky Procurement System*.

Mheshimiwa Spika, nataka nilijulishe Bunge lako Tukufu kwamba Kanuni za *Bulky Purchase* zimeshakamilika, zimeshapelekwa kwa Mchapaji Mkuu na zitatoka kwenye gazeti wakati wowote kati ya wiki hii na wiki ijayo. Baada ya kutoka kazi hii itaanza mara moja kwa kufuata taratibu za manunuzi. Hata hivyo hatua zote hizo za kupunguza bei za mafuta zitachukuliwa kwa tahadhari ili zimpatie mtumiaji bidhaa zenye

ubora na ujazo stahiki na pia zisiathiri au kudhoofisha udhibiti wa biashara ya mafuta na mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) kuharakisha utekelezaji wa mikakati itakayowezesha upatikanaji wa kutosha wa nishati mbadala wa gesi kwa nia ya kutosheleza mahitaji na matumizi kwenye magari na viwandani. Hata hii pia itachangia katika kupunguza gharama za maisha kwa kuwa nishati hii itapatikana hapa nchini na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 upatikanaji wa umeme wa uhakika umepewa kipaumbele cha kwanza. Mikakati mbalimbali ya uendelezaji wa matumizi ya gesi asili itatekelezwa ili kufanikisha azma ya Serikali ya upatikanaji wa gesi asili yenye uhakika. Aidha, Serikali imeliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli kuharakisha utekelezaji wa mikakati hiyo. Hatua hizi zitapunguza utegemezi katika mafuta na kuwezesha kupunguza gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhimiliyu wa deni la Taifa, katika kutekeleza mkakati wa deni la Taifa (*National Debt Strategy*) Serikali iliendelea kusimamia kwa umakini Deni la Taifa kwa kukopa zaidi kutoka vyanzo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuchambua kwa makini athari zinazotokana na mikopo mipya. Kwa mujibu wa tathmini ya uhamilivu wa deni iliyofanyika mwaka 2010 inaonyesha kuwa Deni la Taifa ni himilivu. Aidha, kwa mujibu wa viashiria vya uhimiliyu kwa deni vilivyopangwa na kukubalika Kimataifa deni letu linaonyesha kuwa linahimilika kwa kuwa viashiria vyote vya deni vipo chini ya ukomo. (*Makofi*)

Kwa mfano, kiashiria cha uwiano wa Deni la Taifa kwa thamani ya sasa (*present value*) kwa Pato la Taifa ni asilimia 14.6 ambapo kiwango cha ukomo cha deni kuwa himilivu ni asilimia 50. Kwa deni lote tulilonalo halijafika hata nusu ya uhimiliyu wa deni kwa Tanzania. Kwa maana nyingine ni kuwa tunakopesheka kwa kuzingatia uwezo wetu wa kulipa na kufuata Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura ya 134 na kanuni zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukopa kwa ajili ya kuwekeza katika miradi ya miundombinu inayochochea ukuaji wa uchumi wa Taifa pamoja na kutoa fursa ya kuwa lango kuu la usafirishaji kwa nchi yetu. Pamoja na kwamba deni linahimilika Serikali yenu itahakikisha kwamba tunakuwa waangalifu kwa kukopa. Hatutakopa tu itufikie kiwango cha ukomo, tutakopa kufuatana na mahitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja iliyofuatia ilikuwa Bajeti iliyowasilishwa Bungeni ya shillingi trilioni 13.5 ni tofauti na programu ya chini ya *IMF*.

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la kuandaa Bajeti ya Serikali ni la Serikali yenye. Napenda kueleza kwamba wakati wa maandalizi ya Bajeti wadau mbalimbali huushishwa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu na washirika mbalimbali wa maendeleo zikiwemo ASIZE na AZAKI. Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*), hushirikishwa kama wadau wa maendeleo chini ya Mpango wa *Policy*

*Support Instrument* yaani *PSI*. Katika utaratibu huu, *IMF* hushirikishiana na wataalam wa Serikali kufanya tathimini ya mwenendo wa viashiria mbalimbali vyta kiuchumi na Bajeti na kisha kuandaa makadirio ya awali ya Bajeti ya mwaka unaofuata. Makadirio haya huendelea kuboreshwa kulingana na upatikanaji wa takwimu na taarifa nyingine muhimu. Hivyo mapendekezo ya mapato na matumizi yanayowasilishwa na hatimaye kupitishwa na Bunge yanazingatia mapendekezo ya *IMF* pamoja na maelekezo mbalimbali ya Serikali.

Kwa msingi huo Mfumo wa Bajeti uliwasilishwa Bungeni, umejumuisha maboresho ya mfumo wa awali ambao Serikali ultumia katika kujadiliana na wadau mbalimbali ikiwemo *IMF*. Kwa kifupi Bajeti huandaliwa na Serikali na huidhinishwa na Bunge. Wengine wote ni washauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mikopo kupitia dirisha la kilimo. Dirisha la kilimo linatoa mikopo kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa katika muongozo ulioidhinishwa na Serikali. Vigezo hivyo vimewekwa ili kuweza kuwafikia wakulima wengi kadri inavyowezekana. Kwa kuzingatia vigezo na taratibu zilizowekwa hadi tarehe 15 mwezi wa sita dirisha la kilimo limeidhinisha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 17.89 kati ya shilingi bilioni 21.6 zilizotolewa na Serikali. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 14.13 ni mikopo kwa taasisi zinazowakopesha au kuwanufaisha wakulima wadogo wadogo. Kiasi hiki ni asilimia 79 ya mikopo yote iliyoihdinishwa. Hivi sasa dirisha hilo limeongezewa shilingi bilioni 20 na maombi ya mikopo yenye thamani shilingi bilioni 12.4 yamo mbioni kuidhinishwa, utoaji mikopo utaendelea kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, riba ya mikopo ya dirisha la kilimo imewekwa kwa mujibu wa muongozo wa mikopo ya kilimo iliyoolewa na Serikali. Kufuatana na muongozo huo wakopaji wa moja kwa moja wanatozwa asilimia tano wakati wale wanaopitia *SACCOS* wanatozwa asilimia nane na *SACCOS* inalipa asilimia nne ikilinganishwa na asilimia kumi na sita hadi ishirini na nne zinazotozwa na taasisi mbalimbali. Hivyo kupunguza riba zaidi ya hapo kutazorotesha uendelevu wa dirisha hilo kwani hata sasa riba iko chini ya kiwango cha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, *TIB* imeendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua ofisi za Kanda, Arusha na Mwanza na hivi karibuni ofisi nyingine ya kanda itafunguliwa Jijini Mbeya. Tayari jengo la Ofisi ya Mbeya limepatikana na maandalizi ya kufungua tawi hilo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mikopo wa dirisha la kilimo hautofautiani na ule wa Benki za biashara. Lengo la kuunda dirisha la kilimo ndani ya *TIB* ni kuhakikisha kuwa mikopo inatolewa na inazingatia hali halisi ya kilimo chetu na kulegeza masharti ya mikopo ikilinganishwa na masharti yanayotolewa na Benki za Biashara kama ifuatavyo; riba ya mikopo imepunguzwa kutoka kama nilivyosema asilimia kumi na sita hadi asilimia tano kwa makampuni na kutoka kwa asilimia ishirini nne hadi asilimia nane kwa wakopaji wadogo wadogo. Wigo wa dhamana za mikopo umepanuliwa na kuruhusu hatimiliki za kimila, mali zinazohamishika, bima na kadhalika.

Pia ukokotoaji wa thamani ya dhamana umerahisishwa kwa manufaa ya wakopaji, mtaji au mchango wa mkopaji kwenye mradi unatakiwa uwe angalau asilimia thelathini wa gharama zote ikijumuishwa na gharama za ardhi, mashine na kadhalika, tofauti na masharti ya kibashara ambapo mkopaji hutakiwa kuchangia asilimia arobaini hadi asilimia hamsini wa gharama zote. Tofauti na Benki za Biashara ambazo zinatoa mikopo kwa muda usiozidi wastani wa miaka mitatu, dirisha la kilimo la *TIB* linaweza kutoa mkopo wa muda mrefu hadi kufikia miaka 15. Kwa hiyo, kama Waheshimiwa Wabunge tulikuwa hatuzifahamu hizi tunaweza kuwaambia *TIB* Menejimenti ikaleta nakala ili Waheshimiwa Wabunge mjue, ni Benki inayomsaidia mwananchi. Si sawa sawa na Benki za Kibashara. (*Makofi*)

Mhesimiwa Spika, nawashauri Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwasiliana na *TIB* ili kupata maelezo ya kina kuhusu utaratibu wa kukopa kutoka dirisha la kilimo pamoja na masharti yake. Lakini kama nilivyosema naahidi kwamba nitamwomba Mkurugenzi Mtendaji wa *TIB* alete lile *pamphlet* ili Waheshimiwa Wabunge waweze kujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na dirisha la kilimo kwenye *TIB*, maandalizi ya kuunda Benki ya Kilimo yapo njiani yamefikia mbali na yanasmamiwa na Benki Kuu. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia tu kwamba si kwamba tumelala, maandalizi yapo na sasa hivi tumeshatenga shilingi bilioni 50 zipo Benki Kuu ili maandalizi yakikamilika tu, Benki inaanza na zile shilingi bilioni 50 halafu zingine zitaendelea kupelekwa kwa kadri itakavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufuta au kurekebisha posho mbalimbali, hii ni hoja ambayo ilikuwa na joto kidogo Bungeni na kwa bahati nzuri ilichangamkiwa mno na waandishi wa habari. Nilimsikiliza kwa makini Mheshimiwa Freeman Mboge asubuhi wakati anachangia hoja ya posho. Uamuzi wa kufuta au kurekebisha posho mbalimbali umetolewa na Serikali yenye kama nilivyoeleza katika hotuba yangu niliyoitoa tarehe 8 Juni, 2011 wakati nawasilisha Bajeti ya Serikali. Aidha, mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012 aya namba 63 ukurasa wa 50 hadi ukurasa wa 54. Nilieleza kwa kirefu hatua mbalimbali za kudhibiti matumizi ya Serikali ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo:-

Moja, kupunguza malipo ya posho mbalimbali zisizokuwa na tija. Uweke mstari pale zisizokuwa na tija. Pili, kupunguza safari za ndani na nje ya nchi ambazo hazina tija. *U-underline* hiyo, hazina tija na tatu, kupunguza uendeshaji wa semina na warsha isipokuwa pale inapobidi lakini hata kama ikibidi kwa kibali maalum cha Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati iliyojiwekea katika kudhibiti matumizi yake na itakapobidi kufuta yale ambayo hayana tija. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Kamati ya Fedha na Uchumi waliochangia hoja hii. Nawashukuru sana kwa michango yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili la posho inaelekea limekuzwa isivyo kawaida na pengine kutokana na kutumia takwimu zisizosahihi katika kulijengea hoja. Labda maelezo yafuatayo huenda yakasaidia kubainisha ukweli wa suala hili. Posho zote yaani *personnel allowances* kwa ujumla wake katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zinafikia shilingi bilioni 352.75 na si zaidi ya shilingi bilioni 980. (*Makofi*)

Kati ya posho hizo *sitting allowance* kwa nchi nzima ni shilingi bilioni 25.68 tu na kati yake ni *sitting allowance* za Waheshimiwa Wabunge zilizokasimiwa katika Fungu 42 yaani Fungu la Bunge ni shilingi bilioni 4.92 tu. Kwa hesabu hizo Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuona na kupima tija itakayopatikana katika kuzifuta *sitting allowance* hizo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, endapo Waheshimiwa Wabunge wataamua kufuta *sitting allowance* zao fedha zitakazookolewa ni shilingi bilioni 4.92 tu na kama zitafutwa kwa Serikali nzima fedha zitakazookolewa ni shilingi bilioni 25.86. Posho zingine zote zina utaratibu maalum kwani aidha, ni za kisheria, huwezi kufuta posho ya Jaji ya kununua Joho, Majaji wote wana Majoho ambayo yananunuliwa na Serikali. Sasa huwezi ukakaa hapa mkatungatunga Sheria kwamba kuanzia kesho tuzifute. (*Makofi*)

Huwezi kufuta posho za madaktari na hasa madaktari bingwa, wanajeshi ambao wana sheria maalum iliyotungwa na Bunge hili na ile Sheria imetamkwa rasmi Jenerali aliystaafu anapata nini. Hafanyi kazi lakini anapata mshahara kufuatana na ile Sheria yake. Jaji Mkuu Augastino Ramadhani amestaafu lakini anapata vitu fulani kufuatana na Sheria iliyomteua yeye mpaka kufa kwake, zile hazifutiki. (*Makofi*)

Kwa hiyo, posho ambazo zinawenza kufutwa ni hizi tu tunazopata sisi hapa Wabunge, *sitting allowance* ama tuseme hizo nyingine, lakini nyingine zote zile haziwezi kufutwa kwa sababu zina Sheria zake. Majenerali wale wamefanya kazi chungu mzima pale, leo ukamwambie Jeneral Mayunga kuanzia leo ile posho yako unayopata kama Jenerali Mstaafu haipo. Hapatoshi! Hapatatosha humu Bungeni, umwendee Jenerali Mboma umwambie kuanzia kesho posho yako wewe kama Jenerali uliyestaafu, asilimia hii ya mshahara na kitu gani zimefutwa. Hapatoshi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi wa takwimu za Bajeti za sekta ya nishati na madini. Napenda kutoa ufanuzi wa takwimu za Bajeti za sekta ya nishati za madini ambazo ziko kwenye vitabu vya Bajeti kama ifuatavyo:-

Fungu la 58 - Wizara ya Nishati na Madini kuna Bajeti ya shilingi bilioni 402.402 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 325.448 ni fedha za maendeleo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukimsikiliza Mheshimiwa Waziri itakuwa vizuri, si mahala penu pa kuongea kila mtu anataka kuongea. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 79.9 ni za matumizi ya kawaida. Fungu 50 – Wizara ya Fedha kuna shilingi bilioni 136.867 za miradi ya sekta ya nishati inayoteklezwa kupitiwa mipango ya miradi ya MCC. Wale ambao wanasesma

Mkulo amekokotoa na kuliogopea Bunge wakaangalie Kitabu cha Miradi ya Maendeleo, *Vote - 50* ukurasa wa 91 watakuta *sub-vote* hizi 3142 una shilingi 39,265,895,000/=, *sub-vote* 3143 shilingi 11,415,461,000/=, *sub-vote* 3144 shilingi 86,185,665,000/= ukijumlisha hizo kwenye hesabu za kawada kabisa unapata shilingi 136,866,024,000/= au takribani shilingi 136,867,000,000/= ukizijumlisha hizi na ile bilioni 402.4 ndiyo unapata bilioni 536.9. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vitabu vile nimeviandika mie na mie ndiyo najua jikoni, mwezangu wewe ambaye hukoviandika tatizo lako nini? Kwa hiyo, hatukuongopa pale *figure* zote zipo kwenye vile vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufunguliwa kwa akaunti ya pamoja, Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa taarifa kadhaa na imetoa mapendekezo ikiwemo taarifa juu ya mapendekezo ya Tume kuhusu vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano ya mwaka 2006. Taarifa hii iliwasilishwa Wizara ya Fedha ya Serikali ya Muungano ya Tanzania na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Wizara hizi zilititia mapendekezo hayo kwa kujadiliana na Tume kwa maeneo yaliyohitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hizo, Wizara hizo kila upande wa Muungano ziliandaa taarifa kuitia nyaraka za Baraza na kuziwasilisha katika ngazi mbalimbali za maamuzi. Kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifikishwa hadi Baraza la Mapinduzi na kwa upande wa Serikali ya Muungano wa Tanzania ilifikishwa hadi Baraza la Mawaziri mwaka 2010. Katika Baraza la Mawaziri la Serikali ya Muungano wa Tanzania maelekezo yaliyotolewa kwa Tume ya Pamoja ya Fedha kufanya mapitio taarifa hiyo kwa lengo la kuiboresha na kuwasilisha tena Wizara ya Fedha ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila upande wa Muungano unaendelea kufanya uchambuzi wa mapendekezo ya Tume na utawasilisha maoni yake katika vikao vya juu. Aidha, suala la kufungua akaunti ya pamoja inategemea kukubaliwa na kuitishwa kwa mapendekezo ya Tume juu ya vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Hilo ni muhimu kwa sababu katika akaunti ya pamoja ndipo ambako yataingizwa mapato yote kutoka vyanzo vya Muungano kama vilivyobainishwa katika mapendekezo ya Tume.

Kwa hiyo, huwezi kufungua akaunti wakati hamjakubaliana hata misingi ya kugawana mapato na kuchangia matumizi. Kwa upande wa Serikali ya Muungano, Waraka wa Baraza la Mawaziri umeshaandalialiwa na wakati wowote utawasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri utazungumzwa na kwa hiyo, hatua zihusikazo na vikao vinavyohusika na kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi ni imani yangu haitachukua muda mrefu kabla ya hili suala halijamalizwa.

Mheshimiwa Spika, kupunguza misamaha ya kodi ili isizidi asilimia moja ya Pato la Taifa. Serikali inatoa misamaha ya kodi kuitia Sheria za Kodi na zisizo za kodi kwa lengo la kutoa vivutio vya uwekezaji au unafuu wa kodi kwa wawekezaji na makundi ya

watu kwa nia ya kutekeleza sera mbalimbali za Taifa. Ni kweli kuwa misamaha ya kodi inapunguza mapato ya Serikali lakini imekuwa ikitolewa kwa nia njema ya kukuza uchumi na kuboresha huduma za jamii. Hata hivyo imebainika kuwa misamaha hiyo wakati mwagine hutumika vibaya na hivyo kutoleta matokeo yaliyokusudiwa. Serikali imeendelea kupitia baadhi ya misamaha ili kuangalia kama bado inahitajika. Hatua zilizochukuliwa na Serikali zimeanza kuzaa matunda kwa kupunguza misamaha kutoka asilimia 4.2 ya Pato la Taifa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 hadi kufikia asilimia 2.5 ya Pato la Taifa kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012. Aidha, hotuba ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 imetoa mapendekezo ya kuondoa misamaha zaidi. Vilevile Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia Mfuko wa Dhamana wa Ushauri wa Sera na Usimamizi wa Kodi ulioanzishwa na Shirika la Fedha la Kimataifa utafanyiwa uchambuzi wa kina wa kuangalia misamaha ya kodi na kuleta mapendekezo ya kuondoa misamaha yote ambayo itaonekana kutokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, kupunguza kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani kutoka asilimia kumi na nane hadi asilimia kumi na tano ili zifanane na nchi nyingine za Afrika Mashariki. Napenda kufafanua kuwa kwa sasa hakuna nchi ya Afrika Mashariki yoyote yenye kiwango cha asilimia 15, nchi za Burundi, Rwanda na Uganda zinatoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 18 kama ilivyo Tanzania. Kenya pekee ndiyo yenye kiwango cha chini cha asilimia 16. Aidha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea na hatua za kuvianisha viwango vya kodi vya ndani ikiwemo Kodi ya Ongezeko la Thamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi mabaya ya fedha za Serikali kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ni kweli kwamba taarifa ya Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyotolewa mwezi Machi mwaka huu, imeonesha kutetereka kwa nidhamu na usimamizi wa fedha za umma. Sababu za kutetereka huko zimeelezwa katika hotuba ya Bajeti niliyowasilisha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeendelea kuzingatia na kutekeleza ushauri unaotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kuimarisha nidhamu na usimamizi wa fedha za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua ambazo Serikali imekuwa ikizichukua ni pamoja na kuhakikisha kwamba Watumishi wa kada za uhasibu na ugavi wanapata mafunzo ya muda mfupi na mrefu, kuajiri watumishi wenyе sifa wa kada za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ugavi, kufunga hesabu kwa kutumia utaratibu wa *IPSAS*, kufanya malipo kwa kutumia mtandao wa kibenki na kuhakikisha matumizi ya fedha yanatumia mfumo wa *IFMIs* kwenye Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inatekeleza programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma ambayo mafanikio yake yameongeza uwezo katika usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na udhaifu ulioelezwa kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa ujumla usimamizi wa fedha umeimarika ukilinganishwa na miaka ya nyuma, hali hii inadhihirishwa na ongezeko la hati safi za

ukaguzi kutoka asilimia 57 mwaka 2005/2006 hadi kufikia asilimia 77 mwaka 2009/2010 kwa Wizara, Mikoa na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuongeza juhudhi za kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa kuchukua hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Fungu 21 yaani Hazina kuwa imetengewa fedha nyingi imejitokeza wakati wa majadiliano ya Bajeti kwenye Kamati za Bunge za Kisekta na hapa Bungeni. Hivyo napenda kufafanua kuwa Fungu hili ambalo ni Hazina yenyewe, linakasimiwa fedha za kutekeleza majukumu ya Serikali kwa ujumla na siyo majukumu ya Kiwizara tu. Katika mwaka 2011/2012 Fungu hili limetengewa shilingi trilioni moja na hamsini na saba nukta nne bilioni, sawa na asilimia nane ya Bajeti yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge waelewe kuwa kati ya kiasi hicho shilingi bilioni mia tisa na sitini na moja nukta moja ni kwa ajili ya majukumu ya Kitaifa, majukumu hayo ni pamoja na nyongeza za mishahara ya watumishi wa umma ambao niliahidi hapa, ajira mpya za watumishi wa umma, upandishwaji vyeo, michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, dharura ya Serikali, mfuko wa maendeleo ya Jimbo, matumizi ya uendeshaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, maandalizi ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, mchakato wa Katiba mpya, michango ya Serikali kwenye Jumuiya za Kikanda na Mashirika ya Kimataifa na uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala hususani Mikoa, Wilaya na Halmashauri mpya ambazo mchakato wake haujakamilika, hili nilieleza kwa kirefu sana na Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hazina akaunti maalum ndiyo maana zinawekwa kwenye akaunti hii, kwa hiyo, ningependa niwashawishi kwamba zile fedha siyo kwamba zipo pale kuchezewa tu hapana, zina kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naona muda unaniendea kombo, baada ya kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, naamini kuwa Bunge lako Tukufu limepata fursa ya kuelewa undani wa masuala mengi yaliyoulizwa. Aidha, baadhi ya hoja zilizohusu utekelezaji wa masuala ya kisekta zitaendelea kufafanuliwa na Wizara husika wakati wa kuwasilisha Bajeti zao za mwaka 2011/2012. Hoja zote za Wizara zingine tutawakabidhi Mawaziri husika ili watakaposilisha hoja zao waweze kujibu na kwa zile ambazo ni za kisekta siyo kwamba sikuzijibu kwa makusudi, tumeona kwamba ni vema zikajibiwa na Mawaziri husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikiwasilisha hotuba ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 pamoja na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka ujao wa fedha unalenga kumpunguzia makali ya maisha mwananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kutekeleza vipaumbele nilivyovitaja. Hali hii inatoa changamoto kwa kila mdau kujipanga vizuri zaidi ili kushiriki kikamilifu kulingana na nafasi yake katika kufanikisha azma hii nzuri ya Serikali. Hivyo napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kumtaka kila mmoja wetu kutambua fursa zilizopo na kushiriki kikamilifu katika shughuli halali za

uzalishaji mali na utoaji huduma ili kufikia malengo yote tuliojiwekea katika Bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hoja hii, napenda kuwashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake ambao wanaendelea kunipa ushirikiano mzuri wa kutekeleza majukumu yangu kikamilifu. (*Makofi*)

Nachukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu Ndugu Ramadhani Khijjah na Manaibu Katibu Wakuu Laston Msongole, Dkt. Servacius Likwelile na Elizabeth Nyambibo pamoja na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Philip Mpango. (*Makofi*)

Kadhalika napenda kuwashukuru Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Profesa Benno Ndulu, Kamishana Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndugu Harry Kitillya na Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa Dkt. Albina Chuwa, kwa ushirikiano mkubwa walionipatia wakati wote wa uandaaji wa majibu haya ya hoja mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna wakati tulikuwa tunaagana saa saba usiku ndugu zangu nadhani matunda yake ndiyo mnayaona haya, nawashukuru sana. Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha ambao wameshiriki katika uandaaji wa majibu ya hoja mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila mwanaume anayefanikiwa yuko mwanamke karibu yake, napenda kurudia kumshukuru mke wangu Halda kwa uvumilivu wake na kwa kunilea na kunipa afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imeungwa mkono, kwa hiyo, utaratibu wa hoja hii tunapiga kura za Ndiyo au Hapana. Kwa hiyo, mseme hapana ndivyo tulivyokubaliana. Naagiza kengele ipigwe.

(*Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waliopo nje ya Ukumbi waingie ndani ya Ukumbi wa Bunge kupiga kura*)

(*Hapa upigaji kura ulianza kwa kuita majina ya Wabunge*)

**SPIKA:** Napenda tukiwa tunapiga kura watu wasiwe wanatoka nje na baadaye anafika anasema mimi sikupiga kura. Waheshimiwa tunaanza kupiga kura. Katibu. Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda - Ndiyo

**SPIKA:** Makofi ya shida gani ninyi pigeni kura tu.

*(Hapa Katibu aliendelea kuita majina)*

Mhe. Samuel John Sitta	-	Ndiyo
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu	-	Hayupo
Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli	-	Hayupo
Mhe. Prof. Mark James Mwandomsya	-	Hayupo
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi	-	Hayupo
Mhe. Stephen Masatu Wasira	-	Ndiyo
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa	-	Ndiyo
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia	-	Ndiyo
Mhe. Sophia Mattayo Simba	-	Ndiyo
Mhe. Bernard Kamilius Membe	-	Hayupo
Mhe. Mathias Meinrad Chikawe	-	Ndiyo
Mhe. Mustafa Haidi Mkulo	-	Ndiyo
Mhe. William Mganga Ngeleja	-	Ndiyo
Mhe. George Huruma Mkuchika	-	Ndiyo
Mhe. Celina Ompeshi Kombani	-	Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Emmanuel John Nchimbi	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Cyril August Chami	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. David Mathayo David	-	Ndiyo
Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka	-	Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magoloye Maige	-	Hayupo
Mhe. Samia Hassan Suluhu	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Terezya Pius Luoga Huvisa	-	Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa	-	Ndiyo
Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka	-	Hayupo
Mhe. Omari Rashid Nundu	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda	-	Ndiyo
Mhe. Jaji Frederick Mwita Werema	-	Ndiyo
Mhe. Job Yustino Ndugai	-	Hayupo
Mhe. Dkt. Milton Makongoro Mahanga	-	Ndiyo
Mhe. Eng. Christopher Kajoro Chiza	-	Ndiyo
Mhe. Balozi Khamis Juma Suedi Kagasheki	-	Hayupo
Mhe. Dkt. Lucy Sawere Nkya	-	Ndiyo
Mhe. Adam Kighoma Malima	-	Ndiyo
Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Harrison George Mwakyembe	-	Ndiyo
Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu	-	Ndiyo
Mhe. Benedict Ngalamu Ole-Nangoro	-	Ndiyo
Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa	-	Ndiyo
Mhe. Gregory George Teu	-	Ndiyo
Mhe. Pereira Ame Silima	-	Ndiyo

Mhe. Mahadhi Juma Maalim	-	Ndiyo
Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga	-	Ndiyo
Mhe. Goodluck Joseph Ole-Medeye	-	Ndiyo
Mhe. Athumanzi Rashid Mfutakamba	-	Ndiyo
Mhe. Philipo Augustino Mulugo	-	Ndiyo
Mhe. Ummy Ally Mwalimu	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Fenella Ephraim Mukangara	-	Hayupo
Mhe. Dkt. Abdulla Juma Abdulla Saadalla	-	Ndiyo
Mhe. <i>Eng.</i> Gerson Hosea Lwenge	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Abdallah Omar Kigoda	-	Ndiyo
Mhe. John Momose Cheyo	-	Hayupo
Mhe. Dkt. Augustino Lyatonga Mrema	-	Hapana
Mhe. Kabwe Zubeir Zitto	-	Hapana
Mhe. George Boniface Simbachawene	-	Ndiyo
Mhe. Edward Ngoyai Lowassa	-	Hayupo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta	-	Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama	-	Ndiyo
Mhe. James Daudi Lembeli	-	Hayupo
Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa	-	Ndiyo
Mhe. January Yusuf Makamba	-	Ndiyo
Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa	-	Ndiyo
Mhe. Peter Joseph Serukamba	-	Ndiyo
Mhe. Pindi Hazara Chana	-	Ndiyo
Mhe. Brig. Gen. Hassan Athumanzi Ngwilizi	-	Ndiyo
Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o	-	Ndiyo
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowa	-	Hapana
Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu	-	Hapana
Mhe. Raya Ibrahim Khamis	-	Hapana
Mhe. Esther Nicholus Matiko	-	Hapana
Mhe. Said Amour Arfi	-	Hayupo
Mhe. Mch. Israel Yohana Natse	-	Hapana
Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo	-	Hapana
Mhe. Pauline Philipo Gekul	-	Hapana
Mhe. Leticia Mageni Nyerere	-	Hapana
Mhe. Godbless Jonathan Lema	-	Hapana
Mhe. Ezekia Dibogo Wenje	-	Hapana
Mhe. Joseph Roman Selesini	-	Hapana
Mhe. Sylvester Mhoja Kasulumbayi	-	Hapana
Mhe. Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi	-	Hapana
Mhe. Halima James Mdee	-	Hapana
Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa	-	Hapana
Mhe. John John Mnyika	-	Hapana
Mhe. Salvatory Naluyaga Machemli	-	Hapana
Mhe. Mhonga Said Ruhwanya	-	Hapana
Mhe. Lucy Philemon Owenya	-	Hapana
Mhe. Christowaja Gerson Mtinda	-	Hapana

Mhe. Antony Gervase Mbassa	-	Hapana
Mhe. Regia Estelatus Mtema	-	Hapana
Mhe. Naomi Amy Mwakyoma Kaihula	-	Hapana
Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi	-	Hapana
Mhe. Mustapha Boay Akunaay	-	Hapana
Mhe. Meshack Jeremiah Opulkwa	-	Hayupo
Mhe. Highness Samson Kiwia	-	Hapana
Mhe. David Ernest Silinde	-	Hapana
Mhe. Vincent Josephat Nyerere	-	Hapana
Mhe. Christina Lissu Mughwai	-	Hapana
Mhe. Mwanamrisho Taratibu Abama	-	Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah	-	Ndiyo
Mhe. Anna Margareth Abdallah	-	Ndiyo
Mhe. Rashid Ali Abdallah	-	Hapana
Mhe. Munde Tambwe Abdallah	-	Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeid	-	Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood	-	Ndiyo
Mhe. Chiku Aflah Abwao	-	Hayupo
Mhe. Khalfan Hilaly Aeshi	-	Ndiyo
Mhe. Rukia Kassim Ahmed	-	Hapana
Mhe. Lameck Okambo Airo	-	Ndiyo
Mhe. Abdalla Haji Ali	-	Hapana
Mhe. Juma Othman Ali	-	Ndiyo
Mhe. Mbarouk Salim Ali	-	Hapana
Mhe. Sara Msafiri Ally	-	Ndiyo
Mhe. Hussein Nassor Amar	-	Ndiyo
Mhe. Kheri Khatib Ameir	-	Ndiyo
Mhe. Abdallah Sharia Ameir	-	Ndiyo
Mhe. Abdulsalaam Selemani Amer	-	Ndiyo
Mhe. Amina Abdallah Amour	-	Hapana
Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Ndiyo
Mhe. Rostam Abdulrasul Aziz	-	Hayupo
Mhe. Iddi Mohamed Azzan	-	Ndiyo
Mhe. Mussa Zungu Azzan	-	Hayupo
Mhe. Omary Ahmad Badwel	-	Ndiyo
Mhe. Faida Mohamed Bakar	-	Hayupo
Mhe. Salum Khalfan Barwany	-	Hapana
Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga	-	Ndiyo
Mhe. Gosbert Begumisa Blandes	-	Ndiyo
Mhe. Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba	-	Ndiyo
Mhe. Ester Amos Bulaya	-	Ndiyo
Mhe. Selemani Said Bungara	-	Hapana
Mhe. Felister Aloyce Bura	-	Ndiyo
Mhe. Agripina Zaituni Buyogera	-	Hapana
Mhe. Saidi Ramadhani Bwanamdogo	-	Ndiyo
Mhe. Jerome Dismas Bwanausui	-	Ndiyo

Mhe. Josephine Tabitha Chagulla	-	Ndiyo
Mhe. Kisyeri Werema Chambiri	-	- Ndiyo
Mhe. Mary Pius Chatanda	-	Ndiyo
Mhe. Andrew John Chenge	-	Ndiyo
Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje	-	- Ndiyo
Mhe. Capt. John Zefania Chiligati	-	Ndiyo
Mhe. Diana Mkumbo Chilolo	-	- Ndiyo
Mhe. Muhammad Amour Chomboh	-	- Ndiyo
Mhe. Amina Andrew Clement	-	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Maua Abeid Daftari	-	- Ndiyo
Mhe. Mohamed Gulam Dewji	-	- Ndiyo
Mhe. Deo Haule Filikunjombe	-	- Ndiyo
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke	-	- Ndiyo
Mhe. Ali Juma Haji	-	Ndiyo
Mhe. Khatib Said Haji	-	- Ndiyo
Mhe. Zahra Ali Hamad	-	- Hapana
Mhe. Hamad Ali Hamad	-	Hapana
Mhe. Azza Hillal Hamad	-	- Ndiyo
Mhe. Asaa Othman Hamad	-	Hapana
Mhe. Neema Mgaya Hamid	-	Ndiyo
Mhe. Shawana Bukheti Hassan	-	- Ndiyo
Mhe. Maria Ibeshi Hewa	-	Ndiyo
Mhe. Mansoor Shanif Hiran	-	Ndiyo
Mhe. Agness Elias Hokororo	-	Ndiyo
Mhe. Balozi Seif Ali Idd	-	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Christina Gabriel Ishengoma	-	- Ndiyo
Mhe. Yahya Kassim Issa	-	- Ndiyo
Mhe. Waride Bakari Jabu	-	Ndiyo
Mhe. Jaddy Simai Jaddy	-	Ndiyo
Mhe. Selemani Saidi Jafo	-	Ndiyo
Mhe. Asha Mshimba Jecha	-	Ndiyo
Mhe. Juma Sururu Juma	-	Ndiyo
Mhe. Riziki Omar Juma	-	- Hapana
Mhe. Abuu Hamoud Jumaa	-	Ndiyo
Mhe. Ritta Enespher Kabati	-	Ndiyo
Mhe. David Zacharia Kafulila	-	- Hapana
Mhe. Haji Khatib Kai	-	- Hapana
Mhe. Angellaah Jasmine Kairuki	-	- Hayupo
Mhe. Moshi Selemani Kakoso	-	- Ndiyo
Mhe. Innocent Edward Kalogeris	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Titus Mlengeya Kamani	-	Ndiyo
Mhe. Vick Paschal Kamata	-	Ndiyo
Mhe. Josephat Sinkamba Kandege	-	- Ndiyo
Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya	-	Hayupo
Mhe. Mariam Reuben Kasembe	-	Ndiyo
Mhe. Rosweeter Faustin Kasikila	-	- Ndiyo

Mhe. Eustace Osler Katagira	-	Ndiyo
Mhe. Vita Rashid Mfaume Kawawa	-	Hayupo
Mhe. Zainab Rashidi Kawawa	-	Ndiyo
Mhe. Gaudence Cassian Kayombo	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Kebwe Stephen Kebwe	-	Ndiyo
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa	-	Hapana
Mhe. Ali Kheir Khamis	-	Hapana
Mhe. Sadifa Juma Khamis	-	Ndiyo
Mhe. Salim Hemed Khamis	-	Hapana
Mhe. Yussuf Haji Khamis	-	Hapana
Mhe. Muhammed Seif Khatib	-	Ndiyo
Mhe. Aliko Nikusuma Kibona	-	Ndiyo
Mhe. Mendrad Lutengano Kigola	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla	-	Ndiyo
Mhe. Pudenciana Wilfred Kikwembe	-	Hayupo
Mhe. Modestus Dickson Kilufi	-	Ndiyo
Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga	-	Hapana
Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini	-	Ndiyo
Mhe. Mariam Nasoro Kisangi	-	Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka Kitandula	-	Ndiyo
Mhe. Susan Limbweni Aloyce Kiwanga	-	Hapana
Mhe. Grace Sindato Kiwelu	-	Hapana
Mhe. Silvestry Francis Koka	-	Ndiyo
Mhe. Capt. John Damiano Komba	-	Ndiyo
Mhe. Mussa Haji Kombo	-	Hayupo
Mhe. Kombo Khamis Kombo	-	Hapana
Mhe. Maulidah Anna Valerian Komu	-	Hayupo
Mhe. Al-Shaymaa John Kwegyir	-	Ndiyo
Mhe. Michael Lekule Laizer	-	Ndiyo
Mhe. Devotha Mkuwa Likokola	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Festus Bulugu Limbu	-	Ndiyo
Mhe. Alphaxard Kangi Ndege Lugola	-	Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida	-	Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde	-	Ndiyo
Mhe. John Paul Lwanji	-	Ndiyo
Mhe. Sylvester Massele Mabumba	-	Ndiyo
Mhe. Moses Joseph Machali	-	Hapana
Mhe. Betty Eliezer Machangu	-	Ndiyo
Mhe. Zarina Shamte Madabida	-	Ndiyo
Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu	-	Ndiyo
Mhe. John Shibuda Magalle	-	Hayupo
Mhe. Catherine Valentine Magige	-	Ndiyo
Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge	-	Ndiyo
Mhe. Amos Gabriel Makalla	-	Ndiyo
Mhe. Faki Haji Makame	-	Hayupo
Mhe. Ramo Matala Makani	-	Ndiyo

Mhe. Amina Nassoro Makilagi	-	Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela	-	Hayupo
Mhe. AnnaMaryStella John Mallac	-	Hapania
Mhe. Ignas Aloyce Malocha	-	Ndiyo
Mhe. David Mciwa Malolle	-	Ndiyo
Mhe. Murtaza Ally Mangungu	-	Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya	-	Ndiyo
Mhe. Abdul Jabiri Marombwa	-	Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni	-	Ndiyo
Mhe. Augustino Manyanda Masele	-	Ndiyo
Mhe. Stephen Julius Masele	-	Ndiyo
Mhe. Donald Kelvin Max	-	Hayupo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga	-	Ndiyo
Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka	-	Ndiyo
Mhe. Kuruthum Jumanne Mchuchuli	-	Hapania
Mhe. Zakia Hamdani Meghji	-	Ndiyo
Mhe. Mariam Salum Mfaki	-	Ndiyo
Mhe. Subira Khamis Mgatu	-	Ndiyo
Mhe. William Augustao Mgimwa	-	Ndiyo
Mhe. Zabein Muhaji Mhita	-	Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Minza Midimu	-	Ndiyo
Mhe. Fatuma Abdallah Mikidadi	-	Ndiyo
Mhe. Desderius John Mpata	-	Ndiyo
Mhe. Mohamed Hamisi Missanga	-	Ndiyo
Mhe. Faith Mohamed Mitambo	-	Ndiyo
Mhe. Margareth Agnes Mkanga	-	Ndiyo
Mhe. Dunstan Daniel Mkapa	-	Ndiyo
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono	-	Ndiyo
Mhe. Felix Francis Mkosamali	-	Hayupo
Mhe. Rita Louise Mlaki	-	Hayupo
Mhe. Martha Moses Mlata	-	Ndiyo
Mhe. Rebecca Michael Mngodo	-	Hapania
Mhe. Herbert James Mntangi	-	Ndiyo
Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa	-	Hapania
Mhe. Ally Keissy Mohamed	-	Ndiyo
Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	Hapania
Mhe. Rajab Mbarouk Mohammed	-	Hapania
Mhe. Luhaga Joelson Mpina	-	Ndiyo
Mhe. Maryam Salum Msabaha	-	Hapania
Mhe. Assumpter Nshunju Mshama	-	Ndiyo
Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla	-	Ndiyo
Mhe. Saidi Mohamed Mtanda	-	Ndiyo
Mhe. Abdul Rajab Mteketa	-	Ndiyo
Mhe. Abas Zuberi Mtemvu	-	Ndiyo
Mhe. Philipa Geofrey Mturano	-	Hapania
Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura	-	Ndiyo

Mhe. Thuwayba Idrisa Muhamed	-	Hapania
Mhe. Joyce John Mukya	-	Hapania
Mhe. Hasnain Mohamed Murji	-	- Ndiyo
Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu	-	- Ndiyo
Mhe. Mussa Hassan Mussa	-	Ndiyo
Mhe. Eugen Elishininga Mwaiposa	-	Ndiyo
Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa	-	- Ndiyo
Mhe. Salome Daudi Mwambu	-	- Ndiyo
Mhe. Mch. Luckson Ndaga Mwanjale	-	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa	-	- Ndiyo
Mhe. Clara Diana Mwatuka	-	Hapania
Mhe. Amina Mohamed Mwidau	-	Hapania
Mhe. Charles John Poul Mwijage	-	Ndiyo
Mhe. Hussein Mussa Mzee	-	Ndiyo
Mhe. Yusuph Abdallah Nassir	-	- Ndiyo
Mhe. Richard Mganga Ndassa	-	- Ndiyo
Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo	-	- Hapania
Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile	-	- Ndiyo
Mhe. Stephen Hilary Ngonyani	-	- Ndiyo
Mhe. Cynthia Hilda Ngoye	-	Ndiyo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali	-	Hapania
Mhe. Juma Abdallah Njwayo	-	- Ndiyo
Mhe. Juma Selemani Nkamia	-	- Ndiyo
Mhe. Said Juma Nkumba	-	Ndiyo
Mhe. Albert Obama Ntabaliba	-	- Ndiyo
Mhe. Deogratias Aloyce Ntukamazina	-	- Ndiyo
Mhe. Abia Muhamma Nyabakari	-	- Ndiyo
Mhe. Nyambari Chacha Mariba Nyangwine	-	Ndiyo
Mhe. Tauhida Cassian Galos Nyimbo	-	- Ndiyo
Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka	-	Ndiyo
Mhe. Rashid Ali Omar	-	- Hapania
Mhe. Asha Mohamed Omari	-	Ndiyo
Mhe. Suleiman Nassib Omar	-	- Ndiyo
Mhe. Saleh Ahmed Pamba	-	Ndiyo
Mhe. Ismail Aden Rage	-	- Ndiyo
Mhe. Dkt. Seif Seleman Rashidi	-	- Ndiyo
Mhe. Rachel Mashishanga Robert	-	Hapania
Mhe. Mch. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare	-	- Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza	-	Hapania
Mhe. Jasson Samson Rweikiza	-	- Ndiyo
Mhe. Mwanakhamis Kassim Said	-	Hayupo
Mhe. Said Suleiman Said	-	Hapania
Mhe. Moza Abedi Saidy	-	Hapania
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya	-	- Hapania
Mhe. Kidawa Hamid Saleh	-	Ndiyo
Mhe. Ramadhani Haji Saleh	-	- Ndiyo

Mhe. Masoud Abdalla Salim	-	Hapana
Mhe. Ahmed Ali Salum	-	Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga	-	Ndiyo
Mhe. Muhammad Ibrahim Sanya	-	Hapana
Mhe. Ali Khamis Seif	-	Hapana
Mhe. Haji Juma Sereweji	-	Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby	-	Ndiyo
Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah	-	Ndiyo
Mhe. Haroub Muhammed Shamis	-	Hapana
Mhe. Henry Daffa Shekifu	-	Ndiyo
Mhe. Beatrice Matumbo Shellukindo	-	Hayupo
Mhe. Fakharia Khamis Shomar	-	Ndiyo
Mhe. Mussa Khamis Silima	-	Ndiyo
Mhe. Namelok Edward Moringe Sokoine	-	Ndiyo
Mhe. Jitu Vrajlal Soni	-	Ndiyo
Mhe. Rose Kamili Sukum	-	Hapana
Mhe. Suleiman Masoud Nchambi Suleiman	-	Ndiyo
Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar	-	Ndiyo
Mhe. Jeremiah Solomon Sumari	-	Ndiyo
Mhe. Sabreena Hamza Sungura	-	Hapana
Mhe. Kaika Saning'o Telele	-	Hayupo
Mhe. Dkt. Charles John Tizeba	-	Ndiyo
Mhe. Salim Hassan Abdullah Turkey	-	Ndiyo
Mhe. Martha Jachi Umbulla	-	Ndiyo
Mhe. Zaynabu Matitu Vullu	-	Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura	-	Ndiyo
Mhe. Godfrey Weston Zambi	-	Ndiyo
Mhe. Selemani Jumanne Zedi	-	Ndiyo
Mhe. Said Mussa Zubeir	-	Ndiyo

**SPIKA:** Naomba kura zihesabiwe kwa maana ya idadi. Tumefanya utaratibu mzuri sana kwa hiyo, ni rahisi. Makatibu naomba muendelee kuhesabu. Itachukua dakika chache utaratibu uliokuwepo sasa ni mzuri.

(*Hapa kura zilihesabiwa na matokeo Kutangazwa*)

**ND. JOHN JOEL - KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Idadi ya Wabunge wote ni 350, idadi ya Wabunge waliopiga kura ni 315. Idadi ya Wabunge ambao hawapo Bungeni ni 34. Kura za hapana ni 81 na kura za ndiyo ni 234. (*Makofii/Vigelegiele*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *order* kwanza. Kwa hiyo, waliosema ndiyo, ndiyo wameshinda. Tumeanzisha utaratibu baada ya kupiga kura sasa hivi tunakuwa na kitabu kinaleza kila mtu alivyopiga kura na mwisho anasaini Katibu halafu na mimi pia naweka saini.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, matangazo yafuatayo kama tulivyoeleza kwa utaratibu tuliofanya asubuhi wa kuweza kutengua kile kifungu cha 106 kesho tutakuwa na *Finance Bill*, tutakuwa na Sheria ya Fedha na kesho kutwa tutakuwa na Hotuba ya Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, naamini kabisa Mwenyekiti anayehusika atakuwa amejiandaa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani pia atakuwa amejiandaa kutoa maoni yake katika Sheria tutakayopitisha kesho. (*Makofi*)

Kama nilivyosema Waheshimiwa Wabunge, safari hii Balozi wa Canada ameamua kufanya sheria ya Taifa la nchi yake hapa Bunge. Kwa hiyo, tarehe 24 Juni, 2011 baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge Wabunge wengi naomba mje mshiriki katika sheria hiyo kwa sababu Balozi yule amekuja kufanya huku kwetu kwa hiyo, ametulenga hasa sisi. Kwa hiyo, nategemea siku hiyo mtakuwa tayari na sina matangazo mengine. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wale ambao wataomba kuchangia, sasa muombe kuchangia *Finance Bill* siyo Waziri Mkuu maana mmeshajaza Waziri Mkuu, muanze kujaza kuchangia *Finance Bill* kwa sababu hiyo ndio itakayosomwa kesho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo naomba niwashukuru sana jinsi mlivyoewa kushiriki vizuri katika suala zima la mjadala wa Hotuba ya Bajeti na nadhani sasa tunaanza kuona umuhimu wa kuwaeleza wananchi kile tunachotaka kuwaeleza na siyo vinginevyo. Nimpongeze Waziri wa Fedha, Mawaziri wote na watumishi wote kwa Bajeti nzuri ambayo itaweza kutupeleka mbele. Lakini utekelezaji uwe imara.

Baada ya kusema hivyo naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.25 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano,  
Tarehe 22 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)